

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Thelathini na Mbili - Tarehe 25 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianze Saa Tatuhu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2003/2004.

**MHE. SALOME J. MBATIA (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara katika mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 309

**Barabara ya Kigarama, Bugomora hadi Murongo**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti ya Mwaka 2001/2002 Serikali iliahidi kuifanya matengenezo barabara ya Kigarama - Bugomora hadi Murongo; na kwa kuwa hadi kufikia sasa barabara hiyo bado haijafanyiwa matengenezo na imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa maeneo inakopitia:-

(a) Je, Serikali kwa kutotimiza ahadi yake inawaambia nini wananchi wa Kata ya Mabira, Bugomora na Murongo inakopitia barabara hiyo ambao wamekata tamaa kwa ahadi isiyotekelzwa?

(b) Je, sasa Serikali inaahidi kuitengeneza lini barabara hiyo?

(c) Je, Serikali itatengeneza lini barabara ya Kakanja, Nyakirigita, Kikuku hadi Kitwe ambayo haijawahi kutengenezwa tangu miaka 30 iliyopita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali iliahidi kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa awamu mbili kwa kuanzia kilomita 40 kupitia Mradi wa Uwiano na Maendeleo Vijijini (*KDRDP*) na Mfuko wa Barabara za Serikali za Mitaa (*LGRF*). Lakini Mhisani wa Mradi huo wa Uwiano wa Maendeleo Vijijini kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2002 alifuta Bajeti ya matengenezo ya barabara (*Road Rehabilitation*) kwa kutenga Bajeti ndogo kwa ajili ya kujenga madaraja ya mbao na makalvati tu.

Pamoja na fedha za Mfuko wa Barabara kuwa ndogo na kushindwa kukidhi matengenezo ya barabara hiyo, katika mwaka 2002/2003 Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato ilipanga kufanya matengenezo ya kawaida ya kilometa 40 na matengenezo ya sehemu korofii kilometa 29 ili kupunguza usumbu uliopo kwa wananchi wa maeneo hayo wakati wa kusafiri/kusafirisha mazao yao kwa nyakati za mvua pamoja na kiangazi.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2003 jumla ya kilometa 13.4 za barabara kutoka Murongo hadi Nyamiyaga imetengenezwa kwa gherama ya shilingi 21,015,800/. Kazi ya kuitengeneza barabara hii itaendelea kufanya kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe iliahidiwa kutengenezwa barabara zenye urefu wa kilomita 97.9 na Mradi wa kusimamia Kilimo na Mazingira Mkoani Kagera (*KAEMP*) ambazo ni Kihanga - Rwambaizi, Nyakagoyagoye - Rwabere, Chabalisa - Kayungu, Kayungu - Kandegesho, Kakanja - Kikukuru - Kitwe, Kyerwa – Kagenyi.

(vii) Rugu - Ruhita na Rwabitembe - Kibwera.

Mheshimiwa Spika, mpango huo wote uliotajwa hapo juu nao haukuweza kutekelezwa kutokana na gherama za matengenezo ya barabara hizo kuwa kubwa. Lakini mradi wa kusimamia Kilimo na Mazingira Mkoani Kagera (*KAEMP*) ultenga kiasi kidogo cha fedha ambazo wameamua kutengeneza barabara ya Nyakagoyagoye - Rwabere kilometa 25.2. Pamoja na matatizo hayo Halmashauri ya Karagwe ina mpango wa kuifanyia matengenezo barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge kwa awamu kwa kutumia fedha toka Mfuko wa Barabara wa Serikali za Mitaa.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba hela za Mhisani zimepungua; na katika swal (c) amekiri kwamba hela zilizotengwa na *KAEMP* zilipungua kama alivyokwishakujibu hapa; je, sasa Serikali kwa sababu imetambua hilo na vyanzo vya mapato vya Halmashauri navyo vimepungua, ina mpango gani sasa wa kutafuta katika vyanzo vingine ili iweze kuhakikisha kwamba barabara hizo ambazo hazijatengenezwa kwa miaka 30 sasa zinatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mipango yote niliyoileza ilikuwa ni juhudzi za Serikali katika kujaribu kuboresha mawasiliano ya barabara katika eneo hili. Kwa hiyo, ninachowea kumwahidi tu ni kwamba Ofisi yangu bado inaendelea kushirikiana na Halmashauri yake ili kujaribu kutafuta mbinu nyingine za kuiwezesha barabara hiyo, kuweza kupata mfadhili. Lakini vile vile tumeekubali kwamba katika mipango inayokuja, tutajaribu kuzungumza na Halmashauri hiyo ili tuone ni kiasi gani tunaweza pengine tukarekebisha programu ili kuwezesha fedha zaidi kidogo kupatikana.

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha sheria ya Kodi ya Majengo chini ya Sheria ya Mamlaka za Miji Na. 2 ya Mwaka 1983; na kwa kuwa Mamlaka za Miji zimeweka Kodi za Majengo yaliyothaminiwa Mijini; na kwa kuwa lengo la Sheria hiyo ni kuendeleza Miji hasa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, majengo yanayohusika na maendeleo ya jamii na kadhalika:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekusanya kuititia kodi hiyo tangu mwaka 1995; na ni kiasi gani kinatumika kujengea barabara Mijini ama kuendeleza vitongoji vya Miji?

(b) Kwa kuwa ipo haki ya kimsingi isemayo hakuna haki ya kutoza kodi bila uwakilishi au kuonyesha maendeleo yake yaani *No taxation without representation*; je, ni sababu zipi zinazoifanya Serikali kuwatoza wananchi kodi ambazo haziwajengei miundombinu ya barabara kama ilivyo katika vitongoji vya Mbezi Beach, Tegeta, Mikocheni, Mjini Dar es Salaam na Vitongoji vya Miji mingi nchini?

(c) Je, ni lini Serikali itafuta Sheria kama hiyo ili kuondoa migogoro katika ukadiriaji na ulipaji na badala yake kuleta Sheria ya mipango itakayowanufaisha walipaji wenyewe na kuleta ufanisi katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa Halmashauri za Manispaa 11 zilizopo chini ya Programu ya Uimarishaji Huduma Mijini zilikusanya kiasi cha shilingi 13,417,020,000/= kati ya mwaka 1995 hadi mwaka 2002 kutokana na kodi ya majengo. Fedha hizo zilitumika kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa barabara za Halmashauri. Kwa mfano, katika ujenzi wa barabara iendayo Chuo cha Usafirishaji, Halmashauri ya Kinondoni ilichangia shilingi milioni 36 milioni, Manispaa ya Moshi ilitumia shilingi milioni 25 kusawazisha barabara za Mitaa ya Kibororoni, Majengo na Pasua. Aidha, kutokana na mchango wa Halmashauri ya Manispaa ya Tanga programu ya barabara za lami iliongezeka kutoka kilometra 12 hadi kilometra 18.

(b) Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kutoza kodi ni kuziwezesha Serikali za Mitaa kutoa huduma kwa wananchi na kuendesha shughuli zake za kila siku. Hivyo, Halmashauri zote nchini hutoza kodi na kutumia kwa maendeleo ya wananchi.

Aidha, matumizi ya fedha zinazotokana na kodi au ruzuku ya Serikali inategemea na vipaumbele vya Halmashauri husika ambako Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani. Hata hivyo, ukweli ni kwamba kodi inayotozwa haitoshelezi kukamilisha mahitaji yaliyopo katika Halmashauri husika japokuwa yapo maendeleo yaliyotokana na kodi zinazotozwa na Halmashauri hapa nchini kama nilivyoelezea hapo juu.

(c) Kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kufuta kodi ya majengo kwa kuwa imeonekana ndio kodi pekee inayoweza kukusanya kirahisi bila kuleta kero kwa watu walio wengi. Wakati wote kodi hutozwa kwa kuzingatia mahitaji ya kimaendeleo ya wananchi na si vinginevyo.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri huyu ni hodari sana wa kujibu vizuri maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini kwa swali hili leo naona hakufanya uchunguzi wa kutosha kwani angekuwa amegundua adha, unyanyasaji na ubabe wanaopambana nao wananchi katika ukadiriaji holela usio na kanuni wala taratibu; je, Serikali haioni kuwa hii ni kero kubwa kama ilivyokuwa kodi ya maendeleo na hivyo ifutwe? (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, pili, sehemu nyingi duniani kodi ya majengo ni maalum yaani *specific* kwa ajili ya kujenga miundombinu kama barabara, maji, kuzoa taka na kadhalika; je, kuna maana gani kuwatoza wananchi kodi ya majengo katika mitaa yenyewe mashimo, mabwawa, uchafu uliokithiri ama maeneo ambayo hayakupimwa? (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru kwa kauli yake nzuri kwamba najitahidi kujibu vizuri pamoja na kujaribu kuniponda katika jibu nililolitoa leo. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Raynald Mrope, kwamba kodi hii ni kodi ambayo inatozwa kutokana na Sheria ambayo imetungwa na Bunge hili. Taratibu zake za namna ya kufanya *assessment* ya majengo ziko *very clear* na kwa kweli wala hazina hali ya kudhani kwamba hakuna uwazi katika *assessment* ya majengo hayo na ndiyo maana nimesema kwa sehemu kubwa ndiyo kodi tunayodhani haina kero kubwa kama zilivyoukuwa kodi nyingine. Kwa hiyo, bado tutaendelea na kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, Mheshimiwa Raynald Mrope, anasema katika nchi nyingine kodi kama hizi ni *specific* kwa ajili ya huduma fulani za jamii. Inawezekana kabisa lakini kwa nchi kama yetu ya Tanzania na umaskini ambao bado umekithiri, jambo hilo ni gumu sana. Hata kama tungenesema kodi inayokusanywa katika mtaa fulani ijenge barabara, bado haitawezekana.

Napenda kukupa mfano kwamba katika makusanyo haya niliyokwambia ya miaka karibu saba, ukifanya wastani ni kama bilioni moja kwa kila Manispaa kwa hizo Manispaa 11. Bilioni moja zinazotokana na mchango huo, ni vigumu sana kusema utazitumia kuweza kujenga huduma hizo unazozisema. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba bado tutahitaji mujumuiko wa mapato haya lakini mipango tuanzie wapi bado itabakia ni ya Manispaa.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kodi hizi za majengo zinawekwa na Mamlaka za Miji husika hivyo kutofautiana kwa Mji mmoja na *mwengine*; je, isingekuwa vema kwa Serikali hii ikaweka kiwango kimoja kwa madaraja ya aina ya nyumba zilizojengwa ili tufanane katika nchi nzima? (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wazo lake ni zuri. Lakini naomba tu nisisitize kwamba kwa sehemu kubwa viwango hivi vinawekwa kutokana na tathmini inayofanyika kwa kila jengo na kwa sehemu lilipo.

Kwa hiyo, inaweza ikawa si rahisi sana kuwa na *flat rate* bila kujali kwamba jengo hili lina ubora gani, ni la lini na lina huduma zifi ambazo zinapita katika sehemu hizo. Lakini ni jambo ambalo bado tunawenza tukalitazama katika siku zijazo tuone kama linawezekana.

Na. 311

#### **Mafunzo kwa Watumishi wa Afya**

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa kuwapeleka wafanyakazi wa fani ya Afya kwenye mafunzo kwa lengo la kuongeza ujuzi ni jambo zuri sana na la kupongezwa kwani pia ni motisha kwa wahusika:-

(a) Inapotokea kwamba baadhi ya wafanyakazi nao wamepata mafunzo yaliyolengwa na ya ziada na kuhitimu vizuri kufikia ngazi ya utaalam ambao umepita kiwango kilichohitajika Wilayani; je, kuna utaratibu gani wa kuwahamisha wafanyakazi hao kutoka kwenye Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu?

(b) Je, ni mamlaka gani kwenye Serikali Kuu inayowajibika kutoa kibali cha kupata watumishi wa kuziba pengo linaloachwa wazi katika Serikali za Mitaa?

(c) Je, Halmashauri za Wilaya zina Kauli gani na zinashirikishwa vipi katika zoezi la kupata wafanyakazi wa kuziba mapengo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kila ngazi ya utoaji wa huduma za Afya ina ikama iliyokubalika kuanzia Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa. Endapo mtumishi atajiedeleza na kuwa na kiwango cha taaluma kinachozidi mahitaji ya Wilaya, utaratibu unaofuatwa ni mtumishi husika kuwasilisha vielelezo vyake Wizara ya Afya ambayo baada ya kuthibitisha elimu/mafunzo yake itawasiliana na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Menejimenti na Utumishi wa Umma, ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuhamisha watumishi toka Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu ili mtumishi husika apangiwe kazi kwenye kituo cha juu zaidi ya Wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Menejimenti na Utumishi wa Umma ndio yenye mamlaka ya kutoa kibali cha kupata watumishi wa kuziba pengo linaloachwa wazi katika Serikali za Mitaa.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya ni mamlaka kamili za ajira kupitia kwa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya, hivyo wanayo mamlaka kamili ya kusaili na kuajiri baada ya kupata kibali cha ajira toka Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Menejimenti na Utumishi wa Umma na hivyo huweza kuziba mapengo yatakayokuwa yamejitokeza.

Na. 312

**X-Ray - Chunya**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkao wa Mbeya ulikuwemo kwenye Mpango wa Awamu ya Pili wa kupatiwa mashine ya *X-ray* kwa ajili ya Kituo cha Afya Chunya; na kwa kuwa Wilaya ya Chunya haikupatiwa mashine hiyo:-

(a) Je, ni kwa nini Wilaya ya Chunya haikupatiwa *X-ray* hiyo kwa wakati huo?

(b) Je, ni lini sasa *X-ray* itapelekwa Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Mradi wa *ORET* haikukamilisha uwekaji wa mitambo hiyo kwenye Hospitali ya Chunya kwa kuwa jengo la *X-ray* halikuwa tayari kiutaalam kukidhi mahitaji ya mionzi ayonisha. Hivi sasa jengo la *X-ray* katika Hospitali au Kituo cha Afya cha Chunya liko tayari kwa ajili ya kuwekwa mashine ya *X-ray*.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipeleka mashine ya *X-ray* Wilayani Chunya mwishoni mwa mwezi Novemba, 2002 baada ya kukamilisha ujenzi wa jengo la *X-ray*. Uwekaji wa mashine hiyo ulianza tarehe 30 Novemba, 2002 na kukamilika tarehe 2 Desemba, 2002.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza swalii la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *X-ray* zilizopelekwa kwenye Hospitali za Wilaya ikiwemo Hospitali Teule ya Biharamulo ni za teknolojia mpya hivyo kuhitaji wataalam wenye ujuzi wa hali ya juu; je, ni lini Serikali itawapeleka wataalam hao ili waweze kuzifanyia kazi kwa ajili ya kutimiza lengo lililokusudiwa? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo katika uendeshaji wa *X-ray* hizi ni uhaba wa wafanyakazi. Tunachowashauri Waheshimiwa Wabunge kuititia Halmashauri zao, wahakikishie kwamba wanaomba vibali vyta ajira kwa ajili ya kuwaajiri *Radiographers* na *Radiologist* kwa ajili ya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kusema kwamba mitambo ni mipy. Kwa kweli *Radiographer* yoyote ambaye atapata mafunzo ya muda mfupi tu, atawenza kuiendesha mitambo hii bila wasiwasi wowote.

Na. 313

#### **Ukarabati wa Mtaro wa Ntomoko**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Bajeti yake ya 2001/2002 ilitenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya ukarabati wa mtaro wa Ntomoko; na kwa kuwa mtaro huo sasa haufanyi kazi jambo linalosababisha uhaba mkubwa sana wa maji kwenye Vijiji vinavyoutegemea mtaro huo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuukarabati mtaro huo haraka iwezekanavyo ili kuondoa tatizo la maji katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoaa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Ntomoko unahusisha jumla ya Vijiji 18. Kati ya hivyo Vijiji vitano havipati maji kutokana na mradi kutokufanyiwa ukarabati katika maeneo hayo. Vijiji 13 ambavyo vilifanyiwa ukarabati kutokana na shilingi milioni 60 zilizotengwa katika Bajeti ya 2001/2002 vinapata huduma ya maji kama kawaida na maji hutolewa kwa mgao kila baada ya siku moja.

Ili kuweza kukamilisha ukarabati wa Vijiji vitano viliwyobaki na marekebisho ya chanzo cha maji cha Chemchem ya Ntomoko kiasi cha shilingi milioni 85 zinahitajika. Gharama nyingine ni zile zitakazohitajika kukarabati mtambo wa kusafishia maji na kutibu maji wa Bwawa la Mwisanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji linalowapata wananchi wanaoishi kwenye Vijiji vinavyoutegemea Mradi wa Ntomoko. Kwa sababu hiyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukarabati mradi huu na hatimaye kuwaondolea wananchi kero ya maji inayowapata. Hata hivyo, kwa kuwa Wilaya ya Kondoaa ipo kwenye Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, unaotekelizwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashauriane na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoaa, kuangalia uwezekano wa kuingiza mradi wa mtaro wa Ntomoko kwenye Mradi huo nilioutaja iwapo wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoaa wataupa mradi huo kipaumbele. Serikali itakuwa tayari kutoa ushauri unaohitajika.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baada ya ukarabati mradi huu utahitaji chombo cha kusimamia ili mradi uweze kufanya kazi vizuri; na kwa kuwa niliwhahi kutoa ombi la utaalami wa kuunda chombo cha

namna hiyo; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatusaidia utaalam wa kuunda chombo cha kusimamia mradi huu baada ya ukarabati? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, utaalam anaouomba Mheshimiwa Mbunge ni wa kuunda Kamati ya Uendeshaji wa mradi huu, kitu ambacho kwenye jibu langu la msingi nimeeleza kwamba Wizara iko tayari kutoa ushauri itakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, taarifa tulizonazo ni kwamba maeneo hayo yote wameshaunda Kamati za Watumiaji wa Maji, kitu ambacho ni sharti mojawapo katika miradi hii mipya ambayo inapelekwa Vijijini.

Na. 314

### **Vijana wa Vijijini Kuhamia Mijini**

**MHE. MARTHA M. WEJJA (k.n.y. MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna wimbi kubwa sana la vijana kutoka Vijijini kuhamia Mijini; na kwa kuwa sababu inayowafanya vijana hao wakimbilia Mijini ni umaskini uliokithiri katika Vijiji wanamotoka; na kwa kuwa katika Vijiji wanamotoka ndiko kwenye raslimali nyngi za kuweza kuleta maendeleo; na kwa kuwa vijana hao wanashindwa kuzitumia raslimali hizo na kujiletea maendeleo yao kutokana na umaskini walionao:-

(a) Je, ni athari gani zimepatikana katika nchi yetu kutokana na vijana hao amba ni nguvu kazi ya Taifa letu kuhamia Mijini?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia vijana waliopo Vijijini ili waondokane na umaskini na pia waondokane na tabia ya kuhamia Mijini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vijana wengi kutoka Vijijini wanahamia Mijini kutafuta ajira na maisha bora zaidi. Athari zinazopatikana katika nchi yetu kutokana na vijana hao amba ni nguvu kazi ya Taifa letu kuhamia Mijini ni kushuka kwa viwango vya uzalishaji, kupungua kwa Pato la Taifa na la wananchi kwa ujumla.

Kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu; na kwa kuzingatia kuwa ndio shughuli kuu inayofanya Vijijini, hivyo vijana wakikimbilia Mijini nguvu kazi ya kuendeleza kilimo na shughuli nyngine za maendeleo huko Vijijini hupungua.

Vile vile vijana wakikimbilia Mijini wanapata matatizo ya ukosefu wa ajira, makazi na kupata lishe duni hali ambayo inasababisha vijana kutafuta njia ambazo si halali kama vile wizi, ujambazi, usafirishaji wa madawa ya kulevyo ili kukidhi mahitaji yao muhimu. Hali hii inaongezeka mwaka hadi mwaka na inakuwa ni tishio la amani na utilivu nchini.

(b) Serikali inaendelea kuweka mazingira bora ya kuchochea shughuli za uzalishaji mali Vijijini kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini kama vile kuboresha huduma za elimu ya msingi, huduma za barabara Vijijini, afya na maji. Aidha, tunaweka mkazo mkubwa katika elimu ya ufundi stadi ili kiwango kidogo cha mikopo kwa vikundi vya vijana kiweze kuwa chenye manufaa.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuwahamasishe na kuwasaidia vijana kujunga katika vikundi vya uzalishaji mali na kutumia vyuo vya ufundi stadi ili waweze kunufaika na jitihada za Serikali katika kupambana na umaskini.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua udhaifu wa vijana wetu wanaokimbilia Mijini; na kwa sababu Serikali iliamua kutoa mikopo kwa vijana; je, Serikali haoni kwamba sasa kuna haja kwa mikopo ile ilekezwe badala ya kupewa vijana wa Mijini, ilekezwe moja kwa moja katika Kata za Vijijini ili kuwawutia hawa waliopo Mijini warudi Vijijini wakakutane na hiyo mikopo ili wasirudi tena Mijini? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwetu sisi Serikali kama walezi vijana wote wale waishio Mijini na wale waishio Vijijini kwetu ni sawa, hatuezi tukabagua kwamba iende Vijijini ili vijana wasije Mijini au waliopo Mijini warudi. Tukumbuke kwamba kuna vijana ambaao kwa sababu ya wazazi wao kuishi Mijini wanazaliwa, kukua mpaka kuzeeka wakiwa Mijini, hawa tukitarajia warudi Vijijini watakwenda kuwa wageni na kutakuwa na tatizo kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuangalie mzizi zaidi katika kutatta tatizo hili kuliko kuangalia tawi.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba ufundi stadi ni moja ya nyenzo za kupunguza umaskini, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ile Mikoa maskini zaidi kwa maana ya Mikoa ya Lindi, Kigoma na Pwani ndiyo Mikoa pekee ambayo haina Vyuo vya Ufundu; je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu Mikoa hiyo kupatiwa Vyuo vya Ufundu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha ya kwamba kila Mkao unapata Chuo cha *VETA* na ndio maana hivi sasa Kigoma chuo tunategemea kukimaliza mwakani na kwa mipango ya *VETA*, mara baada ya kumalizwa Mkao wa Kigoma ujenzi wa chuo kipyta utahamia Mkao wa Lindi.

Kwa hiyo, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkao wa Lindi wavute subira, mambo yatakwenda tu. (*Kicheko/Makofî*)

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema tumeweza kuwaelimisha vijana wetu wengi; na kwa hakika ni hawa walioelimika ambaao wamejaliwa kupata mwanga kutoka Vijijini kwenda Mijini kwa sababu ya kuweka maisha yao katika hali nafuu; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni badala ya kufikiria kujenga vyuo tu na vyuo vyenyewe navyo ni vya muhimu, kwamba sasa imefika wakati wa kuunda vikundi vinavyoweza kupewa misaada ya kutosha tukakimbia ardhi hii nyingi ambayo sasa hivi haitumiki vizuri badala ya kuwaacha vijana hawa wakizagaa na kuanza kuwa walevi wa bangi na madawa ya kulevya? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hivi alivyoshauri ndivyo Serikali tunavyofanya. Hata hivyo *syllabus* ya Vyuo vya *VETA* haifanani kwa nchi nzima, tunaangalia hasa mazingira ya eneo husika kwa mfano ukienda kwenye Kanda ya Ziwa tunahangaikia zaidi masuala ya uvuvi, utengenezaji wa boti, kilimo na kadhalika.

Kwa hiyo, pamoja na kutoa elimu hiyo kwa vijana vile vile tunawafundisha ujasirimali (*entrepreneurship*) ili waweze kutumia elimu ile kwa misingi ya kibashara zaidi na waweze kufanya kazi zao kwa makini.

Mheshimiwa Spika, ni vema tukakumbushana hapa kwamba wajibu wa kuhamasisha vijana kutumia ardhi yetu kikamilifu ni wajibu wa kila mmoja wetu pamoja na jamii. Serikali ni sehemu tu ya

Watanzania katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaacha tabia ya kukimbilia mijini maana popote alipo anaweza kupata riziki yake.

Na. 315

### **Kudidimia kwa Mpira wa Miguu**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kudidimia kwa mchezo wa mpira wa miguu nchini kunatokana na uongozi mbovu kuanzia ngazi ya vilabu hadi Taifa?

(b) Je, Serikali imebaini sababu gani za msingi ambazo zinasababisha Chama cha Mpira wa Miguu nchini (*FAT*) na baadhi ya vilabu vyta mpira wa miguu nchini kuwa na uongozi mbovu?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kunusuru mchezo wa mpira wa miguu amba unapendwa na Watanzania walio wengi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbconde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa uongozi mbovu katika vilabu na Taifa ni moja ya sababu zinazoufanya mchezo wa mpira wa miguu kuendelea kuzorota.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imebaini kuwa baadhi ya sababu zinazosababisha Chama cha Mpira wa Miguu na baadhi ya vilabu kuwa na uongozi mbovu ni pamoja na matumizi mabaya ya demokrasia, ubinafsi, umaskini na elimu duni ya wapiga kura wa viongozi hao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua kadhaa ili kuboresha mchezo huo unaopendwa na Watanzania walio wengi. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya uongozi kwa viongozi na wanachama wa Vyama vyta Mchezo wa Mipira wa Miguu kwa njia ya semina na mikutano.

Aidha, Serikali inatoa miongozo kila inapobidi na kusaidia kutatta migogoro kila inapojoitokeza. Vile vile, Serikali imeweka mazingira bora ya kuruhusu Vyama vyetu kujishirikisha na Vyama vyta nje, hatua inayowezesha Vyama vyta nje kuleta wataalam na vifaa kwa ajili ya mafunzo ya fani mbalimbali za michezo.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa sababu zilizoainishwa na pengine Serikali kuipa kisogo zimechangia maendeleo ya Taifa Stars na kwa kuwa hadhi ya nchi kama Cameroon na Nigeria jukumu la kuilea Timu ya Taifa ni la Serikali na wamefanikiwa sana je, si kweli kwamba wakati umefika kwa Serikali kuingilia kati maendeleo ya *Taifa Stars* kwanza kwa kumwajiri Mwalimu mwenye ujuzi na vile vile kuunda Kamati Maalum ya Watu Maarufu ili kusimamia na kuendeleza *Taifa Stars*?

(b) Kwa kuwa Katibu Mkuu na Msaidizi wake huchaguliwa kwa misingi ya ushabiki zaidi kuliko uwezo wao katika medani ya uongozi wa soko kiasi kwamba hata Fundi Cherehani anachaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa *FAT*, je, si kweli kwamba wakati umefika Katibu Mkuu na Msaidizi wake wakawa waajiriwa waliosailiwa na kuchujwa? (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba katika baadhi ya nchi Serikali hubeba jukumu la kulea Timu ya Taifa sio kuteua Timu ya Taifa kulea Timu ya Taifa. Kwa bahati mbaya kwa Tanzania na baadhi ya nchi katika

Afrika uhusiano baina ya Chama cha Mchezo wa Mpira wa Miguu na Serikali unakuwa mbali kama mbigu na ardhi kuliko uhusiano wa Chama hicho na *FIFA*. Inapotokea mazingira hayo, kuundwa kwa timu yenye ya Taifa kunakuwa ni kugumu kwa hiyo hata Serikali huwa haina mtoto wa kumlea.

Waheshimiwa Wabunge, watakubaliana nami kwamba Mwenyekiti wa *FAT* alifikia mahali kuita Waandishi wa Habari na kutangaza kwamba Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Michezo asidiriki sio kufika kukaribia kwenye Ofisi za *FAT*. Katika mazingira haya, ni vema na nampongeza Waziri kuchukua hatua ya kuamua kuzungumza kuliko kupambana maana kupambana ni dalili ya hekima za kinyama zaidi kuliko binadamu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu uchaguzi wa Katibu Mkoo na viongozi wake, ama sina uhakika kama Katibu Mkoo tuliyenaye ni Fundi Cherehani au katika waliopita wamewahi kuwepo Makatibu Wakuu Mafundi Cherehani lakini kwa taratibu za *FIFA* tunashindwa sisi kutoa ajira kwa Katibu Mkoo na Naibu Katibu Mkoo.

Hata hivyo, tulifurahi sana kwa sababu Katibu Mkoo Msaidizi wa *FAT* ni mtumishi wa Serikali na ndio nafuu mnayoiona ndani ya *FAT* kama sio hivyo nafikiri balaa lingekuwa kubwa zaidi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Swali moja la mwisho, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, mambo ya mpira, aah, subiri kidogo tupate majibu ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya michezo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea kidogo majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbonde.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Bakari Mbonde, kwamba huko ndiko tunakoelekea kwa Serikali kuilea timu ya Taifa lakini ilibidi kwanza kufanya vitu vifuatavyo. Jambo la kwanza ilikuwa ni Serikali kujenga uchumi ulio imara ili iwe na uwezo wa kuwekeza katika michezo. Sasa hivi kama mtakavyoona katika Bajeti yetu tayari suala la kuandaa miundombinu mizuri kwa ajili hiyo itakuwa imeanza kwa kasi mpya zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu namna ya kuilea, kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba huko nyuma tulikuwa na Kamati na naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mengi wakati alipokuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum, Kamati zilikuwepo na zilifanya kazi nzuri. Kilichofanya Kamati zile zishindwe kufanya kazi ni uongozi mbovu ulioko *FAT*.

Kwa hiyo, ili tuondokane na tatizo la uongozo mbovu kama nilivyozungumza nadhani kwenye Bunge hili hili tunahitaji msaada wa pamoja. Waheshimiwa Wabunge kule mnakotoka ndiko ambako chaguzi hizi zinaanza kwa nini msiwahamasishe wanamichezo wenu wanaokuja kupiga kura Kitaifa kuwaondoa viongozi wabovu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana Mikoa ambayo ndio michezo imeshamiri kama Dar es Salaam, Tanga, Kagera ndipo ambapo wanashabikia viongozi wabovu, inasitikisha. Sasa Waheshimiwa Wabunge tusaidiane tuwahamasishe wanamichezo huko waliko kuwaondoa viongozi wabovu.

Mheshimiwa Spika, swali la mwisho kwamba inawezekana ukawa na Katibu Mkoo Fundi Cherehani, Katibu Mkoo wa michezo yetu yote ni mtu ambaye hategemei kupata mshahara pale kwa hiyo ni dhahiri lazima atakuwa na kazi yake. Sasa akiwa ni Fundi Cherehani, Mkulima, Mwalimu ili mradi tu ana nia ya kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu na kama anafaa anaweza akachaguliwa kama hafai aondolewe lakini kazi ya kuwaondoa ni yetu wote Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati Naibu Waziri akijibu swali la msingi ameeliteza jitihada mbalimbali ambazo zinafanyika ili kuboresha mchezo huu wa mpira wa miguu na kuwa na timu imara ya Taifa.

Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aelewé kwamba kipimo cha kufanikiwa jitihada zozote zile huwa ni kushinda sasa timu yetu imekuwa inafungwa tu, imekuwa kama kichwa cha mwendawazimu cha kujifunzia kunyoa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kukubaliana nami kwamba kwa timu ambazo zimeonyesha jitihada ya kufanya vizuri kama Simba ikawakilisha Taifa? (*Kicheko/Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mbunge kwamba katika klabu kunakuwa na timu ya Taifa. Timu ya Taifa inatakiwa ichukue wachezaji kutoka katika klabu mbalimbali ile inayofanya vizuri kama klabu lakini kuna klabu inaweza kufanya vizuri kama klabu ikawa na wachezaji wazuri zaidi.

Kwa hiyo, hili wazo la kutaka Simba mwaka huu ikawakilishe Taifa kwa sababu inafanya vizuri katika Kombe la Taifa siwezi kusema kwamba ni ulimbukeni lakini pengine ni kusahau historia kwa sababu ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge na mashabiki wenzake wa Simba kwamba Yangi ilifiki mahali kutolewa kwa shilingi.... (*Kicheko*)

**SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, swali linalofuata. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, *order, order*, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali langu, naomba nichukue nafasi hii kumponegeza Mheshimiwa Bakari Mwapachu, kwa kufikisha miaka 64 tangu azaliwe. (*Kicheko/Makofsi*)

Na. 316

### **Mahakimu wa Mikoa na Wilaya**

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kuwarudisha Mahakimu wa Mikoa na Wilaya (*Honorary Magistrates*) ambao kwa sasa wanalipwa shilingi 10,000 kwa kumaliza shauri moja; na kwa kuwa Mahakimu hao pia wanasiliza mashauri nje ya vituo vyao na wakati mwingine wanakwenda kukagua mashamba nje ya vituo vyao vya kazi bila kulipwa *night allowances*:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ili kupunguza vishawishi vya kupokea rushwa ni vizuri malipo ya Mahakimu hao yakaongezwa pamoja na haki zao nyingine ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, kwa pongezi hizo za kufikia umri wa miaka 64 lakini watu wasitishike bado na *mileage* nyingi na uwezo kama Mzee Mandela vile. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mbunge wa Kilosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuwatumia Mahakimu wa Heshima katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya umelenga ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa Mahakimu nchini. Mahakimu hawa hawafanyi kazi kwa muda wote bali huitwa kusaidia pale mzigo wa kesi unapokuwa mkubwa. Kwa utaratibu ulioainishwa na Tangazo la Serikali Na.43 la mwaka 1996 hulipwa shilingi 10,000 kwa kila shauri wanilosikiliza na kulitolea hukumu na wanaposafiri nje ya kituo cha kazi ama hulipwa shilingi 10,000 kwa kila siku au kulipwa gharama halisi ya chakula na malazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umeleta malalamiko mengi ikiwa ni pamoja yale aliyoyaeleza Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, kubwa ni malipo ya Mahakimu hao kuwa makubwa kuliko ya Mahakimu wa kawaida. Ili kukabiliana na matatizo hayo, imeamuliwa kwamba utaratibu wa kawaida wa

ajira ya mkataba utumike badala ya kuwafanya kuwa Mahakimu wa Heshima. Sasa tumeanza kuutekeleza utaratibu huo.

Na. 317

### **Mshtakiwa Kukata Rufaa**

#### **MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa mshtakiwa anapokata rufaa halafu ikaonekana kuwa bado anayo hatia huongezewa adhabu:-

Je, kwa nini Hakimu aliyetoa hukumu hiyo hapewi adhabu kama mshtakiwa akishinda rufaa yake?

#### **WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa misingi ya Katiba na Sheria, Mahakama zimewekewa ngazi ambapo mtu asiporidhika na uamuzi wa ngazi ya Mahakama moja, anaweza kukata rufaa kwenda katika ngazi inayofuata. Kwa utaratibu huu, yule anayeonekana na hatia katika rufaa anaweza kuongezewa, kupunguziwa, kufutiwa au kubakiziwa adhabu ile ile kutegemeana na sheria inayosimamia kosa husika. Hivyo siyo sahihi kuwa kila rufaa inayoshindwa huambatana na ongezeko la adhabu.

Mahakimu wanapoamua mashauri wanapaswa wafanye hivyo kwa uhuru ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wahusika. Maadili ya kazi ya uhakimu yanataka Hakimu asiamue kwa upendeleo, woga au vishawishi vya aina yoyote. Hali ya kumtaka Hakimu awajibike binafsi kwa maamuzi anayotoa inaweza kusababisha woga na hivyo kuathiri suala zima la utoaji haki. Kwa kuzingatia hilo, sheria zinaleza wazi kuwa Hakimu hawajibiki binafsi kwa maamuzi atakayoyafanya katika kutekeleza majukumu yake kama Hakimu.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa Hakimu hatakiwi kuwajibishwa iwapo mrufaa atashinda, je, Serikali inakuwa na uhakika gani kwamba Hakimu yule hakutoa hukumu ile kwa upendeleo ili kutenda haki na kumfanya atoe hukumu kwa haki?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhakikisha kwamba hukumu imetolewa kwa njia ipasayo kwa upande mmoja ni Serikali lakini wanaowajibika na suala hili ni Idara ya Mahakama yenyewe. Ikiwa Hakimu anatuhumiwa kutotoa haki kwa njia ipasayo kama ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo basi Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anaweza kumchukulia hatua ya kisheria hivyo hivyo mpaka Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

Kwa hiyo, uko utaratibu wa kuwadhibiti Mahakimu ambao hawakutoa haki inavyostahili. Pia waathirika wana haki ya kukataa Rufaa toka Mahakama ya Mwanzo, Wilaya, Mkoa, Mahakama Kuu mpaka Mahakama ya Rufaa.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kupata nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Kwa kuwa Mahakimu ni binadamu kama binadamu wengine na kutokana na ukweli kwamba kwa sasa hivi maamuzi mengine yamefanywa bila kufuata haki kutokana na Mahakimu kujua kwamba hawawezi kuulizwa. Wakati hukumu inapokatwa mhusika anapewa adhabu wakati ule ule je, Serikali

haioni kwamba ni kinyume cha haki za binadamu kumuadhibu mtu baadaye ikagundulika kwamba kaonewa na keshatumikia adhabu na yule aliyemuadhibu hachukuliwi hatua? (*Makofii*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nadhani swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdillah Namkulala, linafanana na hili, nasema utaratibu upo kwa maana kwamba kama Hakimu naye atatuhumiwa hakutoa hukumu sahihi basi anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kipo kitabu cha *Conduct of Ethics*. Ninachojaribu kusema ni kwamba upo utaratibu wa Kimahakama tukifanya vinginevyo tutawafanya hawa Mahakimu wawe waoga. Hatuwezi kulinganisha masuala ya mtendaji Serikalini moja kwa moja na Hakimu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa sheria inayotumika ni ile ile na usikilizaji ni ule ule na kwa sababu tunafuta haki ya aliye na kesi je, kwa nini isimalizwe huku huku kwenye Mahakama ya Mwanzo ili kupunguza usumbufu kwa raia zetu kwenda mpaka Mahakama ya Rufaa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, swali hili pia linafanana na maswali yote mawili ambayo nimeyajibu. Ikiwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo amekosea anaweza akajikosoa lakini ni mara chache kukuta Hakimu anachukua hatua ya namna hiyo ya kuikosoa.

Kwa hiyo, utaratibu ambao ni mzuri kama haki haikutendeka basi kwa yule ambaye amethirika ni budi ye ye kwenda kwenye ngazi ya juu ili waweze kufanya mapitio ya mwenendo wa kesi ile na kuona kama haki kwa kweli haikutendeka na kufanya marekebisho.

Na. 318

### **Kilimo Wilaya ya Kongwa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa mazao ya Mahindi, Nyonyo, MBAazi, Alizeti, Karanga na Zaibibu ni tegemeo kubwa kwa kipato cha wananchi Mkoo wa Dodoma hasa wa Wilaya za Kongwa na Mpwapwa; na kwa kuwa mazao hayo yamekuwa yakikabiliwa na matatizo mengi sana yakiwemo yale ya ukosefu wa masoko ya ndani/nje, ukosefu wa madawa ya kuulia wadudu, mbegu bora na zaidi kuanguka kwa bei ya mazao hayo kwenye masoko ya ndani na nje hali ambayo inawaathiri sana wakulima wa mazao hayo kwenye maeneo niliyotaja na kwenye maeneo mengine ya nchi, hadi baadhi ya wakulima kukata tamaa ya kuendelea kulima mazao hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua ari ya wakulima hao kwa lengo la kuyaendeleza mazao hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Ili kuinua ari ya wakulima na kuendeleza mazao yaliyotajwa na Mheshimiwa Job Ndugai, Serikali inafanya mambo yafuatayo:-

(i) Serikali imeanzisha utaratibu wa kuzalisha mbegu bora kwa kutumia wakulima wadogo vijijini ikiwa ni pamoja na wakulima wa Wilaya za Kongwa, Mpwapwa, Kondoa na Dodoma Vijijini. Mbegu zinazozalishwa ni za Mahindi, Mtama, Uwele, Alizeti, MBAazi, Kunde na Ufuta.

(ii) Kuendelea kuboresha utafiti wa mazao hayo ili kupata jamii ya mazao inayokidhi mahitaji mbalimbali. Kwa mfano, Kituo cha Utafiti cha Ilonga kimefanikiwa kutoa mbegu ya mbaazi iitwayo Komboa ambayo huchukua siku 100 tu kukomaa na hutoa mavuno kiasi cha tani 4 kwa hektaa ikilinganishwa na wastani wa tani 2 kwa hekta zinazoweza kuzalishwa na mbegu za asili.

(iii) Kuimariisa Mfuko wa Pembejeo (*Agricultural Inputs Trust Fund*) ambapo hivi sasa fedha za mfuko huo zitakopeshwa kupitia taasisi za fedha kadhaa zikiwemo Benki ya *Exim; Kilimanjaro Cooperative Bank, Kagera Farmers Cooperative Bank, SCULT* na *Mufindi Community Bank*.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima kupata soko la uhakika wa mazao yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Kuboresha miundombinu ya masoko, hususani barabara za vijijini, magulio/masoko na maghala ya kuhifadhiya mazao. Kwa mfano hivi sasa ujenzi wa soko la nafaka katika Mji Mdogo wa Kibaigwa Wilayani Kongwa chini ya Mradi wa Kuendeleza Masoko unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa utaanza Julai, 2003. Ujenzi wa soko hili ukikamilika utawanufaisha zaidi wakulima wa Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine ya jirani.

(ii) Kuhamasisha wazalishaji wadogo kuijunga katika Vyama vya Ushirika vitakavyoweza kukusanya mazao na kutafuta masoko kwa kuwa ni rahisi kupata soko la uhakika kama uwingu wa zao unajulikana. Ushirika utawawezesha wakulima kupatana bei vizuri kuliko kama kila mkulima atauza peke yake.

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana Wizara ya Ushirika na Masoko, zinaandaa utaratibu wa kuanzisha Bodi ya mazao mchanganyiko ambayo itafanya kazi yenye au kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika kutafuta masoko ya mazao mchanganyiko kama Mahindi, MBAazi, Alizeti, Karanga, Zabibu na mengineyo.

(iv) Kuruhusu uuzaji wa nafaka hususan mahindi katika masoko ya nje na kuhamasisha jumuiya ya wafanyabiashara kutafuta masoko ya mazao hayo katika nchi jirani kupitia Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuia ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

(v) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, *Tanzania Investment Centre (TIC)* na Shirika la Viwanda vidogo Vidogo (SIDO), Wizara ya Ushirika na Masoko itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kusindika mazao na kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu usindikaji wa mazao hususan mbogamboga, matunda na mbegu za mafuta.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza na vile vile nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa tatizo kuu la kufanikisha wakulima hawa kiuchumi ni masoko na Serikali kwa muda mrefu ilishatuahidi kwamba ingeanzishwa Bodi maalum ya kushughulikia mazao madogo madogo kama haya yanayolimwa katika Mkoa wa Dodoma lakini Bodi hii haianzishwi, je, Serikali imejizatiti kuanzisha Bodi hii lini?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa maelezo katika jibu la msingi, moja ya hatua ambazo Serikali inachukua ni uanzishaji wa Bodi ya Kusimamia Mazao Mchanganyiko na hatua za uanzishaji wa Bodi hii ni za kiwango cha juu sana. Hivi sasa nyaraka mbalimbali zinazohusika zinaandaliwa na kufikishwa katika mamlaka za uamuza ili Bodi hiyo iweze kuanzishwa.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa Wizara ya Ushirika na Masoko, ndio mhimili wa mazao yetu, ina mpango gani wa kukusanya mazao na kuyaweka katika maghala amabyo tunayo hasa ukizingati kwamba zaidi ya asilimia 40 ya mazao ya wakulima hipotelea mashambani na hali duni ya utunzaji wa mazao haya yakiwa majumbani. Je, Serikali ina mpango gani wa kukusanya mazao haya na kuyatunza katika sehemu ambazo tayari tunazo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nilipokuwa natoa majibu katika swali la msingi nilieleza kwamba njia mojawapo ambayo itahakikisha kwamba upatikanaji wa masoko kwa uhakika ni uanzishaji wa Vyama vya Ushirika pamoja na kuandaa maghala ambayo yanaweza kutunza mazao hayo.

Kwa hiyo, kimsingi Serikali imeshaanza kufanya maandalizi ambayo Mheshimiwa Mbunge anayaulizia. Kwa hiyo, ningependa tu kutoa wito kwamba njia ambayo inaweza ikayaokoa mazao ya wakulima kuuzwa kwa usalama na uhakika ni kuanzishwa Vyama vya Ushirika ambavyo vitakuwa vimejiandalia utaratibu wa maghala yao na hivyo mazao yao yakauzwa salama. (*Makofisi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha, tunaendelea. Kwanza nina matangazo. Wakati kipindi cha maswali kinaendelea ameingia mgeni wa Kimataifa katika *gallery* naye ni Mheshimiwa Felix Ubor, ambayo ni *Country Representative* wa *UNIDO* hapa nchini, yuko na mke wake. Tunamkaribisha. (*Makofisi*)

Vikao vya Kamati kwa leo ni Kamati mbili, Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa ajili ya kupitia Muswada wa *Finance Bill*, kikao kitakuwa saa 5.00 asubuhi chumba Namba 56. Pia Kamati, hii siyo Kamati ila ni Wabunge Wanawake wote (*TWPG*), Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba Wabunge wote wanawake wabaki humu kwenye ukumbi itakapofika saa 7.00 mchana ili wapewe taarifa aliyonayo.

Mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper*.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### MGONGANO WA KISHERIA KATIKA UTARATIBU WA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA VIJIJI, VITONGOJI NA MITAA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Aprili, 2003 Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijiji, kwa tiketi ya Chama cha *Tanzania Labour Party* aliwasilisha kwako hoja binafsi yenyе kichwa cha habari kinachosema “Hoja ya Kuahirisha Bunge”. Katika hoja hiyo Mheshimiwa Mbunge alianisha masuala yafuatayo:-

Kwamba, kuna mgongano kati ya taratibu za uchaguzi wa viongozi wa ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa zilizotungwa kwa kufuata maelekezo ya Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka ya Wilaya Na. 7 ya Mwaka 1982 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji Na. 8 ya Mwaka 1982 na taratibu za uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa kwa upande wa Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya Mwaka 1979.

Kwamba, Kamati za malalamiko zinapolalamikiwa kwamba mwenendo wa uchaguzi haukuwa huru na wa haki, Kamati hizi huamua bila haki kutokana na chuki binafsi au kwa kupendelea Chama fulani kwa kuwa wajumbe wake ni wanachama wa Chama fulani ambacho mgombea wa Chama chao hicho hakushinda.

Kwamba, wajumbe wa Kamati za Malalamiko walikula njama na kuamua kwamba mwenendo wa uchaguzi katika Vijiji vya Mande, Kata ya *Old Moshi*; Bagala, Wilaya ya Babati, Katesh, Hanang na Rangi Tatu, Temeke, ulikuwa na kasoro na hivyo kufuta matokeo ya uchaguzi na kutaka uchaguzi urudiwe mpaka hapo mgombea wa Chama ambacho wajumbe hao wanaKitaka atakaposhinda.

Kwamba, kubatilishwa kwa uchaguzi katika Kijiji cha Katesh, Jimbo la Hanang, linalowakilishwa na Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge na Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuonyeshi Utawala Bora wala mfano wa kuiga. Kwamba Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge na Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipaswa aingilie kati kwa kukemea kitendo cha kubatilisha matokeo kilichofanywa na Kamati ya Malalamiko.

Kwamba, Mahakama Kuu ya Tanzania katika kesi ya *Miscellaneous Civil Case No. 72* ya 2000, ilito uamuzi kuhusiana na madaraka ya Kamati za Malalamiko na Kamati za Rufaa kwamba hazina uwezo wa kisheria kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa isipokuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Kwamba, alimradi hukumu ya Mahakama Kuu katika kesi ya madai *Miscellaneous Civil Case No. 72* ya 2000, haikupingwa kwa njia ya rufaa maamuzi yake yana nguvu ya kisheria na sharti yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na hili la mgongano kati ya taratibu za uchaguzi ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa na Sheria Na. 4 ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, kwamba hakuna mgongano wowote kati ya taratibu za uchaguzi wa viongozi wa ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya Mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, chaguzi zote katika ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa zinatawaliwa na Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka ya Wilaya Na. 7 ya Mwaka 1982 na Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji Na. 8 ya Mwaka 1982. Chini ya vifungu mbalimbali vyta sheria hizi Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amepewa madaraka ya kutengeneza taratibu zinazohusiana na chaguzi mbalimbali katika ngazi nilizozitaja. Kwa mfano, vifungu vyta sheria vinavyohusiana na chaguzi chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji Na. 8 ya Mwaka 1982 ni kifungu Na. 4, 14(3) na 70(c) kwa ajili ya uchaguzi wa Halmashauri ya Kijiji, Vijiji vile ambavyo vipo katika maeneo ya Miji. Vifungu Na. 14(4) na 70(c) kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati za Mtaa na vifungu Na. 14(4) na 70(c) kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji. Vifungu vyta sheria vinavyohusiana na uchaguzi chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Na. 7 ya Mwaka 1982 ni kifungu Na. 53(3) kwa ajili ya uchaguzi wa Halmashauri ya Kijiji na kifungu Na. 30(4) kwa ajili ya Mwenyekiti wa Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madaraka aliyopewa Waziri mwenye dhamana ya Serikali ya Mitaa chini ya vifungu vyta sheria nilivyoitaja mwaka 1999, Waziri alitengeneza taratibu mbalimbali za uchaguzi kama matangazo ya Serikali Na. 253, 154, 155, 156 zote za mwaka 1999 na 256(a) vile vile vyta 1999 vinavyoinisha. Chini ya sheria hizi ndogo muundo na majukumu ya Kamati za Malalamiko na Kamati ya Rufaa imefafanuliwa waziwazi. Muundo wa Kamati hizi upo kama ifuatavyo:-

Kamati ya Malalamiko katika Mamlaka za Wilaya, kwanza ni Afisa Mtendaji wa Kata inayohusika au Afisa mwagine atakayeteuliwa ambaye atakuwa Mwenyekiti. Afisa ye yeyote wa umma ambaye anafanya kazi katika Kata na Mwakilishi wa Mkurugenzi.

Kamati ya Malalamiko katika Mamlaka za Miji ni mwakilishi wa Mkurugenzi ambaye atakuwa ni Mwenyekiti na maafiga wawili walio katika utumishi wa umma katika eneo la Kata inayohusika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya Mwaka 1979 ni sheria ambayo inaweka taratibu za uchaguzi wa Madiwani katika Halmashauri za Wilaya na Miji na kamwe haina mahusiano yoyote na uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mijini na Wilayani katika ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba madai ya Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge, ya kuwepo kwa mgongano wa sheria hayana msingi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hajui tofauti kati ya Kamati ya Malalamiko na Kamati ya Rufaa. Majukumu ya Kamati ya Malalamiko kama ilivyoainishwa katika vifungu Na. 10 na 16 vyta taratibu za uchaguzi za mwaka 1999, ni kusikiliza na kuamua kuhusu malalamiko kutoka kwa mgombea yeyote dhidi ya uteuzi uliofanywa na msimamizi wa uchaguzi. Jukumu la Kamati hii pia ni kusikiliza malalamiko ya mgombea yeyote dhidi ya uendeshaji wa uchaguzi. Hata hivyo, katika hatua zote hizi mbili maamuzi ya Kamati hii siyo ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Rufaa. Kama jina lake linavyoonyesha ni Kamati inayosikiliza Rufaa zinazotokana na maamuzi ya Kamati ya Malalamiko katika ngazi ya uteuzi na pia

katika ngazi ya uendeshaji wa uchaguzi. Kwa hiyo, siyo kweli kama inavyodaiwa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwamba Kamati ya Malalamiko zimekuwa zinafuta matokeo ya uchaguzi na kutaka uchaguzi urudiwe kwa kuwa baada ya uamuzi huo mlalamikaji anayo haki ya kupeleka malalamiko yake kwenye Kamati ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, hakutoa ushahidi wowote kudhibitisha madai yake ya kwamba Kamati za Malalamiko zimekuwa zikiamua bila haki kutokana na chuki binafsi au kupendelea Chama fulani kwa kuwa wajumbe wake ni wanachama wa Chama fulani ambacho mgombea wa Chama hicho hakushinda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali Kamati za Malalamiko hazina uamuzi wa mwisho kwa kuwa wagombea wamepewa nafasi ya kukata rufaa wanapokuwa hawakuridhika na uteuzi au uendeshaji wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibitisha madai yake Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ametoa mifano ya uchaguzi uliofanyika katika Kijiji cha Bagala Babati, Katesh Hanang na Mande Kata ya *Old Moshi Tela*, Moshi Vijijini na uchaguzi wa Mtaa wa Rangi Tatu Temeke. Uchaguzi wa Vijiji vitatu viliviyotajwa ulifanyika kwa mujibu wa kifungu cha 56(3) na Sheria Na. 7 ya Mwaka 1982 na sheria ndogo katika tangazo la Serikali Na. 254 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, madai ya Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kuhusu Vyama vya Upinzani kushinda katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Bagala, Wilayani Babati siyo ya kweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi wa Kijiji hicho, uchaguzi katika Kijiji hicho ulifanyika mara moja tu na matokeo ya uchaguzi katika Kijiji hicho uliofanyika mwezi Novemba, 1999 yanaonyesha kuwa mgombea wa Kiti hicho aliyeshinda alitokana na Chama cha CCM na alipata kura 349 na mgombea kutoka Chama cha *NCCR* mageuzi alipata kura 29. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika wagombea saba walioshinda katika uchaguzi wa Vitongoji katika Kijiji hicho cha Bagala walitokana na Chama cha CCM. Kitongoji kimoja hakikupata mshindi kwa kuwa mgombea pekee wa CCM aliyegombea alipata kura 55 za hapana na kura 35 za ndiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi mdogo uliofanyika kati ya tarehe 15 na 16 Machi, 2003, katika Kijiji cha Katesh Hanang matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo:-

cheo cha Mwenyekiti wa Kijiji, wagombea walikuwa wanne, Bwana Benard Babisai wa CCM, alipata kura 350, Bwana Mathayo Binamu wa CCM alipata kura 329, Bwana Elias Babai wa *TLP* alipata kura 650, Bwana Gasper Mosi wa *TLP* alipata kura 728. Viti Maalum Bibi Zulfa Ismail wa CCM alipata kura 379 na Bibi Lydia Stephano wa *TLP* alipata kura 647. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo haya waliokuwa wagombee uongozi kutoka CCM walipeleka malalamiko yao kwa msimamizi wa uchaguzi wa Wilaya kutokana na kutoridhika kwao na mwenendo wa shughuli za uchaguzi.

Baadhi ya malalamiko waliyoyapeleka huko ni kwamba orodha ya Wapigakura haikuwa imetayarishwa kama inavyoelkezwa na Kanuni ya 6(1) mpaka (3) ya taratibu za Uchaguzi ya Mwaka 1999. Kwa maana hiyo kuna wananchi walionyimwa haki yao ya kupiga kura kwa kuwa majina yao hayakuwekwa kwenye orodha. Pia baadhi ya majina hayakuwa yamethibitishwa kama ni ya wakazi wa Kijiji cha Katesh. (*Makofî*)

Mwenyekiti wa muda wa kuongoza uchaguzi alishindwa kumudu shughuli za uchaguzi hasa wakati wa kutekeleza majukumu ya Kanuni ya 16(d) inayomtaka kuwapatia wagombea nafasi sawa ya kujieleza mbele ya wapiga kura katika siku ya uchaguzi.

Kwamba utaratibu au mtindo uliotumika katika kufanya uchaguzi haukufuata maelekezo ya kanuni ya 16 na 17 ambazo zinahitaji kupiga kura kwa kuanza na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, kisha

wajumbe Wanawake na hatimaye Mwenyekiti. Vile vile kuwa karatasi za kupigia kura zinatolewa pale kundi fulani linapokuwa linapigiwa kura.

Katika uchaguzi wa Katesh, wapiga kura walipewa karatasi zote tatu kwa mara moja na kutakiwa kupiga kura zote tatu kwa mkuupuo mmoja. Kwa maana hiyo uhesabuji wa kura ulifanyika kwa njia ya mchanganyiko kutokana na kwamba wapiga kura walipewa karatasi tatu na wakawapigia wagombea wa makundi yote matatu kwa wakati mmoja na kwa kutumia kifaa kimoja cha kuwekea kura. Kwamba upigaji kura uliendelea mpaka saa 2.00 usiku badala ya kwisha saa kumi jioni kama ilivyoelekezwa na kanuni ya 16 ya uchaguzi wa Halmashauri ya Kijiji ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, baada ya malalamiko hayo kupokelewa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Wilaya tarehe 18 Machi, 2003, Msimamizi huyu ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya alizielekeza pingamizi hizo kwenye Kamati ya Malalamiko kwa mujibu wa Kanuni ya 11 na 19. Kamati ya Malalamiko ilijadili malalamiko hayo na mengine ambayo hayakutajwa hapa na kisha ikabaini kuwa kulikuwa na ukiukaji wa kanuni ya 6(1) mpaka (3) na 17(1) mpaka (3) ya kanuni za uchaguzi. Kwa matokeo hayo ikaagiza uchaguzi huo urudiwe. Chama cha *TLP* badala ya kutumia haki yake ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa kama inavyoelekezwa na vifungu vya 12 na 19 vya taratibu za uchaguzi kiliamua kumpelekea malalamiko yake Katibu Mkuu wao na hivyo kujipotezea haki yao ya kusikilizwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kwamba si kweli kuwa ni maafisa wale wale waliohusika katika kuendesha uchaguzi ndiyo hawa hawa ambao pia waliunda Kamati ya Malalamiko. Kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi Afisa Mtendaji wa Kata kamwe siye msimamizi wa uchaguzi wa ngazi yoyote kwenye Mamlaka ya Wilaya. Kwa maana hiyo siyo kweli kwamba alipotoa maamuzi kama mjumbe wa Kamati ya Malalamiko alikuwa amefuta matangazo yake mwenyewe bali alikuwa anafuta maamuzi ya afisa mwingine ambaye alionekana kutofuata taratibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ameelleza pia kuhusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mande Kata ya *Old Moshi Tela*, Wilaya ya Moshi Vijijini. Ameelleza pia kwamba mshindi katika uchaguzi wa Kijiji hiki alikuwa mgombea wa *TLP* lakini Kamati ya Malalamiko ilitengua matokeo ya uchaguzi na kuagiza urudiwe. Uchaguzi uliporudiwa mgombea wa *TLP* alishinda tena lakini Kamati ya Malalamiko ilitengua matokeo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wagombea walioshindwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimekwishaeleza taratibu zilivyo kwamba Kamati ya Malalamiko haina mamlaka ya mwisho kuhusu malalamiko yanayowasilishwa kwake. Mgombea wa *TLP* badala ya kupeleka malalamiko yake kwa Kamati ya Rufaa aliridhika na maamuzi ya Kamati ya Malalamiko na hivyo kuhalalisha matokeo ya maamuzi ya Kamati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, amedai pia katika maelezo yake kwamba kubatilishwa kwa uchaguzi katika Kijiji cha Katesh ambacho kimo katika Jimbo la Uchaguzi la Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuonyeshi utawala bora na wala siyo mfano wa kuigwa. Aidha, amedai kwamba Waziri Mkuu alipaswa aingilie kati suala hili kwa kukemea kitendo cha kutengua matokeo ya uchaguzi katika Kijiji cha Katesh.

Nimeshangazwa na kushtushwa sana na maelezo haya ya Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Taifa hili limeazimia kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu na masuala ya uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na taratibu tulizojiweke. Hivi Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anaposema Waziri angepaswa kuingilia kati na kukemea uzingatiaji wa sheria na taratibu ndiyo kuheshimu utawala wa sheria? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kunyamaza wakati wote jambo hili lilipokuwa linaendelea licha ya kwamba tukio hili limetokea katika Jimbo lake la Uchaguzi. Kwa kufanya hivyo amesaidia sana kuimarisha utawala bora kuliko kama angefanya kama Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anavyoshauri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu maamuzi ya Mahakama Kuu katika kesi ya *Miscellaneous Civil Case No. 27* ya mwaka 2000. Nimeeleza katika Ibara ya 3(a) ya maelezo yangu kwamba Waziri mwenye dhamana ya Serikali ya Mitaa amepewa madaraka ya kutengeneza taratibu zinazohusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa chini ya vifungu 14(4) na 70(c) vya sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka ya Miji Na. 8 ya Mwaka 1982. Taratibu hizo zimo katika tangazo la Serikali Na. 255 la tarehe 20 Agosti, 1999.

Mheshimiwa Spika, chini ya vifungu Na. 10 na 18 vya taratibu hizo za uchaguzi Kamati ya Malalamiko imepewa jukumu la kusikiliza na kutoa uamuvi kuhusu malalamiko dhidi ya uteuzi na pia kuhusu malalamiko dhidi ya uendeshaji wa uchaguzi. Aidha, chini ya vifungu hivyo Kamati ya Rufaa ndiyo imepewa madaraka ya kusikiliza na kutoa maamuzi dhidi ya mashauri ya rufaa yanayotoka katika Kamati ya Malalamiko kuhusu uteuzi na uendeshaji wa uchaguzi. Kwa mujibu wa taratibu hizo maamuzi ya Kamati ya Rufaa ndiyo ya mwisho. Pia nimeeleza katika Ibara ya pili ya maelezo yangu kwamba Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya Mwaka 1979 inahusu uchaguzi wa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, taratibu zote za uchaguzi katika uchaguzi wa Mtaa wa Rangi Tatu zilizingatiwa. Hata hivyo mgombea kutoka Chama cha *CUF* aliamua kukata rufaa katika Mahakama Kuu dhidi ya Kamati ya Rufaa na msimamizi wa uchaguzi pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya Kamati ya Rufaa kuamua kuwa malalamiko ya *CUF* hayakuwa ya msingi.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba Mahakama hiyo iliamua kwamba Kamati hiyo haina madaraka yoyote ya kushughulikia malalamiko kama ilivyoainishwa katika taratibu za uchaguzi na kwamba malalamiko yote yanapaswa kusikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi kama ilivyo kwa malalamiko yanayotokana na malalamiko ya uchaguzi wa Madiwani. Ni kweli pia kwamba maamuzi hayo hayakukatiwa rufaa yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na taratibu zetu za nchi zilivyo hivi sasa maamuzi haya hayastahili kujadiliwa nje ya taratibu za Kimahakama hivyo sitawenza kuyatolea maelezo au maoni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na umuhimu wa uamuvi huu katika uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa nimekwishawasilisha suala hili kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata mwongozo wake na mara tutakapoupatu tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumalizia maelezo yangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini kwa kuwasilisha hoja yake ambayo imeniwezesha kutoa ufanuzi ambaa naamini utatusaidia sisi sote.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba madaraka aliypewa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuhusu kutengeneza taratibu za uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa yametolewa kwa nia nzuri na taratibu hizo zimetengenezwa kwa uangalifu mkubwa chini ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Lengo la taratibu hizo ni kutenda haki kwa wahusika wote katika muda mfupi kadri inavyowezekana. Lakini kama nilivyosema baada ya kupata maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu suala hili tutayatekeleza bila kusita na mara moja kwa kuheshimu na kuzingatia msingi wa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Samahani Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya nyongeza ni kwamba kesho hatutakuwa na semina kwa sababu semina iliyopangwa, mwenye dhamana hiyo ameiahirisha kwa hiyo siku ya kesho ipo wazi. Lakini nimeombwa na Mheshimiwa Joel Bendera, nikumbushe kwamba kesho ni siku ya michezo ya Wabunge ile inayoitwa *VIP Race*, itafanyika kesho asubuhi.

Vile vile nimeombwa na Mheshimiwa Anne Makinda, nikumbushe kwamba kesho jioni ndiyo siku ya maonyesho ya Wabunge akinamama yatakayofanyika katika viwanja vyetu kuanzia saa moja usiku. Sasa tuendelee na *Order Paper*, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 Wizara ya Viwanda na Biashara

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara kwa kipindi cha 2002/2003 kwa kiasi kikubwa yametokana na hali ya amani na utulivu ambayo imeendelea kuwa jadi ya nchi yetu. Ningependa kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuendeleza jadi hii na kwa uongozi wake thabitil uliojikita katika kulinda amani na utulivu jambo ambalo ni la msingi katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhud zake za kuratibu programu za Kitaifa za kulinda mazingira na kuondoa umaskini.

Aidha, napenda nimshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, kwa hotuba yake ambayo inajumuisha maelezo fasaha ya utekelezaji wa malengo ya Serikali na ufanuzi wa kina wa mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya viwanda na biashara katika kipindi kijacho.

Aidha, namshukuru pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, ambao hotuba zao zimefafanua mwelekeo wa uchumi wetu na malengo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004. Vile vile nawashukuru Mawaziri wenzangu wote walionitangulia katika kuwasilisha bajeti za Wizara zao, ambao zinatupa taswira ya ushirikishwaji wa utendaji, kila sekta kwa nafasi yake, kwa lengo la kuinua uchumi wa Taifa letu na kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru wote ambao michango yao imesaidia sana katika kuandaa Bajeti ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu. Kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, chini ya uongozi wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli kwa michango yao mizuri wakati wa kujadili Makadirio ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Bajeti la mwaka jana, kumekuwepo na matukio kadhaa yanayoigusa jamii kwa ujumla. Kwanza ni warsha ya Kitaifa kuhusu utandawazi iliyofanyika Dar es Salaam mwezi Agosti, 2002 ambapo Watanzania walipata fursa ya kuelewa na kuchangia maoni yao kuhusu faida na athari za utandawazi. Warsha hii ilifuatiwa pia na warsha ya kikanda iliyohusisha nchi kadhaa za Afrika iliyofanyika Mjini Arusha Mwezi Februari 2003. Warsha hizi zimetupa fundisho moja muhimu kwamba utandawazi sasa ni ukweli usopingika na maamuzi tunayopaswa kufanya sio kama tuijusishe na utandawazi au la, bali ni jinsi gani Taifa linanufaika na utandawazi.

Aidha, Tanzania ni lazima kuhakikisha zinaweka mazingira bora ya kukuza biashara na je, ikiwa ni pamaja na kuweka mazingira bora ya kisera na kimfumo yanayovutia wawekezaji wa ndani na nje na yanayokidhi mahitaji ya uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, tukio muhimu la pili ni chaguzi ndogo za Wabunge na Wawakilishi zilizofanyika mwezi Mei, 2003 katika Majimbo 15 ya Zanzibar na Majimbo manne ya Tanzania Bara. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wale wote waliochaguliwa na kuwatakia kila la heri katika majukumu yao mapya ya uwakilishi wa wananchi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda ilikuwa na mafanikio ya kuridhisha katika kipindi cha mwaka 2002. Uzalishaji wa bidhaa uliendelea kuongezeka, jambo linalodhahirisha kuimarika kwa sekta ya viwanda. Sekta imekua kwa asilimia nane mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia tano mwaka 2001. Ongezeko la uzalishaji viwandani na ukuaji wa sekta kwa ujumla imefanya mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 8.3 mwaka 2001 na kufikia asilimia 8.4 mwaka 2002.

Kwa ujumla mafanikio ya ukuaji wa sekta ya viwanda yamechangiwa na ufanisi unaotokana na mpango wa kubinafsisha mashirika ya umma, uwekezaji katika viwanda vipyta na upatikanaji wa kuridhisha wa nyenzo muhimu kama vile maji na umeme, ikiwa ni pamoja na punguzo la gharama za umeme toka senti 13 hadi senti nane za dola ya Marekani. Matokeo ya mafanikio ya pamoja na ongezeko la ajira viwandani kutoka watu 163,168 mwaka 2001 hadi watu 180,023 mwaka 2002 ambalo ni ongezeko la asilimia 10.3.

Mheshimiwa Spika, viwanda vilivyofanya vizuri katika uzalishaji ni pamoja na viwanda vya madawa ya binadamu, sabuni, usagishaji wa nafaka, mafuta ya kupikia, saruji, ndondo, mabati, vinywaji baridi, bia, sigara, majani ya chai, vifungashio (Makasha na chupa, vifaa vya umeme, magodoro na kamba za katani). Ufanisi katika viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi uliendelea kuwa wa chini kutokana na mazingira yasiyoridhisha katika uwekezaji wa uzalishaji.

Kutokana na hali hii, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na wadau wengine imefanya uchambuzi wa kina wa sekta ya ngozi kuanzia ufugaji hadi uzalishaji wa bidhaa za ngozi. Kutokana na uchambuzi huu mkakati umeandalowiwa ambao tunatarajia utasaidia katika kurejesha uhai katika sekta hii muhimu. Uzalishaji katika sekta ya viwanda vya vyakula na vinywaji uliendelea kukidhi kwa kiasi kikubwa mahitaji ya wananchi ya bidhaa hizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2002, viwanda viliendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yaliyoathiri ushindani.

Matatizo makubwa ni pamoja na ushindani kutokana na bidhaa hafifu za nje, ukosefu wa mitaji ya kutosha ya kufanya kazi kutokana na riba kubwa za mabenki, mitambo mibovu kwa baadhi ya viwanda, teknolojia duni na iliyopitwa na wakati na miundombinu hafifu. Matatizo haya yamechangia kwa kiasi kikubwa gharama kubwa za uzalishaji na kushindwa kumudu ushindani dhidi ya bidhaa kutoka nje.

Serikali iliendelea kushirikiana na wadau kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya ili kuwezesha viwanda kuzalisha kwa ufanisi mkubwa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na uimarisaji wa miundombinu hasa barabara, urekebishaji wa mfumo wa kodi kupitia Kamati Maalum ya Kodi na ukaguzi wa ubora wa bidhaa unaofanywa na Shirika la Viwango Tanzania ili kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Aidha, mashauriano baina ya Serikali na wazalishaji yamekuwa yakifanyika kwa lengo la kubainisha matatizo ya msingi na kuafikiana kuhusu mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha mafaniko yaliyopatikana na kukabiliana na matatizo yaliyojitekeza, Wizara itaendelea kushirikiana na Jumuiya ya wenye viwanda na viwanda vyenyewe kwa karibu zaidi ili kubainisha matatizo ya sekta na kuyatafutia ufumbuzi.

Aidha, kwa kuelewa umuhimu wa sekta ya viwanda katika kukuza uchumi wa Taifa, Serikali itaendelea kubuni mikakati ya kuendeleza sekta hii ikiwa ni pamoja na kuzingatia programu ya utekelezaji wa Sera Endelevu ya Viwanda. Sekta za kipaumbele ambao ni pamoja na sekta ya nguo, usindikaji wa mazao ya kilimo na sekta ya ngozi zitatiliwa mkazo wa pekee ili kuimarisha mchango wa sekta hizi katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo iliendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza na kuboresha uchumi wa Taifa. Sekta hii ina nafasi kubwa ya kuchangia katika ajira na kuongeza mapato na hivyo kupunguza umaskini. Aidha, ni sekta muhimu katika kujenga uzoefu kwa wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo ambao watakuwa wafanyabiashara wa katika na wakubwa wa kesho.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuidhinisha Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (*Small and Medium Enterprises Development Policy*) zimekamilika na nafurahi kutamka kuwa sera hii itazinduliwa rasmi hivi karibuni. Sera hii inalenga katika kujenga mazingira bora ya kuwezesha sekta kukua na hivyo kujumuisha wananchi wengi zaidi katika shughuli za kiuchumi ili kuchangia katika kuondoa umaskini.

Kutokana na umuhimu wake kwa jamii yetu, sera hii itatafsiriwa katika Kiswahili ili kuwawezesha wadau wengi zaidi kuisoma, kuilewa na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Kwa mujibu wa sera hii, maeneo makuu matano yanatakiwa yafanyiwe kazi katika suala zima la ujenzi wa mazingira wezeshaji kama ifuatavyo:-

(a) Urekebishaji wa sheria na taratibu mbalimbali zinazokwamisha wawekezaji wadogo walioko katika sekta isiyo rasmi, ili waweze kukua na kuingia katika sekta rasmi ya viwanda vidogo na biashara ndogo.

(b) Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi zinazozingatia matumizi ya raslimali ya Taifa ikiwa ni pamoja na uteuzi na uendelezaji wa maeneo maalum, hususan mitaa ya viwanda kwa ajili ya shughuli za viwanda vidogo.

(c) Uimarishaji wa huduma za kuendeleza viwanda na biashara ndogo.

(d) Uboreshaji wa upatikanaji wa mitaji na huduma nyingine zikiwemo ushauri wa kitaalm na michanganuo ya miradi inayokopesheka na mabenki na taasisi nyingine za fedha kwa uwekezaji katika viwanda vidogo na biashara ndogo.

(e) Ujenzi wa mazingira wezeshaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo na biashara ndogo katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo yanategemea utekelezaji mzuri wa sera husika ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Kwa hali hii Wizara inawasiliana na kushirikiana na wafadhili mbalimbali, sekta binafsi na taasisi zisizo za Kiserikali kwa lengo la kutekelza kwa pamoja programu zitakazowezesha kuchangia katika ukuaji wa sekta ya viwanda vidogo na uchumi kwa ujumla. Aidha, utekelezaji wa sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo utakutanisha wadau wa sketa hii mara moja kila mwaka kwa lengo la kutafakari mwelekeo wa sekta na ufanisi wa programu za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na uendelzaji wa sekta ya viwanda na biashara ndogo. Wizara kwa kushirikiana na kituo cha Ujasirimali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inakusudia kuchapisha kijarida chenye maelezo ya taasisi za aina hii, ili kuwawezesha walengwa kuzifahamu na kuzitumia hivyo kunufaika na huduma zinazotolewa na taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera Endelevu ya Viwanda yenye upeo wa miaka 25 hadi mwaka 2020, ulihusu ukamilishaji wa awamu ya kwanza ya Mpango Maalum wa Kuendeleza Viwanda kwa lengo la kuviongezea uwezo wa ushindani katika zama hizi za uchumi wa soko na utandawazi. Matokeo ya utekelezaji huu yamekuwa kigezo cha kuandaa awamu ya pili ya mpango huu ambayo tayari maandalizi yake yamekamilika. Lengo la awamu hii ni kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya kilimo ikiwa ni njia mojawapo kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuongeza mapato ya wakulima.

Aidha, uwezo wa kusindika mazao ya kilimo siyo tu utaongeza thamani kwa mazao yetu ya kilimo bali pia utapunguza uharibifu wa mazao ya kilimo ambapo inakisiwa kuwa asilimia kati ya 30 na 40 ya mazao huharibika baada ya kuvunwa. Progamu pia inasisitiza uwiano wa maendeleo ya sekta ya viwanda na kilimo, sekta ya viwanda ikiwa kichocheo cha kusukuma maendeleo ya sekta ya kilimo kupitia mbinu na mikakati ya uzalishaji wa bidhaa zinazozingatia utashi wa soko.

Mheshimiwa Spika, Sera Endelevu ya Viwanda inahamasisha pia ushirikiano na nchi za Afrika katika maendeleo ya viwanda. Tanzania imekuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kuandaa mkutano wa Mawaziri wa Viwanda wa Kanda. Tanzania kwa kushirikiana na *UNIDO* iliandaa Mkutano wa Kanda ya Mashariki mwezi Oktoba 2002, Mjini Arusha. Mkutano huu ulijumuisha Mawaziri wa Viwanda kutoka nchi za Burundi, Kenya, Sudan, Rwanda, Tanzania na Uganda. Nigeria pia ilishiriki kama mtazamaji.

Mkutano ulilenga kuanzisha programu za pamoja za kukuza na kuendeleza uzalishaji viwandani hususan katika sekta za nguo, ngozi na usindikaji wa mazao ya kilimo. Mkutano ulijadili pia mbinu za kupunguza uharibifu wa mazao baada ya mavuno kupitia mkakati wa usindikaji wa mazao ya kilimo. Mkutano huo ulitoa mwelekeo wa pamoja kwa sekta ya umma na ya binafsi utakaowezesha kuimarisha uzalishaji viwandani na hivyo kuongeza thamani ya bidhaa na kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu maalum ya kuanzisha maeneo ya uzalishaji wa bidhaa za mauzo nje kama hatua ya utekelezaji wa Sera Endelevu ya Viwanda, umefikia hatua ya kuridhisha chini ya usimamizi wa Shirika la Taifa la Maendeleo. Wawekezaji kadhaa wamejitokeza katika ujenzi wa maeneo ya viwanda vya aina hii na utekelezaji unaendelea vizuri. Mnamo mwezi Mei, 2003 Mheshimiwa Rais alizindua kiwanda kipywa cha *NIDA Textile Mills Limited*, ambacho ni cha kwanza kinachozalisha bidhaa za kuuza nje chini ya utaratibu wa EPZ.

Aidha, eneo la EPZ la *Millennium Business Park Limited* lililoko Ubungo, Jijini Dar es Salaam ambalo litatumwiwa na wawekezaji mbalimbali watakozalisha bidhaa kwa ajili ya masoko ya nje linatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni. Ili manufaa ya EPZ yaenee sehemu mbalimbali za nchi yetu, *NDC* imebaini maeneo ya EPZ katika Mikoa ya mipakani ya Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Mtwara na Mbeya kwa ajili ya masoko ya nje na hasa ya nchi jirani. Wito wangu kwa uongozi wa Mikoa husika ni kwamba washirikiane kwa karibu na Wizara na NDC katika kuhamasisha wawekezaji katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa shughuli za EPZ.

Mheshimiwa Spika, sera ya kuendeleza viwanda nchini ilihu pia uendelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ukanda wa Mtwara chini ya uratibu wa NDC. Aidha, NDC ilihu pia uendelezaji wa sekta binafsi hususan katika kuunganisha wawekezaji nchini na vyombo mbalimbali vya fedha vya nje. Vile vile Kituo cha Uwekezaji Tanzania kiliendelea kupokea na kudhinisha miradi mbalimbali ya viwanda. Miradi 103 ya viwanda yenye thamani ya shilingi 195 bilioni ilidhinishwa mwaka 2002 ikilinganishwa na miradi ya viwanda 82 yenye thamani ya shilingi 125 bilioni iliyoidhinishwa mwaka 2001. Miradi hii ni sehemu muhimu ya kutuwezesha kufikia malengo yetu ya Sera Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, azma ya kuendeleza sekta ya viwanda itazaa matunda yaliyokusudiwa iwapo wananchi watahamasika kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini. Uhamasishaji wa wananchi kununua bidhaa za Tanzania ili kuimarisha viwanda vyetu itabidi kuwekewa mkazo wa pekee kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wazalishaji kutangaza bidhaa zinazozalishwa hapa nchii ili wananchi wazijue.

Kama sehemu ya azma ya kutangaza bidhaa zetu, *SIDO* imekwishafanya maonyeshao ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na viwanda vidogo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mtwara na Mbeya. Msemo wa zamani kuwa kizuri chajiuza si sahihi tena. Lazima tubadili dhana ya chema chajiuza na kibaya chajitembeza. Katika uchumi wa kisasa wa soko na utandawazi lazima chema kijitembeza kwa bidii na nguvu kubwa.

Katika hotuba yangu hapa Bungeni mwaka jana nilitoa changamoto kwa Watanzania kushabikia kwa nguvu msemo wa nunua bidhaa za Tanzania tuijenge Tanzania. Napenda nirejee tena changamoto hii kwa sababu uimara wa uchumi wetu utategemea sana uimarishaji wa sekta za uzalishaji mali hapa nchini.

Ujenzi wa uchumi wa kisasa unaoijitegemea utakuwa mgumu sana kama Watanzania wataendelea kushabikia bidhaa za nchi nyingine hata zikiuzwa kwa bei nafuu. Wahenga wanafundisha mwanzo ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara imekua kwa asilimia saba mwaka 2002 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2001. Ukuaji huu umetokana na kuimariika kwa uzalishaji viwandani na mwamko kwa wananchi wengi wa kuendesha shughuli za biashara kama fursa ya ajira ya kujitegemea. Kuimariika kwa miundombinu kama barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na mawasiliano ya simu vimechangia pia katika kurahisisha na kukuza shughuli za biashara nchini mwetu. Hii imehamasisha uanzishaji wa biashara mpya na uendelezaji wa biashara zilizokuwepo. Katika hali hii, sekta ilichangia asilimia 16.6 katika pato la Taifa mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia 16.5 mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa biashara katika soko la ndani unaridhisha, hasa kutokana na hali nzuri ya hewa mwaka 2002 ambapo mavuno ya mazao ya kilimo yalikuwa mazuri. Aidha, ongezeko la uzalishaji viwandani lilichangia pia katika ufanisi huu. Pamoja na mafanikio haya bado kuna ushindani usio wa haki kutoka kwa bidhaa zinatoka nje dhidi ya zile zinazozalishwa nchini. Serikali imeendelea kudhibiti uingizaji nchini wa bidhaa za ubora haffifu ili kuleta ushindani wa haki na kulinda afya za wananchi pamoja na mazingira.

Pamoja na kuitisha Bungeni sheria ya ushindani ya mwaka 2003, Wizara inakamilisha rasimu ya Muswada wa Sheria ya Kuzuia Uingizaji Holela wa Bidhaa (*Anti-Dumping Bill*) ili kuzuia Taifa letu kugeuzwa kuwa soko la bidhaa duni na zenye bei chini ya gharama ya uzalishaji huko zinakotoka. Kwa lengo la kuua viwanda vyetu. Tukiacha hali hii iendelea tutakuwa Taifa la biashara tu badala ya kuwa Taifa lenye ulinganifu sahihi wa uzalishaji na biashara. Taifa lolote lile haliwezi kuwa imara kiuchumi kwa kufanya biashara bila wakati huo huo kuwa mahiri katika uzalishaji mali. Tuwe mahiri kwa kufanya biashara ya bidhaa tunazozalisha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 mwelekeo wa biashara ya nje ulionyesha mafanikio ya kuridhisha ambapo mauzo ya bidhaa yaliongezeku kutoka dola za Marekani 776.4 milioni mwaka 2001 hadi dola za Marekani 902.5 milioni mwaka 2002, sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Ongezeko hili limesaidia kupunguza nakisi ya biashara. Ongezeko la mauzo ya bidhaa nje ya nchi limetokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa za viwanda, bidhaa zisizo za asili na bidhaa za madini.

Kwa mfano, mauzo ya bidhaa za viwanda nchi za nje yaliingizia Taifa kiasi cha dola za Marekani 65.9 milioni mwaka 2002 ikilinganishwa na dola za Marekani 56.2 milioni mwaka 2001 sawa na ongezeko la asilimia 17.3. Kwa upande wa huduma, limekuwapo pia ongezeko la mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Marekani 725 milioni mwaka 2001 hadi dola za Marekani 730 milioni mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu hapa Bungeni mwaka jana nilisema kuwa rasimu ya Sera ya biashara ilikuwa imekamilika tayari kwa kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi.

Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa taratibu hizi sasa zimekamilishwa na vitabu vya Sera hii vimechapishwa tayari kwa uzinduzi rasmi mahsusuna otarajiwa kufanya hivi karibuni. Lengo mahsusuna la Sera ya Biashara ni kujenga uwezo wa asasi za umma na za sekta binafsi katika kujenga uwezo wa ushindani katika biashara.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Biashara inabainisha pia nyenzo zinazohitajika kupanua na kukuza biashara kwa kuzingatia misingi ya kuongeza tija na ushimdani katika sekta za uzalishaji mali na utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi nyenzo kuu za kuendeleza biashara zilizoainishwa ndani ya sera ni pamoja na mfumo wa kodi unaohamasisha biashara, taratibu za kuondoa vikwazo visivyo vya kikodi vinavyoathiri biashara, ujenzi wa mila na desturi ya kuthamini viwango vya ubora katika mfumo wa uzalishaji, uandaaji wa mipango maalum ya kuendeleza biashara na mfumo wa vivutio maalum katika uendelezaji wa biashara ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuunganisha wawekezaji wadogo na masoko.

Mhehsimiwa Spika, nyenzo nyingine muhimu ni uwekaji wa taratibu muafaka za kulinda viwanda ambazo hazipingani na matakwa ya *WTO*. Ili sera hii ifanikiwe hapana budi kuhamasisha mabadiliko ya mfumo wa uzalishaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuinua na kuboresha viwango vya bidhaa za Tanzania ziwe za kilimo, viwanda, maliasili, madini na nyingine.

Mheshimiwa Spika, mchango wa nchi changa katika biashara ya ulimwengu, hususan zile za Afrika Kusini mwa janga la Sahara, uliendelea kuonyesha mwelekeo wa kushuka kutoka asilimia tano miaka ya 70 hadi asilimia mbili mwaka 2000. Mfumo mpya wa biashara huru duniani chini ya *WTO*, wenye mwelekeo wa kukuza na kudumisha utandawazi, umetoa changamoto ya kujenga upya ushirikiano baina ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea. Matumaini yetu ni kuwa misingi ya ushirikiano itakayofikiwa itaziwezesha nchi changa kufaidika na ongezeko la biashara ya Kimataifa.

Kwa mantiki hii nchi zilizoendelea hazina budi kuondoa vikwanzo vya kibiashara na kuweka taratibu wezeshaji ili nchi changa ziweze kunufaika na biashara ya Kimataifa. Wengi katika nchi zinazoendelea tunaamini kwamba mfumo huu wa utandawazi hauwezi kudumu bila kungwa mkono na nchi zinazoendelea na nchi hizi zitaunga mkono mfumo huu pale itakapodhihirika kwamba zinanufaika pia.

Kwa kuwa sasa siyo kukubali au kukataa kuwa sehemu ya utandawazi, changamoto iliyopo kwa Tanzania ni kujenga uwezo wa ushindani wa kibiashara ndani ya mufmo huu wa utandawazi. Ili Tanzania iweze kufaidika na mfumo huu inabidi ijenge uwezo wa kuzalisha na kuuza bidhaa zenyenye ubora wa viwango vya Kimataifa kwa kutumia teknolojia ya kisasa na uongozi wa sekta binafsi wenye uelewa mpiana wa matakwa ya soko.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya mfumo wa biashara ya Kimataifa yanaendelea chini ya *WTO*. Majadiliano haya kwa sasa yanazingatia maamuzi ya Mkutano wa Mawaziri wa Biashara uliofanyika Doha, Qatar, mwezi Novemba, 2001. Kwa upande wa Nchi zenyenye Maendeleo Madogo (*Least Developed Countries - LDCs*) maeneo yenye umuhimu wa pekee ni pamoja na marekebisho ya Mkataba wa Kilimo kwa lengo la kupunguza na hatimaye kuondoa ruzuku kwa sekta ya kilimo katika nchi zilizoendelea kwa lengo la kufungua masoko yao kwa bidhaa za kilimo, hususan zile za nchi zinazoendelea, mabadiliko katika Mkataba wa Biashara zinazohusiana na uvumbuzi (*Trade – Related Intellectual Property Rights - TRIPS*) ili kutoa mwanya kwa upatikanaji wa madawa kwa urahisi na kwa gharama nafuu hasa kwa madawa ya magonjwa hatari kama Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria na hivyo kudhibiti milipuko ya magonjwa yanayochangia upotevu wa maisha na nguvukazi hasa kwa nchi maskini.

Pia uimarishaji wa vipengele mahsusini katika Mikataba ya *WTO* vinavyokusudiwa kuleta unafuu kwa nchi changa zinazoendelea na kuhakikisha kuwa Mikataba ya *WTO* inazingatia mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na kuepuka mambo mapya katika kulenda ya majadiliano wakati ambapo makubaliano ya awali na hasa yale yenye manufaa kwa nchi zinazoendelea hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kushirikiana na makundi mbalimbali ya nchi zinazoendelea ili kuweka msimamo wa pamoja katika kuhakikisha kuwa matokeo ya majadiliano ndani ya *WTO* yanakidhi mahitaji maalum ya nchi hizi. Mnamo mwezi Juni, 2003, nchi za *LDCs* zilikuwa na mkutano wa mashauriano wa Mawaziri wa Biashara uliofanyika Dhaka nchini Bangladesh.

Mkutano wa kwanza kama huu ulifanyika Zanzibar mwezi Julai, 2001 kabla ya Mkutano wa Mawazi wa Biashara wa Doha, Qatar. Kama ilivyokuwa katika Mkutano wa Zanzibar, Mkutano wa Dhaka ulitoa tamko rasmi la msimamo wa pamoja. kwa upande wa Kanda ya Afrika Tanzania imeshiriki katika kuweka msimamo wa pamoja katika kikao cha Mawaziri wa Biashara wa *SADC* kilichofanyika Lusaka, Zambia, mwezi Mei, 2003 na katika mkutano wa Mawaziri wa Biashara wa Afrika uliofanyika Grande Baie, Mauritius mwezi Juni, 2003. Misimamo hii itaziwezesha nchi hizi kuwa na sauti moja katika mazungumzo yatakayofanyika katika Mkutano wa Mawaziri wa nchi wanachama wa *WTO* utakaofanyika katika Mji wa Cancun, Mexico, mwezi Septemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi zinazoendelea zinayo nafasi ya kipekee ya kufaidika na programu za masoko nafuu kama *African Growth and Opportunity Act (AGOA)* ya Marekani, *Everything*

*But Arms* ya Umoja wa Nchi za Ulaya na *Programme for Building African Capacity in Trade (PACT)* ya Canada na mipango ya nchi nyingine kama vile Japan, Australia na Ufaransa ambazo ziko mbioni kukamilisha programu za aina hii.

Mheshimiwa Spika, programu hizi zina lengo la kuzipunguzia au kuziondolea ushuru wa forodha kwa bidhaa kadhaa kutoka nchi maskini, pamoja na kuondo vikwazo vya idadi (*tariff free na quote free*). Zipo fursa pia za misaada ya kiufundi na kitaalamu katika maeneo ya kuendeleza biashara, ikijumuisha pia misaada ya kuimarisha mifumo ya uzalishaji. Chini ya kuimarisha mifumo ya uzalishaji.

Chini ya mipango inayotoa fursa za upendeleo katika masoko ya nchi zilizoendelea, Tanzania imeanza kunufaika ambapo mwaka 2002 jumla ya bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani 22 milioni zenye thamani ya dola za Marekani 22 milioni ziliuzwa Marekani ikilinganishwa na dola za Marekani 21.54 milioni mwaka 2001.

Kwa upande wa mpango wa *AGOA*, mwaka 2002 bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani 540 ziliuzwa ikilinganishwa na dola za Marekani 16,000 mwaka 2001. Bado hiki ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na fursa tulizonazo. Wizara inaratibu kwa karibu mpango wa *AGOA* ili kuhakikisha Taifa linanufaika na mpango huu.

Katika azma hii Wizara imeunda Kamati ya kuratibu utekelezaji wa mipango mbalimbali ya fursa za masoko nafuu ambap wadu mbalimbali wamejumuishwa katika Kamati hii. Kutohana na uzito wa masuala haya ya fursa za masoko, Kamati hii inaongozwa na Waziri wa Viwanda na Biashara mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika nyanja ya ushirikiano wa kikanda, tuliendelea na majadiliano ya kuunda rasmi umoja wa Forodha (*Customs Union*) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*). Maandalizi ya msingi ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Nchi za *EAC*, yanaendelea vizuri. Karibu masuala yote ya msingi yameafikiwa na nchi Wanachama wa *EAC*. Mwelekeo uliopo unadhihirisha kufikia muafaka katika kipindi kifupi kijacho. Rasimu ya Mkataba wa itifaki itakayokuwa msingi wa majadilioano kuhusu mfumo wa Umoja wa Forodha imekwishaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kuridhia Mkataba wa Biashara wa Jumuiya ya *SADC*, suala lililofuata ni kuandaa taratibu za kisheria kuhusu masuala ya Forodha na viwango vya ushuru ili kuwezesha utekelezaji wake. Azimio la kuridhia mkataba huo lilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2002, na kuanza kutumika rasmi kama sheria mwezi Juni, 2002. Tangu wakati huo, Tanzania inayo haki ya kushiriki katika biashara ya masharti nafuu katika soko la *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na Itifaki ya Biashara, uanzishwaji wa eneo la biashara huru katika nchi za *SADC* umejumuisha ulegezaji wa masharti ya biashara kwa kuondosha au kupunguza vikwazo vyote kwa biashara ikiwa ni pamoja na Ushuru wa Forodha na vikwazo visivyo vya kiushuru. Aidha, Itifaki inaelekeza nchi Wanachama wa Jumuiya ya *SADC* kufanya majadiliano yenyе lengo la kulegea masharti ya biashara na huduma katika Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kazi hii imeanza na inahusisha majadiliano katika sekta za Huduma zilizopewa kipaumbele ambazo ni ujenzi, fedha, nishati, uchukuzi, na mawasiliano. Wizara itahusisha kikamilifu Wizara nyingine na wadau wote wa Sekta zinazohusika katika majadiliano kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililosughulikiwa katika kipindi cha 2002/2003 ni kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Viwanda katika nchi za *SADC*. Lengo kuu la mikakati ya kuendeleza viwanda katika Jumuiya ni kuifanya *SADC* iwe eneo la viwanda. Lengo hii linatarajiwa kufikiwa kwa kutekeleza programu mbalimbali za kuendeleza viwanda vidogo, viwango na ubora wa bidhaa, teknolojia ya kisasa, uiimarishaji wa sekta binafsi, mafunzo ya ujasirimali na uwekezaji katika sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, inategemewa kuwa programu hizi zikitekelezwa, Jumuiya itaweza kupunguza ama kuzuia kwa kiwango kikubwa, madhara ya kutokuwa na uwiano wa uwekezaji katika sekta ya

viwanda baina ya nchi wanachama. Makubaliano ya awali ya kuendeleza huduma za Viwango na Ubora wa Bidhaa yamekwishafikiwa. Lengo la juhudhi hizi ni kukuza ufanisi, kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa za viwanda na kukuza biashara mionganii mwa nchi wanachama wa *SADC*, na baina yao na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Agosti, 2001, *SADC* ilifanya mabadiliko makubwa katika muundo wake. Badala ya nchi wanachama kuratibu sekta mbalibmali ambapo kila nchi ilikuwa inaratibu maendeleo ya sekta fulani kwa niaba ya wanachama wote, sasa shughuli hizo zinafanywa na Sekretarieti ya Makao Makuu ya *SADC* iliyoko Gaborone, Botswana. Katika misingi hii Tanzania haina tena jukumu la kuratibu sekta ya Viwanda na Biashara kama ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) na nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (*ACP*) zimo katika kukamilisha maandalizi ya kuanza majadiliano mwezi Septemba, 2003 yenye lengo la kuanzisha utaratibu mpya wa ushirikiano wa kiuchumi (*Economic Partnership Agreement – EPA*) ambaao utakuwa badala ya mpango tuliozoea wa Lome. Tofauti kati ya Mkataba wa Lome na Mkataba wa Cotonou ni kwamba chini ya Mkataba wa Cotonou ni nchi za *ACP* nazo pia zitatakiwa kutoa upendeleo kwa bidhaa toka nchi za *EU* ili mradi Mkataba haukiuki misingi ya biashara chini ya taratibu za *WTO*. Hata hivyo Mkataba wa Cotonou unatambua udhaifu wa kiuchumi wa nchi za *ACP* na kwa hiyo nchi za *EU* zitatakiwa kusaidia kujenga uwezo wa nchi za *ACP* ili ziweze kukuza biashara na nchi za *EU*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa zoezi la kubinafsisha mashirika ya umma chini ya Sekta ya Viwanda na Biashara, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, ulihusisha Mashirika sita. Mashirika matatu yalikabidhiwa ama *PSRC* au *LART* kwa wawekezaji. Mashirika hayo ni kiwanda cha Kuzalisha Madawa kwa ajili ya Wadudu Waharibifu wa Mimea (*Pesticide Manufacturers Ltd*) cha Moshi, kiwanda cha Magari ya *Landrover (LRT Motors)* cha Dar es Salaam na Kiwanda cha Nguo cha *MUTEX* cha Musoma. Taratibu za kukabidhi kiwanda cha kutengeneza matrekti cha *TRAMA* zinakamilishwa na *PSRC*.

Aidha, taratibu za kubinafsisha kiwanda cha Nguo cha *Polytex*, Morogoro ziko katika hatua ya Makubaliano ya Awali, wakati kiwanda cha Nguo cha Tabora (*Tabotex*) kimepelekwa *LART* kufilisiwa kutokana na mademi makubwa. Katika kipindi hiki, mali za Kampuni ya Magari ya (*Tanzania Motor Services - TMSC*) ziliendelea kuuzwa kwa utaratibu wa *PSRC*. Taratibu za kumtafuta mwekezaji katika kiwanda cha Karatasi, Mgololo (*Southern Paper Mill Ltd. – SPM*) zinaendelezwa kwa bidii ingawa kazi hii imechukua muda mrefu bila mafanikio. Kwa sasa kuna dalili njema ya kumpata mwekezaji mahiri.

Mheshimiwa Spika, malengo ya ubinafsishaji na urekebishi ya mashirika ya umma ni kufufu uchumi na kuwashirikisha wananchi katika zoezi hili kila inapowezekana. Katika misingi hii Serikali imewashirikisha wananchi katika kumiliki hisa ndani ya mashirika ya umma kwa kuendelea kushikilia baadhi ya hisa katika mashirika yanayobinafsishwa ili baadaye hisa hizo ziuzwe kwa wananchi wa Tanzania. Kutokana na sera hii, Watanzania wamepata fursa ya kumiliki sehemu ya hisa kupitia soko la Hisa la Dar es Salaam katika kampuni nne za sekta ya viwanda na biashara, ambazo zimebinafsishwa na zinaendeshwa kwa faida na kulipia gawio kila mwaka. Kampuni hizi ni Kiwanda cha Sigara, Kampuni ya Bia na Kiwanda cha Saruji cha Tanga. Kampuni nyingine ni Kiwanda cha Gesi cha *TOL Tanzania Ltd.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishauza kwa wafanyakazi hisa zote katika kampuni tano, zilizo chini ya Sekta ya viwanda na biashara, kwa lengo la kutekeleza azma ya kushirikisha wananchi katika miliki ya baadhi ya viwanda na kampuni za kibiashara zinazobinafsishwa. Kampuni husika ni *Moshi Handa Tools*, Arusha, *Metal Industries*, kampuni ya bidhaa za sanaa (*HANDICO*), kiwanda cha uchapaji cha KIUTA na Shirika la Utafiti na Ushauri wa Viwanda la *TISCO*.

Mheshimiwa Spika, hatua za kukamilisha mikataba ya mauzo kwa kampuni zinazouzwa kwa wafanyakazi zinaendelea katika kampuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na *HOSCO*, *S&O*, *BCS*, *RTC* za Dar es Salaam, Arusha na Mwanza, Shirika la Vyuma la Taifa (*NSC*), *Express Tanzania Ltd* na *Tanzania Publishing House*.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuhitimisha shughuli za mashirika mama ambayo hayana majukumu tena kufuatia ubinafsishaji wa yaliyokuwa makampuni tanzu yake ziliendelea katika kipindi hiki. Hadi sasa shughuli za mashirika mama sita zimekwishahitimishwa. Mashirika haya ni Shirika la Viwanda vya Saruji, Shirika la Viwanda vya Kemia, Shirika la Viwanda vya Ngozi, Shirika la Viwanda vya Karatasi, Shirika la Magari na Halmashauri ya Biashara ya Ndani. Taratibu za kuhitimisha shughuli za Kampuni ya Wakala wa Meli (*NASACO*) na kampuni zake tanzu zinaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu mwaka 2002 nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya nia ya Wizara ya kufuatilia kwa karibu utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa ili kubainisha matatizo yake na kuyatafutia ufumbuzi.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa zoezi hili limefanyika na matokeo yanabainisha kuwa viwanda 24 vilivyobinafsishwa vinafanya kazi kwa ufanisi. Baadhi ya makampuni yenye ufanisi ni pamoja na *Carnaud Metal Box*, *Namera Group of Industries Ltd* iliyokuwa *Sunguratex*, *Daesung Tanzania Cables*, *Tanzania Pharmaceutical Industries* cha Arusha, *Keko Pharmaceutical Industries*, *HANDICO*, *KIUTA*, *Kiltex Arusha*, *Morogoro Canvas Mill*, *Blanket Manufacturers*, Kampuni ya Sigara, Kampuni ya Bia, Kiwanda cha Sabuni cha Tanga na Viwanda vya Saruji vya Dar es Salaam, Mbeya na Tanga.

Mheshimiwa Spika, licha ya matatizo yaliyojiteza kwa baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa, zoezi la kubinafsishaji limekuwa na mafanikio ya kuridhisha. Nitoe mifano michache. Kiwanda cha *Sunguratex* kilikuwa kimefungwa kwa miaka mingi kabla ya ubinafsishaji. Kiwanda sasa kimefuliwa na kimeajiri wafanyakazi 2,000. Ni muhimu pia kusema kwamba Kampuni ya *NAMERA* baada ya kununua *Sunguratex* mwaka 1998, imewekeza pia katika kiwanda kipywa cha Nguo cha *NIDA* kilichoko Tabata, Jijini Dar es Salaam ambacho tayari kimeajiri wafanyakazi 500 na uwekezaji utakapokamilika kitaajiri wafanyakazi 1,500. Kwa hiyo, ujenzi wa Kiwanda cha *NIDA* umetokana na ubinafsishaji wa kiwanda cha *Sunguratex*.

Aidha, ujenzi wa Kiwanda cha Bia cha Mwanza umetokana na ubinafsishaji wa Kampuni ya Bia Tanzania (*TBL*) yenye viwanda vya Bia Dar es Salaam na Arusha. *TBL* mwaka 2002 ilichangia katika mapato ya Serikali kiasi cha shilingi 43.5 bilioni. Kiasi hiki ni mara tatu ya mchango wa *TBL* kabla ya ubinafsishaji. *TBL* inaa jiri Watanznaia 1,600.

Kwa upande mwingine Kampuni ya Sigara imewekeza kiasi cha dola za Marekani milioni 26 baada ya kubinafsishwa na imechangia mapato ya Serikali ya shilingi 170 bilioni katika kipindi cha miaka mitano tangu kibinafsishwa. Kiwanda kinaajiri Watanzania 700. Kiwanda cha *NECO* kilikuwa katika hatua za kufungwa kilipobinafsishwa na sasa kimechangia mapato ya Serikali ya shilingi milioni 545.5 tangu kibinafsishwe na kimeajiri wafanyakazi 43. Kiwanda cha *Carnaud Metal Box* tangu kinabinafsishwe mwezi Oktoba, 1997 kimechangia mapato ya Serikali ya shilingi bilioni 3 na kimeajiri wafanyakazi 80 wakati kiwanda cha Saruji cha Wazo tangu kibinafsishwe miaka mitatu iliyopita kimewekeza dola za Marekani milioni 7.3 na kuchangia mapato ya Serikali ya shilingi bilioni 14.8. Kiwanda hiki sasa kinaajiri wafanyakazi 270.

Kiwanda cha Madawa ya Binadamu cha Arusha kilikuwa kimefungwa kwa miaka 3 kabla ya kubinafsishwa lakini sasa kimeajiri wafanyakazi 91 na kuwekeza jumla ya dola za Marekani milioni 3.5. Kabla ya ubinafsishaji Kiwanda cha Mablanketi cha Dar es Salaam kilikuwa katika hatua za kufungwa. Leo hii kiwanda kinaajiri Watanzania 80 na kimechangia mapato ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 4.7 katika kipindi cha miaka 5 baada ya ubinafsishaji. Iko mifano mingine ya namna hii. Ni matumaini yangu kuwa viwanda vilivyobinafsishwa na bado vinalegalega wawekezaji husika watachukua hatua madhubuti za kuvifufua ili navyo vichange katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la viwango Tanzania (*TBS*) liliendelea na majukumu ya uwekaji Viwango vya Ubora wa Bidhaa na usimamiji wa utekelezaji wa viwango. Katika kipindi cha 2002/2003, Shirika lilikamilisha kuweka viwango muhimu vya upimaji wa vijidudu katika vyakula ili kulinda afya za binadamu.

Aidha, katika kukuza na kuendeleza Sekta ya ujenzi, nishati na mawasiliano, Shirika limekamilisha kuweka viwango katika saruji, nguzo za umeme na simu. Hadi kufikia mwezi Juni, 2003, Shirika lilikuwa limetayarisha viwango vya Taifa 790 katika sekta mbalimbali na kutoa jumla ya vyeti 488 vya ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 348. Kutokana na mazingira ya soko huria na utandawazi, Shirika libibuni na kuanza kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2003, Shirika lilikuwa limetoa jumla ya vyeti 4,024 vya ubora wa bidhaa toka nje ya nchi na kukataa zaidi ya shehena 41 za bidhaa haffiu. Mkakati huo ulianzia bandari ya Dar es Salaam na baadaye kuhusisha vituo vya Tunduma, Namanga na Horohoro.

Aidha, utaratibu wa ukaguzi wa magari yaliyotumika yanayoagizwa kutoka nje ili kuhakikisha kuwa Tanzania haiwi dampo la kutumia magari mabovu, unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha sekta binafsi kukabiliana na ushindani wa soko huria na utandawazi, Shirika litaweka msisitizo katika kuandaa viwango vya bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya mauzo nje. Shirika lina mpango pia wa kuanzisha maeneo mpya ya ubora (*quality systems registration*) ili kwenda sambamba na matakwa ya biashara katika mfumo wa utandawazi. Mikakati ya utekelezaji ni pamoja na kuboresha maabara za *TBS* na nyingine zilizoko ili ziwe na hadhi ya kutambulika Kimataifa (*accredited laboratories*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mizani na Vipimo (*WMA*) ambayo ilianza rasmi mwaka 2002, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usahihi wa mizani na vipimo vya biashara kwa lengo la kulinda haki za wafanyabiashara na walaji. Katika misingi hii Wakala imeendelea kusimamia, kuimarisha na kurahisisha biashara kwa njia ya vipimo hapa nchini na baina ya Tanzania na nchi nyingine. Kutokana na ushirikiano mzuri iliyopata toka kwa Taasisi za Serikali na Sekta binafsi, Wakala wa Mizani na Vipimo iliweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Lengo ni kujenga uwezo wa Wakala kuwezesha ushindani wa sekta binafsi katika biashara ya Kimataifa kwa kuzingatia masharti ya viwango na vipimo. Wakala wa mizani na vipimo imeweka mkakati wa kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kupitia vyanzo vyake vyote vya mapato ili kujenga uwezo wa kujitegemea.

Katika kipindi cha mwaka 2001/2002 kiasi cha shilingi 461,165,000 kilikusanya ikilinganishwa na shilingi 472,255,400 zilizokusanya mwaka 2002/2003 sawa na ongezeko la asilimia 2.4. katika kipindi hiki Wakala wa Mizani na Vipimo pia itaongeza ushirikiano na Wakala wa nchi nyingine kupitia *EAC* na *SADC* ili kujihakikishia mahusiano endelevu ya kitaalamu. Jukumu hili litatekelezwa sambamba na kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi mazuri ya vipimo katika sehemu zao za biahsara pamoja na kuwahuishisha wadau wote katika mipango yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatoa kipaumbele katika utekelezaji wa Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 ili kudhibiti ushindani usio wa haki katika soko la ndani kwa kuzingatia umuhimu wa kumlinda mlaji, mzalishaji na mfanyabiashara. Jukumu hili linasimamiwa na Kamisheni ya Maadili ya Biashara. Sheria ya Maadili ya Biashara ya mwaka 1994 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2000, ilifutwa na Sheria mpya ya *Fair Competition Act*, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2003.

Sheria hii inaweka mazingira mazuri ya kusimamia na kuimarisha ushindani wa haki baina ya wafanyabiashara katika shughuli za kiuchumi na kumlinda mlaji dhidi ya udanganyifu unaoweza kufanya katika mazingira ya soko huria. Marekebisho haya yamelenga pia kuwanisha sheria hii na sheria shiriki zinazosimamia ushindani katika Sekta ya Usafiri wa Majini (*SUMATRA*) na Sekta ya Nishati na Maji (*EWURA*).

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya sasa, soko la ndani ni sehemu ya soko la dunia na taratibu na usimamizi wa biashara katika soko la ndani lazima zizingatie mfumo mzima wa soko la ndani. Kwa matanki hii, sheria mbalimbali zinazosimamia biashara zinahitaji kufanyiwa marekebisho kama sehemu ya mikakati ya kujenga mazingira ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mpango wa kurekebisha mfumo wa sasa wa leseni za biashara kwa kuzingatia mapendekezo ya wataalam. Katika misingi hii, Sheria ya Leseni za Biashara Na.

25 ya 1972 imeendelea kufanyiwa marekebisho ili kuondoa kasoro katika baadhi ya vipengele vya sheria hii ambavyo vimekuwa kero kwa wafanyabiashara. Wizara inaandaa mapendekezo yanayolenga kutoa ufumbuzi wa kudumu wa kero zinazowakabili wafanyabiashara kutokana na mfumo wa sasa wa leseni za biashara. Lengo ni kuanza utekelezaji wa mfumo mpya katika mwaka 2003/2004. Hii ni mojawapo ya majukumu yanayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa Sheria ya Leseni za Biashara, katika kipindi cha 2002/2003 Wizara ilitoa jumla ya leseni za biashara 3,888 na kukusanya jumla ya shilingi milioni 2 576 ambapo kiasi cha shilingi milioni 2,334 ilikuwa ada na shilingi milioni 241 ilikuwa adhabu kwa waliochelewa kukata leseni katika muda uliowekwa. Leseni zilizotolewa nchi nzima, ikijumuisha leseni zilizotolewa na Serikali za Mitaa, ni shilingi milioni 96,172 na kuingiza jumla ya shilingi milioni 8,127 kama ada pamoja na adhabu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara ya Leseni (*BRELA*) ina jukumu la kusimamia majina ya biashara, alama za biashara na huduma, hata za sheria ya leseni za viwanda. Kutokana na mazingira ya sasa ya biashara huria na mfumo wa utandawazi, usimamizi mzuri wa sheria ni sharti lazima katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Katika kutekeleza jukumu hili, *BRELA* imeendelea kujenga uwezo wa kutoa huduma zake kwa ufanisi, hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa huduma zake zinawaffikia wananchi walio wengi kwa urahisi zaidi. Katika kutekeleza azma hii, *BRELA* imeanzisha vipindi vya radio kupitia Redio Tanzania, Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa elimu kwa wadau.

Aidha, Wakala inayo Tovuti inayowawezesha wadau kupata taarifa muhimu na imechapisha vipeperushi na vitabu mbalimbali na kuvisambaza kwa wananchi. Hatua hizi zimesaidia kupatikana kwa taarifa haraka na kwa urahisi na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kero kwa wafanyabiashara. Katika kuhakikisha kuwa huduma zinafika karibu na wananchi, *BRELA* inaangalia uwezekano wa kutumia ofisi za Biashara za Mikoa ili kutoa huduma husika. Tathmini ya utekelezaji imeanza katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya 1999 iliunda Chama cha Hakimiliki Tanzania (*Copyright Society of Tanzania - COSOTA*) chenye jukumu la kulinda na kukuza haki za watanzi, wasanii wanamuziki na wachapishaji. *COSOTA* ilianza kazi mwezi Oktoba 2001 na sasa inao wanachama 402 ambao wamesajili kazi mbalimbali za sanaa 1,150. *COSOTA* ni mwanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wasanii (*International Confederation of Societies of Authors and Composers*) kuanzia mwezi Desemba, 2002.

Katika kujitangaza, *COSOTA* imeendesha semina katika Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa ushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Chama kinaelimisha watumiaji wakuu wa sanaa ya muziki, yaani vituo vya radio, na televisheni, mahoteli, maduka makubwa na wengineo kuhusu wajibu na haki zao chini ya sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki. Umuhimu wa kulinda na kukuza haki za wadau wa *COSOTA* unahitajika zaidi sasa kwani vipaji hivi vikitumika vizuri vitachangia kwa kiwango kikubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na utekelezaji wa majukumu ya kusimamia Sheria Na. 13 ya 2002 ya Uwakala wa Meli iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Wizara imeunda Kamati ya Uwakala wa Meli ambayo inasimamia Sekta ya Uwakala wa Meli, kulingana na sheria na kanuni zake, hadi Mamlaka ya *SUMATRA* itakapoanza kazi. Mpaka sasa Kamati imetoea leseni za Uwakala wa Meli kwa Makampuni 27 yaliyokidhi masharti yaliyowekwa na Sheria ya Uwakala wa Meli.

Mheshimiwa Spika, licha ya asasi zinazosimamia sheria, Wizara ina jukumu la kuratibu utendaji katika taasisi zinazotoa huduma mbalimbali zinazohusiana na teknolojia, utafiti, ushauri na elimu. Taasisi hizi ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Utafiti wa Viwanda (*TIRDO*), Kituo cha Kueneza Teknolojia Rahisi Vijijini (*CARMATEC*), Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*), Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*), Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*), Halmashauri ya Kuhudumia Viwanda Vidogo

(SIDO), Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET) na Kituo cha Biashara cha London (*Tanzania Trade Centre*).

Kutokana na umuhimu wa Taasisi hizi kwa uchumi hasa wakati huu wa mazingira ya soko huria na utandawazi, Serikali inabidi kuimarisha taasisi hizi ikiwa ni pamoja na kubadilisha mwelekeo wake wa utendaji na hivyo kubuni mbinu sahihi na muafaka kwa ajili ya kuiwezesha sekta binafsi kuzalisha bidhaa na kutoa huduma mbalimbali zitakazohimili ushindani wa soko la Kimataifa. Wizara inakusudia kuangalia upya mfumo wa asasi na taasisi hizi kwa maana ya kujenga uhusiano wa karibu mionganoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TIRDO* linahusika na maendeleo ya Utafiti wa Viwanda. Katika kipindi cha 2002/2003, Shirika liliendelea kufanya utafiti mbalimbali wa kutoa huduma katika maeneo yanayolenga kumkwamua mzalishaji kutokana na matatizo mbalimbali.

Katika kipindi hiki Shirika limekamilisha utafiti wa awali kuhusu kupunguza sumu ya *Ochratoxin A* kwenye mbegu za kahawa kwa lengo la kuzuia kahawa isiathirike, kuzalisha na kusambaza mbegu bora za uyoga na kutoa mafunzo kwa wakulima wa uyoga.

Aidha, Shirika limefanikiwa kufanya utafiti wa kutumia kemikali zinazopatikana nchini katika kuongeza ubora wa vifaa vya ujenzi. Vilevile Shirika limekamilisha utafiti na utengenezaji wa mashine za kukamua machungwa kwa kutumia vifaa vya hapa nchini. Mashine hizi zitatumwa na wanachama wa VIBINDO ambao *TIRDO* inaendelea kuwapa mafunzo ya usindikaji wa matunda.

Katika jitihada za kubuni teknolojia muafaka kwa ajili ya kuinua ubora wa tumbaku inayosindikwa na kupunguza adha kwa msindikaji, Shirika lilitafiti na kubuni tembe mbadala kwa ajili ya kusindika tumbaku. Shirika liliendelea pia na jitihada za kutafiti, kutathmini na kutoa ushauri wa matumizi bora ya nishati kwa watumiaji wakubwa kama vile viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *CARMARTEC*, katika kipindi cha 2002/2003, kiliendelea na jukumu la kubaini mahitaji ya zana rahisi za kilimo vijijini, kuunda zana husika, kuzisambaza na kutoa elimu kwa walengwa. Aidha, Shirika liliendelea na kubuni na kutengeneza teknolojia za nishati mbadala kama vile kuunda majiko na mitambo inayotumia nishati ya jua kuchemshia maji, utengenezaji wa majiko sanifu na kueneza matumizi ya *biogas* katika kuchangia juhudzi za Serikali za kulinda na kuhifadhi mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 *CARMARTEC* itaanza mpango wenye mwelekeo mpya ambao unalenga kubainisha teknolojia muafaka kwa wakulima zinazolenga katika kutatua matatizo ya uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *TEMDO* iliendelea na ubunifu wa mashine na mitambo kulingana na mahitaji ya wateja mbalimbali. Baadhi ya shughuli zilizotekeliza ni kubuni tanuru la kuunguzia taka (*incinerator*), kuboresha teknolojia ya kuchanganya dawa kwenye mbegu za nafaka na kubuni mashine za kukamulia mafuta kutokana na mbegu za alizeti. Katika kipindi cha 2003/2004, *TEMDO* itaongeza ushirikiano na taasisi nyingine ili kuhakikisha kuwa teknolojia zinazobuniwa zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Elimu cha Biashara (*CBE*) kina wajibu wa kuendeleza mitaala katika fani ya elimu ya biashara na ujasimali. Katika mwaka wa wasomo 2002/2003 Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya juu na ya katika fani ya elimu ya biashara, uhasibu, mizani na vipimo. Tanzania ni mojawapo ya nchi chache za Afrika ambazo zinatoa mafunzo ya elimu ya juu katika fani ya Mizani na Vipimo. Kwa maana hiyo Chuo kina uwezo wa kuwa Taasisi ya kuendesha mafunzo ya Mizani na vipimo kwa Jumuia ya Afrika Mashariki. Ingawa Chuo kinao wataalam wa kutosha, bado kina upungufu wa vifaa muhimu vya kufundishia.

Wizara inatambua mahitaji ya Chuo na jitihada zitaendelea kwa lengo la kukipatia Chuo vifaa mbalimbali ili kiweza kufikia hadhi ya kuwa Taasisi ya kufundisha fani ya Mizani na Vipimo kwa nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara kimeanzisha kitengo cha kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo (*The small Business Development Centre – SBDC*) ambacho kitasaidia utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo.

Aidha, kitengo hiki kitasaidia kuchangia uendelezaji wa Sekta binafsi kupitia elimu ya ujarisimali. Lengo ni kuimarishe *CBE* ili ikidhi mahitaji ya wafanyabiashara wadogo na vikundi vyta wanawake ili washiriki katika mfumo wa kisasa wa biashara. Chuo pia kimepitia upya mitaala ya kozi mbalimbali za Stashahada kwa lengo la kuziwianisha na mahitaji halisi ya wafanyabiashara katika mazingira ya ushindani wa soko na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa (*National Development Corporation – NDC*) ni chombo muhimu cha Serikali cha kuchochea, kuhamasisha na kuratibu shughuli za kiuchumi katika sekta ya viwanda vyta msingi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika mazingira ya uchumi wa kisasa, zipo sekta au shughuli za uchumi ambazo lazima ziongozwe na chombo cha umma kwanza ndipo wawekezaji binafsi wajitokeze. *NDC* ina nafasi muhimu ya kufanya hivyo. Hivyo *NDC* itaendelea kuimarishe katika muundo wa utendaji wake wa kazi katika kipindi hiki cha 2003/2004. Hii ni pamoja na kutunga sheria mpya itakayoipa *NDC* uhai na nguvu mpya ya utekelezaji wa majukumu yake mapya na yaliyopanuka likiwiemo lile la uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Aidha, *NDC* ni chombo muhimu kinachosimamia maendeleo ya Kanda (*Spatial Development Initiative - SDI*) ikiwemo Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (*Mtwara Development Corridor*) ambapo miradi yake ya msingi (*anchor projects*) ni ile ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na ya Chuma cha Liganga.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kuhudumia Viwanda vidogo (*SIDO*) lina umuhimu wa pekee katika kuimarishe na kuendeleza viwanda vidogo nchini. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, mafanikio ya *SIDO* yaliyumuisha utengenezaji na usambazaji wa mashine 170 za kubangua korosho katika maeneo yanayolima korosho. Shirika pia liliendesha mafunzo ya aina mbalimbali, ambapo jumla ya kozi 244 zilizoshirikisha wafanyabiashara 5,098 zilifanyika. Vile vile Shirika lilitoa ushauri wa kibashara kwa wateja 30,398 kufanya maonyesho sita ya kikanda ambayo yalishirikisha miradi 523 na kuwezesha wafanyabiashara 50 kushiriki katika Maonyesho ya 26 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2002 *SIDO* ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 688.5 kwa miradi 1,526 iliyotoa ajira mpya 4,916. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba, 2002 mfuko wa wafanyabiashara wadogo (*NEDF*) ulioanzishwa na Serikali mwaka 1994, ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.85 kwa miradi 14,272. Miradi hii ilitoa ajira kwa wananchi 24,785. Kufikia Desemba, 2002, maombi ya mikopo chini ya Mfuko huu yalifikia jumla ya shilingi bilioni 26.16 kutoka kwa waombaji 69,272. Mikopo iliyotolewa ni asilimia 18 ya thamani ya maombi yote, jambo linalodhahirisha umuhimu wa kuongeza uwezo wa mfuko huu ili kukidhi mahitaji kwa kiwango kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* kwa kushirikiana na wadau wengine inafanya utafiti unaolenga kubaini maeneo maalumu ambayo baadaye yatatengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Juhudi za kufanikisha zoezi hilo zinaendelea vizuri na utafiti umekamilika katika Mikoa kumi na mapendekezo yameanza kufanyika kazi. Aidha, miradi 161 iliyoko ndani ya maeneo ya mitaa ya viwanda vidogo itaendelezwa. Sekta binafsi itashirikisha kikamilifu na kwa makini katika kuanzisha maeneo mapya.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), iliendelea na jukumu la kuhamasisha biashara ya nje. Katika kuendeleza jukumu hili, *BET* ilisimamia maonyesho ya 27 ya Biashara ya Kimataifa ya Dr es Salaam, yaliyofanyika Julai, 2003. Maonyesho ya mwaka huu yalibusha washiriki wa ndani 1,800 ikilinganishwa na washiriki 1,404 mwaka 2002. Nchi za nje 10 zimeshiriki ikilinganishwa na nchi 13 mwaka 2002. Vikundi vyta wanawake kutoka Mikoa mingi ya Tanzania, chini ya udhamini wa Taasisi ya Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), *FAWETA*, pamoja na vikundi vingine vyta wanawake, vilishiriki kikamilifu. Maulizo na *order* za bidhaa toka nchi za nje kutokana na maonyesho haya vilifikia thamani ya dola za Marekani milioni 20.7 ikilinganisha na dola za Marekani milioni 14.6 kwa mwaka 2002.

Kwa msingi huu wa kuendelea kutangaza bidhaa zinazozalishwa Tanzania, *BET* na Wizara, zitakuwa wenyeji wa Maonyesho ya Sita ya Biashara ya Nchi za Kiafrika na Kiarabu ambayo yatafanyika katika Uwanja wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Jijini Dar es Salaam tarehe 5 hadi 14 Desemba, 2003. Maandalizi ya maonyesho haya yanaendelea vizuri. Natoa wito kwa wenge viwanda Tanzania kutumia fursa hii kuonyesha na kunadi bidhaa zao.

*BET* imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kufanya tafiti za masoko ya nje kwa bidhaa mbalimbali. Aidha, *BET* pia imeratibu na kuandaa ushiriki wa Tanzania katika maonyesho mbalimbali ya biashara za Kimataifa nchi za nje. Ili *BET* itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi taratibu zimeanza za urekebishaji wa muundo na mwelekeo wake. Lengo ni kuifanya *BET* kuwa chombo madhubuti cha kuhamasisha sekta mbalimbali kuzalisha bidhaa zinazoweza kuhimili ushindani katika soko la dunia, kuendeleza jukumu la kuwezesha sekta binafsi katika kutafuta na kutafiti masoko ya nje, pamoja na kuwa kiungo muhimu baina ya mfumo wa mauzo nje na ule wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, uwezekano unaangaliwa wa kuanzisha Mfuko wa Kuendeleza Mauzo Nje (*Export Development Fund*) ili kuongeza ufanisi wa *BET*. Mfuko kama huu utawezesha sio tu *BET* bali pia taasisi za wafanyabiashara binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika jukumu lake la kuitangaza Tanzania nchi za nje, Kituo cha Tanzania cha Biashara kilichoko London, Uingereza kiliendelea kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii nchini pamoja na kuliwezesha Taifa kushiriki katika vikao mbalimbali vya taasisi za Kimataifa za kahawa na sukari. Aidha, Kituo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Madola, kilitoa mchango wake wa uhamasishaji wakati wa maandalizi ya mkutano wa wawekezaji uliofanyika Dar es Salaam na Zanzibar mwezi Mei, 2003. Kituo kitaendelea kushirikiana na makampuni ya Uingereza yanayotangaza vivutio vya utalii ili uendelea kutangaza na kukuza sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya msingi mojawapo ya Serikali ya CCM katika kurekebisha uchumi wa Taifa ni pamoja na kuipa sekta binafsi nafasi ya kipaumbele ya kuendesha uchumi ili Serikali ielekeze nguvu zake katika shughuli za kusimamia sera, sheria, huduma za jamii, miundombinu na ulinzi na usalama. Katika azma hii, Serikali imeweka mfumo mzuri kwa sekta binafsi ya kujadiliana na Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara (*Tanzania National Business Council*). Serikali imekusudia kuendeleza sekta binafsi kwa kujengea mazingira mazuri ya kukua na kuendelea. Hii ni pamoja na kujenga mazingira wezeshaji chini ya programu ya uboreshaji mazingira ya kibashara (*Business Environment Strengthening for Tanzania - BEST*) na kuwaunganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje chini ya programu ya *Integrated Framework*.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine chini ya usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, imeshiriki katika kuandaa Sera ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi pamoja na Muswada wa Sheria ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi na mimi mwenyewe nimekupewa heshima ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri ya Uwezeshaji.

Madhumuni ya sera hii ni kuunda mazingira muafaka yatakayowapatia Watanzania fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yao. Sera hii ni maelekezo mahususi ya mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010 na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2000. Sera hii inatoa nafasi kwa kila sekta kubeba jukumu la kutoa msukumo na kusaidia wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Wizara itazingatia jukumu hili ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa nje ya kilimo, viwanda vidogo na biashara ndogo ndiko waliko wananchi wengi wanaotarajiwa kuwa mhimili wa uchumi wa Taifa letu siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kulingana na mpango wa Serikali wa kurekebisha mfumo wa utendaji Serikalini, Wizara ya Viwanda na Biashara imekamilisha maandalizi ya kutekeleza mpango wa kurekebisha mfumo wake wa utendaji ili kujenga uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Katika utekeleza azma hii, muundo mpya wa Wizara, unaolenga kuimarisha ufanisi katika uwezeshaji wa sekta binafsi

katika shughuli za uzalishaji na biashara umeidhinishwa. Muundo huu unalenga pia katika kuimarisha uwezo wa watendaji wa Wizara katika kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi, Wizara imeweka mtandao wa kompyuta na inaendelea kutoa mafunzo kwa wtumishi ili kuwawezesha kutumia vifaa hivyo.

Aidha, Wizara inatekeleza mpango wa kuweka mtandao wa kompyuta katika masijala kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu na taarifa mbalimbali pamoja na ufuatilaji wa taarifa zinazoingia na kutoka Wizarani. Katika mwaka 2003/2004, Wizara inakusudia kuendeleza programu zinazolenga kupanua ujuzi kuhusu masuala ya *WTO* ndani ya Asasi na taasisi za Serikali na za sekta binafsi. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), inatekeleza mipango ya kujenga uwezo wa kutekeleza Sera mpya ya Taifa ya Biashara pamoja na kushiriki ipasavyo katika majadiliano na utekelezaji wa mikataba ya *WTO*. Programu hizi zinatilia mkazo umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi na asasi ziziso za Kiserikali katika kutimiza majukumu haya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, chini ya Programu ya Urekebishaji Mfumo wa Utumishi wa Umma (*Public Service Reform Programme*), inayoratibiwa na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi, Wizara itanza kutumia utaratibu mpya wa kupima utendaji kazi wa watumishi wake kwa kutumia mfumo wa ushirikishwaji ili kuongeza uwazi katika utumishi wa umma na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi. Utaratibu huu unalenga kudumisha nidhamu na maadili mahali pa kazi.

Katika kufikia lengo hili, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi, imeandaa semina mbalimbali kwa watumishi kwa madhumuni ya kutoa elimu kuhusu programu hii. Kwa kutambua kwamba ujenzi wa uwezo wa Wizara ni pamoja na kuwa na watumishi wenye afya njema, Wizara inaendelea kuelimisha watumishi wake kuepukana na janga la Ukimwi mahali pa kazi. Lengo ni kupunguza athari inayojitokeza ya kupoteza uwezo uliowekezwa kwa muda mrefu na gharama kubwa ndani ya taaluma mbalimbali katika Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, tunatarajia kutekeleza programu mbalimbali ambazo makusudio yake ni kuimarisha utendaji katika sekta za viwanda na biashara. Programu hizi zitahusu pia uimarishaji wa uwezo wa Wizara yenye na taasisi zilizo chini ya Wizara. Programu hizi zitazingatia zaidi utekelezaji wa Sera za Viwanda na Biashara kama sehemu ya utekelezaji wa sera za jumla za Kitaifa na hasa zinazohusu masuala ya kiuchumi.

Aidha, utekelezaji utahusu mikakati mbalimbali ambayo tayari imeandaliwa au ambayo ipo katika ngazi mbalimbali au inayokusudiwa kuandaliwa. Kwa mantiki hii, malengo na mtarajio ya Wizara katika mwaka 2003/2004 yako katika makundi matatu: malengo ya sekta ya viwanda, malengo yanayohusu sekta ya biashara na malengo ya jumla ambayo yanazingatia majukumu mengine ya Wizara na ambayo yanazigusa kwa pamoja sekta za viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha mafanikio ya sekta ya viwanda yaliyopatikana katika kipindi kilichopita, Wizara katika mwaka 2003/2004 itaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na Jumuiya ya wenye viwanda na viwanda vyenyewe ili kujuu matatizo yao na kushiriki katika kuyatafutia ufumbuzi. Wizara itaendelea kubuni mikakati na mbinu za kutekeleza Sera Endelevu ya Viwanda kwa kuzingatia sekta za kipaumbele ikiwa ni pamoja na sekta ya nguo, usindikaji wa mazao ya kilimo, sekta ya ngozi na sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo.

Aidha, itaainisha mbinu mbalimbali za kuvisaidia viwanda vyenye malengo na uwezo wa kuzalisha zaidi, hasa kwa ajili ya kuuza bidhaa katika masoko maalum kama *AGOÀ*, *EBA*, *PACT* na masoko mengine ya upendeleo (*preferential markets*) ya Japan, Australia, Ufaransa na nyinginezo. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuandaa mikakati ya kuongeza ufanisi wa sekta ya viwanda; kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na *UNIDO* na wahisan wengine, kuendeleza mpango wa uzalishaji mahusi wa bidhaa kwa mauzo ya nje (*EPZ*), kuandaa programu za kutekeleza Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, kuimarisha utafiti na ukusanyaji wa takwimu za viwanda na kushiriki katika kupendekeza programu za kuhifadhi mazingira kwa kushirikina na taasisi husika. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine katika kuweka mazingira wezeshaji na bora ya uzalishaji katika viwanda ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa kuaminika wa nishati na maji na kuboresha mfumo wa kodi unaohamasisha ukuaji wa sekta ya viwanda.

Aidha, Wizara itatekeleza mikakati ya kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi ambayo imekwishaandaliwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na wenye viwanda vya ngozi. Hatua zimeanza kuchukuliwa katika Bajeti ya Serikali ya 2003/2004 kwa lengo hili. Wizara inakusudia pia kuandaa mkakati wa kuendeleza sekta ya nguo kwa kushirikiana na wadau wa sekta kama ilivyofanyika kwa sekta ya ngozi. Maandalizi yatafanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matatizo katika sekta ya nguo ili kubainisha hatua za kuchukuliwa.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO*, itakamilisha maandalizi ya programu ya Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Viwanda na kuanza utekelezaji wake. Programu hiyo inalenga katika kuhamasisha, kuwezesha na kuelekeza wawekezaji binafsi katika kujenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo na kupunguza uharibifu mkubwa wa mazao baada ya mavuno unaotokana na hifadhi duni.

Kwa kutambua mapungufu ya uwezo wa viwanda vilivyopo katika kuzalisha na kuuza bidhaa za viwanda nchi za nje, hususan katika masoko ya masharti nafuu kwa nchi zinazoendelea, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo ya *EPZ*. Lengo ni kuwezesha Tanzania kushiriki kikamilifi katika masoko hayo ili kufaidika na nafuu hizo kama nchi nyingine hususan katika maeneo ya ukuzaji wa ajira na upatikanaji wa teknolojia ya kisasa. Kwa kuwa sasa tunayo sheria na kanuni za *EPZ*, msukumo utaelekezwa katika kuhamasisha wawekezaji ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa maeneo kwa wawekezaji wenye nia ya kushiriki katika programu ya *EPZ*.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha uandaaji wa programu zitokanazo na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, wafadhili, sekta binafsi na taasisi zisizo za Serikali zitashirikishwa katika kutekeleza programu mbalimbali zinazoandaliwa. Ili kuhakikisha ushirikishaji wa wananchi wengi, Wizara itaendesha warsha za kikanda zitakazoshirikisha Wilaya zote kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha wadau.

Aidha, utaananzishwa utaratibu wa kukutanisha wadau wa sekta ili kufanya mapitio ya pamoja na mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa sera hii, mwaka hadi mwaka.

Wizara, kwa kushirikiana na taasisi husika za Serikali, itaendelea kutoa ushauri na kuhimiza wenye viwanda kuzingatia masuala ya uboreshaji wa mazingira ya uzalishaji ili kuepusha uchafuzi wa mazingira. Hii ni muhimu ikizingatiwa kwamba kampeni zinazoendelezw na baadhi ya nchi, lengo lake ni kutaka bidhaa zitakazouzwa katika masoko ya Kimataifa zizalishwe katika hali ya kujali mazingira. Katika misingi hii, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi zinazohusika na masuala ya mazingira katika utekeleza programu za Kimataifa kuhusu uzalishaji na mazingira. Mkakati huu ni sehemu ya kujihakikishia masoko ya nje kwa bidhaa zetu.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Wizara katika sekta ya biashara ni kuwa na mikakati inayotuwezesha kama Taifa kuhimili ushindani wa biashara Kimataifa na kutupa uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya Kimataifa katika zama hizi za utandawazi. Ili kutimiza lengo hili, Wizara katika mwaka 2003/2004 itajielekeza katika maeneo makuu sita ambayo ni utekelezaji wa Sera ya Biashara, uandaaji wa mikataba ya ushirikiano wa biashara na nchi mbalimbali zikiwemo zile za *COMESA* ambazo siyo nchi wanachama za *EAC* au *SADC*, majadiliano na utekelezaji wa mikataba ya biashara ya Kimataifa, urekebishaji wa Sheria ya leseni za Biashara, usimamiaji Sheria ya Wakala, utekelezaji wa Sheria ya Wakala wa Meli na maandalizi ya Sheria ya *Anti-Dumping*.

Katika kipindi cha 2002/2003, Wizara itatekeleza programu zilizoainishwa katika Sera ya Taifa ya Biashara. Programu hizi zitajumuisha jukumu la kuelimisha wananchi na wadau wengine kuhusu Sera ya Biashara ikiwa ni pamoja na malengo na makusudio yake. Elimu hii itatolewa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa warsha za kikanda. Aidha, Wizara inaandaa tafsiri ya Kiswahili pamoja na makala rahisi (*popular version*) ya Sera ya Biashara kwa ajili ya kufanikisha warsha hizo.

Mheshimiwa Spika, makala hizi zitasambazwa katika Taasisi mbalimbali, Maktaba za Mikoani na za Vyuo mbalimbali, kwa lengo la kuwafikia walengwa wengi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza programu ya *Joint Intergrated Technical Assistance Programme (JITAP)* na Programu ya *Intergrated Framework for Trade Development (IF)* inayolenga kupanua uwezo wa wadau wa sekta ya umma, sekta binafsi na asasi zisizo za Kiserikali kuelewa na kutekeleza mikataba ya Shirika la Biashara Ulimwenguni (*WTO*).

Programu ya *JITAP* inatekelezwa kwa ushirikiano na taasisi za Kimataifa za *International Trade Centre (ITC)*, *WTO* na *UNCTAD*. Utekelezaji wa awamu ya pili ya programu ya *JITAP* itakayochukua miaka miwili, umeanza rasmi Julai 1, 2003. Kwa upande wa *Intergrated Framework* tutaendelea kushirikiana na wafadhili kuendeleza utekelezaji wa programu zilizopo na kubuni programu mpya pale ambapo inadhihirika kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Pia, utaendeleza jukumu la kushiriki katika majadiliano ya uhusiano wa biashara baina ya nchi zinazoendelea na Jumuiya ya Ulaya (*EU*) chini ya mfumo wa Mkataba wa Cotonou. Hii ni pamoja na kushiriki katika majadiliano ya kurekebisha mikataba hiyo kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Kuhusu mikataba ya biashara baina ya nchi mbili, hii ni nyenzo madhubuti ya kupanua na kukuza uwekezaji na biashara. Kwa hiyo, Wizara itaendelea kuandaa na kuingia mikataba ya biashara na nchi za Afrika, Asia, Mashariki ya Kati na Ulaya. Lengo ni kukuza biashara yenyewe uwiano mzuri baina ya Tanzania na nchi husika.

Katika kipindi cha 2003/2004 *BRELA* itafanya uchambuzi wa kuona uwezekano wa kupeleka huduma za Wakala karibu zaidi na wananchi kwa kufungua ofisi za kanda na kutumia Ofisi za Biashara za Mikoa kutoa huduma husika. Katika kipindi hiki *WMA* itaendelea na zoezi la kuimarisha ofisi zake Mikoani ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi. Vile vile, Wakala zote mbili zitatoa elimu kwa walengwa kwa njia ya warsha na usambazaji wa vijarida na vipeperushi kuhusu huduma na malengo ya Wakala hizi. Lengo ni kutoa elimu kuhusu mfumo mpya wa utendaji kazi na Wakala hizi. Aidha, elimu inayokusudiwa itasaidia kuimarisha ulinzi wa haki na maslahi ya walengwa kwa njia ya kuhamasisha matumizi ya huduma zinazotolewa na Wakala hizi.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha kazi ambayo imekwishaanza ya kufanya marekebisho katika sheria na taratibu za utoaji wa leseni za biashara kwa lengo la kuondoa kero kwa wafanyabishara. Aidha, Wizara itaandaa Warsha kwa Jumuiya za wafanyabishara kuhusu mabadiliko katika utoaji wa leseni za biashara utakaowekwa baada ya marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara ili wapate fursa ya kuyaelewa mabadiliko husika.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Wakala wa Meli. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa utoaji wa leseni unazingatia matakwa ya sheria. Usimamiaji wa sheria hii utahusisha pia ukaguzi wa waliopewa leseni kuona kama wanazingatia matakwa ya sheria hii kama vile kuajiri watumishi wenye utaalamu na miliki ya kampuni hizi kuwa mikononi mwa Watanzania.

Kwa upande mwengine Wizara itakamilisha jukumu la kuandaa na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya *Anti-dumping*. Lengo ni kuwasilisha Muswada huu katika Mkutano wa 13 wa Bunge hili. Aidha, tutanza kujenga uwezo wa watendaji husika mwaka huu ili utekelezaji rasmi uanze mara baada ya sheria kuitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na takwimu muhimu za viwanda na biashara kwa matumizi mbalimbali ya Serikali na wadau wengine ni la msingi sana. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara inakusudia kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa takiwmu za viwanda na biashara zitakazowezesha uanzishaji mahususi wa takwimu za sekta (*Sectoral Bata Bank*).

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Ujasirimali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inakusudia kukusanya na kuchapisha jarida lenye taarifa mbalimbali za taasisi zinazohusika na maendeleo ya *SMEs*. Wizara pia itaendelea kufanya utafiti katika maeneo yenyewe matatizo yanayokwamisha maendeleo ya viwanda vyetu, kwa kushirikiana na wadau husika. Kwa kuanzia, utafiti wa kina utafanywa kuhusu

upatikanaji na matumizi ya chuma chakavu hapa nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa Taifa linafaidika na malighafi hii.

Aidha, eneo lingine la utafiti linahusu soko la magunia ya katani yanayozalishwa hapa nchini. Katani ni moja ya mazao ya biashara hapa nchini, hivyo juhudzi za kuongeza thamani ni muhimu kwa mapato ya wakulima na uchumi wa Taifa. Vile vile utafiti utafanywa kuhusu maeneo mapya ya uwekezaji katika viwanda kwa kutegemea malighafi zilizopo hapa nchini na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Wizara itatazama upya mwelekeo wa taasisi za utafiti na utoaji huduma kwa sekta za viwanda na biashara. Miundo na majukumu ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*) na Wakala wa Mizani na Vipimo (*WMA*) ilikwishakamilishwa na jitihada zitaelekezwa katika kuboresha huduma za Wakala hizi. Kuhusu taasisi za utafiti na huduma ikiwa ni pamoja na *BET*, *TEMDO*, *CAMARTEC*, *CBE*, *TIRDO*, *TBS*, *SIDO* na *NDC*, lengo ni kufanya tathmini ya kubainisha nafasi na wajibu wa taasisi hizi kwa kuzingatia mabadiliko ya sera za kiuchumi, Kitaifa na Kimataifa na nafasi yao katika kuendeleza sekta binafsi hapa nchini ili sekta binafsi iwe kweli injini ya ukuaji wa sekta ya viwanda na biashara na uchumi wa taifa kwa ujumla. Tathmini inayokusudiwa itazingatia kuimarishe na kuongeza ushirikiano baina ya taasisi hizi katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayoikabili sekta binafsi hususan katika mfumo wa uzalishaji na mauzo ya bidhaa na huduma nje.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa maeneo ya uwezesajji na uendelezaji wa sekta binafsi yanayopewa kipaumbele ni ujenzi wa mazingira wezesajji yenye lengo la kurahisisha taratibu za uwekezaji na biashara. Mpango huu unajulikana kama Programu ya Kuboresha Mazingira ya Kibiashara (*Business Environment Strengthening for Tanzania – BEST*) ambayo itatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara na taasisi mbalimbali za umma na za sekta binafsi. Mwaka 2003/2004, Wizara itaanza utekelezaji wa mikakati na mbinu za kurekebisha mfumo wa leseni za biashara pamoja na kuimarishe utendaji wa Wakala wa Usajili wa Kampuni (*BRELA*) kama sehemu ya Programu ya *BEST*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizi, Wizara itaendeleza utekelezaji wa sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, ambayo lengo lake ni kudhibiti ukiritimba wa kibiashara na kiuchumi. Sheria hii ni sehemu muhimu ya kujenga mazingira wezesajji kwa ukuaji wa sekta ya biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itafuutilia kwa karibu zoezi la kukamilisha taratibu za ubinafsishaji wa viwanda vya *Polytex* na *SPM* na kampuni za *HOSCO*, *S&O*, *BCS*, *RTC* za Dar es Salaam, Arusha na Mwanza na kampuni ya *NSC*. Aidha, Wizara itafuutilia kwa makini zoezi la kuhitimisha shughuli za *NASACO* na makampuni yake Tanzu. Wizara pia itaendelea kutekeleza zoezi maalum la kufuutilia utendaji wa mashirika ya sekta ya viwanda na biashara yaliyobinafsishwa ili kubainisha mchango na matokeo ya ubinafsishaji wa mashirika haya kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili litajumuisha majadiliano na wawekezaji hasa wale ambao hawaajaendeleza viwanda walivyonyunuwa kwa lengo la kusaidia kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili na pale inapobainika kwamba wawekezaji hao ni wababaishaji au hawana dhamira ya kweli ya kuvienda viwanda hivyo, Serikali itavichukua na kuvitangaza upya kwa lengo la kupata wawekezaji wengine wenye uwezo na dhamira ya kuvienda viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha zoezi la utekelezaji wa muundo wake kama sehemu ya kuimarishe uwezo wake wa utendaji kazi. Aidha, Wizara itaanza kutekeleza mpango mahsus (*Strategic Plan*) unaojumuisha malengo ya Huduma kwa Wateja (*Lients Charter*) na mbinu na taratibu za kupanga na kutekeleza kazi zake. Wizara pia itakamilisha zoezi la kuboresha utendaji kazi wa Masijala ili kuboresha mawasiliano ndani ya Wizara na katika Wizara na taasisi nyininge za wananchi. Licha ya malengo haya, Wizara pia itaendelea kuimarishe uwezo wake katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu ikiwa ni pamoja na uwezo wa utafiti, majadiliano ya Kimataifa (*International Negotiations*) hasa kuhusiana na mikataba ya biashara ya Kimataifa na ya kikanda na uwezo wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu yake. Wizara kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali tayari imeandaa programu zinazolenga kujenga uwezo huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi rafiki na mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa misaada iliyoiiongezea uwezo Wizara yangu kutekeleza majukumu yake. Napenda kuzishukuru nchi za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, India, Japan, Marekani, Sweden, Uhlanzi, Uingereza, Ujeruman na nchi nyininge ambazo zimeendelea kusaidia Wizara.

Aidha, napenda kuyashukuru mashirika ya *SIDA, UNIDO, DANIDA, DFID, GTZ, NORAD, WTO, UNCTAD, USAID, UNDP, OPEC Fund, JICA, WIPO, ARIPO, ITC*, taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) na *Commonwealth Fund for Technical Cooperation* kwa misaada na michango yao ya fedha na utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni matokeo ya kazi nzuri na ushirikiano wa karibu nilioupata kutoka kwa wenzangu katika Wizara, mashirika, taasisi na makampuni yaliyo chini ya Wizara.

Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Katibu Mkuu, Bwana Ahmada Ngemera na watumishi wote wa Wizara, Mashirika, makampuni na taasisi zilizo chini ya Wizara, ambao wamehusika kwa namna moja au nyininge na maandalizi ya bajeti ninayoiwasiliasha leo.

Nazishukuru pia Jumuiya ya Wenye Viwanda (*CTI*), Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (*TCCIA*) na *Tanzania Private Sector Foundation* na taasisi zinazoshughulikia utafiti, hasa Kituo cha Utafiti wa Masuala ya Jamii na Uchumi (*ESRF*), Idara ya Utafiti wa Uchumi (*ERB*) na Kitivo Cha Biashara na Menejimenti cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa michango yao ya mawazo wakati wa mikutano, warsha, semina na makongamano mbalimbali kuhusu sekta ya viwanda na biashara. Ushirikiano huu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha sekta ya viwanda na biashara. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa huduma muhimu ya kuchapa hotuba hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara inaomba shilingi 1,820,469,000/= kwa ajili ya shughuli za Miradi ya Maendeleo ya Viwanda na Biashara. Kati ya fedha hizi, shilingi 200,000,000/= ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo katika taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 1,620,469,000/= ni fedha za nje kutoka kwa wafadhili ambazo zitatumika kulipia tafiti za kitaalamu na vifaa kwa miradi mbalimbali itakayotekelawa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo ya sekta ya Viwanda na Biashara, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara inaomba shilingi 6,607,156,600/= kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, kiasi cha shilingi 2,744,003,652/= ni matumizi ya Wizara yenye na shilingi 3,863,152,948/= ni ruzuku kwa mashirika ya umma yanayosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nimeambaitisha majedwali mbalimbali ambayo yanatoa takwimu zitakazowezesha Waheshimiwa Wabunge kutafakari vizuri zaidi maendeleo ya utendaji katika sekta ya Viwanda na Biashara. Naomba takwimu hizi zichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

*Hapa Naibu Spika(Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. SALOME J. MBATIA (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya

Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2002/2003 na kutoa Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wajumbe wa Kamati kwa kunipa heshima ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) (Toleo la 2003) Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilikutana Dar es Salaam tarehe 5 Juni, 2003 kupitia na kuchambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2003/2004 ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilizingatia maeneo muhimu yafuatayo, Dira, malengo na madhumuni ya Wizara, Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri na maoni ya iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Biashara yaliyotolewa mwezi Juni, 2002, maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2002/2003 na mafanikio na matatizo yaliyojitekeza wakati wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa Dira (*Vision*) ya Wizara imetokana na Dira ya jumla ya Maendeleo ya Taifa (*Vision 2025*) ambapo Sekta ya Viwanda na Biashara inatarajiwa kuwa kichocheo cha mabadiliko ya mfumo wa uchumi wa nchi kutoka kwenye kutegemea kilimo na kuelekea kwenye uchumi unaohimili ushindani na wenyewe Maendeleo ya Viwanda kwa Kiwango cha Kati (*Semi-Industrialized Economy*). Aidha, Dira ya Wizara ni kuwa Kiongozi wa Maendeleo ya Sekta binafsi katika kuendeleza Sekta za Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kuboresha na kuoanisha Dira yake ili Wizara hii ichukue nafasi stahili (*Rightful Role*) katika kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara hususan katika kipindi hiki cha soko huru na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilielezwa kuwa ili kutekeleza Dira na mwelekeo huo, Wizara inadhamiria kutekeleza yafuatayo kwa uboresha Sera na kurejea (*Review*) sheria zinazokwaza Sekta ya Viwanda (*Legal and Regulatory Framework*), kubaini vyanzo mbalimbali vya mtaji kwa Sekta ya Viwanda na Biashara na kuboresha utoaji huduma na kujenga uwezo na mazingira bora kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2002/2003, Kamati ilikuwa imetoa maoni na ushauri mbalimbali ambaao ulihitaji kutolewa Taarifa ya Utekelezaji. Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kama ilivyowasilishwa na Wizara. Hata hivyo, Kamati ilibaini haja ya Wizara kuweka nguvu na msisitizo zaidi katika eneo lifuatalo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli ya kuratibu na kusimamia viwanda vilivyobinafsishwa. Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya Viwanda na Mashirika yaliyobinafsishwa katika Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro mwishoni mwa mwezi Mei, 2003. Katika ziara hiyo, Kamati ilijionea mafanikio ya kuridhisha kwenye viwanda kadhaa na ilisikitishwa na utekezwa jili ya baadhi ya viwanda uliofanywa na wawekezaji waliovinunua. Kwa niaba ya Kamati, napenda kuipongeza PSRC kwa kuiwezesha Kamati kufanya ziara hiyo muhimu ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inadhihirisha wazi kutokuwepo na juhudini za kuratibu na kufuatilia Viwanda na Mashirika hayo, baada ya kubinafsishwa. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kuratibu, kusimamia, na kufuatilia viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuona iwapo wawekezaji wanatekeleza ipasavyo masharti ya mikataba ya ununuzi wake. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuipitia mikataba ya ubinafsishaji kwani mingi ina mianya (*loopholes*) ya kuwalinda wawekezaji wababaishaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka 2002/2003, Wizara iliweka lengo la kukusanya shilingi 451,798,000/= kupitia Kitengo cha Mizani na Vipimo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2003 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 302,927,455/= ikiwa ni asilimia 67.0 ya lengo.

Aidha, katika mwaka 2002/2003, Serikali ilitarajiwa kupata jumla ya shilingi 3,758,200,000/= kutohuna na utoaji wa leseni za biashara zinazosimamiwa na Wizara. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2003 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 2,573,863,447/= sawa na asilimia 68.5 ya kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilishauri Wizara kuleta taarifa za ukusanyaji wa mapato zinazoishia angalau mwezi Mei, 2003 badala ya mwezi Machi, 2003 ili kupata taswira halisi ya hali ya makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumzi kwa mwaka 2002/2003, Wizara ilitumia kiasi cha shilingi 5,808,211,548/= sawa na asilimia 79.2 kati ya jumla ya shilingi 7,332,550,200/= zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 200 fedha za matumizi ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo shilingi milioni 150 zilitengwa kwa ajili ya shughuli za taasisi zinazosimamiwa na Wizara na shilingi milioni 50 kwa ajili ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) ili kuiendeleza shughuli za *EPZ*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipatia Wizara fedha zote shilingi milioni 200 zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa Wizara hii katika maendeleo ya uchumi hususan katika kipindi hiki cha ushindani na utandawazi, Kamati ilitarajia kuona Serikali inaipatia Wizara hii fedha zaidi ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuipeleka nchi hii kwenye hatua ya Maendeleo ya Viwanda ya kati (*Semi-Industrialized Economy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesikitishwa kuona kuwa fedha zilizotengwa mwaka 2003/2004 ni kidogo kuliko za mwaka 2002/2003 pamoja na majukumu ya Wizara kuongezeka. Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele Sekta ya Viwanda na Biashara kama kweli tumedhamiria kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa uchumi wetu kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Kamati ilielezwa kuwa Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kuendelea kujenga uwezo wa Wizara (*capacity building*) kwa kukuza utaalami wa watumishi, kuboresha vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kazi, kuimarisha uwezo wa taasisi na asasi zinazohudumia Viwanda na Biashara, kubuni na kuweka mazingira bora ya uwekezaji endelevu katika Sekta ya Viwanda na Biashara, kukagua na kudhibiti ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi, kutekeleza Sheria ya Ushindani wa Haki katika shughuli za kiuchumi na kumlinda mlaji, kuanzisha maeneo Huru ya Uzalishaji kwa ajili ya kukuza Mauzo ya bidhaa zetu Nchi za Nje (*Export Processing Zones (EPZ)*) na kutunga Sheria ya kudhibiti bidhaa zinazoingia nchini (*Anti-dumping*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kuchambua kwa makini taarifa ya Wizara hii, Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao ili kuleta ufanisi na kuboresha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda ndiyo mhusika mkuu katika Sekta ya Viwanda nchini. Kwa mantiki hiyo, badala ya viwanda vilivyobinafsishwa kusimamiwa na kuratibiwa na Wizara husika (*Sectoral Ministry*) Kamati inaishauri kuwa kazi na jukumu la kuratibu na kusimamia viwanda vilivyobinafsishwa liwe ni la Wizara hii (Viwanda na Biashara). Haja ya ushauri ni kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji wa wazi. Aidha, Wizara ianzishe Kitengo cha Usimamizi (*Monitoring Section*) ili kutekeleza jukumu hili ipasavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuchukua hatua zinazolenga kukuza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi. Baadhi ya hatua hizo ni kuanzishwa kwa Maeneo Maalum ya Uzalishaji, *Export Processing Zones (EPZ)* na kuongeza kasi ya kutumia fursa ya *AGOA* na utaratibu wa *EBA*.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kutoa msukumo zaidi kwa kuimarisha Mfuko wa Udhaminii wa Uuzaji wa Mazao Nje (*Export Credit Guarantee Scheme*) ulioanzishwa miaka ya 1980 kama njia mojawapo ya kukuza na kuimarisha mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje. Kamati pia inaishauri Wizara kuimarisha ushirikiano na Taasisi kama vile *Tanzania Chamber of Commerce Industries and Agriculture (TCCIA)*, *Confederation of Tanzania Industries (CTI)*, Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*) ili kufikia azma hiyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya kiuchumi yaliyoanza kutekelezwa na Serikali yetu kuanzia katikati ya miaka ya 1980 yanatoa changamoto kwa wenyewe viwanda vidogo na vikubwa kubadilisha mtazamo na fikra toka kwene kwenye bidhaa (*Production Oriented*) na kuelekea kwene soko (*Market Oriented*). Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwa ili kuimarisha soko la bidhaa zetu, masuala kama ubora, kujua mahitaji ya mnunuzi, kiasi na aina ya bidhaa ni muhimu sana hususan katika zama hizi za ushindani mkali zaidi na utandawazi. La sivyo, tutajikuta muda wote tunabaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ni nyenzo muhimu ili kuleta maendeleo katika sekta yoyote ile. Pamoja na ukweli huo, Kamati imesikitishwa kuona kuwa Taasisi za Utafiti za Wizara hii yaani Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (*TIRDO*), Kituo cha Uenezaji wa Teknolojia Rahisi Vijiji (*CAMARTEC*) na Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*) vimetengewa fedha kidogo ikilinganishwa na majukumu yake. Pamoja na kutengewa kiasi kidogo sana cha fedha za maendeleo mwaka uliopita, Taasisi hizi hazikupewa fedha za matumizi ya kawaida, hivyo kushindwa kutekeleza kikamilifu malengo waliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuzitengea taasisi hizi fedha na nyenzo za kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika mwaka wa fedha ujao, tukizingatia kuwa hili ni jukumu la msingi la Serikali (*core function*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna taasisi ambazo zinatoa wataalam na kuendeleza Teknolojia, kama vile Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundu Stadi (*VETA*), Taasisi ya Ufundu Dar es Salaam (*DIT*), Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Karakana ya *TANESCO* na kadhalika Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara za Taasisi hizo kwa nia ya kuratibu shughuli zake ili kuhakikisha kuwa zina teknolojia inayohitajika na zinatoa wataalam wenyewe ujuzi unaohitajika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imechukua hatua ili kuimarisha na kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi. Hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa sheria ya kuanzisha Maeneo Maalum ya Uzalishaji bidhaa *Export Processing Zones (EPZs)* na utumiaji wa fursa ya Sheria ya *AGOA* na utaratibu wa *EBA*. Pamoja na hatua hizo nzuri Kamati ingependa kupendekeza kuongeza kasi ya utumiaji wa fursa ya *AGOA*, *EBA* pamoja na sheria ya *EPZ*, utekelezaji wa mikakati na Programu maalum kwa mfano, Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje ya Nchi *Export Development Strategy (EDS)*, *Business Environment, Strengthening for Tanzania (BEST)*, *Business Sector Programme Support (BSPS)* na kadhalika.

Aidha, Kamati ingependa kuona msukumo mkubwa katika utekelezaji wa Mikataba ya biashara ya kikanda kama Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) pamoja na makubaliano ya Cotonou na ya Shirika la Biashara Duniani (*WTO Doha Development Agenda*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya kiuchumi na Sera za Soko Huria yamefungua milango na hivyo bidhaa nyingi kufurika nchini. Hali hiyo inahitaji kuimarisha zaidi vyombo vya kisheria na ukaguzi ili kulinda afya za watumiaji na bidhaa zinazozalishwa nchini dhidi ya ushindani usio wa haki. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha Shirika la Ubora wa Viwango nchini, *Tanzania Bureau of Standards (TBS)*. Aidha, *TBS* iweke utaratibu wa kukagua bidhaa zinapokuwa madukani kama inavyofanya Bodi ya Madawa. Wizara pia, iweke utaratibu maalum wa uwekaji wa viwango kwa wazalishaji wa bidhaa ndogo ndogo hususan kina mama ili kuwapunguzia gharama. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa viwanda vingi vilivyobinafsishwa kwa kiasi kikubwa hauzingatii masharti ya Sheria za Kazi ikiwa ni pamoja na kutekelezwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa

Viwanda. (*Factory Inspection*). Kwa mfano imebainika kwamba nafasi mbalimbali katika viwanda hivyo zimeshikwa na wageni pekee. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri kwamba makubaliano kuhusu utaratibu wa ajira kwa Watanzania yazingatiwe. Aidha, mazingira katika viwanda hivyo yanahatarisha afya za wafanyakazi kwa kutokuwa na vifaa maalum vya kujikinga. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kuhakikisha kuwa wenyewe viwanda wanafuata Sheria za Ajira na Usalama Kazini. Pia, Kamati inashauri kwamba viwanda hivyo vifanyiwe tathmini za athari kimazingira (*Environmental Impact Assessment*).

Vilevile, kuna umuhimu wa Serikali kujua hali ya Mwekezaji (*Investment Portfolio*) katika viwanda hivyo, mathalan mwekezaji anafanya nini hasa katika kiwanda, fedha za kununua kiwanda na kukiendesha zinatoka wapi na namna anavyoendesha shughuli zake pamoja na suala zima la maslahi, mazingira ya wafanyakazi na Usalama wa Nchi. Aidha, nafasi za uongozi na kazi zitolewe kwa wananchi wenyewe uwezo, ujuzi na usoefu katika shughuli mbalimbali kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Biashara ya mwaka 1972 kwa kiwango kikubwa inapingana na azma ya kuendeleza biashara ndogo na kati *Small and Medium Enterprises (SMEs)* kwa namna inavyotumika sasa hususan katika ngazi ya Halmashauri. Kwa mfano, wananchi kutakiwa kulipa kodi za Serikali kabla ya kuanza biashara (*Provisional Taxation*). Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Wizara kuipitia upya sheria hiyo ili iendane na dhamira na Sera ya Kukuza Biashara Ndogo na za Kati, (*SMEs*) itakayokamilishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wajumbe wa Kamati hii, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri wake, kwa ushirikiano walioipa Kamati hii wakati inachambua Bajeti ya Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara.

Aidha, naomba pia kuwapongeza watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Ndugu Ahamada Ngemera, kwa kazi nzuri ya kuandaa kwa makini Mpango na Bajeti hii. Naomba pia kwa namna ya pekee kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na umakini wao wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi uliofanywa na ushauri uliotolewa, Kamati imekubaliana na mpango na makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na kuyapitisha kama yalivyowasilishwa na Wizara. Kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara chini ya Fungu Na. 44 ni Matumizi ya Kawaida shilingi 6,607,156,600/=, Matumizi ya Maendeleo shilingi 1,820,469,000/= na jumla shilingi 8,427,625,600/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kutoa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani maoni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) (b) (c) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu wake Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu na timu ya wataalam na wadau mbalimbali waliosaidiana katika kuandaa hotuba na Bajeti hii. Pamoja na pongezi hizi, Kambi ya Upinzani inadhani itakuwa ni kwa manufaa ya nchi yetu kama maoni, mapendekezo na tahadhari zinazotolewa na kambi hii zitizingatiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kikanuni wa Msemaji wa Kambi kuwa sehemu ya Kamati ya kudumu ni mzuri na unasaidia kuchangiana mawazo. Hata hivyo, kama Msemaji Kivuli, hapa nawasilisha mawazo ya Kambi ya Upinzani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa sasa tuanze utaratibu wa uchambuzi wa kina wa ni kwa kiasi gani tuliyoyapanga katika Bajeti za nyuma yamefanikiwa kwa kutekelezwa. Aidha, kama hayakufanikiwa ni kwa sababu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Wizara inaonyesha mafanikio kadhaa yaliyopatikana kwenye sekta ya viwanda na biashara. Pamoja na kuipongeza Wizara kwa mafanikio hayo kidogo ni vyema sasa tutafakari uwezo wetu wa kufuatilia wawekezaji walionunua viwanda vyetu au kama kuna waliojenga vipyta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa wawekezaji wetu wote hupitishwa na *TIC (Tanzania Investment Centre)*. Ukweli unabakia kuwa baadhi ya wawekezaji hawa wenye vibali vya uwekezaji hawafuatiliwi sawasawa na wengi wao hutumia vibali hivi kama njia mojawapo ya ukwepaji kodi wa bidhaa zisizohusiana na uwekezaji halisi. Wengine hutumia vibali hivi kuhalalisha ukaaji wao nchini pamoja na jamaa zao wakati ukweli sio wawekezaji. Sasa isije ikawa *TIC* inayo orodha ndefu ya wawekezaji wakati hayo Makampuni yanabakia kwenye makabrasha na makaratsasi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoolewa, kila mwaka wawekezaji mbalimbali lazima waandike *Progress Report* na kuiwasilisha *TIC*. Hatuna uhakika kama *TIC* wanafanya ukaguzi wa viwanda hivi? Ni maoni ya viwanda hivi na miradi mingine mbalimbali ya uwekezaji. Ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa sasa Serikali iunde Kamati maalum ya ufuatilaji wa wawekezaji hawa. Kamati hii iwe na nguvu za kisheria na ijumuise wajumbe kutoka wadau wote ikiwemo Wizara ya Fedha na *TRA*, Benki Kuu, *TIC*, *PSRC* na isimamiwe na Wizara ya Viwanda na Biashara. Hii itasaidia wawekezaji wadanganyifu kudhibitiwa mapema zaidi. Aidha, Kamati hii iwe na nafasi ya kusikia vilio au ushauri wa Watanzania wengi ambao leo wanalamikia sana suala la Wawekezaji wa nje. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001 wakati nawasilisha kwa mara ya kwanza maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nilitamka mambo muhimu kadhaa ambayo tulishauri Serikali iyafanyie kazi kwa makini. Miongoni mwa mambo tuliyoshauri kwa kipindi hicho ni pamoja na umuhimu wa kufanya maamuzi na kuyatekeleza haraka. Maamuzi yanapochelewa kutekelezwa, athari zake ni kubwa kwa nchi na wananchi wake wanaendelea kuathirika siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya *Anti-dumping* umechelewa sana. Vivyo hivyo sheria ya uwezeshwaji wa Watanzania kumiliki na kuendesha uchumi wao. Hii ni Bajeti ya tatu tangu Bunge hili lienze na kila mwaka Serikali hutoa ahadi ya aidha kuleta sera au sheria kuhusiana na mambo haya mawili ya msingi. Kambi ya Upinzani pamoja na kujua majukumu mengi ya Mheshimiwa Waziri na timu yake, inamshauri afanye hima kukamilisha haya kwani kasi ya kufanya nchi jalala ni kubwa na yenye athari nyingi kwa nchi na watu wake. Ni vyema Serikali ikajua vile vile kuwa uhai wa Bunge hili umebakia miaka miwili tu, lakini bado tunasema sera, sheria na kanuni zinaandaliwa. Ikiwa Wizara haijaweza kutekeleza haya katika kipindi cha miaka mitatu, Kambi ya Upinzani inashindwa kujua ni miujiza ya aina gani itatumika katika miaka miwili iliobaki ya uhai wa Bunge hili! (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukubali kuwa hatuna ujanja wa kukwepa utandawazi na hivyo soko huru, kwani hii ni mifumo ya kibashara na kiuchumi ya dunia ambayo sisi ni sehemu yake, ukweli unabaki palepale kuwa maendeleo endelevu ya nchi yoyote yataletwa na wenye nchi yao. Wageni na wawekezaji wa nje huwekeza kwa nia moja tu ya kutengeneza faida kubwa iwezekanavyo na tena kwa muda mfupi iwezekanavyo na kuziendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umaskini ni suala ambalo kila mwananchi analielewa na kila mtu anajitahidi kuondokana nalo. Bila shaka, Serikali nayo kwa kupitia *NEDF* imewapatia wananchi wenye vipato vya chini mitaji ya kuanzisha miradi midogo na kujijiri wenywewe. Kwa mfano *NEDF* ilianzishwa mwaka 1994 na hadi Desemba 2002, jumla ya miradi 14,272 ya thamani ya shilingi 4.85 billioni ilianzishwa na kutoa ajira kwa wananchi 24,785

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua hii ya kuanzisha miradi hiyo, ni vyema vile vile Waziri akatusaidia hali halisi ya miradi iliyo hai kwani ni karibu

miaka kumi tangu mfuko huu uanzishwe na kuna uwezekano mkubwa kuwa mingi ya miradi hii imekufa. Mara nyingi biashara huanzishwa lakini kudumu kwake inakuwa ni tatizo. Tungependa hawa wafanyabiashara wadogo watembelewe na *NEDF* na kupewa ushauri pale panapohitajika. Vinginevyo, tutajivunia miradi iliyofunguliwa lakini kumbe ilishafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa pongozi kwa mikopo ya *SIDO* ambayo imewapatia wananchi na vikundi mbalimbali mikopo sambamba na mafunzo mbalimbali. Pamoja na mafanikio haya, miradi hii hufanyika mijini na sasa tunashauri msisitizo uhamishiwe zaidi vijijini ambapo hali ya umaskini ni ya kutisha mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisilofichika kwamba fedha mara nyingi hazitoshelezi wakati wote. Kwa mfano kati ya mwaka 1994 na Desemba 2002, mikopo 14,272 yenye thamani ya shilingi 4.85 ilitolewa ikilinganishwa na maombi 69,272 ya thamani ya shilingi bilioni 26.16. Hii ni asilimia 18 tu ya maombi. Tafsiri yake ni kuwa mkakati huu utachukua muda mrefu sana kuondoa umaskini. Tunashauri Serikali kwamba suala la kuondokana na umaskini sio kazi ndogo na kwa maana hiyo, Serikali iongeze kasma katika mifuko mbali mbali kwa ajili ya kuwakopesha hawa wafanyabiashara wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kusaidia wafanyabiashara wadogowadogo, ni vyema vile vile kutambua kuwa ni lazima sasa wafanyabiashara wa Tanzania wakamate njia kuu za uchumi wa nchi na sio biashara ndogo ndogo. Tukiweka msisitizo kwenye biashara ndogo ndogo tu, tafsiri yake ni kuwa tutaendelea kuwa wachuuzi wadogo wadogo *ilhali* njia kuu za uchumi zimekamatwa na wageni ambao kwa kuwaachia huru katika eneo hili, fedha nyingi huhamishwa toka ndani ya uchumi wetu. Biashara ndogondogo mara nyingi huwa kwenye sekte zisizo rasmi.

Aidha, biashara hizi huchangia zaidi katika kujikimu na mahitaji ya msingi ya binadamu (*subsistence*) hususan chakula na nguo. Kwao hawa wawekezaji wadogo wadogo masuala ya utandawazi, mfumuko wa bei, masoko ya hisa na vigezo vingine vyenye kupima maendeleo ya kiuchumi yanakuwa hawayaelewii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali kuwezesha kwa makusudi wawekezaji wakubwa Watanzania angalao 100 walioonyesha mwelekeo wa kumudu biashara kubwa kwani hizi ndizo ukombozi wa uchumi wetu na hivyo vizazi vyetu. Tusione karaha kuwa na Watanzania wenzetu watakaotunza hadhi ya Taifa hili kwa kuwa na vitega uchumi vikubwa vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema ndani ya Bunge lako Tukufu kuwa taasisi za fedha nchini zina fedha chungu nzima lakini Watanzania wengi hawamudu masharti ya mikopo. Hili ni Tatizo kubwa ambalo Serikali sasa ilifanyie mkakati hata kama ni kwa kutoa *Government Guarantee* ili wafanyabiashara wakubwa wawezeshwe kupanua biashara zao na soko lao lilindwe hadi watakakomaa kushindana na wawekezaji wa nje yaani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yamefanyika nchi nyingi kama zilizoendelea kwa kasi katika miaka ya karibuni kama vile Malaysia, Singapore na nchi karibu zote za Mashariki ya Mbali. Matokeo yake, kwenye nchi hizi pamoja na kuwa na wawekezaji wakubwa toka nje, wananchi wao wana uwezo mkubwa wa kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2002/2003, Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake alieleza kwamba hatua ya kukuza sekta ya viwanda haziwezi kuleta matunda yaliyokusudiwa iwapo wananchi hawatahamasika kununua bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vyetu. Tamko hili vile vile limepewa msisitizo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya leo. Bila shaka hili wazo lilikuwa na bado ni zuri na halina budi liendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kampeni ya Nunua Bidhaa za Tanzania, Tuijenge Tanzania, bado kuna tatizo la ubora wa bidhaa zetu. Hatuwezi kumlazimisha mtu atumie bidhaa ambayo kwake yeye, ubora wake na pengine bei haikidhi matakwa yake. Hivyo tunashauri kwamba pamoja na kuhimiza kununua bidhaa za Tanzania, zoezi hili liendane na ubora na nafuu ya bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama bidhaa zetu zinakuwa aghali zaidi ya za nje, ina maana ya kuwa kuna upungufu mkubwa katika mfumo wetu wa kiuchumi. Somo la kwa nini bidhaa zetu haziuziki kirahisi hususan kwenye soko la ndani linahitaji utafiti wa kina wa sera zetu za uchumi na mazingira ya ki-biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara kwa sasa hivi ni ngumu sana kwani mazingira yamebadilika na yanaendelea kubadilika kwa kasi zaidi pamoja na hili suala la utandawazi. Kwa maana hii, hatuna budi kujizatiti katika ushindani wa kisayansi na teknolojia ili nasi tufanikishe maendeleo ya nchi yetu. Tunatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya mwaka 2002/2003 ya kutangaza Tanzania katika kituo cha biashara cha London kama kituo cha biashara na mahali pa uwekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi wa nchi. Kituo hiki vile vite hutangaza Tanzania kama kivutio cha utalii.

Aidha, kituo cha London kinaiwakilisha Tanzania katika Mashirika ya Kimataifa yaliyoko Uingereza ikiwa ni pamoja na Shirika la Uzialishaji na Matumizi ya Kahawa (*ICO*), Ushirika wa Shirika la Masuala ya Usafiri wa Majini (*IMO*), Ushirika wa Katani (*LSA*) na Shirika la Kilimo la Jumuiya ya Madola (*CAB International*). Kutokana na jitihada za kituo hiki pamoja na juhudi za ubalozi wetu ulioko Uingereza, Tanzani sasa angalau inafahamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitika kusema kwamba Uingereza tu hapatoshi kutangaza biashara na nchi yetu. Tunaishauri Serikali itumie kikamilifu Ofisi za Balozi zetu kuitangaza na kuinua hali ya uwekezaji na biashara kati yetu na nchi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi siasa ni uchumi na uchumi ni biashara. Balozi zetu ziimarishe uchumi wetu. Kama Balozi na Waambata wake hawawezi kufanya kazi ya kutafuta soko la bidhaa za Tanzania, basi ni dhahiri ameshindwa kazi na hatuoni sababu ya kuharibu fedha za nchi kuwaweka watu kama hawa ubalozini. Wenzetu wa Kenya wametumia sana Balozi zao na mtindo huu na sisi sasa tuanze kupima uwezo wa Maofisa wetu kwa mafanikio ya utekelezaji wa mikakati ya kiuchumi na sio madhumuni mengine ya kisiasa yaliyopitwa na wakati! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya kawaida, tungestahili kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa na Vitengo au Taasisi kadhaa zenye jukumu la kutoa huduma za utafiti na teknolojia kwa Sekta ya Viwanda na Biashara. Taasisi hizi, ambazo ni Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda (*TIRDO*), Kituo cha Uenezi wa Teknolojia rahisi Vijijini (*CARMATEC*) na Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*). Hizi ni Taasisi ambazo zimefanya kazi muda mrefu kabla na baada ya kuanza zoezi la ubinafsishaji. Aidha, dhana nzima ya utafiti wowote ule lazima uwe na matokeo na hugharimu fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, bado Kambi ya Upinzani inasikitishwa na hali ya Serikali kutokuthamini umuhimu wa Taasisi hizi.

Kama Serikali inadiriki kutozipatia fedha za kuziendeza na kuziendesha ni bora ikiri waziwazi na kisha ikazifuta na nafasi yake ikachukuliwa na Taasisi zinazojitegemea. Utafiti hauna mbadala wala unafuu. Nchi zote zilizoendelea ziliheshimu na bado zinaheshimu sana *R & D* yaani *Research and Development*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuthamini Taasisi hizi ni kudharau wasomi na wataalam wetu wa ndani. Kamwe hatuwezi kusaidiwa utafiti na wageni. Mara nyingi utafiti unahitaji uzalendo wa hali ya juu. Serikali ilifikirie kwa kina athari ya kutokuzipatia Taasisi hizi fedha za kutosha na ifikirie njia ya dharura ya kuzikwamua badala ya kusubiri mpaka bajeti nyingine tena ya mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanahitaji sana elimu ya uwekezaji na biashara yaani *Entrepreneurship skills* ili kuweza kuogelea katika mawimbi ya utandawazi na soko huria. Biashara za Kimataifa zinahitaji sana elimu tena ya utaalam.

Tunashawishika kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara hajjaweza kukitumia kwa ukamilifu na mkakati maalum Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) Dar es Salaam na hata Dodoma. Pamoja na kuwepo

kwa muda mrefu tangu mwaka 1965, ni muda muafaka sasa chuo hiki kikapanua mitaala yake ili kuwapa utaalum maalum wa makusudi Watanzania ambao wako tayari katika biashara au wanakusudia kufanya hivyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vingi huwa na wataalam wazuri tu na waliobobea katika fani mbalimbali ambazo kama watatumwa vizuri, huenda malengo kadhaa ya Wizara yakakamilika. Bila shaka Chuo hiki kinaweza kuwa kisima cha utalaam cha Wizara. Cha kushangaza ni kwamba, Serikali haijawatumia watalaam hawa kufanya utafiti (*research*) na pengine kutoa ushauri wa kitalaam (*consultancy*). Hakuna mantiki yoyote ya kuwa na raslimali tunazoshindwa kuzitumia. Hii inaweza kusaidia Wizara kumudu changamoto mbalimbali za kiuchumi na kibashara katika ulimwengu huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kiwe mionganoni mwa Taasisi za kufanya utafiti kwani ni chuo na sio Shule ya Sekondari. *CBE* imelala kiasi kuwa hata katika utoaji wa mada sehemu mbalimbali, haisikiki kabis! Napenda kusisitiza kuwa kama hatutaki kubadilisha fikra zetu juu ya umuhimu wa elimu ya uwekezaji na biashara, hatuna sababu ya kupeana moyo kuwa nasi sasa kama nchi kuna siku tutamiliki uchumi wetu bila kutegemea watu wa nje! (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Sekta ya Biashara na Viwanda kuonekana inakua, Kambi ya Upinzani bado inaanmini kuwa kasi hii ni ndogo sana. Bado haujawepo mkakati wa ndani unaomilikiwa na Watanzania wa kupanua Sekta hizi. Tunaamini kuwa tatizo kubwa hapa ni kukosekana kwa ufahamu na uelewa mpiana yaani *business exposure* mionganoni mwa jamii kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kawaida leo kukuta Wilaya nzima kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi na tano haijaona mradi wowote wa uzalishaji. Hapa nazungumzia miradi mbalimbali yenye angalau mtaji wa Shilingi milioni 200 na uwezo wa kuajiri angalau Watanzania 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefika wakati sasa tukizungumzia biashara kwenye Wilaya zetu tunazungumzia biashara za nyumba za kulala wageni, baa na biashara nyingine za huduma. Biashara hizi kamwe haziwezi kutuingiza kwenye ushindani wa Kimataifa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama haya kudai kuwa viwanda ndiyo Sekta Kiongozi kama ilivyo kwenye Ilani ya CCM kunaleta utata mkubwa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi hauwezi kutegemea Mkoa wa Dar es Salaam pekee kuwa na viwanda au *Tanzania Investment Centre* ngazi ya Taifa. Tunaishauri Serikali sasa isaidie kuweka mkakati utakaowezesha Halmashauri za Wilaya kuwa na mpango maalum wa kiuchumi wa kila Wilaya. Mpango huu utokane na upembusi yakinifu wa maeneo yanayowezekana kuwekeza katika kila Wilaya. Aidha, kila Halmashauri iwe na miradi ya uzalishaji ya kiwango cha mtaji wa katiba ya Shilingi milioni 10 na milioni 100 iliyo fanyiwa *feasibility study* (upembusi yakinifu) ambayo wafanyabiashara Watanzania wataweza kushawishiwa kuianzisha, kuisimamia na kuiendezeza. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa India walipiga hatua kubwa na ya haraka sana katika mabadiliko yao ya viwanda baada ya kuanzisha cottage *industries* zinazotumia teknolojia rahisi (*Appropriate technology*). Miradi midogo midogo ya kusindika chakula, matunda, maziwa, kufuma, kutengeneza yifungo kwa kutumia mifupa, mbao na kadhalika, haihitaji mabilioni ya fedha ila Wananchi wanahitaji uelewa na ushauri. Ni imani yetu kuwa kukiwepo mkakati wenye dhamira nzuri ya kisiasa na uelewa wa mambo hatua hii sio muujiza. Hatujaweza hata kukidhi soko letu la ndani achilia mikakati yetu sasa ya kujaribu kuingia soko la nje! (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu Wizara inazungumzia *EPZ*. Tunakubali ni mpango mzuri, lakini hofu yetu siku zote ni kama kweli mkakati uliopo wa utekelezaji ni sahihi! Kwa mara nyingine tena, mpango wa *EPZ* umetengewa Shilingi milioni 50 kama ilivyokuwa mwaka 2001/2002 na 2002/2003.

Kwa *style* hii ya kutenga kiwango maalum kila mwaka hata pamoja na kushuka kwa thamani ya fedha yetu ikilinganishwa na Dola za Kimarekani, tunamtahadharisha Mheshimiwa Waziri kuwa, maeneo yaliyotengwa kwa EPZ ukiacha Dar es Salaam pekee, yatabakia hivyo hivyo atakapomaliza muda wake wa uongozi kwani sasa hatuna uhakika Mheshimiwa Waziri ana maana gani kwa kila mwaka kusema: "Serikali itaananza," kwani hata wadau wa hayo maeneo yanayokusudiwa huko Mikoani wengi wao hawajui nini kinaendelea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali ionyeshe dhamira kwa kuwezesha wawekezaji wa kati kwa kuwasaidia kuwajengea miundombinu katika maeneo yaliyotengwa. Maeneo yote yaliyotengwa kwa EPZ, basi Serikali iwe na mkakati wa ndani wa kutengeneza *infrastructure* yake, yaani yaweze kuwa *industrial estate*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kusubiri wawekezaji wa nje waje watutengenezee *industrial estates* zetu kama tulivyopata bahati ya kuwapata wenzetu wa *Millennium Park* kule Dar es Salaam. Kwa upande wa EPZ za Mikoani itakuwa ni vigumu sana kupata wawekezaji wa nje ambao watakuwa tayari kuja kutengeneza *Industrial Estates* kama walivyofanya wa *Millennium Park* ya Dar es Salaam. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda siyo mrefu sana, labda nizungumzie kwa ujumla fedha ambazo Serikali inakusudia kwa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii. Fedha za ndani ambazo ndiyo za uhakika ni Shilingi milioni 200 tu. Vile vile, kiwango kama hiki kilitolewa katika miradi ya maendeleo kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha uliopita tuliuokamilisha wa 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni asilimia 13.6 tu ya matarajio ya matumizi ya maendeleo. Asilimia 86.4 sawa na shilingi bilioni 1.6 zilizobaki kwa mipango ya maendeleo zinategemewa kutoka kwa wafadhili. Huu ni msingi wa hatari kama kweli tunaheshimu Wizara hii na jukumu zito ililokabidhiwa la kuongoza uchumi wa nchi! Itakapotokea wakopesaji wa nje wakakataa kutusaidia fedha hizi, tafsiri yake ni kwamba Wizara hii haitakuwa na mradi wowote wa maendeleo kwa sababu itakuwa haina fungu na wakati huo huo tunategemea kwamba Wizara hii sasa iwe ni Wizara Kiongozi wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyosema awali, utafiti wowote ni shughuli ya maendeleo na siyo ya uendeshaji. Kama Taasisi za Utafiti zimepewa mgao wa ndani wa mfano: *TIRDO* Shilingi milioni 25 tu kwa mwaka, *TBS* Shilingi milioni 25 tu kwa mwaka, *TEMDO* Shilingi milioni 15 na *CAMARTEC* Shilingi milioni 15, ukweli utabaki kuwa kwa mgao huu utafiti utakuwa vigumu mno kufanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika matumizi ya kawaida ya Wizara, mgao wake wa fedha kwa mwaka huu umepunguzwa tena wakati uchumi wetu tunaambiya na tuna imani umekua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya yote, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa Wizara hii inanyimwa uwezo wa kuijendesha na kusimamia uchumi kikamilifu na kwa msingi huo basi, tuna sababu zote za kumhurumia Waziri, Naibu wake na Watendaji wote chini ya Wizara hii kuwa na mwaka mwingine mgumu wa kusimamia Sekta hizi muhimu za kiuchumi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hayo yote, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wetu ni ule ule. Kwa leo tunao wachangiaji wawili ambao hawajachangia kabisa na kuna wengine sita ambao wamechangia mara moja tu.

Kwa hiyo, kwa kuanza wataanza wale ambao hawajachangia kabisa. Ataanza Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, atafuatia Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, ingawa simuoni. Baada ya hao atafuatia Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, ambaye amechangia mara moja tu. Halafu watafuatia Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Wengine nitawataja kadri muda unavyokwenda. Kwa hiyo, sasa kwa kuanzia namwita Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Vile vile, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Viwanda na biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza katika sehemu kuu tatu na naomba niende moja kwa moja mpaka katika suala zima la uzalishaji wa sigara hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kuna Kiwanda cha Sigara. Kiwanda hicho kimebinafsishwa, lakini Serikali inategemea kupata hisa au kupata fedha kwa asilimia 25. Jambo la kusikitisha ni kwamba, hivi sasa kumetokea mtindo wa kuleta sigara kutoka nje kwa njia ya magendo. Sigara hizi zinatokea Kenya, Uganda na sehemu nyingine za jirani. Jambo hilo linaipunguzia Serikali yetu mapato, kwa sababu sigara hizi haziletwi kwa mpango unaokubalika, zinaletwa kwa njia ya magendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii na Serikali kwa jumla ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutatua tatizo hili. Kwa kuwa hizi sigara zinapitishwa katika mipaka yetu ya Tanzania, ingekuwa vema wale wanaolinda katika mipaka hiyo, wahakikishe kuwa sigara hizo haziletwi. Wangezileta kwa njia inayokubalika nisingekuwa na matatizo na jambo hili, lakini tatizo langu ni kwa wanaoleta sigara kinyume na Sheria wakati Serikali haipati mapato kwa mpango huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu kiwanda cha *UFI*, Dar es Salaam. Kiwanda kile kilikuwa kinatuingizia fedha za kutosha, kilikuwa kinazalisha majembe, *mapauro* na vifaa vingine ambavyo vilikuwa vinatusaidia katika shughuli zetu hapa Tanzania. Labda Mheshimiwa Waziri atakapo-*windup* atupe maelezo ya kutosha kwa sababu suala hili nilikuwa nimeishalieleza kule kwenye Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara, lakini kusema kweli sikupata ufanuzi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup* anipe sababu za msingi ni kwa nini kile kiwanda kimekufa, siyo kimefariki kwa sababu kiwanda hakifariki, anayefariki ni mtu! (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kikifa, unaweza ukakifufua. Nataka kujua kwa hiki kiwanda cha *UFI*, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kinafufuliwa ili baadaye kiweze kuzalisha na Watanzania tulio wengi tuweze kuneemeka? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi bei ya majembe ni mbaya sana. Ninaamini kwamba kama kile kiwanda kitafufuliwa, bei ya majembe itashuka na bei ya mapauro pia itashuka. Kwa misingi hiyo, Serikali itapata chochote na Wananchi watapata chochote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nichangie kuhusu suala la Kiwanda cha Urafiki. Mimi ni mionganini mwa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Hivi karibuni tulitembelea kwenye kile Kiwanda cha Urafiki, ni kiwanda kizuri na uzalishaji ni mzuri. Inavyoonekana, kile kiwanda tumefanya ubia na ndugu zetu wa Serikali ya Watu wa China. Lakini cha kusikitisha, wale Viongozi wakubwa wote wanatoka China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwenzangu mmoja alikuwa akiongelea hili suala. Watanzania walioko pale sifirkii kama wana nyadhifa zozote! Nasema hivyo kwa sababu wakati tulipokuwa tukipewa maelezo, pale aliyekuwa akitoa maelezo hayo ni Mchina! Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, Mchina huyu hajui kuongea Kiswahili, wala hajui kuongea Kiingereza! Yeye kazi yake ni kuongea Kichina tu! Kuna Mswahili mwenzangu mmoja ndio anatafsiri kwa Kiswahili, hatuna uhakika kuwa yanayosemwa ni ya kweli au si kweli! (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo kile kwa kweli sikupenda hata kidogo! Ingekuwa vema kama Kiongozi wa juu mmoja angetoka China na mwingine akatoka Tanzania. Lakini cha kushangaza zaidi hata yule anayeshughulikia miradi, pengine anatoa khanga kupeleka Zanzibar, pia ni binti wa Kichina! Sasa nikajuliza, hivi sisi Watanzania hatuna uwezo au ni vipi? Lakini kubwa zaidi katika kiwanda hicho, kwa maelezo niliyonayo, basi na unyanyasaji wa watu wetu (Watanzania) inaonekana upo! Napenda kusema kwamba itabidi tujitahidi ili tuweze kujirekebisha katika kiwanda hicho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kwa maelezo tuliyoyapata siku ile, tuliambiwa hakina faida yoyote inayoingiza Tanzania. Sasa, nilikuwa najiuliza, hivi kiwanda kile ni cha nini? Kama hakuna faida inayoingia ni kwa nini tuendelee kuwa na kiwanda kile? Ninaiomba Serikali ikae, ifikirie na itafute njia ya kupata faida. Hatuwezi kufanya biashara ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haipati faida. Hii itakuwa ni sawa sawa na kazi ya Pwagu na Pwaguzi! Najua Pwagu na Pwaguzi maisha yao yote walikuwa hawapati faida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuititia Kiwanda cha Urafiki, tuhakikishe kuwa Serikali yetu inapata faida ya kutosha. Vinginevyo, tufanye njia nyingine yoyote, lakini kile kiwanda kisiwe mikononi mwetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hilo ni suala la mwisho, lakini kuna la mwisho kabisa kabisa sasa. Juzi nilipokuwa nikitembelea pale Sabasaba, viwanja vya Mwalimu Nyerere, tulikutana na wataalam waliokuwa wanatengeneza mwani. Mwani unazalishwa na wakulima wadogo wadogo wakiwemo na wazalishaji wa Jimboni kwangu wa Mkanyageni Pemba. Watu wale walitoa maelezo, wakasema kwamba huu mwani unasafirishwa kupelekwa nje ya nchi, ukishapelekwa huko kuna mafuta yanayotoka ndani ya mwani, basi yanatengeneza *colgate*. Najua kwamba Watanzania wengi wanatumia *colgate*, ni kwa nini sasa Serikali haina mpango wa kujenga kiwanda ili yale mafuta yakapatikana hapa yatumike kutengeneza *colgate* badala ya kuagiza mafuta kutoka nje, kwa mwani ule ule tunaozalisha hapa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ijithahidi kufanya utafiti ili kama kuna uwezekano wa kujenga Kiwanda cha Mwani, Tanzania tuweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa sitakuwa na mengi ya kusema, lakini madukuduku yangu yalikuwa ndio hayo. Sitaki nipoteze muda mwangi, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika Wizara hii ya Viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninamtakia kila la kheri Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu wake pamoja na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpungeza Mheshimiwa Waziri kwa uchapakazi wake mzuri na kwa uchangamfu ambao hata mimi mwenyewe naupenda. Nikiingia ofisini mwake, huacha shughuli zake kwanza, yes, utaona kwamba huyu anafanana na Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mzuri ana Majimbo mawili. Jimbo la kwanza ni Wabunge wanapoingia ofisini kwake na Jimbo la pili ni kule kwake anakowakilisha. Sasa Mawaziri wengine wenye jeuri, basi wana Jimbo moja, lile lile la kwao. Lakini hao hatunao, kama wamo, basi binafsi sijafika kwao. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuelezea hapa kwamba, upo uwekezano wa uingizaji bidhaa zinazoharibu viwanda vinavyolipa kodi. Hii ni hatari! Mfano, Kiwanda cha Sigara kinachotengeneza sigara wanazoigiza nembo ya *sportsman* na *SM* ni baadhi tu kati ya matatizo ya viwanda vyetu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuelezea suala hili kwa upana zaidi ili liweze kuelewaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hao wanaiingizia Serikali fedha, sasa kama kuna wengine wanaoingiza kiujanja ujanja, wapi mambo hayo yanafanana katika nchi hii! Ni lazima tuue ile mianya inayoingiza bidhaa hizo. Unapokuta wenzako wanalamamika, basi ujue ipo sababu ya msingi na tunaomba Waziri ajaribu kulielezea kwa undani kweli suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hicho cha sigara kitakuwa kinapoteza mabilioni ya fedha kama hakutakuwa na udhibiti maalum wa kuzuia hii mianya ya sigara zinazotoka nchi za nje *kinyemela*

*nyemela!* Hao wawekezaji wanaruhusu vipi mambo hayo? Hizo leseni haramu zinatoka wapi? Hakuna mpangilio wa udhibiti!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itakuwa inaashiria kwamba ndani ya utendaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara wako watu wanaohusiana na watu hao. Pia, ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ndiyo wanaweka watu mipakani ili kudhibiti suala hilo, lakini wapo watu amba si waaminifu na wanasaidiana nao! Kwa hiyo, Serikali itakosa mapato na wale wenye hivyo viwanda watafunga, sasa wakiishafunga tutafanyaje? Naomba ufanuzi katika suala hili ili tuweze kuerekana na migongano ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, si mara moja tumeshakutana na watu hao wakiwalalamikia Wabunge kwamba jaribuni kulisemea hili. Si Mbunge mmoja, huyo aliyetangulia wala siyo tu mimi, karibu robo tatu ya Wabunge tunalo tatizo hilo. Sasa kama tunalo, hebu Serikali na Wizara inayohusika jaribuni kulinda kitu hicho. Kama mlikuwa hamfahamu, sisi tunafahamu na *datas* tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba Wizara hii ya viwanda na biashara inisaidie katika suala hili. Mfano, mfuko wa sementi inayotengenezwa Dar es Salaam, ukifika Kigoma mpaka kule Kijiji ni nakoishi unauzwa shilingi 20,000/= yaani ndivyo ilivyo! Mtu akijenga nyumba Dar es Salaam kwa shilingi 4,000,000/= au shilingi 5,000,000/=, Kigoma utajenga kwa shilingi 10,000,000/= au zaidi. Kwa bahati mbaya tathmini hii inaonyesha kwamba Mikoa ile iliyoko pembezoni kwa umbali imekuwa *disadvantaged* kwa suala hili. Mabati gharama, nondo gharama na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulimwambia Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba, ukitoa shilingi 3,000,000/= au shilingi 5,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Kijiji, kule Kigoma Kaskazini fedha hizo hazitoshi, zinatosha kwa Dar es Salaam tu! Kule Kigoma ukipeleka *material* yanayolingana kujenga Shule/nyumba kama hiyo kwa Dar es Salaam, haitakuwa shilingi 3,000,000/= itakuwa ni shilingi 8,000,000= (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Serikali ni uwiano, naomba iweke ruzuku. Gharama ya mfuko wa sementi kwa Mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa ni ghali. Mikoa iliyoko mbali na ambako kuna matatizo Serikali igharamie kwa sababu wale watu nao ni walipakodi. Ukiacha sera hii, ina maana kuna miaka ambayo watu wa huko watashindwa kununua hata huo mfuko wa sementi kwa sababu hii bei ni kubwa, bei hiyo niliyokwambia ya shilingi 20,000=. Bandari la bati ni zaidi ya shilingi 100,000=. Kwa sababu vyote vimeandikwa kwa bei ya Dar es Salaam tu, sasa wote tutahamia Dar es Salaam! (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba, je, huo Mji wa Dar es Salaam unatutosheleza. Kule Kigoma nako wakae watu. Kwanza na ye ye ameshawahi kukaa Kigoma, anapajua. Huwezi kusema kwamba sera hiyo unaweza ukaiacha. Ilikuwepo na ilikuwa inasema kwamba: "Kama viwanda vimejengwa mahali fulani, vihakikishe kwamba bei ya mpaka Mkoa fulani haitaachana sana." Sasa huko tunaenda kama kuku wa kienyeji ambapo mtu anasema kwamba: "Hawa nawamiliki," kumbe wanajitafutia chakula wenye huko wanakokwenda! Wakirudi wameshiba, anafungua mlango wanaingia, wanakaa. Hivi ndivyo tunavyoanza kuishi Watanzania wa sasa! Unaona hawa namna gani? Ninachokiomba hapa ni sera ya uwiano kuwa sawa, siyo tuachane kwa kiwango cha namna hii. Hii inasikitisha sana! Naomba suala hili liweze kuwekwa bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ubinafsishaji ambao tumebinafsisha, binafsisha, binafsisha, tunaenda tu. Sijui mmepesta shinikizo gani, yaani mmebakira twende, twende wote humo kwenye kapu ya kubinafsisha! Hakuna hata kutafakari vitu vingine na sisi tukaona kwamba: "Hiki basi kibaki kinalelewa na Serikali." Sasa hivi kuna usemi wanasesma: "Mpaka ifikapo mwezi wa 12 mwaka huu, kila kitu kiwe kimebinafsishwa, mambo yote yaye yamebinafsishwa." Itabaki Benki Kuu tu basi, yenewe hiyo ndiyo msalaba huwezi kugusa huko!

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji kuna mahali umefaulu na kuna mahali pengine bado, Serikali inahitaji kuweka nguvu halafu watu wapewe tathmini kwamba: "Sasa nyie hapa lindenii huu mtaji." Vinginevyo, tutakosa hata ajira. Ndiyo maana mnaona haya yanayosemwa hapa kwa sababu ya kuleta wagoni kwa kipindi kirefu kwamba ndio wawekezaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, manyanyaso yaliyopo huko ni makubwa, huwezi kuamini. Sitaki hata mtoto wangu akafanye kazi huko kwenye hao waliobinafsisha. Hapana, atafanya Serikalini, kazi ya Ualimu au Uganga, kwa sababu najua hamtabinafsisha Waganga au alime tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asiente kufanyakazi kwa hao makaburu, wala hawana nidhamu bwana yaani mtu anakuwa ni mnyonge kweli. Hao wafanyakazi wa Benki ya NBC huko ni wanyonge tu na kwingine wanakotarajia kwenda ni wanyonge tu, hakuna amani wala raha na furaha. Wewe unaishi katika nchi kwa sababu ni mfanyakazi, huna furaha na amani, wapi Mtanzania wa sasa tunayemtaka ajikomboe katika karne hii ya 21. Hapana, hiyo si sahihi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile viwanda ambavyo vitabinafsisha, lakini bado wakati wake haujafika viimarishe. Pale Uvinza katika kile Kiwanda cha Chumvi unyanyaso ni asilimia 250. Nenda ufuatilie na uwaulize. Kwanza wanalipa pesa kidogo sana, isiyolingana na hicho wanachokifanya. Wewe unaweza kukaa na jamii ya aina hiyo! Hata wale amba walipunguzwa mpaka leo pesa zao hawajapata! Naomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ili hizo fedha tuondoke nazo tukawapatie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alimbiwa suala hilo. Pia, Bwana Mangula hilo aliambiwa. Sasa, tusiendelee kuambiwa, hii ni haki yao. Haki zao hawajapewa mpaka leo, watamaliza miaka mingapi? Lakini wewe ukiondoka hapa marupurupu yako yote unaondoka umebeba! Wengine walikuwa hapa hawaajaondoka na pale Urafiki wengine hawaajaondoka, bado wanadai! Sasa tutaendelea kudaiwa katika Taifa hili, mwelekeo ni upi? Hebu tusidaiwe mambo ya namna hii! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine unaweza ukawa umeelezwa yakaleta uchungu sana.

Naomba tufikie hatua twende kwamba hiki tumemeliza na hiki tumemaliza. Sasa, wale wote wanaodai marupurupu yao na kusafirishwa mpaka nyumbani kwao mwisho ni lini? Waziri wa Viwanda na Biashara atakaposimama hapa ku-*windup* atuambie mwisho ni lini ili tuweze kupata taarifa sahihi au kama Waziri wa Fedha hana fedha, basi tuwaambie wasubiri na kama wanasubiri wapeni haki zao zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akifanya kazi kwa uaminifu ametumikia taifa hili, anafanya kazi leo hana posho yake ya kuweza kumfikisha huko anakaa anadai akimwona Mbunge, asubuhi mchana, asubuhi mchana, wewe unaweza hiyo kazi? Naomba kwa heshima zote nakuamini Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, ni mchapakazi mmoja mzuri na mwenye nguvu, nafikiri utajibu kikamilifu haya yote yanayolalamikiwa katika Wizara yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo katika Wizara hii. Kwanza napenda kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Kwa hiyo, ninayoyasema hapa nataka kuweka msisitizo kwenye baadhi ya mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri ambayo ina takwimu muhimu, ambayo ameisoma kwa ufanisi mkubwa sana, hotuba yake ni kubwa lakini yale yote ya muhimu ameweza kuyasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la fursa ambazo tunazipata kwa mfano fursa ya *African Growth and Opportunity Act (AGOA)* pamoja na *Everything But Arms (EBA)* ambayo ilikuwa kwenye Taarifa ya Kamati. Sisi naona tumechelewa. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba hii kazi kwa kweli si kazi ya Waziri wa Viwanda na Biashara peke yake, ni kazi ya Wizara wa Fedha, Wizara ya Ushirika na Masoko, Wizara ya Mipango na Ubinafshaji, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Kilimo na Chakula. Kwa sababu Wizara hizo baadhi zinahusika na sheria na taratibu za mauzo ya nje. Baadhi ya

Wizara hizo zinashughulika na kuhimiza kilimo na ufugaji ili mazao hayo yatumike kutengeneza bidhaa iliyo kamilifu hapa nchini ili tuuze zilizokamilika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati yangu ilitembelea viwanda mwezi wa tano. Kwa kweli ni kitu kinachoudhi, mtu ananunua kiwanda na mkataba amesaini, asafishe ngozi, zikamilike tutengenezee bidhaa hapa hapa nchini lakini kiwanda kimefungwa. Hivi fursa hii kweli tutaitekeleza? (*Makofî*)

Pale Moshi kuna kiwanda cha bidhaa za ngozi kina ufanisi wa hali ya juu kabisa. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Dr. Juma Ngasongwa kwa kutuwezesha kwenda kwenye maonyesho. Watu wengine walishangaa ni kwa nini tumekwenda tarehe 8 hatukwenda tarehe 2. Haja yetu ilikuwa tuone bidhaa zilizotengenezwa hapa nchini. Kama wale walionazo wamezionyesha na wameuza. Tusipokuta hata bidhaa moja tunashukuru kwamba bidhaa zetu zinauzika. Kwa kweli kwenye kiwanda cha kutengeneza ngozi, tumeona wametengeneza hizi *travel bags* za kuchukulia suti. Kama ingewekwa *label* iandikwe ya *Maxensensor* pesa huulizi utanunua kwa bei ya *Maxensensor*. Lakini wanapata matatizo ya ngozi. Hizi ngozi zipo hapa Tanzania lakini inabidi wazinunue kutoka nchi jirani waje watengeneze bidhaa za ngozi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Mifugo na hawa wengine niliowatajaa kwa kweli hivi viwanda vifufuliwe wakishirkiana na Waziri wa Viwanda na Biashara kwa sababu ni kitu kinachoudhi sana. Ngozi za kwetu halafu ziuzwe nje ya nchi, halafu tuzilete tutengeneze bidhaa tuuze tena nje ya nchi. Kwa hiyo, gharama itakuwa kubwa. Kwa hiyo, bidhaa zetu hazitauzika. Nilitaka nilizungumze hili na ningependa kueleza kwamba sisi tumechelewa kuchukua hii fursa ya *AGOA* na *EBA*. Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara nchi ambazo zimekwishanufaika sasa hivi ni Kenya, Madagascar, Malawi, Mauritius na Swazilandna nchi ya Lesotho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lesotho ni nchi ndogo lakini katika muda mfupi wamejenga viwanda 11 vya *textiles* na kuongeza nafasi za kazi 50,000, kwa sababu soko lipo tayari kwa utaratibu wa *AGOA*. Wamarekani wenye we wamefanya *assessment* mwaka 2000 bidhaa za kutoka eneo hili zilikuwa ni asilimia 1.5 ya bidhaa zote zinazoingia Marekani. Lakini kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa hivi hizi nchi nilizotaja hapo juu zimeshaongeza asilimia kuffikia asilimia 3.5 hizi *data* ziko katika *Gazeti* la *African Business* na *title* ya haya maelezo hapa Wamarekani wanasema *The begging have a beautiful relationship, USA new approach to Africa*. Sasa mimi nadhani tujitahidi tufufue hivyo viwanda tutengeneze bidhaa hapa hapa nchini ili tuweze kuuza nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna utaratibu sasa hivi mimi kwa kweli unanipa wasiwasni sana. Tunawavusha wawekezaji hapa nchini wa kuja kuwekeza kuuza bidhaa za kutoka nchini kwao. Tunawakubali wawekezaji kuja hapa nchini kufungua *super market* za kuuza bidhaa za nchini kwao. Tunaomba Serikali itazame hili. Kama wanataka kuwekeza wawekezaji kwenye uzalishaji ndiko tunakotaka zaidi. Lakini hii biashara hata Wamachinga wataweza kuifanya hii ya kuuza humu humu nchini (*Makofî*)

Lakini mtu anaipa *strategic investor* anakuja kuwekeza kuuza bidhaa za kutoka nchini kwao, anapiga vita bidhaa zetu kwa sababu hatutashindana kwa sababu kule kwao wamepewa nafuu bidhaa zile ziingie kwa bei ndogo halafu ziuzike kwa bei ndogo hapa nchini na za kwetu zizalishwe kwa gharama kubwa na tusiziuze, tusiweze kuzisafirisha kutoka nje. Siyo kwenye nguo tu bali na bidhaa mengine hasa magereji. Jamani hizi gereji ndogo za kupiga rangi kweli anahitajika *strategic investor*? Kazi ya kutengeneza magari yaliyogongwa gongwa na *panel beating* ni *strategic investor* huyo kweli? Kazi hizi zipo Dar es Salaam tunaomba Serikali hili suala ilichukulie hatua inayostahili kwa kweli. Kama sheria yetu ya uwekezaji ina matatizo tuikebishe. Lakini sidhani kama *garage, super market* ni *strategic investors* hawa, *no*.

Hizi kazi zingefanya na Watanzania. Uwekezaji upo kwenye maeneo mengine makubwa, kwa mfano kwenye madini, kwenye mashamba makubwa na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, tulitazama sana hili. (*Makofî*)

Pengine kuna wakati tunaonyeshana vidole kama sisi wenyewe tunahusika na hizo, kwa hiyo tutashindwa kuzisema hizi hapana. Basi nadhani tuijweke pemberi tuwapishe watu wengine wafanye hizo kazi kuliko kuchafua uchumi wa nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Hamis Awesu Aboud, tuko wako kwenye Kamati, alizungumzia suala la sigara za pandia. Tatizo sulala la bandia kwa sababu hatuna uhakika na viwango vyake, lakini wametumia majina ya sigara zetu hapa *SM* na *Sportsman* zimeingizwa katika soko. Napenda kumshukuru sana Dr. Juma Ngasongwa, kwa sababu tuliletewa hizo sisi hapa Bungeni na wananchi ambao wana uchungu na nchi hii wakasema chukueni hatua zinazostahili, tukaenda kwa Waziri tukamwambia hilo tatizo.

Nashukuru alichukulia hatua kesho yake iliandikwa kwenye magazeti. Sasa tunataka utekelezaji wa namna hii sisi tutasaidia Serikali kama tunaleta kitu, kinachukuliwa hatua haraka. Lakini kama unapeleka kitu unaambiwa tutatazama *and no action* tutashindwa. Kama walivyosema wenzangu kwa kweli tuwe na ushirikiano na Wizara nydingine. Lakini Wizara nydingine iwe ni jukumu lao, polisi kule mpakani ni jukumu lao siyo jukumu la Waziri wa Viwanda, *TRA* ni jukumu siyo jukumu la Waziri wa Viwanda peke yake na wananchi vile vile ni jukumu lao kama wanaona mahali pengine pana ubovu ubovu watutumie hata sisi Wabunge wao kama walivyofanya wale walioleta sigara hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumza Dr. Juma Ngasongwa, ameingia Wizara hii ana bahati nzuri sana. Mpira wa kutengenezea *tyre* ulikuwa unalimwa Muheza, kulikuwa na shamba chini ya *General Tyre*. Lakini *General Tyre* tukawaambia acheni hiyo kazi ya kulima mpira, mpira tutanunua kutoka Malasia na Indonesia. Shamba likaachwa, linataka kuuzwa kwa mtu binafsi. Hakuna ongezeko lolote kulikuwa na hekta 700 zimetengwa, lakini zilipandwa mpira ni hekta kama 300 tu hivi. Sasa wakati ule kulikuwa na tatizo kwa sababu waliokuwa wanaongoza kiwanda pale *management* wanatoka nchi zilizoendelea na wana mikataba yao ya kununua mpira kutoka kwenye *source* hizo wanazijua wana mikataba nazo.

Kwa hiyo, hawakuchukua hatua ya kupeleka mpira ule ukapimwe na kupewa kiwango ukakubalika. Lakini Meneja Mkuu aliyeo pale tena ni kijana mdogo tu, lakini ana heshima kweli, walimtisha walimwambia *Chairman* yule ni mkali sana huwezi kufanya naye kazi. Nilikaa naye kwa siku nzima nikamwambia hapana, mimi nataka *performance, if you perform, you will be my friend, if you don't I can go.* (*Makofî*)

Yule kijana anatoka Nepal nchi inayoendelea, ametumia juhudhi amepeleka mpira *Continental General Tyre* umekwenda kupimwa. Yeye anatoka nchi inayoendelea, waliokuwepo *management* walikuwa wanatoka nchi iliyoendelea. Kwa hiyo, mpira ule ukawa *condemned* kwamba haufai. Amekuja huyu kijana *no thank you* kwa sababu mimi najua mpira unaofaa huu mpira ni mzuri wakutengeneza *tyre* mpira wa Muheza ni mzuri sana wakapeleka ukapimwa umepata *International Recognition*. Kwa hiyo, tumeongezewa zao lingine la biashara. (*Makofî*)

Naomba Wizara ya Kilimo na Chakula na sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga tulime mpira, mpira hauna kazi kubwa ya kuendeleza kuutunza na ukishaulima katika miaka 4, 5 unavuna. Sasa *version* ni 20, 25 iko *within* hiyo, mtu mwininge anasema kwa nini tuanze upya tuhangaike na hivyo tulivyokuwa tunavielewa?

Kwa hiyo, mimi naomba sana tushirikiana. Hii kazi siyo ya Waziri wa Viwanda wa Biashara, inamhusu Waziri wa Kilimo na Chakula na sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, upo ehee! Nadhani utazungumza baadaye maana iko kwenye jimbo lako. Mali iliyoko pale inakidhi mahitaji chini ya asilimia 10 tu ya mahitaji ya utengenezaji wa tairi pale *General Tyre. Continental tyre from the Africa* wamesema fanyeni kazi mlima huo, mpira tutaagiza mahali pengine tutauununua. Kwa hiyo, soko lipo tena zuri. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka niongeze haya ili kuboresha taarifa yetu ambayo ilisomwa na Mheshimiwa Salome Mbatia, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Lakini nataka kuongeza moja kwamba mpira vile vile unalimwa Kilombero. Kwa hiyo, wenzetu wa Mkoa wa Morogoro kuna mapori, soko lipo, hata Zanzibar mpira unalimwa soko liko. Kwa hiyo, tufanye hii kazi ya uzalishaji. Hii habari ya kuingiza watu wanaokuja kuuza nguo za nchi yao kwa kweli linaudhi sana. Sisi wacha tuwauzie mpira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga tena hoja hii mkono kwa nguvu zaidi. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia leo katika hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Watendaji kwa hotuba yao nzuri. Kwa kweli hotuba hii ni nzuri sana. (*Makofî*)

Lakini nitaanza alipoishia Mheshimiwa William Shellukindo kwa habari ya shamba la mpira. Kwanza namshukuru sana kwa kuanza kutanguliza kusema hilo na kwa bahati nzuri mimi pia ni mjambe katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambapo tulipata nafasi pia ya kutembelea shamba la mpira liliko ndani ya Wilaya yangu ya Muheza. Sasa naomba niipongeze Kampuni ya *General Tyre* kwa jitihada ambazo wamefanya kuweka mpira wa Muheza katika chati ya dunia. Kwa kweli mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, tumekwishapanga mkakati wa kwenda nyumbani na kuhamasisha wananchi wetu waweze kulima mpira sasa kwa jitihada na kwa nguvu zote kwa sababu bei ni nzuri, maeneo tunayo na soko ni kubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipotembelea katika shamba hili la mpira kama alivyosema mwenzangu kuna kiasi cha hekta 318. Lakini kuna tatizo, lakini tatizo hili sasa inabidi tulizungumze vizuri, kwanza ni kujua wajibu na uwajibikaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Ukiangalia kwamba ubinafsishaji unafanywa na Wizara nyingi PSRC. Sasa baada ya PSRC kumaliza kazi yake ya ubinafsishaji wajibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda ni kufuatia na kufuatalia makampuni na viwanda hivi ambavyo vimebinafsishwa kuona *performance*, kujua nini kinachofanyika na kutoa taarifa pale ambapo kwa kweli viwanda vingine viliviyobinafsishwa vinafanya kazi. Nimefurahishwa kidogo na ripoti ya Mheshimiwa Waziri, ambapo ametuonyesha leo kwamba kuna idadi kubwa ya viwanda ambavyo vimebinafsishwa na vinavyofanya kazi. Zaidi ya vile ambavyo tumekuwa tukisikia tu katika ripoti zote watu wakizungumzia ufanisi wa ubinafsishaji hapa wanazungumzia bia, wanazungumzia sigara wamemaliza. Lakini leo tuna orodha kubwa zaidi ya hivyo viwanda viwili. Namshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri vile vile lazima atazame upande wa pili wa shilingi. Unapozungumzia mafanikio ya viwanda ukavitaja basi ni vizuri ukageuza shilingi na ukatuambia kwamba kweli viro viwanda vingine ambayo vimebinafsisha lakini havifanya kazi. Si vibaya pia ukavitajia ukavijua kwa sababu tumeaita na tumeviona. (*Makofî*)

Tatizo kubwa lililoko katika Shamba la Mpira Muheza ni uongozi. Shamba lile limekodishwa kwa mara ya kwanza kwa Msomali mmoja akaenda pale akawafanyisha watu kazi, akakusanya mpira akaenda akaunda, Kenya na baada ya kupata fedha akahama nchi akatoroka, akawaacha wafanyakazi solemba, mpaka leo wafanyakazi hawajalipwa haki zao. Mpaka leo wanadai. Wafanyakazi wamekwenda Mahakamani, baada ya kwenda mahakamani ika-*rule out* kwamba huyu aliyefanya kazi hii amewadhulumu wafanyakazi atafutwe na anawajibika kuwalipa wafanyakazi.

Sasa tatizo liko wapi, Serikali inawageukia wananchi inawaambia ninyi mmeekwenda Mahakamani na kwa hiyo, Serikali haina msaada tena kwenu. Hivi kweli tunataka Watanzania sasa tuanze kufanya maandamano tuvuke mpaka twende Kenya tukamtafute Msomali, Serikali yetu haitaki kutusaidia, hivi kweli tufanye hivyo? Hapana.

Mimi nadhani bado Serikali inawajibika kwa sababu aliyemleta mwekezaji pale Muheza ni Serikali, sasa mwekezaji aliyeletwa na Serikali amewatoroka Watanzania leo tunasema Watanzania shauri yenu mlikwenda Mahakamani siyo sahihi. Nafikiri tuwasaidie wafanyakazi wale waweze kupata haki zao.

Hilo ndiyo tatizo moja kubwa la kwanza na nasema kama Wizara ya Viwanda na Biashara inawajibika kufuatilia naomba sasa muisaidie na muishauri *PSRC* na Serikali kwa jumla kuwasaidia wafanyakazi wale kupata haki. (*Makofî*)

Mwekezaji wa pili amekuja baada ya yule wa kwanza kutoroka na ana matatizo yale yale hana teknolojia, hajafanya kazi kubwa ya kuendeleza shamba lile na yeze hana hata orodha ya wafanyakazi wake, hana mpango wa mafao ya wafanyakazi, anawalipa anavyotaka, siku akiamua ataondoka na wafanyakazi nina uhakika watapoteza haki zao. Sasa najua Wizara inayohusika na mambo ya wafanyakazi ni Wizara nyine, lakini pale hakuna mfumo wa ajira ya wafanyakazi, lazima tuwasaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulitembelea Kiwanda cha *chipboard* Mkumbara. Tatizo ni hilo hilo, mwekezaji anajitahidi sana, sasa ana migogoro na wafanyakazi. Hii vile vile hata *sales agreement* bado mpaka sasa miaka mitano imepita haijasainiwa. Hivi mnashawishi vipi mwekezeji huyu kuendelea kuwekeza pale kama ana hofu hata *sales agreement* haijasainiwa, hivi ataendelea kuwekeza? *Chipboard* wanahitaji mali ya ghafi ya miti kutoka Lushoto.

Sasa angalia Watanzania tulivyochanganyikiwa, badala ya kuisaida *chipboard* ambayo mwekezaji wetu amekwishajitokeza na anafanya kazi nzuri, aweze kupata mali ghafi, Watanzania tunavyojisau, tusipo thamini viwanda vyetu, tusivytaka hata kuwasaidia wawekezaji tunatoa vibali kuwapa watu wengine wa nje wanachukua magogo yale, wanayasafirisha kupeleka Kenya kwenda kuwezesha viwanda vile kupata malighafi, tunakiacha kiwanda chetu. Nani anapaswa kumsaidia mwekezaji yule? Wizara ya Viwanda na Biashara, je mmeshafika pale, taarifa tulizo nazo ni kwamba siku nyangi sana hamjafiki. Kwa hiyo, mnahitaji mwende mkawasaidie ili waweze kupata mali ghafi waendeleze uzalishaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika eneo linalohusu viwanda vidogo vidogo. Katika Wilaya ya Muheza na Wilaya nyangi hapa nchini vikundi vya akina mama na vijana vimefanya kazi nzuri sana katika uzalishaji, hasa katika maeneo ya usindikaji wa matunda na maziwa. Vikundi hivi tunaviona katika maonyesho ya saba saba, nane nane. Ni vikundi vizuri sana, nawashukuru sana *SIDO* ambao kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kutoa elimu katika vikundi hivi, *UNIDO* ambao vile vile wamechangia sana na vile vile Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro, ambao wamesaidia sana kuviboresha vikundi hivi. Sasa tumeshatoa elimu, vikundi vinafanya kazi ya uzalishaji na usindikaji, lakini lazima tukubali kwamba kiwango hicho wanachozalisha hawa siyo kiwango kitakachowasaidia hata siku moja kuondoa umaskini. (*Makofî*)

Wanazalisha viwango vidogo, ubora pia wa bidhaa bado siyo wa kuridhisha sana. Tunachotakiwa kuwasaidia sasa ni kuwaondoa katika hatua hii ambayo kwa kweli ni ya mafanikio tuwapeleke katika hatua nyininge kubwa zaidi, hii ni hatua ya kuweza kuwapatia viwanda vya kati vya kisasa vitakavyowawezesha kuzalisha kwa ubora mzuri zaidi. Lakini vile vile kuzalisha kwa wingi kwa kiwango ambacho kitawafikisha mahali wataweza ku-break even na vile vile kuongeza uzalishaji na kuweza kupata faida baada ya kuzalisha. Hii ndiyo hatua ambayo tunawatakiwa kuwaingiza vikundi vyetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ipo sera ya uwezeshaji inasema wananchi kiuchumi sasa tuitumie sera hii. Viwanda vidogo vidogo vya kati sasa hivi Afrika Kusini vinaweza kupatikana kwa thamani ya shilingi milioni 30, uwezo wa vikundi kupata fedha hizo ni mdogo sana. Sasa tujitahidi, kwanza tunachotakiwa kufanya tuunganishe hivi vikundi. Pale Muheza tunavyo vikundi kama sita vya uzalishaji wa usindikaji, tuviunganishe hivi ili vikundi hivi viweze kuwa na nguvu ya kuweza kununua hisa katika viwanda vidogo vidogo tutakavyoanzisha. Lakini tatizo lingine kubwa ni kwamba hawa wenzetu wazalishaji wadogo wadogo hawana elimu ya kutosha ili uweze kupata mikopo au mtaji wa shilingi milioni 30, lazima uweze kuandika mchanganuo mzuri, uwezo huo wanao? Hawana uwezo huo.

Sasa nashauri na napendekeza Wizara ya Viwanda na Biashara iwe na eneo maalum litakalokuwa linasaidia hivi vikundi na biashara ndogo ndogo kuwasaidia kuandika michanganuo ili iwawezesha kupata nafasi ya kuweza kudhaminiwa na kupata mikopo. (*Makofî*)

Baada ya kupata mikopo hawa watu vile vile lazima tujaribu kuendelea kuwasaidia. Watawezaje kuendesha viwanda vidogo vidogo wanahitaji watalaam wa kuwasaidia, wanahitaji elimu kidogo ya

uhasibu ili waweze kujua fedha zao zitatumika namna gani, vile vile wanahitaji utalaam wa masoko. Naomba tuwasaidie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni hati za ubora wa viwango ambalo kwa kweli linawatatiza sana wafanyabiashara wadogo wadogo na viwanda vidogo na vikundi hivi vidogo vidogo ili kuweza kupata hati ya *TBS* lazima ulipie kiasi cha zaidi ya shilingi laki tatu. Vikundi hivi vidogo vidogo vinakwama katika kulipia. Lazima ufuate Dar es Salaam kwa sababu makao makuu ya *TBS* yako Dar es Salaam, wasafiri kwenda huko kwa gharama kubwa. Sasa hivi gharama hizi tujaribu kuwapunguzia, tujaribu kuangalia kama inawezekana *TBS* kupunguza viwango hivi. Nimeambiwa kwamba upo mpango tayari, lakini vikundi vingi ambavyo tumejaribu kuvihoji hawaujui mpango huu, basi tujaribu kuwaelimisha tuwasaidie ili waweze kupata alama za ubora wa viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine kwa haraka ni leseni za biashara ambayo wenzangu wamelizungumzia. Lakini nitalizungumzia kwa kifupi. Sheria yenye ya biashara ukiisoma haina mahali popote inaposema kwamba leseni itatolewa kwa masharti fulani ya utekelezaji wa ulipaji wa kodi nyingine tofauti na ile kodi yenye ya leseni ya biashara.

Sasa tatizo hili linatokea katika Halmashauri zetu karibu zote, ili waweze kutoa leseni ya biashara wanaambia wafanyabiashara kwamba kwanza nenda ukalipe kodi ya mapato, nenda kalipe kodi ya michango ya shule, kalipe kodi hizi, kodi mbalimbali ili aliye kwanza ili aweze kupata leseni ya biashara. Njia hii ndugu zangu inakatasha tamaa sana wafanyabiashara wadogo wadogo kwa sababu inamtaka aliye kodi nyingine nyingi kabla hajaanza biashara na mnafanya hawa watu wafanye biashara bila kuwa na leseni kwa sababu lazima aliye anakwepa kulipa kwa sababu hana fedha hizo.

Kwa hiyo, atafanya kazi bila kuwa na leseni. Sasa tunafaidika na nini hapo? Sheria lazima isimamiwe, sheria haisemi lazima ulipe kodi nyingine ndiyo upate leseni ya biashara. Sasa tutoe leseni za biashara kwa utaratibu mzuri unaokubalika. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimefurahishwa sana na kauli alizotoa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aliposema: "Ingawa kilimo ndiyo msingi wa uchumi, viwanda ndiyo sekta kiongozi." Sasa nasema hii ni sahihi kabisa na hii inapaswa kuwa ndiyo kauli ya kwanza inayojenga mahusiano ya kibiashara. Kwa hiyo, nakubaliana na kauli hii.

Lakini kauli ya pili japokuwa alisema ye ye Mheshimiwa Waziri lakini nasema hii sasa ndiyo kauli ya kiwanda. Kauli ya pili ya kiwanda lazima iseme "Nunua bidhaa za Tanzania tujenge Tanzania." Hii ni kauli ya pili inayojenga mahusiano ya biashara kati ya Serikali, viwanda na walaji. Sasa nini kauli ya walaji? Kauli ya tatu ni kauli ya walaji ambayo inasema hivi "Tunataka bidhaa bora, kwa bei nafuu." Hizi ndiyo kauli tatu zinazojenga mahusiano ya kibiashara kati ya Serikali, viwanda na walaji. (*Makofsi*)

Narudia kauli ya mwisho ya walaji: "Tunataka bidhaa bora kwa bei nafuu." Kwa hiyo, viwanda lazima vielewe ili vitengeneze bidhaa lazima virudi nyuma na viangalie mahitaji ya walaji kwanza. Mlaji anataka nini? Anataka *quality* gani? Je, mlaji huyu atamudu kununua bidhaa hii kwa bei gani? Hii ndiyo maana ya *demand*. *Demand* lazima iangalie na uwezo wa mlaji kuweza kununua bidhaa. Lazima tulenge vile vile kwamba baada ya kukamilisha mauzo yetu katika soko la ndani bidhaa zetu lazima zifikie viwango na hasa ubora wake na ubora huiwi katika *product* yenye, ubora vile vile unapaswa kuangaliwa katika *packaging*, vile vifungashio vya bidhaa zetu lazima vifikie viwango vya ubora vitakavyoweza kukubalika ndani na nje ya nchi, hapo tutakuwa tumeweza kukuza na kuweza kupata soko la nje. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda huu ulionipa. Ahsante. (*Makofsi*)

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri wake na Watalaam wa Wizara hii.

Labda kabla sijaanza mchango wangu naomba *ni-comment* kidogo kuhusu mchango wa Mheshimiwa William Shellukindo alipolezea kwamba kuna baadhi ya nchi ambazo zimeanza kufanya

vizuri katika Soko la *AGOA*. Katika orodha za nchi alizotaja Kenya, Madagascar, Malawi, zote unakuta kwamba bahati nzuri au mbaya ziko katika *COMESA*. Sasa mimi ningependa kuuliza. Je, Tanzania kutokuwa kwenye *COMESA* kunatuweka katika *position gani?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa *SIDO*. *SIDO* imefanya kazi kubwa sana katika mikopo, imesaidia sana akina na nimeona jitihada zao katika kuanzisha *Website* ambayo inatoa taarifa na inatumia hii fursa ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Sasa changamoto ninayowapa watu wa *SIDO* ni kuhakikisha kwamba habari hizi zinawafikia watu wa vijiji, watu ambao kule hawana *access* ya vitu kama tovuti nakadhalika. (*Makofi*)

Vile vile taarifa hizi ziwekwe katika vipeperushi ili basi akina mama, vijana wanaotaka mikopo ya *SIDO* waweze kujua wanatakiwa wafuate masharti gani, wafuate utaratibu gani, waweze kupata hii mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu za pili ninaomba nitoe kwa watu wa *UNIDO* hasa hasa huyu Mwakilishi Mkazi wa *UNIDO* Tanzania. Kusema kweli anajitahidi sana ana nia kubwa ya kuwasaidia Watanzania na akina mama hususan katika kutengeneza vyakula na bidhaa za kusindika na vile vile katika kutoa mafunzo ya ujasirimali.

Nawaomba watu wa *UNIDO* watusaidie katika Sekta hii ya *E. Commerce*. Kenya wenzetu sasa hivi wameanza kuuza bidhaa zao, wafanyabiashara wadogo wadogo wanauzu sandals kupitia *Website*. Kikoi sasa hivi ambacho Pemba kinauzwa shilingi 3,500/= Kenya kinauzwa Dola 20 kupitia *Website*. Ukipungua *Kikoi.Com* utakuta aina mbalimbali za vikoi na rangi zake, ni Dola 20. Kwa hiyo, naomba basi watu wa *UNIDO* watusaidie. Vile vile watusaidie katika hii biashara ya sasa hivi ya kukata na kusanifu tanzanite. Akinamama wako pale Arusha na maeneo mengine ya Mahenge wanaotoa vito ili watusaidie na sisi tuweze kuingia katika hii biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo hautakuwa mrefu, nimejielekeza katika maeneo matatu tu ya muhimu. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu masuala yangu matatu kwa ufasaha na kwa kuniridhisha ili isinipelekee mimi wakati wa kuitisha hii bajeti, nikatoa Shilingi yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze, ni kwa nini viwanda hivi nya kusokota nyuzi, Kiwanda nya Ubungo na kile cha Tabora za pamba havifanyi kazi? Mimi kama wiki mbili zilizopita nilitoka Mauritius na kule tuliveza kutembelea kiwanda kimoja ambacho kinatengeneza masweta na *T-shirts*. Ni kiwanda kikubwa ambacho kina masoko yake Marekani, Uingereza na *European Union* kwa ujumla. Kule tukawauliza, je, mnapata wapi pamba yenu mnayotumia? Wakasema tunanunua Zambia. Nikasema Zambia! Zambia wana pamba gani? Kwa nini hamchukui Tanzania?

Sasa nikaambiwa sisi hatununui pamba, tunanunua nyuzi. Wakasema, kwa hiyo chukua hii *business card* yetu, nenda kawapelekee wanaohusika na kutengeneza hizi nyuzi wawasiliane na sisi tuweze kuwapa *order*. Tanzania sisi viwanda vyetu viwili ambavyo vingekuwa na *potential* kubwa ya kuweza kupata soko hili la Mauritius sasa hivi Hatuwezi ku-take advantage kwa sababu viwanda viwili vyote vimfungwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ana mikakati gani, ana mipango gani ili viwanda hivi vifanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka kuzungumzia kuhusu udhibiti na ukaguzi wa ubora wa bidhaa. Naomba Waziri aniambie kwa nini bidhaa nyingi zinazozalishwa katika viwanda vyetu hapa Tanzania havina ubora unaoridhisha? Pamoja na mbwembwe nyingi wakati wa Maonyesho ya Biashara, utakuta Jeshi la Magereza linatengeneza *furniture* ya mbao inang'aa utafikiri kioo, utakuta JKT wanaonyesha mboga zao kama ni tungule utakuta kubwa kama kichwa cha mtu. Lakini baada ya maonyesho hautaweza kuona bidhaa tena kama hizo kwenye soko lolote hapa Tanzania. Sasa kama hatuna ile *consistence*, kama hatuthamini ubora tutaweza kufikaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano, khanga hii imetoka Kiwanda cha Tanzania. Khanga hii nimeinunua katika kiwanda cha Tanzania. Khanga hii nilinunua doti 150 kwa ajili ya kuwapa akinamama kuhamasisha Sensa. Kati ya doti 150, doti kumi zilikuwa ni za hali duni ya namna hii.

(*Hapa khanga husika ilionyeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge*)

**MHE. DR. BATILDA S. BURIANI:** Sasa naijuliza, je, khanga hii iliwezaje kutoka Kiwandani mpaka ikanifikia mimi mlaji au mtumiaji bila kupita katika zile *inspection na process* zote? Je, kwa nini kiwanda kama hiki kiendelee kufanya kazi kama kinaweza kuzalisha bidhaa ya hali duni kama hii? Je, bidhaa ya ubora wa hali hii, Tanzania tunaweza kufurukuta katika Soko la *AGOA*? (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. DR. BATILDA S. BURIANI:** Je, *TBS* inafanya kazi gani kama tunaweza tukafikisha kwa mlaji bidhaa ya hali kama hii? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la tatu na la mwisho, naomba Wizara au Mheshimiwa Waziri anieleze, je, ni kwa nini mpaka sasa hivi *Water Guard* bado zinauzwa madukani? Waheshimiwa Wabunge tulipiga kelele, Serikali ikawa sikivu, Wizara ya Maji, Wizara inayohusika na Afya wakaamua kuzuia bidhaa hiyo isitumike kwa ajili ya matumizi ya watu na wala isiuze. Lakini mpaka sasa hivi *Water Guard* zinauzwa madukani na bado wanatengeneza.

Sasa nilitegemea Wizara ya Viwanda na Biashara ingewafanya watengenezaji wa *Water Guard* wazirudishe bidhaa zao zote zilizoko kwenye maduka yote waweze kusitisha utengenezaji na hata waliotumia kama ingeweze kana waweze kuwalipa fidia, kwa sababu watakuwa wameathirika. Sasa Wizara ya Viwanda na Biashara hajafanya lolote, mimi nimekuta *Water Guard* madukani kote zinauzwa mtindo mmoja kama vile hakuna chochote kilichosemwa hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba kwa haya masuala yangu, mimi sitakuwa na msalie Mtume, naomba njibewe vizuri. Japo naunga mkono hoja sasa hivi, lakini kama sitapata majibu ya kuridhisha, basi mimi nitazuia shilingi yangu huko mwisho. Nashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu na niweze kuwahi kwenda Msikitini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenyeye sura ya mwelekeo wa kuondoa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitazungumza kidogo kwa kuunga mkono masuala waliyozungumza wenzangu kuhusu mpira. Kwa kweli eneo la Ukanda wa Pwani lote, zao la mpira linastawi na ushahidi, Kilwa lipo shamba toka wakati wa Mjerumanî, linaitwa shamba la Iyungi na mpira upo. Kwa hiyo, namshukuru ndugu yangu Mheshimiwa William Shellukindo, aliyenikumbusha hilo, nitakwenda kulifanyia kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze katika eneo la Kiwanda cha *TWICO*. Kilwa kulikuwa na Kiwanda cha *TWICO* ambacho kimeuzwa mwaka 1994. Kwa masikitiko makubwa, kiwanda hiki kimeuzwa kwa pesa ndogo mno, kwa shilingi milioni 12. Ndani ya kiwanda hiki kulikuwa na gari mbili isuzu na nyumba, majumba ya wafanyakazi. Nikisema nyumba sio moja, majumba ya wafanyakazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki kimeuzwa kinyemela, sisi wazawa hatukutangaziwa. La kusikitisha zaidi, wale wafanyakazi mpaka leo hawajalipwa na huyu aliyenunua kiwanda hiki ametoa mashine zote na kiwanda hakifanyi kazi.

Naiomba basi Serikali, imwambie mwekezaji huyu arudishe mashine zote na magari na nyumba tumrudishie milioni zake 12. Sisi Wanakilwa tuko tayari kumrudishia shilingi milioni 12. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni la uchungu sana. Hivi leo Kilwa kunavunwa magogo na wewe mwenyewe shahidi, ukitoka Tunduru ukipitia barabara hii ya Kibiti - Lindi - Mingoyo unaona magari yote yanayobeba magogo yanatoka Kilwa kupelekwa Rufiji na Dar es Salaam, sisi wenyewe kule hatuna ajira. Wakati kiwanda hiki kilikuwa kinatoa ajira, lakini pia kinazalisha mbao za kuuza nchini na nje ya nchi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo limeleta masikitiko makubwa na wakubwa hawataki kulitazama hili. Lakini sijui kwa nini. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri kwanza anieleze kwa nini kiwanda hiki kiliuzwa wakati kilikuwa kinazalisha mali na malighafi ilikuwepo? Lakini la pili, kwa nini kiliuzwa kwa bei ndogo? La tatu, kwa nini hawa wafanyakazi hawajalipwa mpaka leo karibu takriban miaka tisa? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna wananchi wametoa maeneo yao kwa ajili ya kujenga kiwanda cha mbolea ... 11.2. Maeneo hayo wameyatoa yakiwa yana mazao, mazao hayo wanashindwa kuyavuna mpaka hii leo na bado kiwanda hikijengwa. Hatima ya mazao yale ni nini na wananchi wale wanafaidikaje kutokana na mazao haya kwa kuwa kiwanda hakijengwi? Maana walikuwa tayari kutoa mazao yao ili kiwanda kijengwe, si kwa kuuza maeneo. Kwa ajili ya kuwa kijengwe kiwanda wapate mbolea na wapate ajira. Lakini leo vyote havipatikani, ajira hakuna, mbolea hakuna na mazao yale hawayavuni tena. Je, Serikali iko tayari kurudisha eneo lile kuwapa wananchi wenyewe waendelee kuvuna mazao yale? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna eneo lingine ambalo kila siku nalipigia kelele hapa kuhusu gesi. Tulielezwa kwamba Kiwanda cha Kusafisha Gesi kitajengwa Kilwa, lakini mpaka leo mradi huu unaendelea, suaona kiwanda kinajengwa kule. Maana yake hii gesi haitasafishwa Kilwa? Nataka kujua. Kwa sababu tulitegemea Kiwanda kitajengwa Kilwa na gesi itasafishwa Kilwa na wananchi Watapata ajira. Sasa hii haipo, maana yake nini? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka hoja hizo zijihiwe na sina zaidi. Naunga mkono hoja, nakimbia Msikitini. Ahsanteni. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, hujazuiliwa kushangilia, lakini punguza kidogo. (*Kicheko*)

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nomba na mimi nitoe shukrani zangu za dhati kwanza kwa kunipa fursa hii adhimu ili na mimi nizungumze juu ya hoja ya Wizara hii. Lakini pia nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Waziri na Viongozi wa Wizara kwa jinsi ambavyo wamepata mafanikio pamoja na kwamba mafanikio ni kidogo lakini mafanikio.

Pia nitoe shukurani kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ameanza kuonesha na kujaribu kuelimisha sasa kwamba na nyanja nyingine pia za uzalishaji zinaweza zikafanya kazi ya kutuongeza Pato Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niseme tu kidogo juu ya uwekezaji. Uwekezaji mimi nafikiri sasa tumefikia mahali ambapo sasa ni lazima tukubaliane kwamba uwekezaji tutakaoufanya Tanzania kuanzia sasa lazima uwe *strategic*. Lazima uwe uwekezaji wenye lengo la kutuelekeza sisi sasa kupata viwanda ambavyo vitatusaidia kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo uwekezaji sasa tuutilie mkazo, uwekezaji utakaokwenda kwenye *Agro process* kuwasaidia wananchi wetu wengi katika nchi, kwa sababu bila hivyo *impact* ya uwekezaji wote huu kila siku itakuwa hakuna. Itakuwa tunasikia tu. kama walivyotangulia wenzangu kusema kwa kweli, uwekezaji ambao unatuongeza tu sisi kutufanya *damping ground* hapa, hautusaidii sana katika maendeleo ya nchi na ninaamini hakuna nchi inaweza kuendelea bila maendeleo ya viwanda. Lakini kwa Tanzania kama kweli tunataka maendeleo ya viwanda, maana yake ni lazima sasa tutafute ni namna gani

huo uwekezaji tutawekeza katika sekta ambayo inajiri watu wengi nchini ambayo ni kilimo ili tuweze kuuza bidhaa ambazo ni *value added*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nizungumze kidogo juu ya utandawazi. Pamoja na kwamba muda hautoshi, hili suala ni pana sana. Lakini niseme tu kwamba utandawazi kwa kweli haukwepeki kwa jinsi ulivoyotanda katika dunia nzima sasa hivi. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Wazi!

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Lakini lazima tukubali kwamba utandawazi huu usipouratibu, ili uweze kukusaidia kwa manufaa yako mwenyewe, basi utakuwa unakufanya kuwa mtumwa wa kutumikia watu wengine. Hapa ninamaanisha nini? Mimi ninaamini kabisa kwamba bado huwezi ukapata maendeleo kwa kutegemea utandawazi wenyewe kama utandawazi na lazima ukubali kwamba nchi itaendelea tu pale ambapo wananchi wake wenyewe watakaposhiwa usukani na kuulekeza utandawazi uwasaidie kuendeleza nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba hii *statement* ya kila wakati kusema kwamba utandawazi hauepukiki, utandawazi ndio hali halisi, mimi nafikiri ni lazima tuuache kwa sababu unaposema namna hiyo maana yake umesha-*despair*, umeuachia sasa utandawazi ukupeleke wewe badala ya wewe kuupeleka utawanda wazi ukusaidie katika maslahi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kidogo tu juu ya suala ambalo Tumekuwa tukilizungumza sana toka mwaka 2001 lakini kwa bahati mbaya kila siku halipati maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine yote haya tuliyonayo, namna gani uwekezaji wetu, tumewekewa viwanda sasa watu wanaleta bidhaa kutoka nje wamefunga vile viwanda wanauzwa hizo bidhaa kutoka kwenye viwanda vyetu lakini zimetenzewa nchi za nje, yote haya yanatokana na kwa sababu tuliomba hapa kwa Wizara hii kwamba kianzishwe kitengo cha *Economic Intelligence Unit*, sasa ukitaka kuita kwamba ni *Economic and Business Intelligence Unit* sawa tu. Lakini ili kuangalia mambo yetu wenyewe kiundani, tuwe na *data* yetu, tunachukua ya siri sasa ya kutusaidia sisi *ku-manage* mambo mengine pamoja na utandawazi huu na wapi tunaibiwa na wapi tunaonewa. Pengine wapi tunahujumiwa ili sisi tusizidi *ku-export* kila siku malighafi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kitengo hiki ni muhimu sana na ningeiomba Wizara tena kwa mara ya tatu kwamba tunaomba hebu *m-draw up terms of reference* tuweze kupata kitengo hiki kiweze kutusaidia sisi katika mwelekeo mzima wa namna gani tutaelekeza uwekezaji wetu katika hali hii ya soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije nizungumzie lile hasa nililotaka kuzungumzia, nalo ni kuhusu Shirika letu la Maendeleo la *NDC* na hususan pale ambapo *NDC* sasa imekuwa *challenged* kusimamia hizi *Spatial Development Initiatives*. Hizi kanda za maendeleo kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri kakubali kwamba anafahamu kabisa ambapo kuna vyombo vyya uchumi lazima viongozwe na umma kwanza ili angalau vifike mahali fulani kusimama kwenye miguu yake ili sasa mwekezaji aweze kuona kwamba vinafaa na mimi nafikiri katika kanda hizi za maendeleo ni *alternative* nzuri tu ya kujiongezea pato kubwa sana katika hii nchi.

Mimi nimekuwa nazungumzia sana hili na nimekuwa natoa mfano ukiacha hii iliyoelezwa kanda ya maendeleo ya Mtwara, lakini nimekuwa nikisema Kanda ya Maendeleo ya Kati, pia kwa kutokuwa na miundombinu peke yake ya kuiunda kanda hii kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma tunapoteza dola milioni 500 kwa mwaka.

Nafikiri *figure* ya kiasi hiki ina umuhimu wake kwa Wizara mkaanza kufikiria ninyi pamoja na Wizara ya Ujenzi namna gani mtashirikiana kuokoa kwa ajili ya watanzania fedha ya kigeni ya kiwango hiki na *ku-accentuate activities* nzima za *EPZ* ile ya Kigoma itafanyaje kazi bila kuiunga na miundombinu na bila ya kuiweka kama ni sehemu muhimu ya kanda hii ya maendeleo ya kati? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kanda ya maendeleo ya Mtwara pamoja na kwamba inazungumza kila kitu lakini mimi suaona *legislation* yake, sijui ikoje. Lakini ningeomba Wizara labda wakati umefika sasa itulee *legislation* Bungeni ya kuainisha na kuhalalisha hizi kanda za maendeleo ya Mtwara na Kanda ya Maendeleo ya Kati. (*Makofî*)

Ningependa pia niulize Wizara tu kwamba kwenye ile miradi ya msingi ya kanda ya maendeleo ya Mtwara, Makaa ya Mawe Mchuchuma, chuma Liganga, hivi vimefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongeze, kulikuwa na mradi mzima wa *Mnazi Bay* na Mwekezaji akaja mpaka Bungeni hapa kwamba yuko tayari kujenga na kuufanikisha mradi huo katika muda wa miaka miwili, kwa maana nyininge kabla ya mwaka 2005 tungekuwa na umeme wa kutoka *Mnazi Bay*. Sio tu kwa kusaidia Mji wa Mtwara na Lindi, lakini kwa kusaidia ukanda mzima wa maendeleo huu wa *Mtwara Corridor*. Sasa mimi ningeomba Wizara itueleze, hivi mradi huu umefikia wapi wakati mwekezaji alikuwepo na tayari alikuwa ame-draw *terms* zake kikamilifu na sisi ndio tulikuwa kikwazo kama Serikali? Ningeomba sana nielezwe hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia niguse kidogo tu juu ya suala ambalo mwenzangu aliyetangulia kalizungumza. Mimi nafikiri tukiwa na hii *Economic Intelligence Unit* itatusaidia sana kuelewa hivi viwanda kama alivyoeleza Mbunge mwenzangu kwa mfano vyta nyuzi. Watu wanavaa kila siku katika dunia hii, siamini kwamba demand imeshuka kiasi hicho ya nyuzi. Ni *demand* ya *consumption* ya kila siku, ni kama ugali tu.

Sasa kuna kiwanda cha nyuzi cha Tabora, kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Batilda Burian. Mimi na ndio maana nimesisitiza pengine ingekuwa vizuri Wizara ikaleta *legislation* kwa ajili ya kanda ya maendeleo ya Kati kwa sababu naamini labda na kiwanda hiki kitapata nafuu kama kikiwa ni kiwanda kimojawapo katika kanda ya maendeleo ya kat. Kwa sababu ninaamini kwamba demand ya nyuzi ni kubwa sana hata kama hapa nchini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunataka tuwekeze kwenye viwanda vinavyotuwezesha *ku-earn value added*, basi hakuna sababu ya kuiiza Pamba kama Pamba. Kwa nini Pamba yetu yote inayotoka Kanda ile ya Shinyanga na Mwanza isitengenezwe nyuzi tukauza nyuzi? (*Makofî*)

Kwa nini tuisitumie mbinu hii kuziba pengo ambalo limetokana na kushuka kwa bei ya pamba katika soko la dunia? Kwa nini tusiongeze ajira kwa mfumo huu na hata kama mwekezaji hakuna, maana yake mbinu hii imekuwa kila siku ukiuliza juu ya kiwanda cha nyuzi cha Tabora unaambiwa tunatafuta mwekezaji, kweli sisi tume-resign kama Serikali wakati *demand* iko kwenye Soko la Dunia?

Tume-resign kama Serikali kwamba mpaka atakapokuja kupatikana mwekezaji basi ndio soko litakuwa linatusubiri tu? Kwa nini tusifanye kama alivyoeleza Waziri hapa kwamba lazima chombo cha umma kwanza kiongoze kwa muda kishike lile soko tuanze kuwa tunalishughulikia lile soko, kazi ianze, basi hapo ndio tutafute mwekezaji? Kwa nini tusifanye hivyo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini itabidi tubadilishe kidogo *philosophy* yetu katika kuzungumzia hawa wawekezaji, kwa sababu kuna viwanda vingine ni muhimu lakini tumedumaa sasa akili zetu kwa kusema kwamba lazima tu tupate mwekezaji, lazima tupate mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ninapozungumzia kwamba tunapoteza kwa kima cha chini kabisa zaidi ya dola milioni 500 kwenye Kanda ya Kati si kazi pengine akili zetu zinafikiria mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunaelewa hilo, hizo hela ziko tayari, soko liko tayari, Kongo inafahamika pale, ina matatizo na bidhaa hizo ni uchumi wa jiografia tu, ni *transtraffic* tu, wala huhitaji kuweka viwanda, ni miundombinu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa yenye hiyo jinsi ambavyo ilivyo na value inaweza ikaenda sasa hivi ikapita kwenye masafa zaidi ya mara tatu, inatoka Kongo kwenda kupita kilomita zaidi ya 2500 kulinganishwa kwa kilometra 1250 hizi za kufika Dar es Salaam *you can imagine* ingekuwa ni kiasi gani.

Kwa hiyo, ni soko ambalo dhahiri liko tayari, linakusubiri uweke muundombinu kidogo wa kutoka Dodoma unaunga lami unakwenda Kigoma. Dola milioni 500 utajenga miundombinu mingapi ukishaweka kiasi hicho? Kwa nini tusiwe na *Intelligent Investment* kama hizo ambazo zinazalisha ili tuweze kuzalisha? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kulitilia mkazo hilo na ninaamini kwa mwelekeo ambao Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ameonesha hata kwenye nyanja hii na kwa kutumia Shirika letu la *NDC* ambalo sasa hivi limeanza kujenga utaalamu wa kutosha kabisa kwenye suala hili la *Spatial Development Initiatives*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tutapata Muswada Bungeni, pengine ikibidi kabla ya mwisho wa mwaka huu kuainisha na kuhalalisha hizi kanda zetu za maendeleo angalau mbili za kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena na ninasema naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naona hapo tumeefikia mwisho. Sasa tutakapokuja jioni, tutaanzia na Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme na atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekiffu. Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 Jioni.

(*Saa 6.55 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu jioni hii na pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na wataalam walioandaa hoja hii ambayo mwelekeo wake sio mbaya ni mzuri. Pamoja na hayo naomba nichangie eneo la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kikubwa sana cha Mikoa ya Kusini kuwa na umaskini ni ukosefu wa miundombinu, vikiwemo pamoja na barabara lakini na umeme unachangia au umechangia kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kusini ilikuwa na bahati mbaya kwa sababu mara tu baada ya Uhuru, Mikoa ya Kusini liendelea kujishirikisha katika vita vya ukombozi dhidi ya Msumbiji. Hali hiyo imefanya mikoa ile kwa kipindi chote hicho isiwe inafanya shughuli zozote za kimaendeleo. Lakini tulikuwa na mategemeo makubwa kwamba, baada ya vita vya Msumbiji, Serikali itatuangalia kwa jicho la huruma kwamba, sasa ingeweza kutuharakishia miundombinu ya kuweza kutuletea maendeleo. Lakini kwa bahati mbaya sana tuliyokuwa nayo, pamoja na kelele nyingi kwa miaka yote hiyo, mafanikio yamekuwa machache sana. Barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi ndiyo kwanza sasa inajengwa. Hatuna mawasiliano kabisa ya Mtwara na Mikoa wa Ruvuma. (*Makofî*)

Hali hii kwa kweli inachangia sana umaskini hata pamoja na jitihada zinazofanywa na wananchi wenyewe, lakini kama hakuna miundombinu, maana yake ni kwamba, hauwezi kupiga hatua ya maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukikosekana umeme mahali athari zinazotokea ni kubwa sana. Hasa kwa karne hii ya sayansi na teknolojia, kwa maana hatuwezi kabisa kwenda, kuna athari kubwa ya ukosefu wa viwanda, kwamba sasa hivi kuzungumzia viwanda katika Mikoa ya Kusini ni kama ndoto. (*Makofî*)

Mashine za kusaga hazifanyi kazi. Mwaka 2002 nilizungumza sana hapa. Mashine za maji hazifanyi kazi, watu wanafikia mahali maji wanaokotaokota, kitu ambacho kinawasababishia maradhi mengi sana. Mawasiliano hayapo. Sasa hivi Mtwara tunayo mitandao ya simu lakini ili kupata nafasi ya

kuweza ku-*charge* simu upate kuzungumza au kupiga inahitaji usubiri zamu ya wiki moja ili ui-*charge* simu yako, yaani lazima utumie umeme. Kompyuta hazifanyi kazi. Sasa hayo yote yanatokana na ukosefu wa umeme na tunajitahidi sana kupiga kelele hapa. Nimekwishakwenda Wizara ya Nishati na Madini mara nyingi tu. Nimeshakutana na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mara nyingi kweli kweli na hivyo sifanyi mimi tu, nadhani katika Bunge lako hili, Waheshimiwa Wabunge wetu waliochangia kutoka Mikoa ya Kusini, walilalamika juu ya suala la umeme. (*Makofî*)

Ilivyokuwa bahati mbaya sana kwa sababu Mikoa ya Kusini vyanzo vya umeme viro vyanzo vingi, chanzo cha kwanza tuna gesi ya *Mnazi Bay*, tuna chanzo cha Gesi ya Songo Songo, tuna chanzo cha Gridi, tuna chanzo cha Mkaa wa Mawe wa Mchuchuma, lakini pia tunacho chanzo cha nchi jirani, umeme kule uko mwingi, hawana matatizo ya kutuletea umeme, lakini bado Serikali ina kigugumizi kutoa maamuzi. Mbaya zaidi ni kuchukua fedha ambazo zilifadhiliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya *gas* ya *Mnazi Bay*, zile fedha zikachukuliwa zikaenda kutumika katika mradi mwingine. Hii inaonyesha ubaya mkubwa zaidi.

Lakini ubaya mwingine ambao hautasahaulika Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba sasa hivi *gas* ya Songo Songo ichukuliwe Songo Songo ije itengeneze umeme Dar es Salaam. Mheshimiwa Mwenda, wakati anachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa mfano, mtu anamwoza mwanawawe lakini hapewi mahari na mimi nimetoea mfano mwingine kwamba, kama kuna kijiji kimetokea njaa lakini kijiji kile kimebahatika kupata maghala ya kutunzia chakula pale, halafu wale watu wanakufa, lakini kuna maeneo mengine wana njaa lakini njaa ya nafuu, sasa unakwenda kusema kwamba, ninyi watu wa kijiji hiki mnaotunza chakula hiki kwenye maghala hapa basi ninyi mtakuwa ndiyo walinzi wa maghala haya lakini hamtapewa hata kibaba. Kwa hiyo, endeleeni tu kufa njaa. (*Makofî*)

Huu ni ukatili mkubwa, kweli kweli kama kuna ukatili na kama kuna jambo ambalo sisi wa Kusini hatutalisau kamwe, ni matendo ya namna hiyo kwamba *gas* ya Songo Songo iletwe Dar es Salaam, wakati Mikoa ya Kusini ni maskini na chanzo cha umaskini unatokana na ukosefu wa umeme. Naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo. Mkataba huu ulikubaliwa vipi. Mkataba unasema kwamba, *gas* itoke Songo Songo ije itumike Dar es Salaam wakati watu wa Lindi, Mtwara na Ruvuma hawana umeme na wanakufa kwa umaskini na matatizo mengi, vianzio vya raslimali vinahamishwa kule vinakuja Dar es Salaam. (*Makofî*)

Umeme wa Gridi uko Kidatu, kutoka Kidatu kwenda Mikoa ya Kusini ni karibu zaidi kuliko kutoka Kidatu kwenda Musoma, umeme umefika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nasikiliza unavyo-*draw relationship* na viwanda, maana tuko kwenye viwanda. Sasa naona uko kwenye umeme tu. Hujengi uhusiano wake na viwanda, ili apate kujibu.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPOME:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Nimezungumzia umeme kwa sababu ni chanzo cha kuwepo kwa viwanda pamoja na vitu vingine vyote. Kwamba, hatuwezi kuwa na viwanda kama hakuna umeme. Leo tunazungumzia suala la *Mtwara Corridor Development Plan*, lakini naona kama hii ni danganja toto tu. Kwa sababu haiwezekani maendeleo ya Kanda ya Mtwara yakawepo kama hakuna umeme, haiwezekani hata kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, umeme unaathiri maeneo mengi ya maendeleo. Hakutakuwa na viwanda nadhani nimeshazungumza kwamba, hata huduma za hospitali haiwezekani. Kwa sababu umeme unahitajika katika operesheni, umeme unahitajika katika kupima kwenye maabara na sehemu zingine. (*Makofî*)

Sasa kungefanyika tathmini, athari zilizoko katika Mikoa au maeneo ambayo hayana umeme, mngefanya tathmini, basi athari zake ni kubwa sana. Naomba Serikali ituangalie kwa kiwango kikubwa.

Mwaka 2002 baada ya kuzungumza hapa kwenye Bunge, ikachukuliwa hatua kwamba, *Net Group Solution* walikwenda Mtwara kuangalia mashine za umeme, wakaenda na Lindi. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Endelea, Mheshimiwa Mbunge, nilichokuwa najaribu kusema, hoja iliyopo mbele yetu ni ya Viwanda na Biashara. Tunajua umeme ni nyenzo inayotakiwa kwenye viwanda. Lakini basi jaribu ku-draw angalau mahusiano yake. Ukienda tu kwenye umeme, umeme, haiwi hoja hii tena.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimekuelewa vizuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli jazba yangu ilikuwa kwenye umeme, viwanda ilikuwa nimegusa tu kwamba kama hakutakuwa na umeme kwa maana hiyo hakutakuwa na viwanda. (*Makofî*)

Naomba niishie hapo kwamba tunaomba sana basi Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa sababu viwanda haviwezi kuwepo bila umeme. (*Makofî*)

Hata hivyo, viwanda vya kusindika korosho hadi viwanda vya korosho vimeathirika kwa sababu ya kutokuwepo umeme na vile vile ukiomba viwanda kwa wahisani kwamba, jamani tunaomba Mikoa ya Kusini kupatikane viwanda, hawaangalii kwa sababu hakuna umeme pia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî/Kicheko*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikuhakikishie kwamba, suala la umeme sitalitaja na nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba, umeme kidogo kule Lushoto, pamoja na kwamba unakatikakatika lakini upo. Ahsante sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba nzuri, yenyé kina, ambayo naamini kama angepata muda wa kuisoma yote, basi tungepata kwa kweli maelezo yenyé kina vizuri sana. Lakini nashukuru uwakilishi wa hotuba yake umekuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, nashukuru sana ametaja suala la malengo ya Sekta ya Viwanda na hii iko katika ukurasa wa 47 na katika maneno meusi ameandika Sekta za kipaumbele ikiwa ni pamoja na Sekta ya Nguo, Usindikaji wa Mazao ya Kilimo, Sekta ya Ngozi na Sekta ya Viwanda Vidogo Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza zaidi katika viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao. Ninaamini kabisa Wizara mpaka sasa hivi na kwa masikitiko nasema bado haijaweka kipaumbele katika usindikaji wa mazao ya kilimo. (*Makofî*)

Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna mahali ambapo dhahiri imezungumzwa tutafanya nini katika usindikaji wa mazao yetu ya kilimo. Natoka katika eneo linalojihusisha na kilimo cha matunda, pamoja na mboga mboga. Ni eneo ambalo linahitaji sana usindikaji ili upate faida ya kilimo chako. Tulikuwa na viwanda vya matunda vyote vimekufa na mpaka sasa hivi hakuna mwelekeo wa dhahiri unaoeleweka, Serikali itafanya nini kufufua viwanda hivi vya usindikaji wa matunda na mboga mboga. (*Makofî*)

Namwomba Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake wakati wa kujibu, ajaribu kutuelekeza tutafanya nini sisi tunaoishi katika maeneo ambayo kwa kweli kilimo chetu kinatalimwa katika maeneo madogo madogo na katika maeneo madogo madogo haya ni lazima uwe na *economies of scale* katika kitu kinachoitwa *a value added*. Usipo-add value to your product na shamba lako ni doyo, siku zote utaonewa na umaskini hautakuondoka. (*Makofî*)

Naomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie tufanye nini ili tuweze kufanikiwa katika suala la viwanda vidogo vidogo hasa katika usindikaji wa matunda na mboga mboga. Kwa sababu muda ni mfupi, niende katika eneo la pili, ambalo ninaamini kwamba, Serikali bado haijaamua kikamilifu kuhusu *Export Processing Zones*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilibahatika kutembelea China, China wanazo hizi *Export Processing Zones*, kwa kweli ambazo zimeanzishwa katika maeneo ambayo yana matatizo ya uchumi kama vile

tunavyoisisikitikia Mtwara na Kigoma na ili tuweze kufanikiwa katika *Export Processing Zones* ni lazima Serikali iwekeze. Unapouomba Mkao, eti uwekeze katika suala la *Export Processing Zones*, unazungumza ndoto. Kwa kweli ni kuwaonea. Napenda kama Serikali kweli imeamua twende katika *Export Processing Zones*, suala hili ni suala la *NDC* na kuwaachia wafanye mazungumzo na Mikoa, ni suala la Taifa kuwekeza katika miundombinu ili wawekezaji waende huko. Hakuna atakayejenga barabara au atakayepeleka umeme Mtwara ili uweke *Export Processing Zones*, itakuwa ni ndoto. (*Makofî*)

Ni lazima Serikali rasmi iamue kwa makusudi na kwa jeuri kwamba, tutawekeza hela zetu katika miundombinu hii ili watu wale waje wawekeze kwetu. Ndivyo nilivyoona katika nchi zinazoendelea kama vile China. Kwa hiyo, naomba sana suala hili la *EPZ* kama kweli tunataka kujikomboa na hakuna nchi ambayo itawenza kuamka kama haiwezi kuwa na *Exports*. Uchumi tulionao leo ni *cosmetic* kabisa, ni uchumi wa kupambwa kwa sababu hela tunazozitumia siyo hela tulizozalisha humu ndani. Ni hela za misaada. Haiwezi kutupeleka mbali misaada hii. Watakapo-withdraw kwa wiki moja, nchi hii itanyooka. (*Makofî*)

Sasa hili tuliangalie na njia moja ya kuwa na *guarantee* ya kuweza kuikomboa nchi ni kuwa na *export* na siyo *exports* tu za mazao kwa sababu hatuna uwezo wa *ku-export with value added*. Lakini tunaweza kuzalisha tu katika bidhaa fulani katika maeneo ya *EPZ* na *tuka-export*, tukawa na uhakika wa masoko ya kupata hela za kigeni. Mimi hili naliomba, Serikali ikae kwa jeuri kabisa, iweke utaratibu wa kuiunda miundombinu kwa makusudi ambayo itawavutia wawekezaji. Suala hili lisiachiwe *NDC* na Mikoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la Sera ya Biashara ambayo naamini iko tayari. Ni ushauri tu, sitaliingiza katika suala la uzawa. Lakini napenda tuelewe wazi duniani kote uko utaratibu wa upendeleo wa makusudi kwa wazawa wa nchi hiyo. (*Makofî*)

Zipo biashara ambazo makusudi zinazungumza, zimetengwa kwa ajili ya watu fulani. Hata kama itabidi wafichwe na hao matajiri lakini anayeonekana ni Mswahili na Mswahili si suala la rangi, ni suala la mtu yeoyote ambaye kweli ana Uzalendo hapa Tanzania. (*Makofî*)

Mimi nashangaa leo ukienda Dar es Salaam unakuta maduka ya Wachina, maduka ya watu wanaiza vitu ambavyo Watanzania tungeweza kufanya. Lakini kwa sababu hatuna mitaji, wao wanakuja kuchukua biashara hizi. Ni kwa nini zisifanywe na Watanzania? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, awajibike katika hili. Huku ni kutudhalilisha kwa sababu hatuna mitaji ya kuweza kununua kutoka nje, ni lazima hawa waje wawekeze. Sasa twende nao, atumie jina la Shekiffu, lakini biashara ni yake na mimi nipate asilimia tano katika hicho alichoweka. (*Makofî*)

Leo ukienda Dubai huwezi ukafanya biashara pale, wewe unaitwa Shekiffu eti ukaanzishe biashara Dubai pale, hata siku moja. Utakuta Al-Hilal, lakini huyu amekopa kwenye mabenki, ndio utaratibu wa dunia nzima, ni vitu vyatanya kawa, mtu hawezu kutoka nchi nyingine aje apate leseni kuendesha *petty business* ya *bakery* katika nchi hii. (*Makofî*)

Hili namwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie sana na hili litawezekana kama Mheshimiwa Waziri, kwa makusudi atalitamka wazi kwamba, biashara hizi ili ukitaka kuingia uingie kwa mgongo wa mwananchi, wala tusione woga kulisema, wala tusione aibu maana inafanya dunia nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika ubinafsishaji. Mheshimiwa Waziri, ameeleza vizuri sana kuhusu ubinafsishaji na maeneo ambayo tumefanikiwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara na ni kweli tumefanikiwa kwa kiasi fulani. Lakini kwa kweli ukilinganisha kile tulichofanikiwa na kile ambacho tumebadilisha ni kama vile umetoa pishi ya sukari ukapewa nusu kibaba. Naamini hivyo. (*Makofî*)

Nasema hivi kwa sababu katika maeneo ambayo Wizara ya Viwanda na Biashara na kwa bahati mbaya ndio Wizara iliyoanza ubinafsishaji, maeneo mengi yamekwenda bila kufanyiwa tathmini ya kutosha. Tulikwenda kwa Msukuma tukijua kwamba, ubinafsishaji haraka haraka, kwa hiyo ndio maana utakuta kuna viwanda karibu 14 vimefungwa. Lakini ufuutiliaji umekuwa mdogo, kuona kwamba wale waliopewa dhamana ya kuvienda wamefanya nini. (*Makofî*)

Viwanda hivi watu wake wamekosa ajira na ni kweli vilikuwa havizalishi vizuri wakati huo. Sasa ni juu yetu kusimamia na kuhakikisha waliochukua viwanda na ambao wameweka malengo na mikataba wanatti mikataba hiyo. Linalofanana na hili ningependa Mheshimiwa Waziri, baadaye atusaidie kuniambia, hivi zile hisa zetu ambazo tuliacha katika viwanda kama nya madawa ziko wapi na anazisimamia nani? Ninajua mtaniambia ni Hazina. Lakini wale watu wamepewa mkataba gani kwamba katika kipindi hiki sisi tunapenda mfikie hapa ili tuweze kuona *shares* zetu zinazalishwa. Maana tunapowekeza hisa ni lazima tumdhibiti huyu ambaye anazalisha kwa niaba yetu ili atengeneze faida, vinginevyo atakudanganya kwamba hana faida, lakini marupurupu anachukua yeye, ndiyo biashara ilivyo. (*Makofi*)

Nimewekeza katika Mashirika ya Umma, *High Land Soap, Embassy*, Mheshimiwa Mbatia, anajua vizuri. Nilimwachia uongozi, lakini hakuna siku ambayo tumesemlea *Balance Sheet* yenye faida. Kila mwaka *Balance Sheet* ina hasara. Lakini wenyewe wanajua jinsi ya kuficha faida na kuzipata kwa manufaa yao. Wewe anakwambia hakuna faida, lakini yeye anajenga viwanda vingine, inawezekanaje? (*Makofi*)

Utakuta kama hatutakuwa wajanja, zile hisa zetu tulizowekeza, bado wataendelea kuzitumia na watajinufaisha na vifaa pamoja na majengo ambayo tulikubali kwamba labda tuwape asilimia 60 sisi tubaki na asilimia 40. Nasema ni lazima mikataba ionyeshe wazi kwamba, katika kipindi fulani, tunataka tujue *Balance Sheet* yake na tunataka kwa kweli tujue mnafanya nini. Kwa bahati mbaya katika maeneo hayo kuna Bodi, napenda niseme tu wazi wazi kwamba, hawa walioko kwenye hizi Bodi wana utaalam gani wa kutosha kwa shughuli za biashara. Kwani biashara ni utundu tu, kama hutakuwa mle kwenye Bodi ukaelewa mwenzako anafanya nini, atakuja kukudanganya ukishapata posho ile unaondoka. Aah! Bwana mimi nina Bodi nyding. Lakini hujafanya kwa maslahi ya Taifa lako na mifano iko mingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko eneo la mwisho ambalo naona muda unakimbia sana. Naomba nzungumzie ushindani usio wa haki. Hivi leo tunazungumzaia kwamba, hili linafuatana na lile la biashara ndogo ndogo. Nenda wakati wa Saba Saba uone, biashara zinavyouzwa, biashara zote zinazouzwa mwisho wa maonyesho zinarudi mjini na zinaporudi Dar es Salaam mjini, inakuwa ni biashara ya kawaida. Utakuta wale wanaendelea ku-*import* vitu kama *toys* na ndivyo unavyoviona leo, ukizunguka hapa kwenye mnada siku ya Jumamosi, redio za ajabu ajabu, vipisto nya watoto!

Nasema hata kama mtu analeta kwa ajili ya kuuza katika nchi hii, basi awe Mtanzania na hana mtaji mkubwa, lakini utakuta wale ambao wana mitaji mikubwa ndiyo wanakuja na vibashara hivi na kwa bahati mbaya katika nchi hii ndiyo nchi ambayo unaweza kutoa hela unavyotaka. (*Makofi*)

Hizo *Bureau de Change* ukishauza leo kesho unakwenda kununua bei unatoa nje, nchi itafilisika. Natabiri nchi itafilisika. Nilikwishazungumza katika Bajeti ya Waziri wa Fedha, hizi *Bureau de Change* ndiyo zinazomaliza hela za nchi hii na biashara inapofanyika pale asubuhi mtu anahamisha anakwenda ananunua tena vitu nya ajabu ajabu kule. Sio vitu nya kutusaidia katika maendeleo. Hawa watu kama wanataka kutusaidia, walete matrekta, walete spea za magari siyo kutuletea vipulizo. (*Makofi*)

Kwa uchungu sana napenda kulitamka hili kwamba, Wizara ya Viwanda na Biashara, ndiyo msimamizi wa yote haya na kama kweli kwa dhahiri kabisa hatutaamua kufanya kazi kwa *commitment*, tutaendelea kuchezewa na uchumi wetu utaendelea kuyumbishwa na hawa wenzetu. Naomba sana nimalize kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri, namwamini sana ana uwezo mkubwa, hebu wadhibiti biashara hizi ndogo ndogo ambazo Waswahili tuna uwezo nazo. Nasikitisha sana ninapomkuta mtu ameweka duka kwao ni Hongkong, duka hili limepata wapi leseni ya kufanya kazi hii humu nchini? Naomba Mheshimiwa Waziri, utusaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo, naomba nianze na pongozi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote, kwa hotuba nzuri, ambayo inaonekana ni hotuba ya matumaini kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na kuzungumzia Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam. Lakini kabla sijaanza, naomba kuwapongeza Halmashauri ya Nje kwa kazi nzuri wanayofanya na jinsi wanavyosimamia Biashara ya Kimataifa hususan maonyesho yetu ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maonyesho haya ya Dar es Salaam ni maonyesho ambayo yamekuwa kivutio kikubwa katika Taifa letu na nchi jirani. Lakini kadri siku zinavyokwenda maonyesho haya yanapoteza mwelekeo na yanaanza kugeuka badala ya kuwa *Trade Fair*, naona sasa yanakuwa *Trading Center*. Ukipika katika maonyesho ya Dar es Salaam sura ya maonyesho inakuwa kwa siku ya kwanza na siku ya pili, siku zinazobakia zote maonyesho yale yanakuwa ni maonyesho ya wachuuzi, watu kuuza biashara zao na bidhaa zao. Ile sura ya maonyesho hasa inakuwa siku ya kwanza na ya pili peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake, walione hili. Nia ni njema kuwashirikisha wananchi wengi waweze kufaidika na bidhaa zao na waweze kununua bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi yetu, lakini utaratibu unaotumika ndani ya maonyesho yale unaleta bughudha kwa wale amba wana nia ya kutaka kununua bidhaa na kuzipeleka katika nchi mbalimbali hususan nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri Halmashauri ya Biashara ya Nje, ikae na kuandaa sura mbili tofauti katika *Trade Fair* zetu kwa siku za usoni. Sura ya kwanza iwe ni kulinda heshima ya *Trade Fair* yenye na sura ya pili ni kuwapa nafasi Watanzania walio wengi washiriki, kuona na kununua bidhaa za ndani. Mle ndani kuwe na sura mbili tofauti. Sasa hivi ukienda baada ya siku ya kwanza na ya pili, utakuta ni eneo tunakwenda kununua vitu rejareja na kuondoka. Mwelekeo wa Saba Saba umepotea katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie umeme, lakini umeme ninaouzungumzia mimi ni tofauti na ule umeme amba wewe ulikuwa unataka uuzungumzie. Naomba kuzungumzia umeme wa viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi, ilipata nafasi ya kutembelea viwanda mbalimbali katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro. Tatizo moja ambalo tulilipokea ni kuhusu *tariff* za umeme kuwa juu sana katika nchi yetu. Hili ndilo tatizo ambalo linaonekana limekua kiasi kwamba, malalamiko yote yanaelekezwa kwenye umeme na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana ndani ya Bunge lako Tukufu, mimi nilipata tatizo kidogo pale nilipomsikia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, alipotoa taarifa ya kwamba, nchi jirani za Kenya na Uganda *tariff* zao ziko juu kuliko Tanzania. Ile kauli imenitia mashaka makubwa sana. Miaka yote tunaambiwa sisi bei zetu ziko juu mno, lakini jana jambo la kushangaza sana ni ile taarifa iliyoolewa, imenitia wasiwasi, inawezekana tathmini haikufanywa sawa sawa. Miaka yote tunaambiwa Kenya na Uganda *tariff* zao ziko chini, jana tunaambiwa wao *tariff* zao ziko juu. Hebu tuambiwe ni kitu gani ambacho tathmini imekiona katika suala hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini imefanywa na walioifanya tathmini hiyo ni *TANESCO* na Wizara. Lakini ningependa kushauri tathmini ile iletwe kwenye Kamati za Bunge, mfano, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Kamati nyingine, ili zichambue kwa kina tathmini ile ambayo imetolewa kauli jana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona. Mimi kauli ile inanipa mashaka na kauli ile inaweza ikasababisha wale wawekezaji wengine badala ya kuja kuwekeza kwetu wakakimbia wakaenda kwenye nchi hizo ambazo *tariff* zao ziko chini. Hili ni tatizo ambalo tutakuja kuliona hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba, katika ziara yetu kama Kamati, tulibahatika kutembelea Kiwanda cha Karatasi cha *SPM-Mgololo*, Mkoani Iringa. Hili limezungumzwa sana na mimi nina wazo tofauti kabisa katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambayo tulipewa pale katika uongozi wa kiwanda, kwanza napenda kuwapongeza sana viongozi na wafanyakazi wa *SPM-Mgololo*, kwa kazi nzuri wanayoifanya na moyo wa Uzalendo wanaouonyesha kwa ajili ya faida ya Taifa letu. Kile kiwanda kiko hatarini, pale kuna matanki zaidi ya 30 yana sumu na matanki yale yameanza kuoza na taarifa tuliyopewa pale ni kwamba, wakati wowote sumu ile ikitiririka ikienda kwenye vyanzo vya maji au ikienda kwenye mito, basi viumbi hai na binadamu wote wanaweza wakadhirika na kwa kiwango kikubwa kama ilivyotokea nchini Brazil.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kikubwa ambacho tuliambiwa pale ni kwamba, Serikali imetoa masharti magumu kwa wale ambao wanapenda kuwekeza pale. Ushauri wangu leo kwa Serikali ni kwamba, ilegeze masharti haya haraka iwezekanavyo na ikiwezekana masharti yale yalegezwe kwa utaratibu wa kumtafuta mwekezaji, ambaye ana uwezo mkubwa katika kiwanda kile. Kile ni kiwanda kikubwa mno na kinahitaji mtu ambaye ana uzoefu na ana nguvu na tumeambiwa wako wawekezaji wawili ambao mazungumzo yalikwishaanza na Serikali. Mimi ningependa kushauri kwamba, mazungumzo yale yaendelezwe na masharti yalegezwe. Viwanda vile vyote ambavyo vina matatizo kama yale viweze kupata wawekezaji haraka iwezekanavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la viwanda katika Mkoa wa Morogoro. Suala la Mkoa wa Morogoro, miaka yote tumelizingumza, kulikuwa na viwanda vingi ambavyo vilikuwa vinatoa ajira na pia Pato la Taifa lilikuwa linaongezeka lakini leo Morogoro imebaki ni hadithi, wenzetu wengine humu ndani mpaka wamefika kusema maneno mengine ambayo hayafai kusemwa. Lakini ningependa kuomba kwamba, Mheshimiwa Waziri atueleze nini kimefanyika katika viwanda vya Morogoro, hususan Kiwanda cha *POLYTEX*. Kwa muda mrefu wawekezaji ambao wamepatikana ni wale wale, wanatumia udanganyifu, leo mwekezaji yule yule anasema niko tayari kununua kwa dola milioni saba, kesho analengeza kamba, Serikali inamfuata, anasema niko tayari kwa dola milioni tatu, mtu ni yule yule mmoja. Sasa Mheshimiwa Waziri, hivi kweli nchi itaendeshwa kwa utaratibu huo? Tunaomba kauli ya Serikali kuhusu Kiwanda cha *POLYTEX* na Kiwanda cha Viatu cha Morogoro. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Viatu cha Morogoro leo ni zaidi ya miaka saba kimefungwa. Lakini tunaambiwa kuna mtu pale ameng'oa mashine zote za Kiwanda cha Viatu cha Morogoro na mashine zile amezipeleka Dar es Salaam, amefungua kiwanda kipyga na anazalisha viatu na anaviuzia Taasisi za Serikali likiwemo Jeshi, Polisi na Magereza. Mashine za Kiwanda cha Morogoro zimehamishwa. Ninaomba kauli ya Serikali leo ndani ya Bunge letu Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje mtu anahamisha mashine na huyo aliyehamisha mashine hizo hakuweka dhamana yoyote na wala hakubinafsishiwa kile kiwanda cha viatu, alikodishwa kwenye Kiwanda cha Viatu, Serikali ipo, ina macho na pia inaona na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, ni mzawa wa Morogoro, naomba leo aonyeshe Uzalendo wake katika suala la Viwanda vya Morogoro. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri, amevitembelea sana viwanda vya Morogoro, amefanya ziara, anajua na pia ameona. Leo naomba nipate kauli ya Serikali kuhusu Kiwanda cha Viatu na Kiwanda cha *POLYTEX*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niungane na wenzangu katika kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni machache lakini ni ya msingi kweli. Napenda nianzie alipomalizia msemaji wa mara ya mwisho. Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu wake, sijui kama walishawahidi kufika katika Mkoa wa Rukwa na kama walifika, walifika mwaka gani? (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Kabla ya Uhuru.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa hivi sasa tunanunua *petrol* kwa Sh. 780/= kwa lita, *diesel* Mpanda wananchi kwa Sh. 800/= kwa lita. Sasa Mheshimiwa Waziri, hebu fikiria wananchi katika Mkao huo wa Rukwa, bidhaa muhimu ambayo inasambaza bidhaa katika Mkao wote iko kwa bei hiyo, wananchi wananchi bidhaa hizo kwa bei gani? Hili ni jambo la kusikitisha sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rukwa katika Jimbo langu la Kalambo limesahaulika kabisa wala sidhani kama kuna mipango yoyote ya kufikiria jinsi ya kuwasaidia wananchi katika Jimbo la Kalambo ili na wao wajione kwamba, wana nafuu yoyote katika kufanya biashara au kuweza kupata bidhaa muhimu.

Hayo si matatizo ya Kalambo peke yake, Kigoma ni hivyo hivyo, Mtwara wanalamika hivyo hivyo, Lindi wanalamika na pia Tabora wanalamika. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunaomba uanzu kufikiria kwa misingi hiyo ambayo nimeanza mimi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kunukuu katika kitabu chako ukurasa wa 43, kifungu cha 63: "Sera ya msingi mojawapo ya Serikali ya CCM katika kurekebisha uchumi wa Taifa ni pamoja na kuipa sekta binafsi nafasi ya kipaumbele ya kuendesha uchumi ili Serikali ielekeze nguvu zake katika shughuli za kusimamia Sera, Sheria, huduma za jamii, miundombinu, ulinzi na usalama". Tunashukuru sana kwa kauli hiyo.

Sasa miundombunu Rukwa ikoje na pia miundombinu Kigoma ikoje? Mnaisaidia vipi ili miundombinu hii ikiwa bora wafanye biashara na wao vizuri au ni geresha tu. Katika ukurasa wa 44, sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na Muswada wa Sheria ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na wewe mwenyewe umo ndani ya hii sasa unalisaideaje Jimbo la Kalambo, pamoja na Mkao wa Rukwa? Unatuwezeshaje ili watu wanaofanya biashara katika eneo hili kwa bei hiyo ya *diesel* waweze kufanya kazi na wao wachangie katika Pato la Taifa? Katika ukurasa wa 48 (a) unazungumzia juu ya mazingira ya uwezeshaji na uzalishaji bora katika viwanda ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa kuaminika wa nishati na maji na kuboresha mfumo wa kodi unaohamasisha ukuaji wa sekta ya viwanda. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya biashara mahali popote na hasa katika Mkao wetu huu wa Rukwa, umeme ambao tumeupata kutoka Zambia umefika Sumbawanga lakini tunahitaji uende na sehemu nyingine ili uwezeshe uzalishaji wa viwanda vidogo vidogo. Tumekwishaomba mara kwa mara kutoka Wizara zinazohusika na kwa sababu wewe mwenyewe umezungumza kwamba umeme ni kitu muhimu. Kasesya ni kituo cha mpakani na Zambia lakini umeme umepita juu juu tu. Wananchi wa Vijiji vya Kasesha, Sopa, Matai, Singiwe, Msanzi na Katuka wanauangalia umeme umepita angani, wao ni wasindikizaji wa maendeleo na siyo washiriki wa maendeleo. Sasa watashiriki vipi maendeleo kama hawawezi kupata umeme ili waweze kusindika mazao yao? Umeme ule ungeweza kuchukuliwa pia kutoka Matai ukapelekwa katika Gati ya Kasanga kwa kupitia Vijiji vya Mbuza, Mkowe, Kisumba na ungefika katika Gati ya Kasanga, tungeweza kufanya biashara nzuri sana pale Kasanga kwa sababu tungeweza kuanza kupambanisha bidhaa za samaki zinazotoka katika nchi yetu ya Tanzania ambapo sehemu ya ziwa ni kubwa sana.

Tukaweza kunyang'anya biashara katika Mji wa Mpulugu katika Zambia ambao ndiyo umemiliki biashara yote ya samaki katika eneo lile na tunapoteza fedha nyingi sana kutokana na samaki wanaokwenda kuuzwa katika nchi ya jirani. Umeme ungefika pale tungeweka viwanda vya kusindika samaki au kuwaweka samaki katika barafu, kuwashafadi katika barafu na tungeweza kuwafikisha samaki hao mahala popote katika Afrika lakini hakuna umeme. Tunapozungumza haya mambo viwanda haviwezi kushamiri katika nchi hii kama hatutafikiria suala la umeme katika nchi hii. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Sera ya Uwezeshaji, kwa sababu umesema na wewe umo humo, Jimbo la Kalambo linakusubiri lione ni jinsi gani utakavyoweza kutusaidia hasa kwa ajili ya Kituo cha Kasesha. Bwana Elvis Msiba, kwa bahati nzuri alifika pale Kasesya, alipofika pale niliandamana naye nikamweleza mipango ambayo tumeipanga Kiwilaya na mambo ambayo tumeshaanza kuyafanya pale. Tumejenga machinjio kwa sababu wenzetu wa Zambia wanahitaji *carcass*, ng'ombe aliyechinjwa, hawataki ng'ombe aliye mzima avuke pale. Ng'ombe walikuwa wanachinjwa katika mazingira ya ovyo ovyo sana, wakawa wanalamika. Halmashauri imejenga machinjio ambayo inaweza kuwahudumia ng'ombe wanne kwa mara moja, tunachohitaji ni msaada wa kujengewa mahala ambapo watu wanaweza

kufanya biashara zao vizuri, umeme na maji. Bwana Elvis Msiba alitupatia shilingi milioni nne ambazo ninajua zimeshaanza kutumika vizuri kujenga mabanda yatakayofanya biashara mahali pale, Wizara ya Viwanda na Biashara mko wapi? Mnatusaidiaje wakati hata katika Mkoa hamjawahi kukanyaga? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaomba sana, tuna matatizo ya miundombinu, barabara siyo nzuri ya kupita Kasesya. Sasa Wizara hii kama inataka kutuwezesha sisi tufanye biashara kwa urahisi na Zambia, tusaidieni kuzungumzia kuhusu suala la umeme na pia kuhusu maji, tuvipate ili tuweze kufanya na sisi biashara kama Watanzania wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme huo ambaa una-*fly-over* unaingia katika Mji wa Sumbawanga, maana yake ni kwamba, alizeti itoke Vijijini ije Mjini Sumbawanga ndipo isindikwe na mpunga utoke Bonde la Ziwa Rukwa uje Sumbawanga ndiyo uje ukobolewe, uwe mchele ili uweze kuuzwa mahala pengine. Lakini umeme huu ungefika katika Vijiji ninavyovieleza hapa ni kwamba, usindikaji ungefanyika kule kule Vijijini na wasingelazimika kusafirisha magunia kwa magunia kuyaleta Mjini kuyasindika. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ambaye wewe unataka kutuwezesha sisi ili tuweze kufanya biashara, unayo maoni gani kuhusu suala hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* Sumbawanga imesamaratika, vifaa vyake vingi vimeuzwa, majengo yake mengi yamekodishwa kwa watu binafsi na mambo mabaya yamefanyika. Mashine zilizokuwa zimeletwa miaka mingi iliyopita zikawekwa pale kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Mkoo wa Rukwa zimeng'olewa zimepelekwa Dar es Salaam na mfanyakia biashara mmoja, jamani hivi sisi hatuhitaji huduma katika nchi hii? Tunayotendewa ndiyo hayo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, unasema nini kuhusu masuala kama haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nazungumza kwa uchungu kwa sababu wakati mwingine mambo yanayofanyika ni kuonekana kwamba, tuko pembezoni ndiyo maana hatutiliwi maanani lakini tukitiliwa maanani tutazalisha zaidi na nchi hii itafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu angalia kuhusu suala la upungufu wa chakula katika nchi hii. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa mpango wake walau wa *subsidiize* kwenye mbolea, itatusaidia sana. Sasa na Wizara ya Viwanda na Biashara inatusaidiaje ili walau tuweze kufanya biashara katika mazingira mazuri tuisitofautiane na Watanzania wenzetu eti tu kwa sababu tuko mbali na hakuna mtu ambaye hataki hata kufika katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu maelezo machache kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu masuala haya ili na sisi tuweze kupata unafuu wa kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwanza kabisa, napenda nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kusema ya kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Maraisi wote wawili, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa utulivu uliokuwepo nchini, ambaa unatuwezesha kufanya biashara kwa amani, *there is no trade without peace*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara nyingi zinashindikana nchini kutokana na riba kubwa zinazotozwa na Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, *export credit facility* ameitaja katika hotuba yake na napenda kukumbusha tu kwamba, wenzetu nchi za nje wanapewa *export subsidy facility*, kwa hiyo tuwe imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji wa leseni za biashara, ningependa kuishauri Wizara ipunguze urasimu, *everything should be under one roof*, wakati huu ni wakati wa sayansi na teknolojia wenzetu wana *paperless office*.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi vimefeli na ambavyo vimebinafsishwa na hii inaashiria ya kwamba Serikali isijiingize katika biashara, *the business of Government is to stay out of business*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza ubinafsishaji kwa kuleta mabadiliko ya uchumi na kuchangia katika mapato ya Serikali. *PSRC should move world wide*, iwe inavitangazia viwanda ambavyo vinabinafsishwa nchi za nje siyo hapa Tanzania tu kwa mfano, Hoteli ya Kilimanjaro imenunuliwa na mfanyakbiasara wa *UAE*. Napenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Biashara cha London kiitangaze *EPZ* siyo kinatangaza mambo ya utalii na mengine tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuipongeza Wizara kwa kuipa sekta binafsi kipaumbele, kwa kuijengea mazingira mazuri. Sekta ya biashara imechangia takriban asilimia 17 ya Pato la Taifa. Bila ya uchumi mzuri nchi yetu itayumba. Biashara na Serikali ni kama ndugu waliokuwa mapacha lazima vitegemeane. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nzuri ni muhimu kwa ukuaji wa biashara, *easy transportation make the business easier*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), kupewa shilingi milioni 50 ni kidogo sana kwa ajili ya kuiendeleza *EPZ*, *less effort is done to promote EPZ*. Ningependa kuishauri *NDC* ipigwe jeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *WTO* na *GATT*, *World Trade Organization* na *General Agreement of Trade and Tariff*, vyombo hivi si vyetu, tushirikiane navyo, lakini tusivikumbatie sana kwa sababu wenyewe wana msemo wanasesma, “*when the going get tougher the tougher get going*”. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *AGOA*, *EBA* na *PACT* ya Canada ukitazama bado Tanzania hatujavitumia ipasavyo. *Export under AGOA* mwaka 2001 ni dola 16,000 tu na mwaka 2003 ni dola 540,000, wenzetu Kenya mwaka 2002 dola milioni 50, Afrika ya Kusini ndiyo inayofaidika. Ukiangalia lazima tuangalie *the high cost of production*, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani mojawapo ikiwa ni umeme, malighafi na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, urekebishihi wa mfumo wa kodi ni muhimu sana na *customs union is not a joke*, tujipime kwanza. Nashukuru ni jambo zuri tuungane lakini kuna *East African Community Market* na pia kuna *SADC Market* na sisi ndiyo kama mnavyoona viwanda vyetu vinayumba, bado tuna gharama za juu; je, tutaweza kushindana na viwanda vya nchi za jirani au tutakuwa tayari tuwe wa mwisho ili tuwe tunauza bidhaa zao? Nunua bidhaa za Tanzania uijenge Tanzania! Wazalishaji wa bidhaa watangaze bidhaa zao, kuuza bidhaa bila ya kutangaza ni sawa sawa na kutongoza kwenye giza. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri huu ni wakati muafaka wa kudumisha biashara baina ya pande mbili za Muungano yaani Tanzania Visiwani na Tanzania Bara. *Zanzibar Mainland Trade Route should be promoted, right now is a right time*. Tukomeshe ule msemo unaosema kwamba, Zanzibar ni njia ya panya, msemo huo umeshapitwa na wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, kwa kazi nzuri. Ahsante sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Kicheko/Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu mno katika vita vya kupambana na umaskini iwapo kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa kusindika matunda na mboga mboga. Pili, kujikomboa kwa nchi hii ni kuwekeza katika miundombinu na hata *EPZ* ilenge kujenga barabara zenyenye kuelekea kwenye soko la *Mtware Corridor, Western Corridor*, kwenda nchi za Zambia, Rwanda, *DRC*, Burundi na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawatachia kheri. Naunga mkono hoja hii.

**BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na Mungu awajalie. Kwanza, ombi la kusaidia uanzishaji wa viwanda vidogo katika maeneo yenye ardhi ndogo na wingi wa watu kama Ukerewe. Tunaomba mtaa wa *SIDO*.

Pili, Ukerewe itapata umeme mwezi Oktoba, 2004 saidieni mbinu kwa wavuvi kupata kiwanda cha samaki kuondoa *middlemen* wa Viwanda ambao ndiyo wanaiza samaki nje ya nchi na kupata faida kubwa na *forex*.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa makini na umahiri mkubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri na hivyo naiunga mkono hoja hii. Lakini nashauri kwamba, kwa kuwa Watanzania wengi hawana utamaduni wa kufanya biashara na nchi nyingine, Wizara iandae mpango mahsus wa kuwafundisha Watanzania *Entrepreneur Skill* za kuweza kuwekeza na kuuza bidhaa mbalimbali nje zikiwemo zile za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wawekezaji ni wababaishaji na matapeli, wengine wanapata mitaji yao kutokana na madawa ya kulevyta. Kwa hiyo, sharti Wizara iwe na *Economic Intelligence System*, itakayowezesha kutoa tahadhari mapema ili kuiwezesha nchi kuepukana na utapeli wa kibiashara ambao unaweza kujitokeza kwa kivili cha utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maeneo ya pembezoni mwa nchi kama vile Mbinga, ambayo infanya biashara na chi jirani za Malawi na Msumbiji. Je, Serikali inaweza kutusaidia ili biashara isiyo rasmi ambayo imeshamiri ikahalalishwa na hivyo kuendeleza biashara hiyo.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii, kwa namna walivyochambua hotuba na yenye mwelekeo mzuri na matumaini ya kutuletea maendeleo kwenye Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nijielekeze kuchangia sehemu ya viwanda vya ndani hatuna budi kuvilinda kwa nguvu zote kwa maslahi ya Taifa. Hivi sasa wapo wafanyabiashara kutoka nje wanaoingiza bidhaa ndani ya nchi yetu bila ya utaratibu wa kisheria, hivyo kudhalilisha bidhaa za ndani, lakini zaidi wanaikosisha Serikali mapato ya fedha nyingi. Imebainika kwamba, sigara nyingi zinaingizwa nchini kinyemela tena kwa kasi kubwa sana, *Sportsman* na *Sweet Menthol*, kitu ambacho kinahatarisha mpaka afya za wavutaji kwa sababu pengine hazikaguliwi na *TBS*. Katika suala hili Serikali lazima iliangulari kwa uangalifu ipasavyo, katika nchi jirani zetu wafanyabiashara wa aina hii

wanafukuzwa, hivyo wasiwasni wangu ni kuwa hivi sasa wamekimbia kwetu. Inavyosemekana kuna Kampuni moja inayoitwa *Master Mind* hujihisisha sana na masuala haya ya biashara haramu ya sigara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naishauri Serikali itumie mbinu za kitaalamu kuwashamasisha wananchi kijiunga pamoja na kuanzisha viwanda vidogo vidogo Mijini na Vijiji ili kulenga katika kujitegemea na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono tena hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii kwa mashirikiano yao mazuri katika kuiongoza Wizara hii kwa kushirikiana pia na Maafisa wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kweli imejitoa katika uendeshaji wa biashara, lakini napenda kuishauri Serikali isiwe mbali sana na ukaguzi wa viwanda ili kuona kwamba, uendeshaji hasa katika usalama wa wafanyakazi unafuatwa, hii ni kutokana na ukweli kwamba, usalama kazini ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupigana na suala la kuondoa umaskini, lazima Wizara hii iongeze mtandao wa kuwaelimisha wananchi juu ya soko la *AGOA*, sisi kwa kuwa ni wanachama tunapaswa tushiriki kikamilifu, hivyo Wizara ina jukumu kubwa la kuhamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna budi kuvilinda viwanda vya ndani kwa nguvu zote kwa maslahi ya Taifa, hivi sasa wapo wafanyakaziwa kutoka nje wanaoingiza bidhaa ndani ya nchi yetu bila utaratibu wa kisheria, hivyo hudhalilisha bidhaa za ndani, lakini zaidi wanaikosesha Serikali mapato ya fedha nyangi. Imebainika kwamba, kuna sigara nyangi zinaingizwa nchini kinyemela tena kwa wingi sana, *Sportsman* na *Sweet Menthol*, kitu ambacho kinahatarisha mpaka afya za wavutaji kwa sababu pengine hazikaguliwi na *TBS*. Katika suala hili Serikali lazima iliangularie kwa uangalifu sana. Katika nchi za majirani zetu wafanyakaziwa wa aina hii wamefukuzwa, hivyo wasiwasni wangu ni kuwa hivi sasa wamekimbia kwetu. Inavyosemekana kuna Kampuni moja inayoitwa *Master Mind* hujihisisha sana na masuala haya ya biashara haramu ya sigara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi wanayo matumaini makubwa katika sera ya biashara ya *EPZ* ambayo Wizara hii tayari ina mikakati nayo, ingependeza kama wananchi wakaelezwa hatua kwa hatua katika uendeshaji wa biashara hii ambayo ikifanikiwa tutakuwa tumepiga hatua.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itumie mbinu za kitaalamu kuwashamasisha wananchi kijiunga pamoja na kuanzisha viwanda vidogo vidogo Mijini na Vijiji ili kulenga katika kujitegemea na kupiga vita umaskini. Ahsante.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumponegeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, inayoleza utendaji mzuri na mwelekeo wa Asasi nyangi zilizo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu inafanya juhudini kubwa ya kuvutia wawakezaji katika shughuli za Viwanda na Biashara, zoezi ambalo linaungwa mkono na wananchi kwa matumaini kwamba, litafanya maisha yao yawe bora zaidi. Lakini imani hii ya wananchi inaweza kutiwa doa iwapo sera ya Viwanda na Biashara itakaa kimya juu ya kuwashirikisha wananchi katika umiliki wa hisa katika Viwanda na Biashara hizo. Lazima katika sera ielewewe kuwa katika kiwango fulani cha ukuaji wa kampuni za kigeni, hisa fulani lazima ziuzwe kwa wananchi, hili ni lazima liwe jambo la kisera. Katika kipindi cha faida napendekeza kuwa asilimia 51 ya hisa iwe ni kampuni za kigeni lakini asilimia 49 iwe ni hisa za wananchi wa kawaida. Pamoja na kwamba makampuni kama *TBL*, *TCC* na kadhalika, yanafanya biashara ya kuuza hisa katika soko la hisa la Dar es Salaam. Lakini hisa hizo zinazouzwa ni mzunguko wa

hisa zilizokuwa za Serikali zikauzwa kwa wananchi. Nadhani ifike mahali Makampuni hayo yawekewe utaratibu wa kuuza hisa zake kwa wananchi ili nao washiriki katika kumiliki uchumi wa nchi yao. Niipongeze sana Kampuni ya Chai Bora kwa kuwa kampuni ya kwanza binafsi kuwauzia wananchi hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 34 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, kwa sasa kuna dalili za kumpata mwekezaji mahiri katika Kiwanda cha *SPM-Mgololo*. Pamoja na kupongeza juhudhi hizo za Serikali ni dhahiri kuwa mwekezaji huyo bila shaka atakuja na mtaji ambao hautapungua Dola za Kimarekani 30 milioni, hiki kikiwa ni kiwango cha chini kabisa cha fedha kitachofanya *SPM-Mgololo* ifanye kazi yake kwa ufanisi. *SPM-Mgololo* kwa sasa haiangaliwi kwa maslahi ya kiuchumi tu lakini zaidi inaangaliwa kwa maslahi ya kimazingira kwani makosa madogo yanaweza kusababisha janga kubwa kwa maisha ya binadamu na mazingira. Vipo viwanda vilivyotelekezwa baada ya kununuliwa, madhara yake tunayashuhudia, lakini ni madhara ya kiuchumi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inatujibu swali letu Bungeni ilisema kwamba, zitahitajika fedha kiasi cha Dola za Kimarekani 40.0 milioni, kuharibu madawa ya sumu yaliyoko *SPM-Mgololo* iwapo Serikali itaamua kukifunga, je, iwapo Serikali itamuuzia mwekezaji wa kiwango cha chini nani atagharamia uondoaji wa madawa hayo iwapo mwekezaji huyo atashindwa kukiendeleza *SPM-Mgololo*, asipewe mtu wa kubahatisha, makosa ya kuibinafsisha *SPM* yataiingiza nchi katika historia mbaya, historia inayoweza kuepukika nadhani na ni imani yangu kubwa kuwa ufumbuzi uliopo kwa sasa ni Serikali kutoa fedha Dola za Kimarekani 2.8 milioni ili kiwanda kile kiendelee kufanya kazi wakati mwekezaji anatafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa namna ya pekee kwa namna inavyoisaidia *SPM-Mgololo*. Kwa kweli Serikali yetu imekuwa jirani sana kusikiliza matatizo mbalimbali ya *SPM-Mgololo* na naamini hata hili la mwekezaji mwenye uwezo anayetafutwa kuendesha *SPM-Mgololo* tutakuwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mwelekeo sahihi katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Sekta ya Biashara. Aidha, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa na Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri sana wanayofanya kuendeleza, kusimamia na kuratibu shughuli za Wizara hii. Hotuba ya leo ya Bajeti na mafanikio makubwa ya *Dar es Salaam International Trade Fair* mwaka huu wa 2003 ni vielelezo vizuri vya juhudhi hizi. Naipongeza sana Serikali na Wizara hii kwa mfano huu unaong'ara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa ni soko kubwa la bidhaa ambazo hazina ubora, bidhaa za kughushi na bidhaa feki. Bidhaa hizi zimekithiri katika sekta ya spea na vipuri vya magari, matrekta na mashine. Aidha, matairia na *tube* feki zimejaa nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inahatarisha walaji. Ninaipongeza Serikali kwa dhati, kwa mapendeleko yaliyomo kwenye Bajeti ya Wizara hii, kwa mpango wa kudhibiti mpango huu. Ninaiomba Serikali ilipatie nyenzo zaidi Shirika la Kuhakiki Viwango (*Tanzania Bureau of Standards*), ili liweze kulitatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika wa kuwa na chombo thabiti cha kuwalinda walaji katika biashara. Nimeeleza juu ya ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni bei ya bidhaa. Katika eneo la bei, kuna udanganyifu mkubwa sana hasa katika bei za magari mapya hususan yale ya *Four Wheel Drive* na *Saloon Vehicle*. Aidha, bei za mabasi, malori na magari mengine yakiwa mapya, bei zake kabla ya kodi ni kubwa mnaji kulinganishwa na bei ya magari hayo (*CIF Dar es Salaam*) huko yanakotengenezwa ukiweka Bima na bei za usafirishaji mpaka *Dar es Salaam*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gari ya *Toyota Land Cruiser (VX)* mpya kutoka *Africa Division* ya *Toyota International Tokyo CIF Dar es Salaam* sio zaidi ya Dola za Kimarekani 18,000/=. Lakini bei

ya gari kama hilo kutoka kwa wasambazaji hapa nchini karibu Dola za Kimarekani 40,000 (kabla ya kodi). Hii ni pamoja na ukweli kuwa mapato ya wasambazaji yanatokana na *commission* na haitegemewi kuhusisha uongezekaji wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya aina nyingine ya magari kuanzia magari madogo mpaka makubwa, mabasi malori na kadhalika ni kama mfano nilioutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya bei hizi za kuruka za magari ni pamoja na Watanzania wengi kushindwa kununua magari mapya na kununua magari mengi ya *second hand (used cars)*, ambayo ni hatari kwa mazingira, afya zetu na matumizi makubwa ya spea. Vyote vinaathiri sana uchumi wetu. Pili, kwa kuwa Serikali ni mnunuzi mkubwa wa magari mapya, bei hizi za kuruka zinaumiza sana uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iunde chombo thabitii cha kuangalia suala hili. Niko tayari kuishauri Serikali kwa karibu ili kutekeleza azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo kupitia *SIDO*. Wananchi wa Mwanga wamenituma nikuombe rasmi, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, utuweke kwene Wilaya zitakazofaidika na Mfuko huu. Aidha, tunakukaribisha Mwanga, ujionee mwenyewe faida itakayotokana na Mfuko huu. Hongera sana.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, pamoja na uongozi wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie yafuatayo: Kwanza, kuhusu uingizaji wa sigara kutoka nje ya nchi yetu kinyemela. Hivi sasa kumejitokeza uingizaji wa sigara nchini hapa kwa njia ya magendo, sigara hizo zinatoka Uganda, Kenya na nchi nyingine mbalimbali. Hivyo basi, naiomba Serikali kuchukua hatua za makusudi kuzuia uingizaji huo. Kwa kuwa uingizaji huo wa sigara huletwa kwa njia ya magendo na unaikosesha Serikali mapato Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuzuia uhalifu huo.

Jambo lingine ninalopenda kulizungumzia ni Kiwanda cha *UFI* cha Dar es Salaam, kiwanda hiki kimekufa kwa muda mrefu sasa, je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni Kiwanda cha Urafiki Dar es Salaam. Kiwanda hiki Serikali yetu imejiwekea ubia na Serikali ya China, lakini hakuna faida inayopatikana. Sasa naiomba Wizara ifuatilie ili faida ipatikane. Vilevile wafanyakazi wetu wananyanyaswa sana kwa sababu wenye sauti ya kiwanda hicho ni viongozi kutoka Jamhuri ya watu wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Rita Mlaki na Maafisa wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanazofanya kwa ushirikiano wa hali ya juu na hivyo naunga mkono hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2003/2004 mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kuhusu hoja hii ni kupata ufanuzi kuhusu maombi maalumu katika kuboresha biashara ndogo ndogo kama ifuatavyo:-

Moja, kuna baadhi ya Viwanda vyta Nguo vinatengeneza vitenye kwa nyuzi za khanga lakini wanauza kwa bei kubwa kuliko ya khanga. Je, Wizara hii inafuatiliaje ubadhirifu wa aina hiyo na ushahidi upo?

Pili, Viwanda nya Sufuria, Vijiko na kadhalika, huko ndiyo dhuluma tele. Unapakua chakula kwa kijiko lakini kinakunjika ndani ya bakuli la chakula. Cha kusikitisha utaona alama ya *TBS* imegongwa katika vyombo hivyo. Wananchi watawezaje kujiondoa katika umaskini iwapo kila mwezi watalazimika kununua vyombo nya nyumbani? Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ufuatilie na kuwaagiza Maafisa wako waweke utaratibu wa kukagua viwanda hivyo. Hali kadhalika ubora wa baisedeli haupo kwa baadhi ya baisedeli nchini na wananchi wanangu'unika baisedeli zinachakaa na kuwapa hasara ya kununua baisedeli mara kwa mara.

Tatu, Kiwanda cha Sungura Gongolamboto kimejenga Msiki ndani ya Kiwanda kwa ibada za wafanyakazi wa Kiislam na wamiliki wa kiwanda hicho.

Je, watakapoacha kuendesha kiwanda hicho msiki huo wataubomo au mwekezaji akiwa Mkristo naye atajenga kanisa, hii ni sahihi? Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ufuatilie nani kamruhusu kuweka mambo ya dini eneo la kazi? Nataka majibu.

Nne, Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wanashindwa kushiriki Maonesho ya Kitaifa wakati wa Sabasaba kutohana na uchumi duni unaowakabili. Kwa hiyo, nakuomba uone uwezekano wa Wizara yako kutoa uwezesho kwa akinamama kifedha, malazi na usafiri kama anavyofanya Mwenyekiti wa Fursa Sawa kwa Wote, Mama Anna Mkapa, ili waweze kuja wengi kwani Sabasaba ya mwaka huu mabanda yalikuwa wazi kwa sababu hiyo hiyo.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii tena mia kwa mia.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Wilaya ya Kongwa wanalima mazao ya karanga, alizeti, nyanya na kadhalika. Mazao ambayo kwa kiasi kikubwa yanahitaji viwanda vidogo vidogo na nya katika *processing* na *packaging* na masoko ya ndani na nje ya nchi. Pia tunalima mahindi sana, tunahitaji uwezeshwaji wa *processing* na *packaging* na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunasikia upo mfumo maalum na mipango ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa wananchi, ninaomba Wizara iwasiliane na mimi ili tuwawezeshe wananchi. Sehemu kadhaa za Wilaya ya Kongwa tayari zina umeme na maji ya uhakika na Wilaya ina *tractors 200* na plau zaidi ya 3,000, tukiwapa nafasi wananchi wanaweza kufanya maajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba na mipango mizuri ya maendeleo ya Sekta hii kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza mchango wangu kwa kutoa kauli tatu muhimu zitakazoonyesha umuhimu wa mawasiliano katika biashara. Kauli ya kwanza, ni kauli ya Wizara inayosema: "Ingawa kilimo ndiyo msingi wa uchumi, viwanda ndiyo sekta kiongozi".

Kauli ya pili, ni kauli ya viwanda inayosema: "Nunua bidhaa za Tanzania tujenge Tanzania".

Kauli ya tatu, ni kauli ya walaji inayosema: "Tunataka bidhaa bora kwa bei nafuu".

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hizo zinaonyesha mahusiano makubwa katika biashara, lakini inafundisha zaidi viwanda kwamba bidhaa zao zilenge mahitaji ya mlaji, mahitaji ya ubora wa bidhaa ikiwi ni pamoja na ubora wa vifungashio (*packages*) na bei nafuu. Yakizingatiwa hayo, lengo la viwanda litafanikiwa kwanza kwa kutosheleza soko la hapa nchini na baadaye kuvuka mipaka na kuuza nje ya nchi na hivyo kukua kwa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la viwanda vidogo vidogo limeanza kuboreka na kukua. Vikundi mbalimbali nya akinamama na vijana katika Wilaya mbalimbali vimepata mafunzo ya usindikaji wa mazao ya kilimo na matunda kwa msaada wa *SIDO, UNIDO* na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine cha Morogoro. Wilaya ya Muheza ina vikundi kama hivyo na vimeboreka sana kielimu na vikundi hivyo vinaonekana katika kushiriki katika Maonyesho mbalimbali ya Biashara Dar es Salaam na Maonyesho ya Kilimo Morogoro. Vikundi hivi sasa vinahitaji utekelezaji wa sera ya Wizara “Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi”

Mheshimiwa Naibu Spika, tusaidiane katika kuwatafutia mashine za viwanda nya kati nya usindikaji ili waweze kufikia viwango nya ubora na viwango nya uzalishaji vitakavyoweza kuhimili gharama za uzalishaji na kupata faida ya shilingi 30,000,000/= kiwango ambacho hawawezi kumudu bila msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Muheza kazi ya kwanza ni kuunganisha vikundi vilivyopo ili kupata idadi kubwa ya wanahisa katika mtaji utakaotafutwa. La pili ni kuwasaidia kuunda kampuni ya kiwanda chao na kukisajili. La tatu, ni kuwatafutia mkopo wa mtaji na kuwatafutia mashine kwa kiwanda chao cha uzalishaji na jengo la kiwanda. La nne ni kuwapa msaada wa utalaamu wa kuzalisha na kusimamia kiwanda, uhasibu na masoko. Kwa kuwa Wilaya ya Muheza ina uwezo wa kukaribia utekelezaji wa hatua nilizotaja hapo juu, basi naomba wahisani waliopo *SIDO, UNIDO* na wengine, waelekeze nguvu zao kwa vikundi nya akinamama na vijana wa Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napendekeza sasa Wizara ya Viwanda na Biashara, iwe na Idara au Kitengo maalumu kitakachowajibika kuwasaidia vikundi vidogo kuandika michanganuo na mpango wa biashara ili kusaidia kukuza sekta ambayo itasaidia sana kuondoa umaskini na kupunguza tatizo la ajira kwa akinamama na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, pamoja na watendaji wao, kwanza kwa utendaji mzuri wa shughuli zote za Wizara na pili kwa kuandaa hotuba ya Bajeti kwa umahiri sana. Maoni yangu ni machache nayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, viwanda vilivyobinafsishwa Morogoro, vingine vinafanya kazi wakati vingine vimefungwa tangu viuzwe. Viwanda hivi ni *Tanneries, Magunia* na *Morogoro Shoe Company*, ambayo ilifanya kazi na baada ya muda mfupi kiwanda kiliungua katika mazingira ya utata. Mpaka leo hii kiwanda hiki kimefungwa na hatma ya wafanyakazi wake haijulikani. Mpaka sasa hivi hao wafanyakazi hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara itoe maelezo ya hatma ya kiwanda hiki. Imekuujie kiwanda kiungue halafu mmiliki au mbia aondoke kimya kimya na kuanza kuwekeza katika sehemu nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vingine vidogo vidogo ambavyo havifanya kazi. Ningependa kuomba Wizara iangalie namna ya kuwapa Wazalendo au vikundi ambavyo vitaweza kuvitumia kwa shughuli za uzalishaji, pamoja na kutoa mafunzo kwa vijana wetu hususan watoto yatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri kwamba, shughuli za *SIDO* zipelekwe vijijini ili kuongeza ajira, pamoja na kuboresha hali ya maisha ya wananchi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa hotuba nzuri, yenye ufanuzi na mwelekeo mzuri.

Aidha, nawapongeza sana Watendaji wa Wizara hii chini ya Katibu Mkuu Bwana Ahmad Ngemera na wafanyakazi wote wa Mashirika, Makampuni na Taasisi mbalimbali, pamoja na Jumuiya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, baada ya pongezi hizo nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Viwanda, naipongeza Serikali kwa kujitahidi kuweka mazingira mazuri ili kutoa nafasi kubwa ya kuchangia katika ajira, kuongeza kipato, hatimaye kupunguza umaskini. Naipongeza Serikali kwa kufanikisha sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Hii itawasaidia sana wanaviwanda na wafanyakishi wadogo wawe na ufahamu na mwelekeo wa vipi wanatakiwa wajitahidi ili waweze kumudu ushindani wa soko huria. Ni matumaini kuna tafsiri ya Kiswahili kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, itatolewa mapema na kusambazwa kwa wafanyakishi wadogo na wenye viwanda ili waelewe hasa wale walioko vijijini na miji midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu na unyeti wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara na kupanuka kwa wigo wa maeneo ya kuhudumia wananchi hususan walioko vijijini, inashangaza kuona Serikali imepunguza Bajeti ya Wizara tofauti na ile Bajeti ya 2002/2003. Tunaomba Serikali kama kweli ina nia ya kutekeleza sera ambayo sasa imekamilika ya biashara na viwanda, iwe *serious* na kuiwezesha Wizara kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa huduma za teknolojia, utafiti na ushauri, licha ya Wizara kuwa ndio waratibu wakuu bado Serikali haijaonyesha dalili za kudhamiria kuboresha uratibu. Mgao wa fedha za maendeleo kwa *TIRDO*, *TEMDO*, *CARMATEC* na *SIDO* ni mdogo sana kuwezesha kufanya kazi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mchango wake mkubwa kwa *SIDO*. Ni ukweli *SIDO* ina mtandao mkubwa hadi Mikoani na wengi wanaanza sasa kuifahamu *SIDO* hivyo, kuvutiwa kutaka kuitumia *SIDO*. Sasa Mheshimiwa Waziri, jambo la kushangaza ni kuona Bajeti aumgao wa *SIDO* umepunguzwa kwa asilimia zaidi ya 50. Mimi nilidhani kwa mwaka uliopita, Serikali ilipowapatia fedha kwa vile tulikuwa tunazindua/kujenga upya *SIDO*, sasa ingeongezewa nguvu iendelee vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia *SIDO* kwa kushurikiana na *CARMATEC*, *TEMDO*, *TIRDO* na *EOTF* na kadhalika, kwa kujitahidi kuandaa maonyesho mbalimbali ya kikanda na hata ya Kimataifa. Hii inasaidia kuwahamasisha wanaviwanda vidogo hasa wanawake kujitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora wa bidhaa, nashauri Serikali iweze kufanya utaratibu mzuri na kuwapatia nembo ya *TBS* kuuzia bidhaa zao ili ziwe na ubora, wafanyakishi wanashindwa kuuza bidhaa kwenye *supermarkets* kwa vile hazina viwango vya ubora, matokeo yake unakuta bidhaa nyingi toka nje na zetu zinakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa Mfuko wa Udhmini wa Uuzaji wa Mazao Nje (*Export Credit Guarantee Scheme*). Ni matumaini kwamba, ukishirikiana na watalaamu wote, watashirikiana sana ili kuwezesha wanaviwanda na wafanyakishi waweze kuwawezesha kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa lakini suala la wale wawekezaji kwenye viwanda na kuvitelekeza, naungana na wenzangu, Serikali iwafuatilie kwani maeneo mengine wawekezaji wasioendegeza uwekezaji wao, wanachangia kurudisha maendeleo ya maeneo yale yenye kuwekezwa. Hivyo, asiyeweza basi Serikali imbane na hata kumnyang'anya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza tena Serikali bila kusahau *UNIDO* kwa kusaidia sana *SIDO* katika nyanja za usindikaji wa vyakula na hasa wanawake wengi wanahuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naomba sasa nielekeze mchango wangu kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Kiwanda cha Nguo Mbeya (*Mbeya Textile Mills*), moja kati ya vigezo vya kuwepo kiwanda hiki ilikuwa ni upatikanaji wa malighafi (*Raw Materials*) za kusindika katika kiwanda hiki. Kwa kiwanda hiki pamba iliyokuwa inalimwa Chunya na Mbeya Vijijini ndiyo iliyokuwa malighafi muhimu kwa uzalishaji wa kiwanda hiki. Yafuatayo yamejitokeza dhidi ya kiwanda hiki:-

(a) Kuongezeka kwa gharama ya kufuata malighafi Mwanza na wakati mwingine kuagiza toka Nigeria na Cameroon, hivyo gharama za uzalishaji kuongezeka. Hii yote imesababishwa na Serikali kuzuia kilimo cha pamba Mbeya. Je, Wizara inatengeneza mazingira gani bora ya kukiokoa kiwanda hiki?

(b) Kupungua kwa ajira mara baada ya kuzuia kilimo cha pamba Mbeya, hivyo kiwanda kiliamua kupunguza wafanyakazi 200 kwa sababu mzigo wa malighafi ulipungua.

(c) Baadhi ya mashine zilikosa kazi ikiwemo mashine ya *grey fabric*, ambayo sasa ameikodisha kwa *Mwatex*, ukodishaji huu wa mashine ndiyo uliozua uongo kwenye magazeti kuwa mwekezaji ameng'oa mashine na kuipeleka nje ya nchi. Rejea magazeti yafuatayo:-

(i) *The Guardian May 27, 2003, Editorial Comments* yenye heading “*Rogue investors should be dealt with.*”

(ii) *The Guardian 4 June, 2003* yenye kichwa “*The dirty side of Privatization...*”

(iii) *The East African, June, 2 - 8* yenye kichwa “*Dar May repossess privatized companies.*”

*“In Mbeya and Kiimanjaro regions for example, some of the privatized factories have been looted and vandalized.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni kwamba, kwanza, maelezo haya yalikuwa sahihi? Je, utafiti wa kufika kiwandani ulifanyika au ni njama za kutaka mwekezaji huyu aondoke Mbeya?

Pili, je, Mazingira ya *Mbeya Textile Mills* ya kuzuia Mkoa wa Mbeya kulima pamba ambayo ni malighafi ya kiwanda, yanachukuliwa vipi na Wizara ya Viwanda na Biashara. Hivi si jukumu la Wizara hii kuhakikisha viwanda vyote vina *thrive* ili kuongeze tija na Pato la Taifa?

Tatu, je, maamuzi yetu ya haraka pengine ya bila *research* ya uhakika huoni kwamba yanachangia kuua uchumi wa nchi na hatimaye kuwanyima ajira watu wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya (ZZK), aliyekuwa Makamu wa Rais, Marehemu Dr. Omar Ali Juma, alikitembelea kiwanda mwaka 1999 na alitoa ahadi ya kuhakikisha madai ya wafanyakazi yanalipwa haraka. Je, Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, ni lini watu hawa watalipwa stahiki yao kama alivyoahidi Makamu wa Rais? Pia ni lini kiwanda hiki kitapata mwekezaji na kuanza tena uzalishaji?

Kufa kwa Viwanda Jiji la Mbeya, zaidi ya viwanda 10 mpaka sasa havifanyi kazi vimefungwa sababu moja ikiwa ni kukosa malighafi na mitaji ya kutosha mfano, *Mbeya Industries, Mbeya Ginneries, Highland Ginneries, Hisoap, Mbeya Oil Mills*. Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yako umetamka kuwa Mbeya nayo ni mojawapo ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ* utekelezaji upo vipi? Ni nani mwenye jukumu la kuwasiliana na *NDC*. Kuanza kwa *EPZ* kutasaidia ajira kwa vijana na kuirudisha Mbeya katika hali yake ya uchangamfu na kuinua uchumi wa nchi na wa kipato binafsi.

Nne, Mheshimiwa Waziri, vijana wetu wengi wakiwemo vijina wangu wa *SOWETO* Mbeya, wanajibidiisha sana kufanya kazi na biashara yao kubwa ikiwa ni uingizaji wa matairu kukuu, hata hivyo, ushuru wanaotozwa ni mkubwa mno.

Je, Wizara ipo tayari kuliangalia hili ili itengeneze mazingira ya kuwafanya vijana wajajiri na hatimaye kuinua kipato chao na cha Taifa vile vile?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuhakikisha viwanda na biashara vinaleta tija kwa Taifa letu. Nawatakia maisha marefu Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ili muendelee kutuongoza.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kutoa nafasi hii ili nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri, ilioandaliwa vizuri, kwa ushirikiano mzuri wa Katibu Mkuu wa Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nipate jibu hapa Bungeni juu ya uvumi uliozagaa wa sigara bandia zinazoharibu uchumi wa nchi yetu, afya za Watanzania wanaotumia sigara na juhudzi za wawekezaji kupanua huduma yao hapa nchini. Je, ni kweli na hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti nilioufanya Jijini Mwanza, Ofisi Kuu ya Sigara Tawi la Mwanza, walinithibitishia kuwa ni kweli tatizo hilo lipo na hali hivi inatishia kuharibu soko la sigara kwani wanatumia nembo ile ile ya *T.C.C.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi kupata jibu toka kwa Waziri wakati wa majumuisho yake, kwani taarifa za malalamiko haya zilishafikishwa Ofisi kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kero hiyo bado nasema kuwa Wizara hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na nina imani na Waziri na Naibu wake, hivyo naunga hoja mkono kwa asilimia 100. Nawatakia heri na mafaniko mema katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie suala la Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*). Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 38, ameelezea umuhimu wa chuo hiki lakini pia amezungumzia matatizo yanayokikabili chuo hiki. Naiomba sana Wizara iangalie katika Bajeti yake ili kukiweka Chuo katika hali inayoendana na umuhimu wake.

Mfano lengo lake kwa sasa linahitaji ukarabati wa hali ya juu baada ya kuathirika na tetemeko lililotokea. Mwaka 2002 hapa Dodoma, watumishi na wanafunzi ni hatari kama halitafanyiwa matengenezo, naomba sana hilo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru tena naomba Wizara iruhusiwe kutumia pesa ilizoomba. Ahsante sana.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kutoa nafasi hii ili nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri, ilioandaliwa vizuri, kwa ushirikiano mzuri wa Katibu Mkuu wa Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nipate jibu hapa Bungeni juu ya uvumi uliozagaa wa sigara bandia zinazoharibu uchumi wa nchi yetu, afya za Watanzania wanaotumia sigara na juhudzi za wawekezaji kupanua huduma yao hapa nchini. Je, ni kweli na hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti nilioufanya Jijini Mwanza, Ofisi Kuu ya Sigara Tawi la Mwanza, walinithibitishia kuwa ni kweli tatizo hilo lipo na hali hivi inatishia kuharibu soko la sigara kwani wanatumia nembo ile ile ya *T.C.C.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi kupata jibu toka kwa Waziri wakati wa majumuisho yake, kwani taarifa za malalamiko haya zilishafikishwa Ofisi kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kero hiyo bado nasema kuwa Wizara hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na nina imani na Waziri na Naibu wake, hivyo naunga hoja mkono kwa asilimia 100. Nawatakia heri na mafaniko mema katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie suala la Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*). Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 38, ameelleza umuhimu wa chuo hiki lakini pia amezungumzia matatizo yanayokikabili chuo hiki. Naiomba sana Wizara iangalie katika Bajeti yake ili kukiweka Chuo katika hali inayoendana na umuhimu wake.

Mfano lengo lake kwa sasa linahitaji ukarabati wa hali ya juu baada ya kuathirika na tetemeko lililotokea. Mwaka 2002 hapa Dodoma, watumishi na wanafunzi ni hatari kama halitafanyiwa matengenezo, naomba sana hilo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru tena naomba Wizara iruhusiwe kutumia pesa ilizoomba. Ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kuimarisha viwanda vyetu na kukuza biashara huria kwa wafanya biashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia juu ya viwanda vidogo vidogo, ambavyo ndiyo vingi vipo mikoani ukiwemo Mkoa wa Singida. Naiomba Serikali iweze kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kupewa mitaji ama kukopeshwa mashine kubwa ili waweze kuongeza uzalishaji na kuwa na miundombinu ya kisasa kulingana na uzalishaji mkubwa wa mazao sasa hivi wakulima, mfano, alizeti, pamba, karanga, ufuta, nyonyo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali izingatie kujenga mashine au viwanda vidogo vidogo sehemu ambazo mali ghafi inapatikana kuwapunguzia gharama wakulima za usafirishaji kwa kupeleka mazao mbali kufuata viwanda, mfano, zao la pamba linalimwa Singida na kupelekwa kuuzwa Mikoa ya Tabora na Shinyanga, hali hiyo huwakatisha taamaa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kwamba, wakulima wanajitahidi sana kulima mazao ya biashara kwa wingi kwa ajili ya kuinua vipato vyao. Pamoja na soko huria, ni vema Serikali iwatafutie soko la uhakika wakulima hao ili kuwatia moyo. Niiombe Wizara ya Viwanda na Biashara, ishirikiane na Wizara ya Ushirika na Masoko, kutatta tatizo hili. Mfano zao la alizeti halina soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sera ya ubinafsishaji viwanda na kuongeza uzalishaji, hivi sasa bado vipo viwanda vingi ambavyo vinakufa ama vimefungwa. Hali ambayo imesababisha kushuka kwa uzalishaji kwa baadhi ya mazao ya biashara na vijana wetu wengi kukosa ajira. Naiomba Serikali itoe ufanuzi, ni sababu zifi zilizofanya viwanda vifungwe mfano, Viwanda vya Magunia, Viwanda vya Mafuta (Moproko) na vingine vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo ambaa ni imani yangu kubwa nitajibiwa na Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho yake, kwa lengo la kuleta faraja kwa wakulima, wafanyabiashara wa Singida na Taifa kwa jumla, naomba nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa silimia mia kwa mia.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba semina kuhusu Mikataba ya Kibiashara ya Kimataifa ili tuielewe wazi biashara yetu na biashara ya dunia inaendelea vipi. Sisi Waheshimiwa Wabunge, tutachangia vipi kuhamasisha wananchi wetu kufanya biashara nje?

Naomba Wizara iflikirie kuanzisha Kituo cha Biashara Zanzibar ili Wazanzibari wafaidike na utaalamu wa Kibiashara kama vile Tanzania Bara wanavyofaidika na *CBE*, kwa kutekeleza swali hili, Wizara ya Biashara Tanzania Bara iwe na ushirikiano wa karibu na Wizara ya Biashara Zanzibar.

Tunatoa pongezi kwa mikopo ya *SIDO*, ambayo imesaidia wanawake na vikundi vyao kufaidika na mikopo hiyo. Tutashukuru likifunguliwa Tawi la *SIDO - Zanzibar*

Tunawashukuru *PSRC* kwa kutuwezesha kuelewa shughuli zote za viwandani, kwa kutusaidia kufanya ziara mbalimbali hapa nchini kwetu ili Kamati yetu kujionea wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawapongeza Wizara kwa kutuandalia Sera Mpya ya Biashara

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu na nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa juhudhi wanazozichukua kuimarishe uchumi wa nchi hii kwa kupitia sekta ya viwanda.

Mchango wangu kwa mara nyingine tena naomba nипанue uzuri wa kazi zenu hizi katika wigo mpana zaidi kwa kusaidiana na upande wa pili wa Muungano, hali ya Zanzibar kiuchumi ni mbaya sana na nadhani njia moja ya kupanua uchumi ni kuwa na mpango wa kiuchumi wa pamoja baina ya SMZ na SMT.

Zanzibar kule sasa kuna tatizo kubwa la ufunguaji wa viwanda mfano *EPZ*. Viwanda vingi vimefungwa kwa mfano, *Zanzibar Garments, Window 2000* na *Eidable Oil*. Hiki *Window 2000* kilikuwa kinatengeneza bidhaa na kuleta Dar es Salaam, lakini walishindwa kutokana na adha waipatayo pale Bandarini Dar es Salaam. Kutokana na mashaka hayo, wamehamisha Kiwanda hicho na kukileta Dar es Salaam na kuua dhana ya kuwa kuna hata wengine kule watafunga na kuja Bara hasa kwa kufuata soko.

Sasa Mheshimiwa Waziri, ningelikuwa basi mnapatwa wakati, mkakaa pamoja wewe na Waziri mwenzako wa Zanzibar, mkawa mna mipango kama nchi, kusaidiana na kupeana maelekezo.

Zaidi ya hili Mheshimiwa Waziri kuna uwezekano mkubwa kuisaidia sekta hii. Kwa umahiri mlionao mkaona kuwa vipi mnawekeza katika ushindikaji wa samaki, Zanzibar imezungukwa na bahari kila upande, saidia Mheshimiwa Waziri, kututafutia wawekezaji wa soko hilo.

Mheshimiwa Waziri, mwani ni moja katika zao linaloitokeza na kuzalishwa kwa wingi sasa Visiwani, tusaidie nalo kututafutia uamuzi wa hakika, kwani waliopo bei zao ni ndogo na zinakatisha tamaa. Ahsante.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia katika sehemu chache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*), Wakala huu hivi sasa umeboresha utendaji kazi wake kwa hali ya juu ukilinganisha na ilivyokuwa zamani. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara iharakishe kazi ya marekebisho katika Sheria ya Leseni za Biashara ili kuwaondolea kero wanazopata wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 24 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, anaeleza kuwa Kiwanda cha Nguo cha Tabora (*TABOTEX*), kimepelekwa *LART* kufilisiwa eti kutokana na madeni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kusema kuwa, imechukua muda mrefu kubinafsisha Kiwanda hiki muhimu kwa wananchi wa Tabora. Wananchi wa Tabora wanakitegemea kiwanda hiki kwa maisha yao, maana Mjini Tabora hamna kiwanda ambacho kinaweza kuajiri wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majonzi makubwa napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa katika kiwanda hicho cha *TABOTEX*, ambacho kilikuwa chini ya usimamizi wa *PSRC*, mashine karibuni zote muhimu zimeibiwa! Jambo hili limegundulika wakati wa makabidhiano kati ya *PSRC* na *LART*. Naiomba Serikali kwa ujumla wake, ipeleleze wizi huu na kutueleza mapema iwezekanavyo ni nani katuhujumu wananchi wa Tabora. Mheshimiwa Waziri, atueleze Wizara yake inafanya nini kwa wizi huu? Vile vile watueleze juhudi gani wanachukua katika kutupatia mwekezaji katika Kiwanda cha *TABOTEX*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri anayehusika na Wizara, kwa utekelezaji wa majukumu yake na kwa kuandaa hotuba nzuri yenyé ufanuzi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara imeshindwa kudhibiti uingizaji wa Bidhaa kiholela zinazoingia nchini zilizo chini ya ubora unaokubalika (*Sub Standards*). Mifano ni sigara nyingi zenye *label* ya *Sportsman*, *SM Sweet Method* na kadhalika. Sigara hizo zimefurika katika maeneo yote ya nchi yetu bila Wizara kushirikiana na Wizara nyingine ili kuzuia uingizaji huo holela. Aidha, kitendo cha kuacha sigara hizo ziingie kwenye soko letu zinalipunguzia Taifa letu kupata mapato yaliyolengwa na kuihujumu Kampuni ya Sigara Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ana kauli gani kuhusu hujuma hii iliyofumbiwa macho na vyombo kadhaa vya dola?

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri.

Naishukuru Wizara kwa kuweka Mkoa wa Kigoma kama eneo la *EPZ*. Hata hivyo, malengo ya *EPZ* hayawezi kufanikiwa kama hakuna miundombinu muhimu eneo husika. Nashauri Wizara hii iwasiliane kwa karibu sana na Wizara ya Nishati, ili umeme wa uhakika upatikane Kigoma kwani hili ni jukumu la msingi la Serikali. Hakuna uwekezaji unaowezekana Kigoma bila umeme!

Shirika la *SIDO* Kigoma sasa linafanya kazi Mjini Kigoma tu kwa sababu Ofisi haiwezi kusimamia na kufuutilia miradi Wilayani. Hii ni kuwanyima haki wafanyabiashara wanaotaka kukopa Wilayani. Ofisi iwezeshwe kufanya kazi mkoa wote.

Uchaguzi wa viwanda vinavyoingizwa kwenye *EPZ* uwe wazi. Hailelewski, kwa mfano, kwa nini *NIDA Textile Mills* kiwekwe kwenye utaratibu wa *EPZ* wakati Kiwanda cha Korosho cha *Supreme* cha Vingunguti hakimo.

Soko la asili la bidhaa za Mkoa wa Kigoma ni nchi jirani za *DRC*, Burundi, Zambia na Rwanda. Wafanyabiashara wa Kigoma wasaidiwe kupata soko hili hususan wakati huu ambapo nchi za *DRC* na Burundi ziko vitani. Wapewe elimu ya biashara kuititia Tawi la *TCCIA* Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba yake mwanana, iliyojaa mafanikio mazuri ya Wizara yake kwa mwaka uliopita na malengo mahsusini yenyewe mwelekeo kwa mwaka ujao. Kwa hakika katika kipindi kifupi cha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imojiwekea historia nzuri ya mafanikio hasa kwenye nyanja za viwanda vilivyokodishwa na vile vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo viwanda ambavyo vilikuwa vimekufa au kufungwa kabisa, lakini sasa vimefufuka na kutoa ajira kwa Watanzania. Viwanda kama *Sungura Textile*, *Metal Box*, *Morogoro Canvas Mill*, *Sigara, Tanzania Breweries*, Tumbaku, Viwanda vya Saruji na vingine vingi, ni mfano wa kujivunia ingawa vipo pia ambavyo bado vimefungwa kama *Morogoro Shoe Company*, Kiwanda cha Ngozi pale Morogoro, *Ceramics* na vingine vingi katika Jimbo langu la Uchaguzi la Morogoro Mjini. Niiombe Wizara iendelee na jitihada zake kufufua viwanda hivi ili azma ya kuvijenga ifikiwe kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimefanya haki kama pia sitaipongeza sekta binafsi katika nyanja hii kwa kuliongezea nguvu Taifa kwa kuwekeza hapa nchini. Pongezi za dhati ziende kwa kiwanda cha *NIDA Textile Mills*, ambacho hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifikunga pale Dar es Salaam, lakini pia pale Morogoro wapo wawekezaji wengine ambaao wanatujengea Kiwanda cha Kusindika Matunda aina ya mananasi, maembe na machungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa nchi yetu sasa ni usindikaji wa mazao yetu ili yapate soko kwa kutouza ghafi. Hivyo, Wawekezaji hawa, licha ya kuwahakikishia soko zuri wakulima wetu, wanahuisha kusudio letu hili ili kuliongezea Taifa pato lake linalotokana na matunda yake.

Mwisho, niseme kuwa naiunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara mia kwa mia.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara na timu yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja hii, kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kutoa ushauri kwa Wizara hii, kuangalia uwezekano wa kuwasiliana na Wizara ya Nishati na Madini na kuweza kupunguza gharama kubwa za umeme hasa viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa sasa tunaingia kwenye Muungano wa Nchi za Afrika Mashariki, hivyo endapo gharama zetu hazitaangaliwa upya, tutashindwa katika ushindani na bidhaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongee kidogo kuhusu suala la umeme kwa akili ya kuvutia wawekezaji. Kuna viwanda kama *SPM-Mgololo* tunashindwa kupata wawekezaji kwa sababu ya kuogopa gharama za uendeshaji ukiwemo umeme. Hivyo, ili tupate mwekezaji lazima tupunguze gharama za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu mkubwa ningependa nichangie hili suala la Kiwanda cha Karatasi Mgololo(*SPM*). Pamoja na matatizo mengi ya kiwanda hicho, ninapenda nikupe taarifa rasmi endapo kiwanda hicho hakitapata mwekezaji, ningependa nitoe pendekezo kwa Serikali ikiendeshe bila kujali.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yake kama kiwanda hakitofanya kazi ni haya yafuatayo: Kiwanda kina tani 4,200 za madawa mbalimbali yenyewe sumu kali yaliyohifadhiwa kwenye matangi. Hivyo, kuendelea kusimamia uzalishaji kwa muda mrefu kutasababisha madhara makubwa sana kwenye mazingira ikiwa ni pamoja na vifo kwa binadamu, wanyama, wadudu, mimea na viumbe vyote hai katika sehemu kubwa za Wilaya za Mufindi, Kilolo, Njombe, Ulanga na Bonde lote la mito ya Ruaha, Kilombero na Rufiji hadi Bahari ya Hindi (Watanzania wote tutaangamia).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri alitolee ufanuzi. Ahsante.

**MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge linajadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Waheshimiwa Wabunge, waliishauri Serikali kuiendeleza sekta ya mifugo kwa nia ya kukuza kiwango cha uzalishaji na hatimaye kumwongezea kipato mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii tunaambiwa kwamba ufanisi katika viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi uliendelea kuwa wa chini kutokana na mazingira yasiyordihisha katika uwekezaji na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapelekea kwamba, kuna uchambuzi wa kina unaofanywa wa sekta ya mifugo kuanzia ufugaji hadi uzalishaji wa ngozi. Uchambuzi huu unafanywa ili kusaidia katika kurejesha uhai katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kuangalia uwezekano wa kutufuta wawekezaji watakaoweza kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa gundi inayotokana na kwato za ng'ombe na mbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gundi ya aina hii ni nzuri na ina bei nzuri katika soko la ulimwengu. Tutakopofanikiwa kuanzisha kiwanda hicho ni imani yangu kwamba, kipato kwa mfugaji kitaongezeka. Siku za nyuma kabla utamaduni wa matumizi ya magodoro na mito ya kulalia ya aina ya sponji haujashamiri, wananchi wengi hasa sehemu za mijini, walikuwa wanatumia bidhaa hizo zinazotokana na manyoya ya kuku. Mito na magodoro ya aina hii yalikuwa maarufu sana. Lakini bahati mbaya katika miaka ya hivi karibuni matumizi ya sponji kwa uzalishaji wa magodoro na mito ndio ambayo yameshamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini kwamba, bado magodoro na mito ya manyoya yanapendelewa sana kutumiwa hasa kwa wale watu ambaa ni wazee na wale wenye matatizo ya kuumwa na mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Mheshimiwa Waziri, akafikiria kupata wawekezaji wataowekeza katika uzalishaji wa mito na magodoro yatokanayo na manyoya ya kuku, ili kutumia mali ghafi ya manyoya ambayo inaongezeka siku hadi siku kutokana na idadi kubwa ya kuku wanaochinjwa kila siku.

Hatua hii ikitekelezwa, itawaongeza wananchi kipato, kadhalika pia utunzaji wa mazingira kwa kuepusha kutupa ovyo manyoya ya kuku ambalo tatizo hili limekuwa kubwa huko mitaani.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa hotuba nzuri ya Waziri. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, kwa jinsi anavyojitahidi katika kujibu maswali Bungeni. Nisiwe mnyimi nampongeza pia Katibu Mkuu, Mkurugenzi na wataalam wote wanaopanga kazi na kushirikiana katika kuleta maendeleo Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana *SIDO*, kwa kazi wanazofanya za kufanya jitihada kuinua Pato la Taifa hili kwa kuwapatia elimu vijana na wanawake, makundi haya ndio hasa wanaoteseka au wanaohangaika na maisha ya uchumi. Tumeshuhudia Maonyesho ya Saba Saba vijijini na kadhalika na kuwapatia mikopo midogo kwa vikundi vidogo vidogo. Lakini pamoja na pongezi hizi nashauri *SIDO* iangalie vitu vinavyotengenezwa viwe bora, taratibu za mikopo ziboreshwe na tabia ya maonyesho iendelezwe na maonyesho ikiwezekana yafanywe hata ngazi za Kata - Tarafa, sababu ndiko waliko walengwa. Usindikaji wa vyakula utiliwe maanani. Taratibu za uendeshaji shughuli zozote zile zinapofanywa mikoani kwa maana ya uongozi wa pamoja, ushirikishwaji wa viongozi wa maeneo husika ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ilipoanza nchini walijenga majengo mazuri na ya gharama, kwa ajili ya vikundi kufanya kazi. Majengo haya yameachiwa popo wamezagaa, je, kwa nini tusiendeleze majengo hayo, je, wananchi wanatuelewaje, kwa vile majengo haya nadhani yapo kila mko? Hatua za haraka sasa zifanyike za kuwezeshwa matumizi ya majengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hotuba ya Waziri ukurasa wa 65, Jedwali Na. 3, ufanisi wa biashara ya nje inavyojionyesha, mimi sijaridhika na tusidanganyike kuwa uchumi wetu unakua, ni kweli unakua kwa asilimia ndogo sana. Tanzania tangu tupate uhuru ni miaka mingi sasa imepita na wataalam wa kutosha tunao, kwa nini mpaka sasa uchumi wetu haukomai? Jitihada zifanyike za makusudi za kuketi pamoja, wataalamu ikiwezekana na wadau, kuona jinsi gani ya kuboresha kazi, ikiwepo uzalishaji na Serikali kuwapatia wananchi pembejio kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo halijapatiwa ufumbuzi nalo ni ubora wa bidhaa zetu. Kwa mfano, wanawake na vijana kubangua korosho katika vikundi vyao lakini inakuja shida ya jinsi ya kuzifunga kinadhifu na kuweza kukaa muda mrefu bila kuharibika. Je, kweli haiwezekani tatizo hili kulimaliza na kuwapatia soko la uhakika wana vikundi? Imekuwa wimbo tu kuwa tuko mbioni kuwainua wakulima, wakati umefika sasa iwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara, vijana na wanawake katika vikundi vyao wameonyesha nia ya kujinasua na hali ngumu ya maisha. Nashauri Wizara itoe kila msaada kwa hawa ambaeo wako tayari na uwe mko wa mfano, wakishaimarika mikoa mingine kuja kujifunza sawa na wengine wanavyokuja kuangalia mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mama Mkapa, kwa jitihada zake anazofanya za kujaribu kuwaunganisha wanawake na wakati wa maonyesho wamekuwa wanajipatia fedha za mahitaji. Sambamba na hilo ieleweke kwamba, elimu ya kufanya maonyesho Saba Saba imeeleweka kwa wananchi, lakini wengi wanashindwa gharama za kiingilio, banda na kadhalika huwa kubwa kwa mwananchi wa kawaida. Tathmini ifanywe na ikiwezekana gharama zipungue ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha vizuri sana hoja yake. Vile vile nimpungeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii kwa ushirikiano na umahiri wao katika kuiandaa taarifa hii nzuri iliyo mbele yetu hii leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inamaanisha maeneo kadhaa ya mafanikio ambayo kwayo yote ningelipenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii kikamilifu na mchango wangu nakusudia kuuelekeza katika eneo la ajira.

Kwa kipindi cha miaka saba ya kati ya miaka 1995/96 na 2001/2002, ajira za wananchi wetu katika viwanda vyetu imekuwa katika mwenendo wa kukua mwaka hadi mwaka.

Kumekuwa na ongezeko la nafasi za ajira viwandani kwa ukuaji wa asilimia moja katika mwaka 1996/1997, asilimia tatu mwaka 1997/98, asilimia tano 1998/99, asilimia sita mwaka 1999/2000, asilimia tano mwaka 2000/2001 na asilimia kumi kwa mwaka 2001/2002. Katika kipindi hicho cha miaka ya 1996/2002 ajira za viwandani zimekuwa katika wastani wa wafanyakazi 148.536. Wastani huo ni juu ya ajira halisi zilizokuwepo viwandani kwa asilimia 13 (1996), juu ya ajira halisi kwa asilimia 12 (1997), juu ya ajira halisi kwa asilimia 8 (1998) na juu ya ajira halisi kwa asilimia tatu katika mwaka 1999.

Wastani huo wa wafanyakazi 148,536 walioajiriwa viwandani umekuwa chini ya ajira halisi kwa asilimia tatu katika mwaka 2000, asilimia tisa chini ya ajira halisi katika mwaka 2001 na asilimia 21 chini ya ajira halisi kwa mwaka 2002. Haya ni mafanikio makubwa na ni vizuri yakaeleweka vizuri na

tukawapongeza kwa dhati kabisa Waziri, Naibu Waziri, viongozi, wataalam wote wa Wizara kwa hili na mengine mazuri kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mazito sana na ya msingi kiuchumi ni pamoja na suala zima za ukosefu wa ajira (*Un-employment*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapolikabili tatizo hili la upungufu wa ajira kwa sura inayoonekana ndani ya taarifa hii aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri, ni jambo la kutia moyo sana na kutujengea matumaini makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara na naiunga mkono hoja hii kwa dhati kabisa.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja niliyoitaja hapo juu kwa asilimia 100. Kwa kweli hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri, ni nzuri na inaleta matumaini makubwa katika suala zima la uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kufurahisha sana ni jinsi baadhi ya viwanda vyetu vinavyoshamiri na kukua kwa nguvu na inafaa viwanda hivyo viorodheshwe, vipongezwe na vipewe kila aina ya msaada wa hali ya mali ili viweze kuendelea zaidi na hii itasaidia sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu kwa upande wa viwanda na hata kwa ajira ya wananchi wetu kwa ujumla. Baadhi ya viwanda ambavyo kwa haraka haraka ninavyovikumbuka kwa hivi sasa ni kama Kiwanda cha Sabuni Foma, Sigara (*T.C.C.*). Viwanda vya Chai, *Whitedent* na kadhalika, kwa kweli vinahitaji pongezi maalum na iwe ndio mifano mizuri wa viwanda ambavyo vimeweza kuleta heshima kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la kusikitisha sana na inapelekea kuna baadhi ya wafanyabiashara wenyе tamaa binafsi, ambaо hawapendi maendeleo ya viwanda vyetu, wanaweka mikakati ya makusudi ya kuvuia viwanda hivyo kwa kutengeneza bidhaa ambazo zinalingana na bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu na kuziingiza katika soko letu kwa bei nafuu. Pia bidhaa hizo kwa kuwa zinaingia kwa njia za magendo huwa *sub-standard* na hii inaweza hata kuhatarisha maisha ya watumiaji wa bidhaa hizo. Inaelekeea pia kwamba, bidhaa hizo zinazalishwa katika nehi jirani na baya zaidi huandikwa kwamba zinazalishwa na viwanda vya hapa nchini na hii inapelekea kwamba, kuna *syndicate* kubwa kwani hupitishwa kwenye Mikoa ya Maziwa na Mikoa ya mipakani bila ya kukamatwa. Mfano hai, katika Mkao wa Mwanza, kuna sigara nyingi aina ya *Sweet Menthol* na *Sportsman*, ambazo zimezagaa sana katika mikoa hiyo. Jambo hilo kama Wizara husika italfumbia macho, nina wasi wasi ya kwamba, viwanda vyetu vingi vitaanguka hapo baadaye na kusababisha hata kuanguka kwa uchumi wetu. Ningelishauri Wizara ikafanya angalau utafiti kwa jambo hilo na hasa kwa sigara hizo *fake* kwa kushirikiana na Kampuni ya Sigara ya hapa nchini (*T.C.C.*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Wizara kuangalia ni jinsi gani inaweza kuweka Kitengo Maalum, kitakachofuatilia masuala hayo ya bidhaa *fake*, ambazo huangusha viwanda vyetu. Kwa hayo, machache ninaunga mkono hoja.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Moja kwa moja naunga mkono hoja hii. Ni hoja iliyobaini mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu kimaendeleo na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia kwa kina hotuba hii, hisia zangu zinaniambia kuwa jitihada na Teknolojia ya Wizara haitazaar matunda bila ushirikiano wa dhati na Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Ujenzi, ambayo inapongezwa sana kwa umakini wake katika utekelezaji na Wizara ya Ushirika na Masoko.

Naomba sana Waziri akae na Waziri wa Nishati na Madini, kuhusu uenezaji wa umeme nchini, maana hakika vyanzo vya umeme vya awali viro hasa maporomoko ya maji. Mambo mengi ya mimea na mifugo inaharibika kwa sababu inakosa hifadhi nzuri (*Cold Storages*), hasa Wilaya kama ya Ngara ambayo soko lake liko Bukoba km 360 hivi, Mwanza km 440. Shinyanga karibu km 500 na kwingineko. Ngara ina maziwa, matunda na mboga mboga kwa mwaka mzima, nyama kwa aina zote za wanyama

waliwao, lakini wakulima wanaendelea kuwa maskini. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aonane na Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Mheshimiwa Capt. John Chiligati na wote waliowahi kufika Ngara. Wilaya ya Ngara ina madini ya *Nickel*, *Cobalt* na *Tin*. Huwezi kuchimba madini mazito na mengi kama *Nickel* kwa jembe la mkono

Mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri, atembelee Wilaya ya Ngara, aje aone mwényewe vijana wetu wanavyokosa ajira kama kazi za *welding* za madirisha, milango na kadhalika zingefanyika Ngara, lakini vinaagizwa kwa gharama kubwa kutoka Mwanza, Tabora hata Dodoma kwa sababu havitengenezwi Wilayani kwa ukosefu wa umeme!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena na naunga sana mkono hoja hii.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Juma Alifa Ngasongwa. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Ngasongwa, kwa mawasilisho yake mazuri ya hotuba ya Bajeti. Lakini vile vile nitumie nafasi kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Hotuba ya Bajeti.

Hali kadhalika ninawapongeza sana kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika hoja hii muhimu unalenga katika masuala ya uzalishaji viwandani na kuwawezesha wananchi kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuyasindika kwanza kabla ya kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina viwanda vingi hivi sasa na baadhi ya viwanda hivyo bado vinafanya kazi chini ya viwango vyake. Viwanda vingi bado vinafanya kazi kwa kutumia *shift* moja kwa siku kutokana na sababu mbalimbali. Ukosefu wa mtaji ni sababu kubwa kwa viwanda kufanya kazi kwa *shift* moja. Naomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha kwa nini viwanda vyenye kufanya kazi kwa *shift* moja kwa siku visiwe na *shift* mbili au tatu kwa siku ili kuongeza uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zinazopatikana kwa viwanda kufanya kazi kwa *shift* nydingi ni kubwa zaidi kuliko kwa viwanda kufanya kazi kwa *shift* moja moja. Faida nydingine kubwa ni ongezeko la wafanyakazi zaidi kwa ajili ya *shift* zitakazoongezeka. Kwa hiyo, nashauri iwe katika sera ya viwanda kuwa njia zote zitumike katika kuongeza uzalishaji viwandani kwa kuongeza *shift* sambamba na uanzishwaji wa viwanda vipyta na upanuzi wa viwanda vya zamani. Kwa njia hiyo, nina hakika kuwa Tanzania itapatia mchango mkubwa kutoka sekta ya viwanda kiuchumi. Lakini vile vile viwanda navyo vitafaidika kwa tija kuongezeka kwani kwa mashine zile zile uzalishaji utaongezeka na mauzo yake kuongezeka pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana Serikali kukaa na wenye viwanda ili kujua matatizo yanayoweza kukwamisha viwanda kushindwa kufanya kazi kwa *shift* mbili au tatu kwa siku na kuyapatia ufumbuzi mara moja. Kwa njia hii inaweza ikawa chanzo cha bidhaa zetu kupungua bei hivyo kushindana vizuri na bidhaa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie kwenye suala la kuongeza thamani ya mazao yetu kwa kuhakikisha kuwa mazao hayo yanayosindikwa kwanza kabla ya kuuzwa. Naomba Serikali ifanye mambo kadhaa ili kufanikisha mipango ya kuhakikisha kuwa mazao yanayosindikwa kwanza kabla ya kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ambacho Serikali inatakiwa kufanya ni kueneza teknolojia ya usindikaji wa mazao huko vijijini. Ninaomba wataalamu wazunguke nchi nzima hadi vijijini kuelimisha wananchi kwa nadharia na kwa vitendo jinsi ya kusindika mazao mbalimbali yanayopatikana katika sehemu husika. Tumeona wataalamu wengi wakiishia kwenye miji mikubwa na kusahau vijijini ambako mazao mengi yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili ambacho Serikali inatakiwa kukifanya ni kuhakikisha kuwa, wananchi wanawezeshwa kupata mikopo ya mitaji ya kuanzishia viwanda vidogo vya kusindika mazao yao. Mikopo hiyo iwe nafuu sana na itolewe bila ya mizengwe yoyote na usumbufu usiokuwa wa lazima. Ninayasema haya kwa sababu yapo manung'unico mengi kutoka kwa wananchi kuwa mikopo hutolewa kwa kujuana na baada ya kutoa chocohote kwa wale ambao wameteuliwa kusimamia utoaji wa mikopo hiyo. Aidha, masuala ya dhamana ya mikopo nalo ni kikwazo kwa wananchi wengi. Ikiwa mwananchi anazo raslimali kama mashamba, nyumba, kwa nini anyimwe mkopo anapoomba? Ni vizuri Serikali ikalegeza masharti magumu ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo mbalimbali ili wasindike mazao yao na kuyaongezea thamani.

Naomba kutoa ombi maalum kwa Serikali kuhusiana na wakulima wa korosho. Naomba wakulima wa korosho wasaidiwe katika ubanguaji wa korosho zao. Kusubiri hadi viwanda vya korosho vipate wawekezaji ni kuwachelewesha wananchi wanaolima korosho kufaidika na zao hilo. Serikali ikazanie usambazaji wa viwanda vidogo au mashine ndogo za ubanguaji wa korosho nchini kuliko kutafuta wawekezaji wa viwanda vya korosho ambavyo vimeonekana kuwa na mashine au teknolojia ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mwisho, nashukuru tena kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ahsante sana.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100% na naitakia Wizara utekelezaji mwema wa malengo ya Wizara iliyojiwekeza kwa mwaka wa fedha ya 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba kutoa ushauri ufuatao:-

- Katika kuhakikisha tunaendelea kiviwanda na kibashara ni sharti Serikali itilie maanani katika kuipa nguvu *SIDO* kwa kutoa fedha za kutosha. Nchi ya India imeweza kusaidia Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo hadi kufikia mtaji wa zaidi ya Dola za Kimarekani 34 bilioni na viwanda vikubwa sasa hivi nchini India vilianza kama viwanda vidogo. Kwa kuwa sasa hivi imekamilisha sera ya viwanda vidogo hii iendane na Serikali kutoa fedha za kutosha katika kuendeleza viwanda vidogo vidogo na pia wafadhilli waombwe kuendeleza juhudhi za kutoa misaada mikubwa ya kukuza uwezo wa Shirika la *SIDO*, kuweshezwa Shirika kukabiliana na uboreshaji na ukujali wa viwanda.

- Serikali naishauri izidi kuboresha fedha kwa ajili ya mikopo midogo midogo kwa Watanzania. Fedha walizopewa *SIDO* miaka ya nyuma zimetumika vizuri na fedha hizo bado zipo, ni vyema zikaongezwa kila mwaka hadi kufikia kiwango kikubwa hata kufikia kiwango cha Shirika la Viwanda Vidogo huko India.

- Kutokana na kukua sana viwanda vya wachimbaji madini ya dhahabu na almasi, ni vyema Serikali ikaona jinsi gani kukua kwa biashara hizi kutawahuisha Watanzania hasa katika maamuzi ya vitendea kazi vya madini kwa kutumia *agents* wa Tanzania katika manunuzi ya viwanda.

- Pia nashauri Serikali isaidie kuanzisha viwanda vikubwa vya kutengeneza *final products* kutokana na dhahabu hata na almasi ili kuipa thamani vito hivi na kuongeza ajira ya watu wetu.

- Natoa shukrani zangu kwa Wizara hasa kuleta sera ya kulinda viwanda vyetu ili navyo viweze kukua ili iendane na udhibiti wa uingizaji bidhaa za nje kwa njia ya magendo.

- Katika kuboresha miundombinu ya biashara sharti kutilia maanani suala la upatikanaji rahisi wa fedha. Hii napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Udhaminii wa Sh. 500 milioni na ninaomba kadri tunavyoendelea, Mfuko huu sharti uendelee kuboreshwa ili uje usaidie wengi zaidi.

- Tatizo la ajira kwa vijana katika miji yetu sharti lizingatiwe na utaratibu wa kuwapatia mahali pa kufanya kazi watu hawa ni muhimu na ni vyema vikaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100% na Mola awabariki kutekeleza malengo ya Wizara.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi, kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mbunge wa Kawe, pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Ahmada Ngemela na safu nzima ya uongozi wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya hoja, wakiwa wameshauriana kikamilifu na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa Wizara hii ni kuomba ianze haraka iwezekanavyo kuwawezesha Wananchi wa Majimbo ya Uchaguzi ya Kilombero, Ulanga Magharibi na Ulanga Mashariki kuanzisha usindikaji wa machungwa (*Juice*) kule Taweta na Tanganyika Masagati. Usindikaji wa *Mango Juice Utengule*, Malinyi na Mahenge ili kuinua vipato na kupunguza umaskini wa raia hao, ukizingatia programu ya utekelezaji wa sera endelevu ya viwanda, hususan kama ilivyoelezwa katika sentensi ya tatu, Ibara ya 14 ya hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Pia, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya ya kuimarisha viwanda na kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kukipatia Kiwanda cha *Kagera Sugar*, mwekezaji makini, ambaye hadi sasa anafanya kazi nzuri sana. Aidha, tunaomba Serikali vile vile iwe makini katika zoezi la kubinafsisha Kiwanda cha Kusindika Kahawa Kagera (*TANICA*). Naomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo ya mwelekeo na maoni ya Serikali katika mpango wa kubinafsisha Kiwanda cha *TANICA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa utendaji wao. Pia, napenda kumpongeza Mkurugenzi wa *BREDA*, kwa kufanya kazi zao kwa ufanisi, bila urasimu mkubwa, jambo lililofanya malalamiko ya rushwa katika *agency* hiyo kupungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Lindi Mjini, lipo eneo la viwanda la *SIDO*. Eneo lile ni kwa ajili ya kuwapatia elimu na ajira wakazi wa Lindi Mjini. Zipo taarifa kwamba, Uongozi wa *SIDO* unataka kulikodisha eneo hilo ili iwe ni *yard* au karakana ya Kampuni iliyopewa kandarasi ya ujenzi wa barabara. Haya si madhumuni ya ujenzi wa eneo hilo la *SIDO*. Kwa kufanya hivyo, Wananchi wa Lindi, watanyimwa fursa yao halali ya kulitumia eneo hilo kama ilivyokusudiwa. Aidha, Makandarasi hao wanao wajibu wa kujenga *garage* au *yard* yao na si kuhamia tu katika majengo yaliyojengwa kwa madhumuni mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, asimamishe mpango huo kwa manufaa ya Wananchi wa Lindi. Kwani kwa kuachiwa Makandarasi kujenga eneo lao wenywewe, ingekuwa ni hatua ya kimaendeleo kwa Mji wa Lindi. Naomba Waziri achukue hatua inayostahili.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi na hongera kwa hotuba nzuri sana. Kwa muda mfupi Mheshimiwa Waziri, ameweza kutoa hoja kwa mambo yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna Wizara fulani zinafikiri kuwa *sub-sector* fulani ni zao na mtu mwingine anaingilia badala ya kufikiria kuwa Serikali ni moja na nchi ni moja. Tukubali kila Asasi ya Serikali ishiriki na ishirikishwe. Sioni kwa nini Waziri ajiweke katika *hard time* kutekeleza miradi muhimu miwili ya *Mchuchuma Coal and Power and Liganga Iron Ore*. Miradi hii ni *base* ya *basic industries* nchini. Madini ndiyo hayo *base metals* itakayojenga *basic industries*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, suala la *chemicals* za Mgololo *SPM* siyo la kulifanya mchezo ni *bomb, atomic bomb*. *One third* ya Tanzania itaangamia! Hasa watani na ndugu zangu Wandamba na Warufiji watakuwa hawapo. Binafsi nimesimamia *SPM for 5 years*, lazima Waziri apige la mgambo ili Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu, waelewe. Ikibidi *NDC* wahuishwe *either* kwa ushauri au kwa mikakati zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nichangie kwa kuzungumza, lakini bahati mbaya imenipasa niende kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tangu awali kuwa naiunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo, napenda kuchangia yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali ifanye makusudi mazima ya kuboresha huduma za kiuchumi katika maeneo ya *EPZ* kwa kuzingatia *Corridor Development Strategy*, kwa kuangalia milango ya Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar. Kwa mantiki ya *comparative advantages*, basi maeneo hayo yawe na mazao/bidhaa maalum za kuzalishwa ili kusiwe na *unnecessary duplication*. Kwa *spirit* ya maendeleo ya Tanzania, basi Zanzibar ishirikishwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumo katika kuwashamasisha Wananchi kuendeleza uchumi kwa kusindika mazao ya kilimo. Kwa wale waliokwishaanza, basi *TBS* iwasaidie ili waweze kuzalisha bidhaa zinazokubalika Kimataifa na wapewe nembo (*TBS*), ili wapate soko kirahisi. Hivi sasa wengi wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nimesikitishwa na fedha kidogo sana walizopewa Asasi kama *TEMDO, TIRDO* na *CARMATEC* na kadhalika. Naomba sana Asasi hizi za utafiti wapewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa, hizi *supermarkets* zilizoanza kushamiri hapa nchini, zilazimishwe kutumia mazao au bidhaa zilizozalishwa humu nchini.

Kama ni suala la *standards*, basi washiriki kikamilifu katika kuboresha *packaging* na *promotion* ya mazao haya ili yafikie ubora na hii itasaidia sana kuongeza ajira na jitihada zetu za kupunguza umaskini. Ahsante.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, wakishirikiana na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kufufua hamasa katika Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara kwa kupitia Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*), imeanzisha utaratibu mzuri katika ufufuaji wa kazi za kubangua korosho katika Vijiji vilivyo katika maeneo yanayolima korosho, pamoja na kusaidia kuongeza thamani ya zao hili kwa wakulima na kutoa ajira katika maeneo ambayo hayana viwanda kabisa kama vile katika Wilaya ya Ruangwa. Mikopo inayotolewa na *SIDO* katika Sekta hii, imesaidia sana kuwapatia mtaji vikundi ambavyo kwa vyovyote vile havina sifa za kupata mikopo kutoka Taasisi zetu za fedha. Natoa pongezi sana kwa Wizara na hususan *SIDO*, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na *NDC* katika uanzishaji wa maeneo maalum ya uzalishaji bidhaa kwa masoko ya nje (*EPZ*), hazina budi kuungwa mkono na watu wote.

Matatizo ya miundombinu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati, ni lazima yapewe kipaumbele katika utatuza hususan Mradi wa *Mtwara Development Corridor*, ambao ungeweka miundombinu ingewezesha utumiaji wa Bandari ya Mtwara, uwe na ufanisi zaidi. Aidha, mradi huo una sifa zote za kuiwezesha *EPZ* ya Mtwara (*proposed*) kuanzishwa kwa vishindo. Naipongeza Wizara kwa jitihada zake kupitia *NDC* kuhalikisha utekelezaji wa mradi huu ambao unaelekea una vipingamizi vingi ndani ya Serikali. Natoa rai kuwa wakati sasa umefika na pengine umepitwa wa kutoa maamuzi ya kuanzishwa kwa mradi huu ambao faida zake zitaenda pia kwa nchi jirani za Msumbiji, Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni juu ya malipo ya mafao kwa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo *MUTEX (SU)*, wakati kikiwa chini ya Serikali. Suala hili ni la muda mrefu toka mwaka 1994 na hii ina maana imekuwa ni adha kubwa kwa Wananchi ambao walikuwa watumishi wa kiwanda hicho. Kwa vile wapo watumishi ambao si wakazi wa Musoma, wameendelea kuwa na matumaini ya kulipwa mafao yao ili waweze kurejea kwenye maeneo wanayotoka. Nashauri Waziri wa Viwanda na Biashara, afuatilie suala hili ili mafao haya yawewe kulipwa.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu yao kwa kuliendeleza gurudumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri mambo yafuatayo ili kuleta uwiano wa kijinsia katika Wizara hii: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuanzisha Dawati la Jinsia (*Gender Desk*) na kumteua Afisa atakayeshughulikia suala hili. Hadi sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, haijapata kujua jina la Afisa huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashauri kila mara mtakapotoa *data* (takwimu), muwe mnatofautisha (me na ke), yaani *desegregated data*. Hii itatusaidia sana sisi humu nchini na nje ya nchi kuthibitisha ushiriki wa Wanawake, *let us all wear gender lenses*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kuhusu idadi ya washiriki Wanawake katika *DITF*. Mnamo mwaka 1996, Wizara ya Viwanda na Biashara, ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ilianzisha mabanda ya akina mama katika suala zima la kuwatafutia soko ndani na nje ya nchi. Pia, kuboresha ubora wa bidhaa, *packaging* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mama Anna Mkapa, kwa kutusaidia katika kufikia azma yetu. Lakini sasa matatizo yafuatayo yamejitokeza: -

- Idadi ya Wanawake imeanza kupungua. Hii imeanza mara tu dhana ya *cost sharing* ilipojitekeza. Kuna haja ya wadau wakiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara (*BET*), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, *EOTF*, *FAWETA* na kadhalika, tuketi ili tulitafutie jambo hili ufumbuzi kabla mambo hayajatuharibikia.

- Nilipotembelea banda la *SIDO*, *WIPE*, wanawake bado walikuwa wanalamikia upatikanaji wa *packaging materials*.

- Upatikanaji wa nembo ya *TBS*. Kupatikana kwa nembo hii kuna umuhimu wake, bila nembo acha soko la nje, hata la ndani ni shida. Je, Wizara haiwezi kufanya kitu kama *fast track* ili tuweze kuwasaidia hawa akinamama? Kilio kingine ni ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushiriki wa wafanyabiashara katika maonyesho nje ya nchi, Wizara inafanya juhudhi gani kuhakikisha wafanyabiashara wanashiriki kikamilifu? Napenda kuwapongeza akinamama watatu kutoka *FAWETA*, walioshiriki maonyesho ya biashara Blantyre mwaka huu. (*The only participants from Tanzania*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 20 kuhusu *AGOA*, natoa pongozi kwa kuunda Kamati ya Kuratibu Utekelezaji wa Mipango mbalimbali ya fursa za masoko nafuu. Ningependa kufahamu hao wadau ni akina nani? Pia, napenda kufahamu uwiano uliopo kati ya wadau Wanawake na Wanaume. Hii itasaidia sana utekelezaji wa *SME Development Policy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *EPZ*, katika kufanikisha azma hii *infrastructure has to be in place* hususan mawasiliano, umeme wa uhakika na kadhalika. Mfano, Kigoma usafiri ni wa shida, umeme hakuna. Ni *criteria* gani iliyotumika licha ya kuwa Mkoa wa mpakani?

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani kwa kupewa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Wizara hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na timu yake yote, kwa matayarisho mazuri ya taarifa ya kazi za mwaka uliopita na mpango wa mwaka ujao wa 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana kama iliyyo Sekta ya Kilimo. Ni kweli kilimo ni uti wa mgongo, lakini kilimo bila ya viwanda hakitafika popote. Tunakazania mapinduzi ya kilimo, tukifanikiwa tutapata mazao ya ziada ambayo yatahitaji kuwa *processed, packaged* na kadhalika. Vile vile, kupata mapinduzi katika kilimo tutahitaji *mechanization*. Kupata vifaa vya *mechanization* kama *tractor, harrows, harvesters* na kadhalika, tunahitaji viwanda. Kwa hiyo, viwanda ni Sekta muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatujaona namna Serikali inavyoipa umuhimu Wizara hii, kwanza kwa kuipa fedha zinazoweza kuiwezesha kufanya kazi yake kwa kiwango kikubwa na pili hata kienzi kama inavyofanya kwenye kilimo, ni kwa nini? Au labda Waziri amekuwa mpole mno? Nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapo jumuisha hoja yake atueleze hili, ni kwa nini Wizara hii haipewi *prominence* inayostahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwengine ni maendeleo ya *EPZs*. Hivi fedha kiasi cha Shilingi milioni 50 zinatosha ku-mobilize, kuanzisha, *including infrastructure et cetera* na kuendesha maeneo hayo ambayo kwanza ni dhana mpya kwetu? *Are we serious?* Kwa nini *besides Namela group, NIDA textiles* na wenzake 2 - 3 dhana ya *EPZ* haijapamba moto, wakati tunajua fika kuwa maeneo haya yanachangia uchumi kwa kutupatia *foreign exchange*? Vile vile, wenzetu nadhani wameshafika mbali wakati wazo hili lilikuja *almost at the same time!* Tutajibu nini kwa kuendelea kukawia ku-take advantage ya *AGOA, EBA* na kadhalika? Nitaomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara, pamoja na *Board of External Trade*, kwa bidii, maandalizi na namna wanavyosimamia *The Dar es Salaam International Trade Fair* kila mwaka hasa mwaka huu. Maonyesho haya yameendelea kuimariika, *product range on display* imeongezeka, *quality* imemarika, mabanda yamezidi kupata sura kweli ya *exhibition* ya Kimataifa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ninaipongeza Wizara kwa namna inavyoshirikiana na *First Lady*, Mama Anna Mkapa, pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuwapa akina mama wa kila Wilaya (*representatives*) nchini, fursa ya kuleta bidhaa zao kwenye maonyesho haya. Akina mama hawa wanapata manufaa mengi yakiwemo, kufungua macho (*exposure*), wanajifunza mbinu za *display, pricing of products* na pia kupata soko la bidhaa zao. Lakini kikubwa zaidi ni changamoto, chachu wanayorudisha Wilayani kwa akina mama wengine. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipiga kelele kuhusu Wizara kufanya shughuli zake katika majengo ya kupanga! Wizara hii siyo tu inakaa katika nyumba/jumba la kupanga na kulipa fedha nyingi kila mwezi, bali inakaa katika jumba ambalo halitunzwi na hivyo kuleta sura mbaya na aibu kwa Wizara! Si hivyo tu, Wizara iko ghorofa ya 6, 7 na 8!

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ukizimika Viongozi wa Wizara hii akiwemo Waziri hulazimika kutumia ngazi tena katika giza kubwa! Si hivyo tu, ni majuzi tu jengo hili lilipata ajali ya kuungua *ground floor!* Kwa ujumla halifai hata kidogo kwa Wizara yoyote hasa hii. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapojuuisha aseme ana mpango gani wa kuhama katika jengo hili.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, Ndugu Ahmad Ngemera, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam na Viongozi wote wa Wizara hiyo na Taasisi zake kwa hotuba nzuri na jitihada zao kubwa katika kufufua na kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Wizara imepiga hatua kubwa katika kufufua viwanda, kukamilisha sera ya biashara, kuanzisha shughuli za EPZ, kutafuta ufumbuzi wa vikwazo mbalimbali, kudhibiti ubora wa bidhaa, kukamilisha na kutekeleza sera ya uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo (*SMEs*), mafunzo na uendelezaji wa ujasirimali, kusimamia sera ya uwezeshaji Wananchi, kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa (*anti-dumping*), kudhibiti ushindani usio wa haki, kuhamasisha mauzo nje, kusimamia kampeni ya “Nunua bidhaa za Tanzania”, kushiriki katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Viwanda na Biashara, kutoa msukumo kuhusu Tanzania kutumia ipasavyo fursa zinazopatikana kutokana na *AGOA, EBA, PACT, EAC, SADC, ACP/EA EPAs*, kusimamia Taasisi zilizo chini yake, kuratibu maendeleo ya viwanda kwa jumla na kusimamia utafiti na maendeleo (*R & D*) kuhusu shughuli za viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka itaonekana kwamba, Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kuhudumia Sekta mbalimbali za uzalishaji hapa nchini na kuwa daraja imara la kuratibu biashara nchini na kuunganisha Taifa letu na Mataifa mengine duniani. Jukumu hili ni kubwa na zito hasa katika zama hizi za utandawazi na ushindani unaozidi kuwa makali. Ili kuweza kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi, hapana budi Wizara hii kupewa uzito zaidi kuliko inavyofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Wizara nilizoziorodhesha hapo juu, hasa utafiti na uendelezaji masoko, kwa kiwango kinachotarajiwa, ni nzito na zenye ghamama kubwa. Pamoja na sera ya Serikali kujitoo katika kufanya biashara, bado Wizara hii ina jukumu kubwa kama mhimili na mdhamini mkuu wa kuiendeleza na kuhudumia Sekta binafsi ili iwe katika hali nzuri zaidi ya kuzalisha na kuhimili makali ya ushindani yanayozidi kushamiri katika soko huria duniani na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara bado ina wajibu unaoendelea kukua kuhusu kutoa miongozo na sera, huduma za ugani, ushauri wa kitaalamu, taarifa za masoko, pamoja na sheria na taratibu ambazo zitawezesha wazalishaji mali na wafanyabiashara wa Tanzania, kuhimili ushindani kwa kuboresha bidhaa na huduma zao mbalimbali kwa ghamama ndogo zaidi. Jukumu hili ni muhimu zaidi hivi sasa kwa kuzingatia kwamba, muda si mrefu kabla ya kufikia wakati ambapo nchi kama Tanzania hazitakuwa na nafasi ya kulinda viwanda vyao na masoko yao dhidi ya ushindani.

Kutokana na mantiki yaliyotangulia, hapana budi Wizara hii ikapewa fedha za kutosha kuiwezesha kutekeleza majukumu yake mengi na mazito niliyoyaorodhesha. Vinginevyo, tutaendelea kuimba nyimbo na kuachwa kwenye mataa badala ya kuwa katika hali ya kuhimili ushindani! Hata Serikali za nchi zinazoendelea zinaweka mkazo mkubwa kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuzichukulia kwa wepesi shughuli za utafiti na uendelezaji viwanda na biashara kama vile *BET, CARMATEC, SIDO, TIRDO, TEMDO, TBS* na *NDC*, zipewe umuhimu mkubwa zaidi na fedha nyingi zaidi ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa kiwango kikubwa zaidi na ufanisi mkubwa zaidi. Hapana budi kwa Wizara kujenga hoja rasmi kuhusu uzito unaostahili kutolewa. Aidha, ni muhimu *Export Development Fund* ikaanzishwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote waliohusika kuandaa hotuba hii. Pia, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuishauri Serikali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kushauri kuhusu biashara ya sigara nchini kwetu. Hivi sasa kumejitokeza wimbi la biashara haramu ya nembo ya sigara za Tanzania. Sigara hizi zinazotoka nchi jirani, zina madhara makubwa kwa uchumi wa nchi kwa vile hazilipiwi kodi na pengine kukosa ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuanzishwa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Watanzania wengi wamenunua hisa za *TCC* kwa mategemeo ya kuongeza kipato. Lakini kutokana na hujuma hizi, ongezeko la faida halipandi kwa kasi inayotarajiwa kutokana na ushindani wa soko nchini la sigara zisizo halali. Vile vile, sigara hizi hazilipiwi kodi. Ni vema sasa Serikali ichukue hatua kali dhidi ya biashara hii idhibitiwe ili kuziba madhara yanayotokea. Hii pia inachangia kushuka kwa bei ya tumbaku kwa mkulima wa Tanzania, pamoja na madhara mengi kwa uchumi wa nchi yetu. Kama wahusika wanataka kufanya biashara hii, ni bora wafuate taratibu za uwekezaji, wajisajili kwa kuwekeza nchini ili Taifa lipate mapato na faida nyingine nyingi, lakini siyo ubadhirifu wa uchumi wa nchi kama inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wakati wa majumuisho, Mheshimiwa Waziri, aongelee suala hili kwamba ni hatua gani atazichukua.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalam mbalimbali wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya. Wizara hii kwa muda mfupi imeweza kufanikiwa kuinua viwanda vingi vilivyojwa vimekufa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga karibu Wilaya zake zote za Lushoto, Korogwe, Handeni, Muheza, Pangani, Kilindi na Tanga, zimelima sana matunda ya aina mbalimbali kama vile machungwa, maembe, *passions, pears*, nyanya na kadhalika. Wananchi wengi wanategemea sana uchumi wa matunda kwa maisha yao, kusomesha, kujenga, kuvalaa na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Serikali baada ya kuliona hilo, walifanya utafiti wa uhakika na kuamua kujenga Kiwanda cha Matunda Korogwe *TANGOLD*. Kiwanda hiki kilikuwa mkombozi kwa Wananchi wengi na walianza kuhamasika kulima matunda kwa wingi. Kiwanda hiki kimesaidia sana kuinua uchumi wa Wananchi wa Mkoa wa Tanga. Aidha, Kitaifa pia Kiwanda cha *TANGOLD* Korogwe kiliiletea sifa nchi yetu kwa kupata *Gold Medals* kwenye *juice ya passion*. Si hilo tu, hata ajira ilipatikana kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba, aliyepewa kiwanda hicho kwa njia ya kukikodisha (*JITU PATEL*), ameshindwa kuzalisha ambapo sasa ni zaidi ya miaka kumi, naomba sasa Serikali iokoe jahazi. Hali ya matunda kuvoza sidhani kama Serikali haifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali izingatie hali hiyo, wakubali kutafuta mwekezaji wa kuwekeza katika Kiwanda cha Matunda Korogwe au Serikali yenyelewe ikubali kufufua Kiwanda cha *TANGOLD* Korogwe.

Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imeokoa matunda yanayooza katika Mkoa wa Tanga. Pia, itakuwa imejenga uwezo wa kiuchumi wa Wananchi wa Mkoa wa Tanga, hasa ikizingatiwa kwamba, mkonge umekufa katika Mkoa wa Tanga na zao mbadala la kiuchumi ni matunda. Ni aibu kwa Wananchi wetu kuuza matunda kwa wafanyabiashara wa Kenya kwa bei ya kutupa tu. Hivi kweli Serikali inashindwa kufanya uamuzi wa makusudi wa kujenga kiwanda hiki? *Infrastructure* zote zipo, naomba na kushauri Serikali ifufue kiwanda hiki muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote vilivyopewa wawekezaji matapeli kama vile *TANGOLD* Korogwe, *Mkumbara Tembo Chipboard*, wanyang'anywe na wapewe wenye uwezo na ni busara kabisa kabla ya mwekezaji kupewa kiwanda achunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanaouziwa viwanda wawekeze kwenye lengo lilokusudiwa badala ya kuvifanya viwanda *godowns* au kuzalisha kitu kingine.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge katika Bajeti yetu ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kawe, kwa imani walijonayo kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kufanya kazi zangu za Jimbo na za Wizara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuzipongeza Wizara zote zile zilizotangulia kutoa *Budget Speech* zao. Nintaje kipekee Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye hotuba yake ilikuwa nzuri na maelekezo mazuri ambayo huwa anatupatia mara kwa mara kuhusiana na viwanda vidogo vidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge napenda niseme kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajitahidi kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa makundi kwa sababu ni hoja nyingi. Wengi wamechangia kwa maandishi na hoja zimejirudia rudia sana kwa hiyo tumeziweka katika makundi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi kubwa kabisa ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Freeman A. Mbwe, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya na Mheshimiwa Henry D. Shekiffu ni kuhusu viwanda vidogo vidogo, uvezeshaji kwa wananchi, uboreshaji wa mfuko, utekelezaji wa hiyo mifuko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo nitajelezea hapa ni kuhusu uwekezaji au uhamasishaji wa wawekezaji katika viwanda vya vyakula hasa matunda huko Muheza, Lushoto, Iringa na Mikoa mingine. Mwisho, nitaongelea biashara nyingine zikiwemo biashara za nje na masoko ya Kimataifa kama *AGOA*, *EBA*, *Community SADC* na *COMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka kabisa naomba nianze na hoja ya viwanda vidogo vidogo. Naona nitajibu kwa ujumla ambapo itatusaidia pia kuweza kupata majibu ya kila Mheshimiwa Mbunge ambaye aliulizia sana kuhusu mikakati ya *SIDO* na uvezeshaji wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi sana na ninaweza nikasema imetoa kipaumbele au tuseme *affirmative action* katika kutoa au kufufua *SIDO* nchi nzima. Tumeanza na Mfuko wa *SIDO* ulikuwepo wa *NEDF* ambao unapitia Wizara ya Viwanda na Biashara na unasimamiwa na *SIDO*. Huu mfuko umeanza kuanzia mwaka 1994 kama tulivyoongea leo na mpaka mwaka 2003 sasa hivi mzunguko wa fedha unafikia Shs. 1,460,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, wamepongeza sana juhudzi za Serikali na vile vile wakawa wanazidi kuulizia kwamba sasa kinachofuatia ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali la kwanza kabisa tumeona sasa tunapajaribu kufufua *SIDO* tuwe na sera maalum ya viwanda vidogo vidogo, ambayo tayari imekwishatengeza na tayari imekwishapitishwa bado kuitangaza. Lakini wakati tukisubiri kuitangaza tumeamua tuanze utekelezaji kwa sababu hatuwezi kusubiri zaidi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kugusia vipengele vichache vyta sera ambayo itatusaidia kuona mambo ambayo Serikali imefanya. Kwa ujumla madhumuni ya hii sera ni kuwapatia wananchi ajira, kuongeza kipato cha kuanzisha biashara ndogo ndogo, kuondoa umaskini na kukuza uchumi kwa ujumla.

Katika sera hiyo pia tumezingatia urahisishaji wa upatikanaji wa vitu kama leseni, kutazama kodi ili zipunguzwe zinapofikia katika mambo ya biashara ndogo ndogo na kadhalika. Mheshimiwa Mwananzila aliulizia kuhusu mambo ya maeneo, tunashirikiana na Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba yanapatikana maeneo ya kufanya biashara hizo. Vile vile tunatizama mambo ya miundo mbinu mbalimbali. Kubwa kuliko yote, unaweza kufanya hayo yote lakini kama hakuna fedha bado watashindwa kuanzisha biashara hizo.

Kwa hiyo, tumetizama upatikanaji wa fedha na nitawaeleza kuhusu mfuko ambao tumekwishauanzisha tutautumia kuanzia mwezi wa nane. Vile vile tumekwenda kutizama jinsi ya kutoa mafunzo ya biashara na jinsi ya kuanzisha biashara, kuendesha biashara, kuandika michanganuo na jinsi ya kufanya biashara kwa faida. Pia kutizama uwerekano wa kupata taarifa mbalimbali kwa kutumia tovuti na pia tunaanzisha vituo vytaa taarifa katika kila Mkao. Mikakati mikubwa zaidi ni kusaidia uanzishaji wa viwanda hivi vijijini kama alivyouliza na kusisitiza Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi ni nini tumefanya? Hapa nimewaeleza sera na mikakati yake na vipengele mbalimbali vyta sera hiyo. Tumekwishatoa mafunzo ya wasimamizi wa mikopo wa kuwasaidia kuwafundisha watu mambo mbalimbali kama jinsi ya kuanzisha biashara kwa Mikoa yote 20. Kwa maana hiyo basi, kila Mkao una Afisa ambaye ana ujuzi wa jinsi ya kuanzisha biashara, kusimamia, masoko na kadhalika. Naomba msikilize kwa makini kwa sababu hii imekuwa ni shauku na kiu cha Waheshimiwa Wabunge wengi na tukitoka hapa kuna wengine ambao tumekubaliana kuandamana kabisa ili kuhakikisha kwamba tumekwenda pamoja ili kutimiza haya ambayo nayasema hapa sasa hivi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa hiyo 20, Mikoa 17 tumewapatia *computer* ili kuweka kumbukumbu za usimamizi na uendeshaji wa mfuko huo ambao ulikuwepo wa *NEDF*. Pia tumpata magari machache tulitaka kila Mkao uwe na gari ili liweze kuwapeleka wale Walimu kwenda kuwafundisha watu mpaka vijijini mpaka kule Mbozi. Kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamelalamika kwamba kwa kweli hawapati mafunzo hayo tutahakikisha kwamba mnakuwa wa kwanza kupata magari ili kufikisha Walimu wale mpaka vijijini kwa ajili ya kuwafundisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeliona tatizo la watu kutokujua biashara za kufanya, kutokujua jinsi ya kuanza na wengine wanaanzisha biashara lakini wanaziendesa kwa hasara. Kwa maana hiyo basi tuko tayari, kuna timu kubwa kabisa ya *SIDO* nikiwemo mimi mwenyewe kama kiongozi wao, iko pale na wenyewe wana nguvu kama mimi tu. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane tusaidiane katika jambo hili ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafanikisha mfuko huu na kazi hii inawezekana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeandaa Mfuko wa *Credit Guarantee Scheme* ambaopu tumekwishaomba shilingi milioni mia tano na tumepewa *allocation* sio kwamba tunazo na mfuko huu utakuwa unasimamiwa na Benki Kuu. Tutawapa maeleo zaidi kwenye vipeperushi kama mlivyoomba ili muweze kuelewa lakini pia katika Ofisi za *SIDO* kila Mkao utapata maeleo haya ambayo naeleza hapa sasa hivi. Mfuko huu unakisiwa kuongezeka mpaka ufikie shilingi bilioni tatu na utaratibiwa na *SIDO* kwa kupitia Benki za Biashara. Kiwango cha juu kabisa cha pesa ambazo mnaweza kuzipata au mtu anaweza kupata kwa mkopaji mmoja ni shilingi milioni thelathini. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuhakikisha tunautumia mfuko huu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu la nyongeza kwamba Mikoa ya Kusini, Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Membe, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Murji, Mheshimiwa Abdultif mmeongelea sana kuhusu zao la korosho na kuna wakati mlisema mnahitaji mashine za kufikia dola elfu kumi, dola elfu ishirini, naomba tuanze mfano na Mikoa hii michache. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaahidi kwamba baada ya Bunge hili nitapenda sana kutembelea Mkoa wa Lindi, Mtwara, Iringa na Tanga ambao tayari wamenionyesha wanayo miradi inayohitaji fedha. Naomba Waheshimiwa Wabunge watangulie huko tukitoka hapa msiende Dar es Salaam muende kwenye Majimbo halafu mnatuandalia miradi hiyo tutakuja na timu nzima ya *SIDO* tuanze kuzitumia fedha hizi haraka iwezekanavyo. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaposimama hapa mwaka ujao kama fedha hizi hazikutumika ndio zimeshakwenda hivyo na haitatupa moyo kuongeza fedha hizi kwa sababu mfuko huu mradi ambao tumeuandika unakwenda bilioni moja, bilioni mbili, bilioni tatu. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge, ninalewa ni vigumu kwa Mtanzania wa kawaida, mwananchi wa kijijini kuelewa kwamba kuna fedha hizi hilo la kwanza. La pili kuelewa jinsi hata ya kuzipata na tatu kuelewa hata cha kufanya. Lakini Mheshimiwa Shekiffu kama utaenda kuwachukua wale watu wako pale kijijini Lushoto uwaelekeze kabisa kwamba mtapata mafunzo haya na haya, tuko tayari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee zaidi kuhusu uwekezaji wa viwanda vya usindikaji mboga na matunda. Mheshimiwa Mlawa ametuandikia na hasa akanitaja mimi binafsi kwamba mwaka uliopita nilisimama hapa hapa nikasema nitakwenda naye Iringa na akawaambia wananchi wa Iringa wamesikitika sana. Naomba kuwaambia wananchi wa Iringa kwamba bado mikakati ipo tumekwishiandaa vizuri zaidi kwanza ningekuja wakati ule sikuwa na kifua kama sasa hivi kwa sababu sasa hivi nina hakika ninazo fedha. (*Makofî*)

Wakati ule ningekuja kukuuliza kwamba je, wako tayari kutoa mashamba yao tukamwombe *investor* anayeyitwa *Delamonte* ambaye yuko Kenya na ni *international or multinational company* ambaye iko Uingereza. Niliwasubiri sana mwaka jana mwezi wa tisa walikuwa watume timu ya kuja kutizama hali halisi ya nchi yetu. Kwanza, kutizama utafiti wa udongo kama tunaweza kupanda vitu namna gani kwa sababu sio kila tunachokipanda kinafaa kusindikwa na kupelekwa nje lazima kuwe na utaalam kamili ili ukila chungwa la hapa na la mti mwengine yote yafanane. Kwa hiyo, walinieleza jinsi ambavyo inahitajika na kule Kenya eneo la *Athi River* wamechukua eka nyingi sana wamelima wenyewe na ndio wakasindika kuweza kutengeneza juice na bidhaa mbalimbali. Mheshimiwa Mlawa bado tutatizama uwezekano huo na katika ziara yangu ya Mikoa ya Kusini nakuhakikishia na wananchi wa Iringa kwamba nitakuwepo huko kabla ya mwezi wa tisa, 2003. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kwa ufupi kabisa kuhusu biashara ya nje. Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian na wengine wameongelea sana kuhusu mikataba mbalimbali ya *AGO*, *EBA*, *PACT* na mingineyo. Waheshimiwa Wabunge wanasiskitika kwamba tumechelewa sana kuingia katika masoko haya. Nakiri tumechelewa na pia nakiri ni aibu sana kwa nchi yetu tunapewa fursa kama hii ambayo tunaweza kuitumia kupata kazi na ajira kwa wingi. Lakini mpaka sasa hivi bado hatujaweza kuitumia sawasawa. Namshukuru Mheshimiwa Abdulatif ametaja mpaka *data* kwamba Tanzania tume-exports dola milioni 16, mwaka unaofuata dola laki tano labda na arobani ni kweli na ipo kwenye data mpaka huko America na inaonyesha Tanzania ya mwisho katika soko la *AGOA*.

Serikali tumetekeleza wajibu wetu kabisa, Mheshimiwa Salome Mbatia ameandika nataka sababu, naomba kueleza sababu hizi ambazo pia zitafahamika kwa wengine. Tumefanya kazi yetu vizuri sana labda pale mwanzo tulichelewa kutohana na urasimu wa hapa na pale tukajikuta kwamba imetuchukua miaka miwili kukubalika kupeleka vitu America, naomba niongelee kwa kirefu soko la *AGOA*. Imetuchukua miaka miwili 2000-2002 baada ya Rais Clinton kutangaza kwamba sasa soko lipo kwa ajili ya nchi zilizoko *South of Sahara*. Baadaye tukafanikiwa, wakafanya utafiti wa nchi zote za Sahara ku-check je, hawa watu tulioiwapa hii fursa wameweza? Wakakuta wengi tunasuasua. Wakaongeza ule muda ulikuwa 2002-2004 kwa awamu ya kwanza mpaka 2008 bado wakitubembeleza. Wakaja Tanzania wamefanya semina za kila aina, wamejaribu kutumia kila njia ya kutuinua na kutufundisha kuhusu soko hili. Serikali

tumewapokea na tumewachukua washikadau wote wanaohusika na tukafanya semina hizi kwa pamoja. Baada ya hapo, Serikali tukaanza kutangaza nchini, tumewaeleza wafanyabiashara, wananchi kwa ujumla uzuri wa soko hili na manufaa kwa nchi yetu.

Wafanyabiashara hawakujitokeza kwa wingi kwa soko hili. Tumefuata viwanda ambavyo vilikuwepo kuanzia zamani tukaona tuzingatie zao moja la nguo, ziko bidhaa 1800 zikiwemo vyakula, nguo na vitu mbalimbali vinavyotengenezwa na mikono. Lakini bado kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge tukapeleka bidhaa za dola elfu 16 ambapo Kenya, Lesotho, Swaziland na wenzetu *South Africa* wamepeleka mpaka dola milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona hivyo, Serikali hatukuishia hapo japo tumeambiya tusifanye biashara lakini tukaona tuendelee bado kumsaidia mfanyakibashara ili aweze kuinuka na kuelewa cha kufanya. Tukaona tukatafute wataalam kutoka nije tukaenda nchi za Asia ambazo ndio wengi wanashughulika zaidi na mambo ya *garment manufacturing* na mambo ya *textiles* kama nyuzi na kadhalika. Tukapata wataalam kutoka Sri-Lanka Mauritius, Malaysia ambao walikuwa tayari kabisa kuja kuanzisha viwanda nchini kwetu. Kiwanda kimoja kinachukua sio chini ya watu 1000, mikakati yetu ya mwaka 2002 ilikuwa tuanzishe viwanda 10 tuweze kuajiri watu 10,000 kwa mwaka wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukupata Watanzania waliokubali hata kujiunga na watu hao. Mtanzania, sitaki kuwataja majina, anakuja anasema niweke jina langu humo lakini mimi sina mtaji wowote kwa vile mimi ni Mtanzania. Kama alivyokuwa anaongea Mheshimiwa Shekiffu tutayaongea hayo kama yanawezekana, kweli tungependa sana. Tukaona uwezekano unazidi kuwa mgumu lakini tukaona kuliko tuache hii fursa ya *AGOA* itupite nafuu sasa Serikali tuingilie kati tuwalete wataalam hapa waje waanzishe kiwanda tuwakopeshe na kama kawaida akija mtu hapa hajajenga kiwanda hicho kwa hiyo hana kitu cha kuweka dhamana. Kwa hiyo, Serikali kwa kutumia mfuko ambao unaithwa *Export Guarantee Scheme* unaosimamia na Benki ya Tanzania tukaamua tuutumie huo tuhakikishe kwamba tumedhamini kiwanda kimoja cha nguo angalau kianze. Hapo hapo mwaka huu tutenge fedha nyingi kwa ajili ya Watanzania ambao watakuwa tayari kuanzisha kiwanda kingine na kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwatangazie kwamba mwezi wa kumi na mbili au wa kumi na moja mwaka huu tutapeleka nguo *America* kwa kiwanda ambacho Serikali imekidhamini na huo ni mfano kwa viwanda vingine. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi zoezi ambalo tunalifanya ni la kujaribu kuajiri watu 1000 kutoka maeneo kadhaa ili tuweze kuanzisha kiwanda cha kwanza cha kupeleka nguo *AGOA*. Kuna viwanda viwili tayari vimekwishaanza kama *Sunflag* ndio waliopoleka hizo nguo za dola laki tano pamoja na Kiwanda cha *Leed* ambao Rais alikifungua mnamo mwezi wa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba fedha hizo zipo. Mheshimiwa Mramba ametusomea hapa kwamba fedha za *Export Guarantee Scheme* zipo na nimemwuliza je tufanye tena akasema sawa tuanze sasa hivi. Kama kuna ye yeyote ana uwezo wa kuanza aje tumwandikie, tumwelekeze ili tuweze kuanzisha kiwanda kingine ili tuweze kupeleka nguo *America*. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja nyingine kuhusu biashara za nije ambayo Mheshimiwa Fatma Said Ali ameomba kuwepo na semina kuhusu Mikataba ya Kibiashara ya Kimataifa kwa Wabunge ili kuelewa wazi biashara zetu na za dunia. Nadhani alikuwa anamaanisha mambo kama haya. Pengine kama Wabunge mngekuwa mme Fahamu au mngekuwa mme Fanyiwa semina mngeweza kuja hata ninyi wenywewe. Tunaomba Mtanzania ye yeyote anayetaka kuanzisha kiwanda tuwasiliane tuweze kusaidiana katika hili. Lakini vile vile tunaahidi kwamba tutakuwa tunafanya semina kabla ya mwisho wa mwaka 2004 ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kujua mikataba mbalimbali ya kibiashara na nchi za nije. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Fatma Said Ali ameomba kianzishwe kituo cha biashara Zanzibar ambacho kama *Board of External Trade* ilivyokuwa huku Bara. Sasa hivi tumewasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara, Mawasiliano na Utalii wa Zanzibar

amekwishatupatia Afisa mmoja. Tumekwishajua jengo na tumetenga shilingi milioni 42 za kuanzisha *Zanzibar Trade Center*. Wajumbe wa Bodi tumekwishawateua na tunasubiri kuwatangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile aliomba tufunque tawi la *SIDO Zanzibar* ili hii mikakati ambayo tunayokwenda nayo huko ifike Zanzibar. Sisi tutakuwa tayari kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa sababu kufuatana na shughuli za Muungano baadhi ya Taasisi za Serikali za Muungano hazifanyi kazi Zanzibar na *SIDO* ni mojawapo.

Mheshimiwa Shamim Khan aliuliza wafanyabiashara na akimaanisha zaidi wanawake wanashiriki maonyesho ya nje kwa kiwango gani. Ushiriki wetu kusema kweli kwa kipeleka wanawake katika biashara za nje unafanyika kikamilifu. Cha kufurahisha ni kwamba unapotangaza kwamba kuna maonyesho kwamba kwa mfano Japan wafanyabiashara wanawake wanajitokeza kuliko hata wanaume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka 2000 walikwenda watu 36 Ujerumani ilikuwa *Expo-2000* kati ya hao 32 walikuwa wanawake. Kukafanya maonyesho mengine yanaitwa *Tanzania Land of Kilimanjaro and Zanzibar* yaliyofanyika Japan wanawake 15 kati ya watu 30 walikwenda katika maonyesho hayo na mengine mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya alisema shughuli ziende vijijini, kuna kitabu tulikitoa kwa Wabunge wote kinaitwa, *SIDO* kwa Maendeleo. Kinaonesha tumefanya kazi gani vijijini kwa kupitia *SIDO*. Kusema kweli shughuli zinaandaliwa vizuri sana katika vijiji. Kila Mkoa unazo Ofisi za *SIDO* na yale majengo ambayo mengi tumeyaona yameharibika tuko katika mpango wa kuyakarabati na yale ambayo yalitumika vibaya tunataka tuyachukue na namhakikishia Mheshimiwa Mwananzila ambaye amesema hatuaenda Rukwa tutafika Rukwa na tutafutilia jengo hilo ambalo anaona limechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Shellukindo aliyeongelea kuhusu *investmenst* za wageni zikiwemo *supermarkets na garage*. Kulingana na Sera ya Biashara au Soko Huria, hatuwezi kuzuia kabisa bila kukiuka Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania ni washiriki. Kwa maana hiyo basi inabidi tukubali waje hapa kuwekeza lakin tunaongea nao kwa mfano binafsi nilikwenda katika hizi *supermarkets* *Shoprite* na *Shoppers Plaza* kutizama kuna nini cha kwetu pale na nimeongea nao. *Shoprite* walikuwa tukawa na mazungumzo. Mkubwa wao alitoka Afrika Kusini na akaja Ofisini tukaongelea masuala haya wamekubali kabisa kuchukua bidhaa zetu. Ni aibu yeye kwenda kuchukua fresh tomato kutoka Afrika Kusini, viazi, maziwa, mayai, achali na bidhaa nyingine.

Baada ya muda tukakuta wamejaza *ma-shelf* yao bidhaa za Kitanzania na wanatuonyesha kwamba hii ni *yogurt* kutoka Kiwanda cha Arusha, hii ni achali kutoka wanawake waliofundishwa na *SIDO* na *UNIDO* na *order* nyingi wamekwishachukua. Isipokuwa wamesema kwamba wako tayari kuwafundisha wafanyabishara ndogo ndogo hao ili waweze kukidhi ubora wa bidhaa ambazo wangependa kuuza katika supermarket yao. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba vile vile tuwahimize wananchi wa Tanzania waweze kufunga hizi supermarket na kuuza bidhaa zinazotoka katika viwanda yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shellukindo pia aliuliza kuhusu bidhaa za viwanda vya ngozi na alitoa mfano wa zao moja ambalo aliona ni zuri sana isipokuwa anasikitika kwamba kwa nini haziendelei kuzalishwa. Ni kweli sekta hii ilizorota sana kwa kiwango kikubwa, Serikali tulifanya utafiti wa kina kabisa mpaka tukawahuisha *UNIDO* wakatusaidia tukaandika mchanganuo mzuri sana na tukajua matatizo yanayovikabili viwanda vya nguzi. Tulitaka kujua ni wa nini Tanzania nchi ya tatu kwa ufugaji ng'ombe duniani ati leo hatuna hata kiwanda kimoja cha ngozi na ngozi zinakwenda nje. Tuna viwanda vitano vikubwa ambavyo vinazalisha ngozi. Tulipata mambo mengi yakiwemo ngozi hazipatikani kwa wingi watu wanakimbiza kipeleka nje, tukaambiwa ubora wa ngozi pia mbaya wale wanaofuga zile ng'ombe wanazichapa mijeledi, wanaziandika kwa hiyo zinabakia na michoro kwa hiyo ngozi ikija unakuta sehemu ndogo tu ndio inayofaa, utaalam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukaamua tushirikiane na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na washikadau kujaribu kutatua matatizo haya. Lakini la muhimu kwanza hizi ngozi ambazo zinakwenda nje zinazuwa kwa minada katika miji michache mfano Mwanza, Arusha na wanapeleka nchi

jirani ya Kenya na wanazitengeneza mpaka inakuwa quality ya white/blue na wanapeleka Italy na nchi mbalimbali. Tukaona tuenze kwanza kudhibiti suala hilo. Tukapeleka Waraka Baraza la Mawaziri, Waraka Na.2 wa mwaka 2003 na kupeleka mapendekezo na mikakati ya kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi. La kwanza ambalo tumelitangaza hapa tumeweka ushuru wa 20% kwa ngozi ghafi zitakazouzwa nje na ushuru huu basi utatumika kuinua sekta hii ya ngozi. Vile vile fedha hizo zitakazopatikana zitaunda mfuko ambao utatumika kuboresha huduma za ugavi (*extension services*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, narudia tena kusema kwamba naunga mkono kwa asilimia mia, ahsante sana. (*Makofsi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kauli na kwa maandishi. Kwa ujumla michango yao imetusaidia sana kuimarisha utendaji kazi wetu katika Wizara. Michango yao unaweza kuigawanya katika sehemu tatu. Kwanza ni ushauri ambao tunaupokea na tutaushughulikia kikamilifu kwa sababu tuna maandishi kwa sababu utaboresha utendaji kazi katika Wizara. Pili kuna hoja ambazo zinataka maelezo tutazitolea maelezo kama alivyotoa maelezo mwenzangu hapa Naibu Waziri lakini na mimi nitasaidia kufanya hivyo. Tatu, ni maelezo ambayo yametolewa katika hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara lakini kwa kweli yanahusu Wizara nydingine kuna suala la kilimo, umeme, haya yote tumeyapokea kama Serikali na tutayakabidhi kwa Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao walitoa maelezo hapa Bungeni nao wako 14. Nao ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Halimensi Mayonga, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Ali Omar Mohamed Mwenda, Mheshimiwa Ali Amani Karavina, Mheshimiwa Alhaji Ahmadi Hassan Mpeme, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail na Mheshimiwa Rita Mlaki ambaye ni Naibu Waziri. (*Makofsi*)

Waliochangia kwa maandishi ni kama hivi ifuatavyo: Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Mwadini Abas Jecha, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Maghembe, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Phillip A. Magani. Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalifan, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, Mheshimiwa Aridi Uledi na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

Wengine ni Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Nyaburi Kerenge Nyaburi, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa John Elineza Singo, Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Gwassa Sebabilii na Mheshimiwa Ibrahim Wankanga Marwa, jumla ni wachangiaji 44. (*Makofsi*)

Naomba nianze kutoa maelezo kuhusu kusimamia viwanda vilivyobinafsishwa, Kamati ya Uwekezaji ndio iliyotoa hoja hii kwa kupitia Mheshimiwa Mbatia. Kwanza tunaitpongeza Kamati kwa hotuba yao nzuri, Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji ilianda Waraka wa Serikali ambao ulizungumzia suala la ufuutiliaji wa viwanda vilivyobinafsishwa. Hizi hatua za Wizara ya Viwanda na Biashara ni mwendelezo ya hatua ile Serikali imeshaagiza. Kwa hiyo, ndani ya Wizara tuna Kitengo mahsus kwa lengo hili la kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa. Ndio maana tukaweza kutoa ile taarifa tuliyotoa kwamba viwanda 24 vinafanya kazi vizuri, viwanda 12 vinafanya kazi kwa ufanisi mdogo na viwanda 14 vimefungwa. Hiyo inatokana na kazi hii ya ufuutiliaji ambayo tumeanza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kusositiza hapa kwamba lengo la ufuatiliaji huu ni kubainisha nini matatizo ya viwanda hivi ili kwa pamoja tukae nao, tujadiliane nao namna ya kuvifufua sio kuwa-harass au kuwafanya jambo lingine lolote, hapana. Shabaha ni tukae nao tujifunze nini matatizo yao halafu tuwasaidie kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato ya Wizara, hili nalo lilisemwa kwamba mapato yale yalikuwa mwisho Februari lakini wakati tunatoa maelezo yetu tulisema mapato yale mpaka mwisho mwa mwezi Mei 2003 hasa kuhusu lile Shirika la Mizani na vipimo tulitoa mpaka mwisho Desemba na hizo ziko kwenye hotuba kwa hiyo hili tumelisahihisha vizuri na linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara kupewa fedha kidogo. Kwa kweli tunaishukuru Kamati kwa concern hii. Hili pia limezungumzwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Mwandoro. Hili nalo tunaliunga mkono tunasema, sawasawa, lakini lazima vile vile tuliseme kwamba Kiserikali fedha ni kidogo. Kwa hiyo, lazima kuna wengine watapata zaidi na wengine watapata kidogo. Kwa hiyo, hili tuna matumaini kwamba katika siku zijazo wakati Serikali itakuwa na uwezo zaidi viwanda vitapewa fedha nyingi zaidi ili kuweza kuhudumia sekta hii muhimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha kidogo kwa ajili ya taasisi za utafiti. nalo tunaliunga mkono tunashukuru kwa kutueleza hili sisi wenyewe tunalifahamu vile vile na tatizo ni lile lile la usifinyu wa bajeti na tuna hakika Serikali inatambua kabisa umuhimu wa taasisi hizi za usafiri kama vile *TIRDO*, *TEMDO*, *CARMATEC*, ndiyo maana tunesema vibaki mikononi mwa Serikali, lakini na huko tunakokwenda tutaendelea kuimarisha uwezo wetu na kuziwezesha kupata fedha za kutosha ili ziweze kufanya utafiti unaotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria ya *anti-dumping* Msemaji wa Upinzani amesema kwamba, kwanza amesema huduma nzuri, tunampongeza kabisa kwa hotuba yake nzuri na tunaridhika kwa yote aliyosema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunataka kusema kwamba suala hili la *anti-dumping Bill* halicheleweshwi kwa urasimu, ahaa, *actually* tulishaamua na kukamilisha kwa ajili ya kikao cha Bunge cha mwezi Aprili mwaka huu 2003. Lakini kwa sababu Miswada ilikuwa mingi haikuwezekana ndiyo maana lenyewe likaaahirishwa na kwa sababu kikao hiki hakizungumzii Miswada maana yake mpaka kikao cha mwezi Novemba, 2003. Kwa hiyo, mimi nina hakika kabisa katika kikao cha mwezi Novemba, 2003 Muswada huu utakuja na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtapata fursa ya kuujadili na kuupitisha kama mtakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *NEDEP*. Kuna kitabu kabisa kimetolewa na *SIDO* kuhusu suala hili kwa miaka kumi iliyopita na kitabu hiki kimegawiwa. Ukitazama katika kitabu kile utaona kwamba kwa kweli hali ya urejeshaji ni nzuri asilimia 83 mpaka 87. Kiwango hiki ni cha juu cha urejeshaji mikopo na ni dalili kuwa miradi hiyo haijafa, bado inaendelea. Ukitaka kupata taarifa zaidi ukisoma taarifa ile utaona ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *economic diplomacy*. Hili nakubaliana na Msemaji wa Upinzani kwamba ni suala muhimu na ndiyo maana sera mpya ya mambo ya nchi za nje imizingatia suala hili. Sisi wenyewe kama Wizara tumeimarisha ofisi zetu za Geneva na Brussels ambako kunafanyika mazungumzo ya mara kwa mara kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Biashara, Chuo hiki kinashiriki katika shughuli mbalimbali za kitaalam kama kutoa mada katika warsha mbalimbali, lakini vile vile kinafanya ushauri wa kitaalam (*consultancy*). Kwa msfano, mwaka jana peke yake *CBE* ilifanya *consultancy* mbalimbali ambazo ziliikingizia Chuo shilingi milioni 35. Kwa hiyo, kazi inafanyika na ni nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usambazaji wa viwanda nchini. Maendeleo ya viwanda kwa kweli yanategemea sana miundombinu muhimu na ndiyo maana Serikali inasambaza miundombinu, barabara zinajengwa, nimemsikiliza kwa makini hapa Mheshimiwa Alhaji Mpeme akizungumzia Kusini

kule. Barabara ya Kusini sasa hivi sasa ni imara zaidi baada ya kufunguliwa daraja lipya na litazinduliwa nadhani tarehe 2 Agosti. Kwa hiyo, hiyo ni juhudhi mojawapo ya Serikali yetu katika kuimarisha miundombinu. Kwa hiyo, kule tutakakokuwa tuna uwezo tutafanya kazi inayostahili lakini lazima tutambue kwamba uwezo wa Serikali wa kujenga miundombinu imara kwa nchi nzima haupo na ndiyo maana tunawakaribisha wawekezaji binafsi. Ndiyo maana tunalitilia mkazo hili kwamba lazima sisi wote tuwatafute wawekezaji binafsi, kila mtu pale alipo na tuwahamasishe. Kuna mfano mzuri tu hapa wa Mkoa wa Kilimanjaro, wameitisha semina ya investment, itakuwa tarehe 14 mpaka 16. Sasa wamewakaribisha watu mbalimbali wa nje na wa ndani watakwendwa pale, pamoja na mimi nitashiriki. Kwa hiyo, na ninyi kila mtu afanye kwa mahali pake namna ya kuhamasisha uwekezaji, siyo kazi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vile vile hatua zingine tumechukua sisi Serikali kama hii ya *SME Policy* ambayo nayo inatarajia kuhamasisha wazalishaji wa viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo na uanzishaji wa maeneo maalum yaani mitaa ya viwanda ili kuwawezesha wananchi hawa waweze kuzalisha mali katika viwanda hivi na kujiongezea kipato. Ni muhimu kusema kwamba hawa viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndiyo wafanyabiashara wa kati na wafanyabiashara wakubwa na wenye viwanda vya kati na viwanda vikubwa wa kesho. Haiwezekani watu wote hawa waanze na kuwa na viwanda vikubwa, hapana, wengine wanaanza hivi vidogo vidogo na baadaye wanafikia ngazi ya kati na ya juu. Kwa hiyo, hili jambo ni zuri na tumelifanya kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhusu fedha ndogo za maendeleo hasa kwa ajili ya *EPZ*. Hili nalo tunalikubali kwamba fedha zile ni ndogo na ndiyo maana Wizara inatafuta bajeti nje ya Bajeti ya Serikali kwa kushirikisha wawekezaji binafsi na tumepata michango hiyo ya wawekezaji binafsi na tutaendelea kuitafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uingizaji wa sigara bandia. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboot na vile vile Mheshimiwa Halimenshi Mayonga. Bahati mbaya jambo hili nilishalielekeza na taarifa ilishaandaliwa lakini wakati ilivyokuja hapa mimi ndipo nilipokwenda Dar es Salaam kwa ajili ya ziara ya Mheshimiwa Rais Mwai Kibaki na baadaye kwenda nchi za nje kwa ajili ya shughuli za kikazi. Lakini taarifa ile tunayo, kwa muhtasari tu ni kwamba kazi hii ni kubwa ya kupambana na hawa waingizaji bidhaa kwa magendo. Hizi magendo si hao tu kuna vibiriti, sukari, kuna vitu vingi vinaingizwa ndani ya nchi yetu kwa magendo. Kwa hiyo, tumekubaliana katika Serikali pale kwa kutumia uongozi wa *TRA* pamoja na *TBS* na Polisi tutasimamia kudhibiti suala hili la magendo na tutapenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge pale mtakapoona bado linaendelea basi mwendelee kutuarifu na sisi kama Serikali tutaendelea kujitahidi kulishughulikia jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu URAFIKI, kwa kweli Wizara haina habari kuhusu unyanyasaji lakini ni muhimu niseme kwamba URAFIKI pale pana ubia kati ya Wachina na Watanzania, lakini Wachina ndiyo wawekezaji wenye hisa nyingi yaani *majority owner* au *shareholder*. Kwa hiyo, hata mmiliki na Menejimenti ya kiwanda inafanana kwa maana hiyo basi Meneja Mkuu lazima atakuwa Mchima ndivyo tulivyokubaliana na hilo katika sehemu zote za uongozi ndani ya kiwanda cha URAFIKI isipokuwa tu kwenye utawala ambapo kiongozi mkuu anakuwa Mtanzania. Mimi nina hakika wale waliokwenda katika kiwanda kile walimwona Naibu Meneja Mkuu ambaye ni Mtanzania Ndugu Nasoro Baraza na yupo hapa.

(*Hapa Ndugu Baraza - Naibu Meneja Mkuu wa Kiwanda cha URAFIKI alionyeshwa kwa Wabunge*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yule pale aliyesimama, hakukaa amesimama pale kwa hiyo anaonekana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili ndiyo makubaliano yetu na katika suala hili lazima nisisitize vile vile kwamba sisi Serikali ni sera ya Chama chetu cha CCM kujitoa katika shughuli za kibiashara. Hii ndiyo sera yetu na Mheshimiwa Abdullatif Esmail katukumbusha kwamba kazi kubwa ya Serikali ni kujitoa katika biashara. Ndivyo alivyotukumbusha hapa isipokuwa kazi yetu sisi kama Serikali ni facilitation, lakini kazi ya kufanya biashara kabisa siyo yetu, ndiyo maana tumejitoa lakini tunapenda wenzenzu wengine hasa katika sekta binafsi waendelee kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mwani. Ni kweli mwani unaweza ukamkomboa mkulima mdogo na ni kweli kuna hiyo substance ambayo imegunduliwa na *TIRDO* kwamba ipo. Kwa hiyo kazi muhimu hapa ni kuendelea kuwahamasisha wananchi kuzalisha mwani mzuri kuondoa mchanga na uchafu. Hili ni muhimu sana maana tunazungumzia juu ya ubora hapa wa bidhaa, huwezi kukubali kupata haya matarajio au unayotaka kuyapata kama ubora wa bidhaa ile ni mbaya. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu na tutaendelea kulifuatilia kwa karibu ili tuone jinsi gani wananchi wanaweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya saruji. Ufumbuzi wa kudumu wa bei ya saruji Mheshimiwa Mayonga siyo kwamba Serikali iwe na bei ya nchi nzima, haiwezekani, huko ndiyo tulikokuwa zamani *pan territorial pricing system* ndiyo kilikuwa kitu cha zamani ambacho tulikuwa tunakifanya. Lakini katika uchumi wa leo haiwezekani na hicho kitu hakiwezi kuruhusiwa. Hatuwezi vile vile kama Serikali tutoe ruzuku kwa bidhaa hizo, tunaweza kutoa kwa chache kwa mfano mbolea kwa ajili ya kuhimiza kilimo, hilo ni muhimu. Tunapenda kwa kweli wananchi wawe na nyumba bora na mimi najua kwamba Kigoma zamani walikuwa wanaishi katika nyumba za ngondaki lakini siku hizi hazipo, wamejitalidi kweli kweli na naomba waendelee kujitalidi kwa sababu hayo ndiyo maendeleo yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Shellukindo. Mimi namwunga mkono katika jambo hili lakini lazima niseme kwamba kuhusu *supermarket* ni kweli ina mwelekeo wa kutumika kuuza bidhaa za nje ambako hao wenyе *supermarket* wanatoka lakini vile vile tunatakiwa na sisi tuanzishe za kwetu ambazo zitauza bidhaa zetu tunatakiwa tufanye hivyo. Ingawa ni kweli vile vile kwamba tunajadiliana nao ili pale inapowezekana wauze bidhaa zetu lakini la muhimu hapa ni kuzingatia ubora. Jambo hili la supermarket ni jema kwa nini? Kwa sababu kwanza bidhaa ile tunaweza kuifuatilia (*monitoring*) na hivyo basi wanaweza wakalipa kodi, lakini hao wanaotembeza mitaani *Matching Guys* siyo Machinga, *Matching Guys*, hawalipi kodi. Kwa hiyo, msimamo wetu ni kuendelea kuweka vituo muhimu vya kuuzia bidhaa badala ya kutaka watu watembeze tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shamba la mpira. Hili nalo nalikubali na hili kwa kweli linahusu kilimo na tutalifikisha. Hili amelitoa Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Mntangi na Mheshimiwa Mwenda. Lakini vile vile mpira unapatikana Mkoani Morogoro, kwa hiyo Wabunge wa Morogoro hasa Mheshimiwa Abu Kiwanga na nadhani Mheshimiwa Hamza Mwenegoha , pia wanaweza kushiriki katika jambo hili la kuendesha na kuwa na mashamba makubwa ya mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora wa khanga. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, standards za vitenge na khanga zipo na ni jambo la lazima bidhaa zote zinazozalishwa na zinazoingia nchini lazima zifuate standards za vipimo hivyo. Lakini vile vile napenda niseme kwamba katika process ile ya kuzalisha bidhaa kwa mfano katika kiwanda cha URAFIKI au cha Karibu Textile Mills ile process ya uzalishaji kuna khanga ya kwanza ya *grade A*, kuna *grade B* na *grade C*. Ile process ya uzalishaji lazima kutakuwa na uchafuzi wa ile *material* sasa ile *material* inayochafuka kama ile khanga tulioonyesha hapa ninaweza kusema ni *reject*. Sasa ukienda kiwandani ukauziwa khanga ile kwa bei ya *grade A* au *B* ni kosa. Lakini kama unauziwa kama *reject* basi utapokea kwa bei ya *reject* na hatuna njia pale ya kukusaidia kwa sababu yenewe siyo yenewe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili linaweza kutokea. Mheshimiwa Burian hakuniambia na mimi napatana naye sana, hakuniambia mapema, labda tungekaa vizuri tungeshauriana tukajua namna alivyopata ile khanga na tukachukua hatua. (*Kicheko*)

Lakini mimi nahisi watu wangu wa URAFIKI ambako ndiko inakozalishwa wanasema hakwenda kwoo. Kwa hiyo, ina maana kwamba alipata kwingine ambako inawezekana katika zile khanga alizonunua doti ishirini wakamekeea zingine mbaya, jambo ambalo namwonea huruma lakini sina njia ya kufanya. Lakini ni muhimu kuzingatia hilo kwamba katika zile khanga zina madaraja matatu na inatakiwa ulipe bei ambayo inayofanana na khanga au kitenge unachotaka kununu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu water guard. Hili tunalifahamu na Wizara yangu imewandikia *TBS* kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Wizara ya Afya kwa kuititia Mkemia Mkuu, tumekubaliana kwamba tuunde Kamati ichunguze jambo hili kwamba hii dawa kweli ni sahihi, ina meet standard na wao wenywewe tumewapa mamlaka kabisa watangaze kama inafaa au haifai maana wao ndiyo

wataalam. Kwa hiyo, hili jambo tunalishughulikia kwa kushirikiana na taasisi zingine katika Serikali ambazo tuna mamlaka nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada za kulipa ili kupatiwa idhini ya kutumia alama za ubora wa *TBS* ambalo limeletwa na Mheshimiwa Mntangi Mbunge wa Muheza. Hili tunapenda kusema hivi gharama za utoaji wa alama ya ubora ya *TBS* ni hizi zifuatazo:-

Kwanza kuna gharama ya kupima bidhaa yaani *testing charges*, gharama za usafiri na malazi kwenda kuchukua *samples* na kuzipima na gharama ya *guarantee costs* ambayo ni asilimia 25 of the direct costs ambazo hizo nimezitaja hapo mwanzo. Sasa tumekubaliana bado katika Wizara kwamba hizi gharama sasa zote hasa kwa wale wanaviwanda vidogo na wafanyabiashara ndogo wasidaiwe tena. Isipokuwa wale wenye makampuni makubwa. Lakini wale wadogo kama mimi wale hatutawadai hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masharti ya leseni. Hili pia lilizungumzwa na Mheshimiwa Mntangi, ni kweli sisi kama Serikali Wizara ya Viwanda na Biashara hakuna masharti tena katika utoaji wa leseni. Lakini kule kwenye Wilaya kule ndiko kwenye matatizo kule bado wanaweka masharti, lakini wameagizwa na Serikali na wao waondoe kero hizi. Kwa hiyo, hili nadhani linashughulikiwa na kwa kweli Waziri wa Fedha alitangaza hapa Bungeni, kwa hiyo hili jambo linashughulikiwa vizuri na nina hakika litakwisha. Lakini pia nataka kusema kama nilivyo sema kwenye hotuba ya bajeti kwamba Serikali inaipitia upya Sheria ya Leseni ya Mwaka 1972 kwa lengo la kuondoa kero kwa wafanyabiashara na wenye viwanda. Kwa hiyo, hili tutalishughulikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *KILAMCO* na *TUICO* na vile vile *Chipboard* haya ni mambo yanayohusu Wizara ya Maliasili na Utalii. Hili la *KILAMCO* linahusu Wizara ya Nishati na Madini tumeyasikia, tutayazingatia na tutyawakilisha kwa Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Boma na Mheshimiwa Sadiq, kwanza Mheshimiwa Boma alisema kwa nini pale kwenye maonyesho ya biashara kuna gharama za kiingilio. Sasa tunasema hivi gharama zile siyo kubwa sana ni chache tu ambazo zinasaidia kwa kweli katika kuboresha huduma zinazotolewa pale ndani ya uwanja wa Sabasaba. Ule uwanja una gharama kubwa kuukarabati na kadhalika. Kwa hiyo wale wanaoingia ndani lazima kidogo wachangie ili waweze kusaidia kupunguza gharama za maonyesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwelekeo wa maonyesho Mheshimiwa Sadiq amezungumzia suala hilo. Maonyesho haya ni *general trade fair* yanaruhusu mauzo haya siyo maonyesho ambayo unaonyesha tu halafu watu wanatoka. Haya ni *general trade fair* ambayo maana yake unaonyesha lakini vile vile watu wanunua, ingawa kuna mabanda mle ambayo kazi yake ni kuonyesha tu. Yapo mabanda yametengwa kwa ajili ya kuonyesha tu na kama wanauza wanauza katika muda wa mwisho siyo pale mwanzoni, hiyo nayo ipo lakini kwa ujumla ile ni *general trade fair* lazima watu wanunue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Polytex*, hili pia lilizungumzwa na Mheshimiwa Sadiq. Hili limechukua muda mrefu lakini sasa nataka kukuthibitishia kwamba mwekezaji huyu tumewekeana masharti mapya ili aweze kukifufua kiwanda na mpaka sasa maendeleo yake ni mazuri. Tumempa miezi sita mpaka minane au kumi ili kama atashindwa kiwanda kitachukuliwa na Serikali, lakini ahadi alizotupa na mwelekeo unaonyesha sasa kiwanda cha *Polytex* kitafufuka na kitaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha *Moro Shoe*, hili pia lilizungumziwa na Mheshimiwa Sadiq. Mheshimiwa Sadiq ukweli ni huu kwamba kile kiwanda kilibinafsishwa mwaka 1992 kwa kampuni moja ya *Somalia Gullet Limited* lakini wao walichukua asilimia 70 na Serikali ilibakia na asilimia 30.

Kiwanda hiki kiliajiri watu kama unakumbuka karibu 200 na kilianza kufanya kazi vizuri na kutengeneza viatu vizuri. Baadaye mwekezaji huyu alishindwa kukiendesha kiwanda hiki, lakini wakati huo anashindwa kukiendesha, kiwanda hiki kikaungua moto.

Kwa hiyo, wenyе hisа ya kiwanda yaani yule Msomali na Serikali wakakubaliana kwamba hawawezi kukikarabati, kitu watakachofanya watakilisi, sasa ndiyo maana baadhi ya vifaa ambavyo vilipona vilichukuliwa kama sehemu ya ufilisi. Hiyo kufilisi kiwanda siyo jambo jipya, viwanda vingi sana vinafilisika hasa katika uchumi huu wa sasa wa soko, suala la kufilisi viwanda na maduka makubwa ni jambo la kawaida kabisa. Kwa hiyo, hilo lazima tulikubali, lakini vile vite tukazane kujenga zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shekifu alizungumzia juu ya kutenga aina ya biashara kwa Watanzania. Mimi natambua umuhimu wa suala hili kwa Watanzania kumiliki uchumi wa Taifa lao na ndiyo maana nikazungumzia kwamba kama Sera ya CCM Kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu ambayo mimi niiiongoza tulianaa Sera maana ile sera yenyewe iliyoko katika mwelekeo wa CCM ni *paragraph* moja hata kwenye Ilani ni *paragraph* moja tu.

Lakini sasa huku sisi tumeandika kitabu kikubwa ambacho kinatoa maeleo zaidi lakini tukatunga vite vite na Muswada. Sasa Muswada ule utakapokubaliwa, utakapokuja hapa Bungeni mtapata fursa kubwa zaidi ya kujadili na kuona mambo gani yanafaa kutengwa kwa ajili ya Watanzania tu, mambo gani tuwe na ubia na wageni na mambo gani yawe ya wageni tu. Hili tunaweza kulifanya kwa ushirikiano wa sisi sote. Lakini sera ya Chama chetu ni uvezeshaji wa wananchi wa Tanzania wote bila kujali rangi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu ya muda naomba niseme kwamba bado zipo hoja ambazo ningependa kuzieleza lakini haiwezekani, tutaandaa majibu haya na tutaweza kuwafikishia Wabunge baada ya kikao hiki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani wanankumbusha wenzangu hapa kwamba katika kuwataja wachangiaji sikusema sawasawa, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboot, alichangia kwa kusema na pia kwa maandishi. Nilisema nafikiri kwa maandishi tu sikusema kwa kuongea. Halafu nafikiri Mheshimiwa George Francis Mlawa, nilisema Mheshimiwa Joseph. Sasa yeze ni George siyo Joseph, naomba radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 44 - WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ... .. .	Shs. 1,753,183,841/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ... .. . .. .	Shs. 46,692,500/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> ... .. . .. .	Shs. 668,052,452/=
Kif. 2001 - <i>Industry</i> ... .. . .. . .. .	Shs. 2,451,650,772/=
Kif. 3001 - <i>Commerce</i> ... .. . .. . .. .	Shs. 1,321,118,782/=
Kif. 3002 - <i>SADC</i> ... .. . .. . .. .	Shs. 200,591,551/=
Kif. 3003 - <i>Weights and Measures</i> ... ..	Shs. -
Kif. 3004 - <i>Trade Practices Bureau Agency</i> ...	Shs. 141,001,700/=
Kif. 3005 - <i>Trade Practices Tribunal</i> ... .. .	Shs. 24,865,002/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 44 - WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... .. . .. . .. . Shs. 1,820,469,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko voyote)*

*(Bunge lilitrudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya Mwaka 2003/2004, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofî)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara Kwa Mwaka 2003/2004 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujuahirisha shughuli za Bunge ni ma tangazo hapa. Mheshimiwa Mwamoto ni kiongozi wa ile klubu ya michezo ya Wabunge, anatangaza kwamba Wabunge wote tubaki humu ndani baada ya Kuahirisha Bunge, ili mpate vifaa vya michezo kwa ajili ya mashindano ya kesho. *(Makofî)*

Kwa sababu michezo hii inaanza asubuhi sana ni vizuri ukahakikisha umepata vifaa leo ili kesho uwe tayari kwa michezo hiyo. Baada ya tangazo hilo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.00 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 28 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*

